

**SIFA ZA MASHUJAA NA UMUHIMU WAO
KWA JAM11 ZAO: ULINGANISHI WA FUMO
LIYONGO NA SHAKA ZULU**

NA

JULIUS MUNGAIGICHAMBA

**IDARA YAISIMU NA LUGHA
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

University of NAIROBI Library

'ill

2005

**SIFA ZA MASHUJAA NA UMUHIMU WAO
KWA JAMII ZAO: ULINGANISHI WA FUMO
LIYONGO NA SHAKA ZULU**

NA

JULIUS MUNGAI GICHAMBA

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI
YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (*MASTER OF
ARTS*) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

SEPTEMBER, 2005

IKIRARI

**TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA
HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI VA SHAHADA KATIKA
CHUOKIKUU KINGINE**




JULIUS MUNGAI GICHAMBA

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI
VETU KAMA WASIMAMIZI WALIOTEULIWA NA CHUO
KIKUU CHA NAIROBI**

DKT. KINEENE WA MUTISO

NA



DKT. AYMAN AL-ASAR

TABARUKU

Kwa ukumbusho na heshima ya marehemu dada yangu mpendwa, Lucy, aliyetuaga mnamo tarehe 12 Disemba 2003, miezi michache tu baada ya kuanza masomo yangu ya uzamili.

Pia, kwa heshima na ukumbusho wa mwalimu wetu, Ndugu Richard S. Mgullu (Mwanaisimu) aliyetuaga tarehe 28 Agosti 2004

Kwenu nyote, Mola awaruzuku na awape mbawazi huko mliko. Sisi pia tumo safarini na punde si punde...

Jogoo lilipolia watu waliosimama,
Mbele ya Mkahawa "Fungua mwango" wasenia,
Maisha mnaelewa kuwa mafupi daima,
Haturudii dunia mara moja tukihama."
(Shaaban Robert)

"Dunia ni mabadili ya usiku na nichana,
Ndani watu na ajali milele ni kushindana,
Huku na huko shughuli kuoana na kuuana,
Mwisho hulala niahali mtu padoogo sana."
(Omar Khayyam)

SHUKRANI

Kwanza, ninamshukuru ghaya Mwenyezi Mungu (shujaa wa mashujaa) kwa kuniuoni na kunipa hekima, moyo mkunjufu, afya bora na uvumilivu sio tu katika kuiandika tasnifu hii ball pia katika mchakato mzima wa mfumo wa elimu na pia maishani kwa jumla Shukrani zake kwake Mola zinatokana pia na kule kuniwezesha kuikamilisha shahada yangu ya uzamili nikiwa bado mwenye umri mdogo.

Pili, ninakishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunifadhili kikamilifu katika masomo yangu ya shahada ya uzamili. Ama kwa hakika, huu ni ufadhili ambao sitausahau dahari kwani ni wachache waweza kupata fursa hii. Ninakiomba Chuo hiki kiendeleee na moyo huo huo wa kuwafadhili wanafunzi na watafiti zaidi kwani katika kufanya hivi, kitakuwa kikistawisha mbegu ambazo zitakuja kuwafaa sio tu wanafunzi wa baadaye bali pia mbegu zitakazokuwa zenye manufaa kwa ustawi wa nchi na ulimwengu kwa jumla.

Pia, ninawashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Kineene wa Mutiso na Dkt. Ayman Al-Asar kwa ushauri wa busara, mwongozo na masahihisho ya hapa na pale katika hatua mbalimbali za kuiandika tasnifu hii. Ninawapa hongera pia kwa namna walivyopitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa haraka na kwa umakini na kwa hiyo kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu kwa muda mfupi. Aidha, midahalo mbalimbali niliyoshiriki pamoja nao ilinipa mshawasha wa kuwaza zaidi na kuandika kazi bora. Mola azidi kuwapa hekima na neema.

Aidha, ninawashukuru wahadhiri walionifunza katika hatua mbalimbali za masomo yangu katika Chuo Kikuu Cha Nairobi hadi kufikia kuhitimu katika shahada ya uzamili. Wale walionifunza katika shahada ya uzamili ni pamoja na: Prof. Abdulaziz Mohammed, Dkt. Mwenda Mbatiah (ambaye kwa sasa ndiye mwenyekiti wa Idara ya Isimu na Lugha), Prof. Kithaka wa Mberia, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Tom Olali, Bi. Margaret Njuguna, Bi. Hannah Mwaliwa na marehemu Ndugu Richard Mgullu. Nawahongera pia wahadhiri walionifunza katika masomo ya shahada yangu ya

kwanza katika somo la Kiswahili miongoni mwao wakiwemo: Ndugu Nyachae Michira, Ndugu Timothy Arege, Ndugu Basilio Mungania na Ndugu Mwangangi wa Musyoka Kadhalika, sitasita kuwashukuru wahadhiri wengine katika Idara ya Isimu kama vile, Prof. Okoth Okombo, Dkt. Marete, Ndugu Akida, Dkt. Eshun, Ndugu Hezron Mogambi walionisaidia kwa njia moja au nyingine. Shukrani zangu pia ziwafikie wahadhiri katika Idara ya Isimu ambao wamechangia pakubwa katika kukiendeleza Kiswahili nao ni pamoja na: Dkt. K. W. Wamitila, Dkt. John Habwe, Dkt. Rayya Timammy, Dkt. Zaja Omboga, Ndugu Ayub Mukhwana na Dkt. Mbuthia. Kwenu nyote, Mola awape hekima ya kuiendeleza elimu hadi katika viwango vyajuu zaidi.

Isitoshe, ninawashukuru wazamili wenzangu tuliohudhuna mihadhara pamoja na kushirikiana katika midahalo anuwai ya kiusomi nao ni pamoja na: Daniel Theuri, Lilian Nkonge, Wepoh Wesah, Veronicah Maina, Paul Mungai, Mary Oichoe, Rukiya Harith, Wycliffe Were, Assumpta Mulila, Kyallo Nguku, Mediatrix Rapando, Njiru Kimunyi, Fridah Kaviti, Vince Nyabunga na Eddah Karanja. Ninawashukuru pia wazamili wa kundi la isimu ambao tulihudhuria mihadhara pamoja na kushirikiana kwa njia moja au nyingine miongoni mwao wakiwemo Kenneth Ngure na Nobert Basweti. Ninawatakia nyote maisha yenye ufanisi na kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awape maisha marefu ili mpate kuyasherehekea matunda yajuhudi zenu pamoja na kuchangia katika ustawi wa nchi yetu pamoja na ulimwengu mzima kwajumla.

Utafiti wetu ulijikita hasa kwenye maktaba. Kwa hiyo, nilitumia muda wangu mrefu kwenye maktaba mbalimbali ambapo nilipata huduma murua kutoka kwa wakutubi wa maktaba hizi. Ni kwa mintarafu ya huduma nilizopata ndiposa natoa shukrani zangu za dhati kwa wakutubi wa maktaba ya Taasisi ya Uingereza ya Afrika Mashariki (B.I.E.A) na hususan mabwana Timothy Muleke na Innocent Mwangi. Mlinielekeza katika kuipata hazina iliyokuwa yenye manufaa katika mchakato mzima wa utafiti wangu. Aidha, ninawahongera wakutubi wa maktaba ya ukumbusho wa hayati Mzee Jomo Kenyatta (J.K.M.L) ya Chuo Kikuu cha Nairobi na hasa wale wa kitengo cha AfVicana ambao walinihudumia kwa moyo mkunjufu. Hawa ni pamoja na: Bw. John Kamau, Bi. Mercy

Waithaka, Bw Reuben Waweru, Bi. Inviolata Sikuku, Bw. Willy Mwatumia na Bi Eunice Ongoro Mwisho, ninamshukuru Bw. Boaz Adaji Saava, mkutubi wa maktaba ya Taasisi ya Masomo ya Kiafrika (I.A S) ya Chuo Kikuu cha Nairobi kwa msaada wake wa tangu nilipokuwa nikisomea shahada yangu ya kwanza Endeeleni na moyo huo huo wa kuwasaidia watafiti na maulama wa halafu.

Ninamshukuru ghaya mama yangu, Hannah Njeri, kwa ushauri wake wa miaka nenda miaka rudi ambao umempa mwelekeo mwafaka katika kuyatazama na kuyakabili maisha Ninaomba Mola amzidishie hekima na ampe miaka mingi ya kuishi duniani ili apate kuona ndoto yake ya siku nyingi ikitimia. Aidha, ninawahongera ghaya ndugu zangu Gerald na Amos; dada zangu Eunice na Lydia; na wapwa wangu Grace na Paul kwa mapenzi, uvumilivu na usaidizi wao wa kanbu na wa muda mrefu katika hen na katika shari. Sitasahau daima hatua mbalimbali ambazo tumepitia nanyi maishani. Ombi na tumaini langu ni kwamba, hali itakuja kubadilika.

Kuna marafiki wengi ambao walinitia moyo wakati nikiandika tasnifu hii na pia katika masomo ya hapo kabla na ambao pia ningetaka kuwahongera. Hawa ni pamoja na: Bw. Jacktone Nyonje, Bw. Samuel Ng'ang'a, Bi. Elizabeth Katola, Bw. Okumu Oloo, George, Jane, Nick, Lucy, Reuben, Cate, Ahmednassir, Jacque, J P. Maina, Milka... Sitasahau mijadala ya kiusomi tuliyoshiriki pamoja na mabwana Nyonje na Ng'ang'a, zikiwemo pia warsha nyingi za kiusomi tulizohudhuria pamoja na mikakati ainati tuliyoratibu ili kuinua hali ya Kiswahili ulimwenguni. Ndoto zetu zitakuja kutimia. Shime ndugu zangu.

Kazi hii imeandikwa ili kusomwa na maulama kadhaa duniani. Ninawapongeza wale wote watakaoisoma tasnifu hii kwa makini na kuifanyia uhakiki wa kina na wa haki. Pongezi pia ni kwa wale watakaoendeleza utafiti kuhusiana na mapendekezo ya utafiti wa ziada niliopendekeza kuhusu majagina. Waaidha, shukrani zangu ni kwa wote wanaokienzi Kiswahili na waliojitoa mhanga kuona kuwa kimepewa hadhi inayostahili duniani.

Mwisho, ninamshukuru Bi Rachael kwa kupiga chapa baadhi ya sehemu za tasnifu hii kwa haraka na kwa moyo mkunjufii. Mola akubanki.

YALIYOMO

Ikurasa

Ikirari.....	'
Tabaruku.....	"
Shukrani	
Yaliyomo.....	vii
Muhtasari	
Orodha ya vifupisho vilivyotumika.....	*"i

FASLU YA KWANZA: USULI WA TASNIFU

1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Somo la utafiti.....	3
1.2 Madhumuni ya utafiti.....	4
1.3 Nadharia tete.....	5
1.4 Sababu za kuchagua somo.....	5
1.5 Msingi wa kinadharia.....	6
1.6 Mipaka na upeo wa somo.....	12
1.7 Udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu somo	
1.8 Mbinu za utafiti.....	21
Tanbihi.....	22

FASLU YA PILI HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA SHAKA ZULU KWA KUFUNGAMANISHWA NA ILE YA JAMII ZAO

2.0 Utangulizi.....	23
2.1.0 Historia ya Waswahili.....	24
2.1.1 Misukosuko ya kivita iliyomzua Fumo Liyongo.....	31
2.1.2 Historia ya Fumo Liyongo.....	36
2.1.3 Thibitisho la kuwahi kuwepo kwa Fumo Liyongo.....	38
2.1.4 Tungo zinazohusishwa na Fumo Liyongo.....	40

2.1.5	Muhtasari wa hadithi ya Liyongo kwa mujibu wa <i>Utenzi wa Funut Liyongo</i>	43
2.2.0	Ihistoria ya Wazulu.....	47
2.2.1	<i>Mfecane</i> : kipindi cha vita kilichomzua Shaka Zulu.....	52
2.2.2	Ihistoria ya Shaka Zulu.....	53
2.2.3	Hitimisho.....	62
	Taubihi.....	63

FASLU YA TATU: SIFA ZA KISHUJAA ZA FUMO LIYONGO NA SHAKA

ZULU

3.0	Utangulizi.....	67
3.1	Ulinganishi: Sifa /a kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu.....	68
3.1.0	Kuzuka kwa mashujaa.....	68
3.1.1	Ubashiri wa kuzaliwa kwa jagina.....	69
3.1.2	Jagina kwa kawaida huwa ni mwanamume.....	70
3.1.3	Utoto na ujana wa jagina.....	72
3.1.4	Shujaa hutokana na ukoo bora / ukoo wa kifalme.....	73
3.1.5	Utetezi wa cheo.....	74
3.1.6	Maadui / wapinzani wa shujaa.....	75 [^]
3.1.7	Shujaa huwa kipenzi cha wanajamii.....	77
3.1.8	Jina la shujaa	
3.1.9	Kugura kwa shujaa kutoka nyumbani kwao / safari ya shujaa.....	83
3.2.0	Mashujaa huwa na akili pevu / uwezo wa kung'amua au kutabiri.....	84
3.2.1	Mashujaa kwa kawaida huwa ni washairi.....	87
3.2.2	Maisha ya mashujaa huwa ya dhiki tupu.....	89 [^]
3.2.3	Kimo na nguvu za shujaa.....	90 [^]
3.2.4	Maisha na matendo ya mashujaa huwa ya kimiujiza.....	92 [^]
3.2.5	Mapenzi ya mama kwa jagina.....	93
3.2.6	Mashujaa huwa hawaeleweki kwa uwazi.....	96
3.2.7	Majagina aghalabu huwa magwiji katika vita.....	97 [^]

3.2.8	Shujaa na suala la ndoa.....	102
3.2.9	kifuasi cha shujaa.....	105
3.3.0	Shujaa huhusishwa na zaidi ya jamii moja.....	107
3.3.1	.Janibo au kitu chochote kizuri katika jamii huhusishwa na shujaa.....	109
3.3.2	Usaliti na kifo cha jagina.....	—110 [^]
3.3.3	Mashujaa aghalabu huwa hawarithiwi na wanao.....	112
3.3.4	Shujaa huwa MiafV na hukumbukwa daima.....	113
3.3.5	Umuhimu wa shujaa kwa jamii yake.....	114
3.4	Hitimisho.....	114
	Tanbihi.....	115

FASLU YA NNE: UMUHIMU WA FUMO LIYONGO NA SHAKA ZULU KWA JAMII ZAO

4.0	Utangulizi.....	116
4.1.0	Umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu.....	116
4.1.1	Fahari ya watu weusi.....	116
4.1.2	Kitambulisho cha kitaifa.....	118
4.1.3	Kioo cha jamii / historia ya jamii.....	119
4.1.4	Ukuzaji wa utamaduni wa jamii zao.....	123
4.1.5	Ukombozina muungano wa jamii.....	125
4.1.6	Mabadiliko katika mfumo mzima wa jamii.....	127
4.1.7	Ruwaza bora ya kufuatwa na wanajamii.....	128
4.2	Hitimisho.....	128
	Tanbihi.....	130

FASLU YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0	Hitimisho
5.1	Mapendekezo

MAREJELEO.....	138
KIAMBATISHO 1: Utenzi wa Fumo Liyongo.....	143
KIAMBATISHO 2: Takhmisa ya Liyongo.....	156
KIAMBATISHO3: Qisacha Lamu.....	161
KIAMBATISHO 4: Rarnani Is Eneo La Shungwaya.....	163
KIAMBATISHO 5: Ramani 2: Pwani ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa ramani ya Idrisi ya mwaka 1154 B.K.....	164
KIAMBATISHO6: Ramani 3: Maguro yaliyosababishwa na <i>Mfecane</i>	165
KIAMBATISHO 7: Shaka Zulu.....	166

MUHTASARI

Tasnifu hii inajumlisha matokeo ya utafiti wetu uliolenga kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu pamoja na kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao. Tumeibawibu tasnifu hii katika faslu tano kila mojawapo ikishughulikia kipengele fulani maalum. Hata hivyo, vipengele vyote vilivyomo vinaingiliana na kukamilishana.

Faslu ya kwanza ni usuli wa tasnifu. Katika faslu hii, tumeelezea masuala muhimu na ya kijumla kuhusiana na mchakato mzima wa utafiti. Tumetanguliza kwa kuifasili dhana ya shujaa na kutoa mifano ya baadhi ya mashujaa duniani miongoni mwa masuala mengine ya kijumla kuwahusu majagina. Pia, tumelifafanua somo la utafiti na kisha tukaelezea madhumuni na nadharia tete za utafiti wetu. Ni katika faslu hii ambapo tumezielezea sababu za kulichagua somo pamoja na kufafanua nadharia ambazo zimetuongoza katika mchakato mzima wa utafiti wetu. Hatimaye, tumezielezea njia za utafiti ambazo tulizitumia kupata data ili kutekeleza madhumuni ya utafiti wetu.

Faslu ya pili inalenga katika kufafanua salua ya Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa kuifungamanisha na salua ya jamii zao; yaani, ile ya Waswahili na ya Wazulu. Katika kuelezea salua ya jamii hizi, tumelenga katika kuyafafanua mazingira ya kitamaduni (ya kijamii, kisiasa na kiuchumi). Majagina huwa hawazuki katika ombwe tupu na kwa hiyo lengo hasa la faslu hii ni kutoa taswira ya mazingira, hali za kijamii na kipindi ambacho Shaka Zulu na Fumo Liyongo walizuka pamoja na kuelezea masuala muhimu katika maisha yao.

Faslu ya tatu inatalii kiulinganishi sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Tumezifafanua kwa undani sifa zao za kishujaa huku tukionyesha kiwango cha kushabihiana na kutofautiana kwa sifa hizi.

Faslu ya nne inafafanua umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamu zao Tumeitazama 'taasisi ya shujaa' kama taasisi nyingine yoyote katika jamu ambayo huzuka ili kutekeleza mahitaji fulani katika jamii. Ni kutokana na kuyatimiza mahitaji haya ndiposa umuhimu wao umedhihirika.

Faslu ya tano inajumlisha hitimisho ya tasnifii na mapendekezo kuhusu utafiti wa ziada Tumetalii kwa kifupi masuala ya kijumla na hususa yanayohusu matokeo ya utafiti wetu na kisha tukapendekeza baadhi ya masuala ambayo watafiti wa halafu wanaweza wakatalii.

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

Bi.	Bibi
B.I.E.A -	British Institute in Eastern Africa
B.K	Baada ya Kristo
Bw.	Bwana
Co.	Company
Dkt.	Daktari
I.A.S	Institute of African Studies
J.K.M.L -	Jomo Kenyatta Memorial Library
khj	kama hapo juu
Ltd	Limited
Mh.	Mhariri
Mtar.	Mtarjumi
Na.	Nambari
Ph.D	Doctor of Philosophy
Prof.	Profesa
SOAS -	School Of Oriental and African Studies
SPLA -	Sudanese People's Liberation Army
SPLIM -	Sudanese People' Liberation Movement
taz.	tazama
TUKI -	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
uk.	ukurasa

FASLU YA KWANZA

USULI WA TASNIFU

1.0 Utangulizi

Jamii yoyote ile huwa ni mfiimo wenye taasisi nyingi ndani yake Taasisi hizi huamili kukidhi mahitaji kadhaa Kama zilivyo taasisi nyingine, 'taasisi ya ushujaa' huzuka ili kutimiza mahitaji fiilani kama tutakavyoona hapo baadaye. Jamii nyingi duniani hujitambulisha na mashujaa wao. Mashujaa au majagina wamekuwepo tangu kadimu. Waumini wa dini mbalimbali duniani humchukulia Mwenyezi Mungu kuwa shujaa wa mashujaa. Aidha, wanajamii huchukulia kwamba shujaa wao ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na hutolewa ili kutekeleza jukumu fulani, aghalabu la kuwakomboa kutoka kwenye dhiki au kuwaongoza kwenye ustawi wa maisha duniani na hata ahera.

Shujaa au jagina ni nani? *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:372), inamweleza shujaa kama, Mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari; jasiri, nguli, jogoo, jabali. abtali, ghazi, nyamaume.' Fasili hii inamwelezea tu jagina kwa mujibu wa uthabiti au kuwa jasiri. Si lazima shujaa awe jasiri. Anaweza kuwa mpole na mnyenyekevu na hasa tunaporejelea sajili ya kidini. Maelezo tuliyoayaona mwafaka katika kumwelezea jagina ni yale ya Mutiso (1999:1) na Gaster (1987:302). Mutiso anadai kuwa shujaa ni kiumbe wa kweli mwenye sifa za kiajabuajabu na ambaye amekuzwa na wanajamii pamoja na kwamba yeye mwenyewe amejikuza. Gaster naye anaeleza kuwa, jagina ni mtu ambaye humiliki uwezo zaidi kuliko ule wa watu wa kawaida na hutumia uwezo huu kiujasiri na huwa tayari kuyahatarisha maisha yake kwa manufaa ya watu wengine. Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya maulama hawa, shujaa huwa na tabia au sifa fulani za kipekee. Tabia au sifa hizi huwastaajabisha wanajamii ambao humwona kuwa kiumbe asiye wa kawaida. Aidha, jagina huzuka kwa manufaa ya watu wake (wanajamii) na huwa tayari kuyahatarisha maisha yake ili kuwakomboa. Si ajabu kwamba, wanajamii humwona shujaa wao kama mkombozi na baadhi yao wameishia kumwabudu.

Wanajamii huamini kwamba shujaa hata baada ya kifo chake huendelea kuishi na kutawala fikra, mienendo, matendo na hali zao zote za maisha Katika mazishi ya Papa John Paul II (1920-2/4/2005) - shujaa wa Wakatoliki - huko Vatican, tarehe 8/4/2005, mhashamu Joseph Ratzinger, kiongozi wa ibada aliwaambia mamia ya maelfu duniani:

**Tuna uhakika kuwa papa wetu mpendwa amesimama
leo kwenye dirisha la nyumba ya Baba (Mwenyezi Mungu)
na kwamba anatuona na kutubariki.**¹ (Tafsiri Yangu)

Majagina hukumbukwa daima na husifiwa kwa kutungiwa nyimbo na tenzi Isitoshe, tangu jadi, hadithi kuwahusu zimepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya ngano. Tangu kuasisiwa kwa maandishi, kuna kazi nyingi ambazo zimeandikwa na nyingine zinaendelea kuandikwa kuwahusu majabari wa jamii mbalimbali kote ulimwenguni.

Mashujaa sanasana huwa ni wa kiume ingawa tuna mashujaa wachache wa kike². Mifano ya majagina wa kihistoria duniani ni kama vile: Mtume Musa na Samshuni wa Waisraeli; Mtume Muhammadi wa Waislamu; Shaka Zulu wa Wazulu; Buddha wa Wahindi; Sundiata wa jamii mojawapo ya kale ya huko Mali; Fumo Liyongo wa Waswahili; Lwanda Magere wa Wajaluo; Sakawa wa Wakisii; Yesu Kristo wa Wakristo; Kimathi wa Wakikuyu; Lianja wa Wamongo walioko katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (utenzi kumhusu Lianja umesawiriwa kwa weledi na Maneniang 1999); na Kibwebanduka wa Wazaramo. Tumewajumlisha mashujaa wa kidini na wale wa kijamii katika kundi moja - mashujaa wa kihistoria. Sifa za mashujaa hawa kwa kiasi fulani zinafanana. Kwa mujibu wa dini mbalimbali duniani, zipo imani kwamba, majagina wa kidini hawastahili kulinganishwa kwa vyovyote vile na majagina au viumbe wengine wowote. Wao huchukuliwa kuwa wametoka kwa Mwenyezi Mungu kwa manufaa ya watu wote ulimwenguni na kwamba matendo yao huwa hayana dosari. Utafiti huu umewajumlisha pamoja mashujaa hawa kwa sababu za kiusomi - kujaribu kuzipambanua sifa za kishujaa ambazo zinashabihiana baina ya mashujaa wote duniani. Kwa kufanya hivi, hatuna nia ya kudhalilisha au kudunisha dini yoyote ile.

Vilevile, tuna mashujaa katika kazi bunilizi za kifasihi kama vile tamthilia, riwaya na ngano. Mfano mzuri wa shujaa katika riwaya ya Kiswahili ni Mvita, katika riwaya ya

S.A. Mohamed (1988) ya *Kiza Katika Num*. Mfano wa shujaa katika tamthilia ni MfaJme Edipode katika tamthilia maarufu ya Sofokile ya *Mfalme Edipode*. Katika ngano za jamii nyingi barani Afrika na hata katika jamii zingine ulimwenguni, sungura anasawiriwa kama nguli. Ingawa kimaumbile ni mnyama mdogo, anawapiku wanyama wengine wakubwa kama vile simba, ndovu na nyati kutokana na weledi wake wa kutumia akili. Shujaa au nguli wa kazi bunilizi sanasana huwa ndiye mhusika mkuu.

Maulama katika utafiti wao wamepata kuwa mashujaa wote duniani huwa na sifa zilizo karibu sawa - kuna sifa bia za mashujaa (Neno 'bia' katika tasifu hii limetumika kama kisawe cha umalimwengu). Vilevile, umuhimu wao katika jamii pia hushabihiana sana. Katika utafiti wetu, tumewalinganisha mashujaa wawili wa kihistoria ambao ni Shaka Zulu, shujaa wa Wazulu wa Afrika Kusini na Fumo Liyongo, shujaa wa Waswahili. Tumezipambanua kiulinganishi sifa zao za kishujaa pamoja na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zao.

1.1 Somo la utafiti

Suala la sifa za mashujaa ulimwenguni limeshughulikiwa na maulama anuwai (baadhi ya maulama hawa ni kama vile: Carlyle (1924), D. Kunene (1971), Butler (1979), Raglan (1965), Mutiso (1985 na 1999) na Gaster (1987)). Maulama hawa wamejaribu kuziorodhesha sifa kadhaa zinazodhihirika katika mashujaa wa jamii mbalimbali ulimwenguni kwa viwango tofauti tofauti. Wamepata kuwa kuna sifa bia zinazodhihirika katika mashujaa wote; mashujaa aghalabu huwa na sifa zilizo karibu sawa. Sifa zilizoonyeshwa na maulama hawa sizo sifa tu za kipekee za majagina. Kuna sifa nyingine nyingi ambazo zinaweza zikajitokeza na hususan iwapo ulinganishi zaidi wa mashujaa mbalimbali duniani ungefanywa. Waaidha, majagina hawa wana umuhimu mkubwa kwa jamii zao na ambao aghalabu hulandana.

Katika historia ya jamii za Kiafrika - kama ilivyo katika jamii zingine ulimwenguni - mashujaa pia walipatikana. Fumo Liyongo wa Waswahili na Shaka Zulu wa Wazulu ni mifano mizuri ya mashujaa wa kihistoria wa Kiafrika. Mashujaa hawa wawili ndio msingi au mhimili wa utafiti wetu.

Utafiti wetu, kwa upande mmoja, umelenga katika kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa ukiwemo pia ufafanuzi wa mazingira ya kijamii yaliyowazua Fumo Liyongo na Shaka Zulu Maswali ambayo tumejaribu kujibu ni: Ni mazingira yepi ya kijamii yaliyowazua mashujaa hawa? Ni sifa zipi za kishujaa zinazowafanya Shaka na Liyongo kuwa majagina? Ni kwa kiwango kipi ambapo sifa za mashujaa hawa zinafanana na kutofautiana?

Kadhalika, kwa upande mwingine, tumejikita katika kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa wawili kwa jamii zao. Katika kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa, tumeongozwa na maswali yafuatayo: Ni kwa vipi mashujaa hawa walichangia katika kuukuza utamaduni wa jamii zao? Ni kwa vipi waliweza kuimarisha uhusiano baina ya jamii zao na jamii zingine? Ni mabadiliko yepi ya kijamii ambayo Shaka na Liyongo walileta katika jamii zao? Ni hidaya zipi ambazo mashujaa hawa waliachia jamii zao? Je, zawadi hizi zina umuhimu gani kwa jamii hizi? Je, majagina hawa wanatusaidia vipi kuelewa bayana mfumo wa kiuchumi, kisiasa na mahusiano ya kijamii yaliyokuwepo katika jamii zao? Yaani, kwa kuwatalii Shaka na Liyongo, ni kwa vipi tunaweza kuelewa historia ya jamii zao katika kipindi walichopata kuishi? Katika kiwango cha kimataifa, majagina hawa wana umuhimu gani na hasa wanapotazamwa katika muktadha mpana wa jamii zingine ulimwenguni? Je, umuhimu wa mashujaa hawa unaelezwa kivipi na wanajamii wenzao? Majagina hawa wa kihistoria wana umuhimu gani kwa kizazi cha sasa?

1.2 Madhumuni ya utafiti

Utafiti wetu ulikuwa madhumuni yafuatayo:

1. Kuelezea historia ya Shaka Zulu na Fumo Liyongo kwa kuifiingamanisha na ile ya jamii zao ili kuonyesha mazingira na hali za kijamii zilizowazua.
2. Kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu.
3. Kuchunguza kiwango cha kufanana na kutofautiana katika sifa za mashujaa hawa wawili.
4. Kuelezea umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamii zao.
5. Kutilia nguvu au kubatilisha madai ya maulama mbalimbali kwamba, majagina wote ulimwenguni wana sifa zilizo karibu sawa.

1.3 Nadharia tete

Nadharia tete za somo letu ni kama zifuatazo:

1. Shaka Zulu na Fumo Liyongo ni mifano mizuri ya mashujaa wa kihistoria wa kijamii katika jamii za Kiafrika.
2. Sifa za mashujaa hawa wawili kwa kiasi kikubwa zinafanana
3. Mashujaa hawa wawili wana umuhimu mkubwa kwa jamii zao, ambao kwa kiasi kikubwa unashabihiana

1.4 Sababu za kuchagua somo hili

Sababu zifuatazo zilitupelekea katika kulichagua somo hili:

Kwanza, tuna imani kwamba ili mtu aweze kulichunguza suala filani na hususan suala la kiusomi, ni lazima mwanzo, awe amevutiwa nalo na pili ni sharti awe na uwezo wa kuweza kulichunguza. Kwa muda sasa, tumevutiwa na suala nzima la usawiri wa mashujaa - sifa zao za kiajabuajabu, uwezo wao, namna wanavyosifiwa na wanajamii, mshabaha uliopo katika sifa zao na umuhimu wao katika jamii wanamopatikana. Isitoshe, nimevutiwa na namna wanajamii kote duniani wanawapa mashujaa nafasi kubwa hata kuliko jamaa wao wa karibu. Kwa mfano, inaniwia vigumu - na hata kwa mtu mwingine yeyote - kumkumbuka au hata kumfanyia utafiti nyanya ya nyanya yangu ilhali ninaona rahisi kumfanyia utafiti shujaa aliyeishi miaka takriban mia sita au hata hapo kabla. Katika kufanya utafiti huu, tulikuwa na imani kwamba tuna ule uwezo wa kuzichunguza sifa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu pamoja na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zao.

Pili, hakuna utafiti wa kina tuujao unaowalinganisha Shaka na Liyongo kama mashujaa wa kihistoria wa Kiafrika. Hivyo basi, utafiti huu ni muhimu kwani umesaidia katika kuliziba pengo lililokuwepo; utafiti huu ni wa kwanza kuwasawiri kiulinganishi na kwa kina mashujaa hawa wawili. Umezipambanua sifa zao za kishujaa na kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao.

Vilevile, kabla ya kuanza utafiti, tuliadini kuwa utafiti wetu ungekuwa kielelezo kizuri kwa maulama wengine ambao hapo baadaye watakuwa na azma ya kuwalinganisha majagina wa jamii mbalimbali duniani; awe ni Fumo Liyongo na shujaa mwingine /

wengine kutoka katika jamii nyingine licha ya Shaka au wawe ni mashujaa wengine kutoka jamii nyingine mbali na jamii ya Waswahili au Wazulu

Suala la kuwahi kuwepo kwa Fumo Liyongo limetiliwa shaka na baadhi ya wasomi. Kwa mfano, Kitsao (1982:65) anaiona hadithi ya Liyongo kama iliyo na usuli wake katika kisakale kilicho kwenye *Bihlia* kumhusu Samshuni (Samsoni). Utafiti wetu kwa hiyo umekuwa wenye mchango mkubwa katika kujaribu kutatua suala la kuwepo au kutokuwepo kwa Fumo Liyongo kama shujaa wa Waswahili. Kwa kuchukua mtazamo wa kiulinganishi na kwa kuzingatia sifa bia za mashujaa, tumejaribu kuonyesha kuwa ni bayana kwamba Liyongo aliwahi kuishi.

Mwisho, kwa kuzipambanua sifa za kishujaa za Liyongo na Shaka na kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao, tuliamani kuwa matokeo ya utafiti huu yangetilia nguvu au kubatilisha madai ya maulama mbalimbali duniani kwamba, sifa za majagina duniani kwa kiasi kikubwa zinafanana.

1.5 Msingi wa kinadharia

Katika mchakato mzima wa utafiti huu, tumeongozwa na nadharia mbili. Nadharia ya kwanza ni nadharia ya uhakiki wa vikale (*Theory of Archetypal Criticism*) ilhali nadharia ya pili ni nadharia ya uamilifu (*Functionalism*). Nadharia ya uhakiki wa vikale imetuongoza katika kupambanua kiulinganishi sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Nadharia ya uamilifu nayo imetuongoza katika kuelezea umuhimu wa Shaka Zulu na Fumo Liyongo katika mfumo mzima wa jamii zao.

Nadharia ya vikale huhusishwa sanasana na uhakiki wa visasili. Kwa mujibu wa Meyer (1993:2010), wahakiki wa visasili hujishughulisha na ruwaza ambazo hujirudiarudia na ambazo hudhihirisha maana bia na tajiriba za kimsingi za binadamu licha ya wakati au mahali wanamoishi. Kwa jumla, sifa, taswira na mada zinazojumlisha maana na tajiriba hizi ndizo hujulikana kama vikale. Vikale hushirikisha ishara bia ambazo huibua hisia na athari nzito kwenye akili laza ya msomaji wa fasihi Binadamu tangu zama ni yule

yule. Kwa hiyo, vikale huradidi matumaini na woga wa binadamu tangu kuwepo kwake duniani.

Abrams (1981:11-12), anadai kuwa chimbuko la nadharia hii hutoa maelezo yake kuwili. Kwa upande mmoja, chimbuko la nadharia hii ni kwenye idara ya anthropolojia linganishi katika Chuo Kikuu cha Cambridge kutokana na kazi ya James G. Frazer ya *The Golden Bough* (1890-1915). Kazi hii huchunguza ruwaza ya sifa za visasili na matambiko ambayo inadai kuwa hujitokezatokeza katika visakale na taratibu nyingi za tamaduni za watu mbalimbali duniani.

Kwa upande ule mwingine, nadharia ya vikale hutokana na maelezo ya Carl G. Jung kuhusiana na akili laza. Ikumbukwe kuwa Jung alikuwa mwanafiinzi wa Sigmund Freud, mtaalamu aliyeeasisi taaluma ya uchanganuzi nafsia (*psychoanalysis*). Jung alitumia neno vikale kwenye taswira za asili za akili zinazorudiwarudiwa kutokana na tajiriba katika maisha ya tangu mababu wa kale kabisa. Alishikilia kuwa taswira hizi hurithiwa na kutiwa kwenye akili razini za jamii ya wanadamu na hudhihirika katika visasili, ndoto, dini, mawazo ya binadamu; mathalan katika vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote duniani.

Katika uhakiki wa kifasihi, Abrams (khj) anadokeza kuwa, vikale hutumiwa kurejelea miundo ya kisimulizi, aina za wahusika au taswira ambazo zinafanana katika tungo mbalimbali za fasihi na pia katika visasili na mitindo anuwai ya kijamii. Kufanana katika masuala haya anuwai huchukuliwa kuakisi seti ya ruwaza bia ambazo zimekuwepo tangu jadi. Inaaminika kwamba vikale huibua hisi au mvuto kwa upande wa msomaji.

Kwa mujibu wa nadharia ya fasihi, fasihi huwa na sifa bia. Ubia huu uliopo katika sifa za fasihi ndio huipa fasihi uwezo wa kulinganishika. Wamitila (2002:xi) anadai kuwa, fasihi mbalimbali duniani huingiliana kwa kuwa msingi wa fasihi hizo ni binadamu mwenyewe. Kwake yeye, maadamu jamii mbalimbali zimeundwa na wanadamu, mwingiliano wa aina mbalimbali hauwezi ukaepukika. Mwingiliano katika masuala anuwai katika maisha ya binadamu ndio huiwezesha fasihi kulinganishika. Licha ya

maelezo haya, ulinganishi huu hutokana na sababu kwamba, Kwanza, fasihi zote ulimwenguni hutumia lugha kama mali ghafi Lugha zote duniani huwa na sifa zinazoshabihiana. Pili, fasihi huchota maudhui yake kutoka katika jamii za wanadamu. Wanadamu wote duniani huwa na sifa zinazofanana Tatu, fasihi hulenga katika kutekeieza dhima fulani katika jamii Kwa mfano, kuburudisha, kuelimisha, kuzindua na kuonya. Hatimaye, fasihi hujengwa kutokana na fani na maudhui. Ingawa kila fasihi ni zao la jamii mahsusi, kuna vipengele vingi vya kimaisha na katika jamii mbalimbali duniani ambavyo hushabihiana na hivyo kuwezesha fasihi zote duniani kutazamwa kiulinganishi.

Kwa jumla, vikale hurejelea ruwaza za kimsingi, jumla au bia za aina moja au nyingine. Ruwaza hizi aghalabu hudhihirika katika jamii za watu mbalimbali duniani

Katika utafiti wetu, tutaongozwa na mtazamo wa anthropologia linganishi Hii ni kwa sababu, somo letu ni la kianthropolojia zaidi kuliko kisaikolojia kama ilivyo katika mtazamo wa Jung. Hata hivyo, mtazamo wa kisaikolojia vilevile unaweza ukatumika kuhlalisha kulandana kwa sifa bia na kushabihiana kwa umuhimu wa mashujaa wote duniani. Swali tunalofaa kujiuliza ili kuelewa madai ya mtazamo wa anthropolojia linganishi ni: 'Kwa nini ruwaza za visasili na matambiko hujitokezatokeza katika visakale na taratibu nyingi za watu mbalimbali duniani?' Katika kulijibu swali hili, itatubidi tuchukue mwelekeo wa kijumla kuhusiana na uelewa wa hulka za binadamu wote duniani.

Ni bayana kwamba watu wote duniani ni sawa. Jamii zote duniani huwa na vipengele vya kimaisha vinavyoshabihiana. Kwa mfano, hakuna jamii ya watu duniani isiyokuwa na: dini, mavazi, lugha, katiba (iwe imeandikwa au haikuandikwa), mapenzi, kilimo/ufugaji, fasihi, elimu, mauguzi, ukahaba, uchochezi, muziki, malezi, ndoa, talaka, utu, wizi, ufisadi, ulanguzi, namna ya kufanya mazishi, sheria, utabaka, mayatima, wajane, mapishi; na masuala mengine yote tuyafikiriayo kumhusu binadamu.

Vipengele hivi huwa na uamilifu ulio sawa katika jamii zote. Kwa mfano, uamilifu wa mavazi (ya aina yoyote yale) ni kusetiri uchi wa binadamu ilhali sheria ipo kuhakikisha kuwa haki inatendeka katika jamii yoyote ile. Hata hivyo, ingawa uamilifu wa vipengele hivi ni sawa, tofauti hutokea katika utekelezaji au njia za utendaji. Kila jamii huwa na njia mahsusi za kutekeleza masuala au matamania fulani kutegemea kiwango cha teknolojia na pia mazingira ya jamii husika.

Kushabihiana katika ruwaza ya sifa za visasili na matambiko katika tamaduni za jamii mbalimbali duniani kumethibitishwa na maulama anuwai wanaoziangalia kiulinganishi visasili, visakale na matambiko ya jamii tofauti tofauti. Werner (1968:18) katika kuvichunguza visasili na visakale vya Wabantu, anathibitisha ukuruba uliopo katika mila na desturi zao anaposema:

Licha ya kuwepo kwa uhusiano katika lugha, Wabantu wote wana mila na desturi nyingi zinazofanana. Wote ingawa kwa mashaka wana takriban dhana ya kuwepo kwa Mungu mmoja, licha ya kwamba wengine hawamtofaotishi bayana na mawingu au jua, au kama tutakavyoona na mhenga wa awali kabisa wa kabila lao. Wanaamini katika maisha ya baada ya kifo na huwa na mawazo kwamba roho za waliokufa zinaweza zikaathiri hali zao za maisha kwa kiwango chochote kile... (Tafsiri Yangu).

Eliade (1957:15-17) akizungumzia kuhusu visasili anadai kuwa visasili hufichua muundo wa kweli na uanuwai wa hali za wanadamu duniani. Hii ndiyo sababu visasili huwa vielelezo mwafaka kwa tabia za wanadamu. Anaendelea kudai kuwa visasili huelezea hadithi za ukweli kwa vile hujihusisha na maswala ya ukweli. Kwa hiyo, kutokana na fasiri ya visasili, tunapata kuwa visasili haviwezi kuwa mahsusi, vya kibinafsi au vya kipekee. Visasili hutilia mkazo ubia kwa vile huchukuliwa kama kielelezo bora kwa wanadamu wote duniani. Kuhusiana na mashujaa - wawe wa kweli au wa kufikirika tu - anadai kuwa (uk. 32), mashujaa wana jukumu muhimu katika uumbaji wa vijana wa huko Ulaya na hasa kutokana na uigaji wa sifa na tabia za wahusika kwenye ngano zilizo na vitushi vyenye hatari, zilizo na majabari wa kivita miongoni mwa masuala mengine sawia na hayo.

Genep (1960), anaeleza kuhusu matambiko mbalimbali ambayo hukumba wanadamu wote duniani. Matambiko haya ni kama vile: ujauzito na kuzaliwa kwa watoto, kipindi

cha utoto, kushiriki kwa wanadamu katika hafla mbalimbali katika jamii, tohara au jando, kuoja na kuolewa, na hata kifo. Anadai kuwa ingawa matambiko haya hutekelezwa kwa njia tofauti tofauti na jamii mbalimbali, uamilifu wao huwa sawa toka jadi za mababu zetu.

Kwa mintarafli ya maelezo haya, jamii zote duniani huwa na mashujaa ambao aghalabu hupewa sifa zilizo karibu sawa. Shujaa kwa kawaida huwa ni kiumbe wa kawaida. Walakini, kutokana na mawazo yaliyo katika akili laza za wanadamu kutoka jadi, shujaa huchukuliwa kama kiumbe asiyekuwa wa kawaida. Yeye huchukuliwa kuwa kiumbe aliye na sifa za kiajabuajabu na za kipekee tofauti na wanajamii wengine wote. Kwa hiyo, sifa wapewazo mashujaa katika jamii mbalimbali duniani hushabihiana sana.

Nadharia ya vikale kutokana na ubia wake imekuwa yenye umuhimu katika utafiti huu kwa vile imetuongoza katika kulinganisha sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu.

Nadharia ya uamilifu huhusu ufafanuzi wa taasisi mbalimbali ambazo huunda jamii; huelezea uamilifu wa taasisi na kuonyesha mchango au umuhimu wa kila taasisi katika kuelezea na kudumisha hali anuwai zilizoko katika mfumo mzima wa jamii. Kwa mujibu wa McGee na Warms (2000:158), nadharia ya uamilifu kwa jumla hugawanywa katika mitazamo miwili kila mojawapo ikiwa inahusishwa na maulama mahsus. Mitazamo hii ni pamoja na uamilifu wa kisaikolojia (*Psychological Functionalism*) na uamilifu wa kimuundo (*Structural Functionalism*).

Uamilifu wa kisaikolojia unahusishwa na Bronislaw Malinowski (1884-1942). Kwa mujibu wa mtazamo huu, taasisi za kitamaduni huamili kutimiza mahitaji ya kimsingi ya kisaikolojia na kimwili ya watu katika jamii. Kwa upande ule mwingine, mtazamo wa uamilifu wa kimuundo unahusishwa na A.R. Radcliffe-Brown (1881-1955). Wafiasiri wa mtazamo huu ambao walichota pakubwa kutoka kwa kazi za Emile Durkheim waliniuia kuelewa jinsi taasisi za kitamaduni zilidumisha utangamano na kusawanyisha hali mbalimbali katika jamii. Kazi za Durkheim zinalenga katika kuiangalia miundo ya ndani katika mfumo mzima wa jamii. Radcliffe Brown na

wanafunzi wake waliniua kuelewa sheria bia za kijamii ambazo zingechipuka kutokana na mtalaa kiulinganishi wa tamaduni mbalimbali duniani

Katika kuelezea umuhimu wa mashujaa, tumeongozwa na mtazamo wa uamilifu wa kisaikolojia unaohusishwa na Bronislaw Malinowski. Kwa mujibu wa maulama huyu, kila jamii duniani huwa na mahitaji yake. Ili kuyatimiza mahitaji haya, kuna haja ya kuwepo kwa taasisi za kitamaduni. Malinowski aliamini kuwa taasisi za kitamaduni huibuka ili kuyatimiza mahitaji yaliyopo au yanayoibuka katika jamii.

Jamii ni mfiimo ambao uko wazi na ulio changamano ajabu. Kama mfumo mwingine wowote ulio wazi, jamii hukumbwa na matatizo na mahitaji fulani (ya kimwili na kisaikolojia) ya ndani kwa ndani na mengine kutoka nje. Ili kusuluhisha matatizo au kushughulikia mahitaji haya, taasisi mbalimbali za kitamaduni huibuka katika jamii. Kila mojawapo wa taasisi hizi huibuka ili kutimiza mahitaji fulani mahsusi. Waaidha, taasisi hizi huwa haziko pweke bali hushirikiana na taasisi nyingine ili kutimiza mahitaji ya jamii na hivyo kulenga katika kuifanya jamii kuwa 'kamilifu'. Taasisi hizi huibuka kadiri jamii inavyozidi kuendelea (kutoka katika hali ya ushenzi hadi katika ngazi za ustaarabu mkubwa). Maendeleo katika jamii huashiria kuwepo kwa mahitaji anuwai ambayo bila shaka huhitaji kushughulikiwa kwa dharura ili kuepusha dosari za aina zozote zile ambazo zinaweza zikauporomosha mfumo mzima wa jamii.

Malinowski alidokeza kuwa taasisi za kitamaduni huzuka ili kutimiza mahitaji saba ya kimsingi ya binadamu ambayo ni: lishe (*nutrition*), uzazi (*reproduction*), faraja za kimwili (*bodily comforts*), burudani (*relaxation*), mwondoko (*movement*), usalama (*safety*) na ukuaji (*growth*). Katika kutoa msururu wa mahitaji haya, alikuwa na nia ya kuonyesha namna ambavyo mila na desturi mbalimbali zilichangia katika kuona kuwa jamii inaendelea kama inavyohitajika, huku ikitimiza mahitaji ya kimwili na kisaikolojia ya watu katika jamii.

Baadhi ya taasisi (mifiimo) za kitamaduni ambazo huamili kutimiza mahitaji ya mfumo mzima wa jamii ni pamoja na: uchumi, afya, utawala, sheria, elimu, kilimo, kawi, ulinzi, mahusiano ya ndani na nje, uchukuzi, utalii, dini, miongoni mwa taasisi

nyingine Katika msururu huu huu, tunayo 'taasisi ya ushujaa' ambayo huzuliwa na mahitaji fulani ya kijamii Kama tutakavyoona hapo baadaye, jagina huwa hazuki tu vivi hivi Yeye huzuka katika mazingira, hali na kipindi fulani mahsusi katika jamii yake - jagina huzuka ili kutatua mgogoro fulani ambao huwa umeitatanisha jamii yake.

Jagina huzuliwa na mahitaji ya jamii katika kipindi mahsusi katika historia ya jamii yake. Shida ambazo jamii hupitia huwa haziondoki hadi pale ambapo jagina ataibuka na kuziondoa Si ajabu kwamba, jamii inaweza ikakaa katika ugumu fulani kwa muda mrefu hadi pale ambapo shujaa atakapozuka. Jambo muhimu katika mtazamo wa nadharia ya uamilifu wa kisaikolojia ni kule kutimizwa kwa mahitaji ya kisaikolojia na kimwili ya wanajamii. 'taasisi ya ushujaa' kama ambavyo tumekwisha kuona, huibuliwa na mahitaji ya kijamii na hushirikiana na taasisi nyingine katika mfumo mzima wa jamii ili kuyatimiza mahitaji haya. Ni katika kutekeleza mahitaji haya ambapo umuhimu wa shujaa katika jamii hujitokeza.

Kwa jumla, mtazamo wa nadharia ya uamilifu wa kisaikolojia umetuongoza katika kuelezea umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamii zao.

1.6 Mipaka na upeo wa somo

Kuna mambo mengi yanayoweza kutafitiwa kuhusiana na suala nzima la mashujaa. Kwa sababu ya wakati, ilituhalisi kujifiinga katika kupigia darubini masuala maalum. Kama ambavyo tumekwisha kueleza, utafiti wetu umepambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Tumechunguza kiwango cha kufanana na kutofautiana kwa sifa zao na umuhimu wao kwa jamii zao. Tumetaja, ingawa kwa kupitia tu, baadhi ya sifa za majagina wengine duniani ili kuweza kutoa taswira pana kuhusu sifa na umuhimu wa mashujaa kwa mujibu wa somo letu.

Kuna kazi nyingi ambazo zimeandikwa kuhusu Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Kazi za kimsingi ambazo tumerejelea na ambazo tuliamini zingetufaa katika utafiti wetu ni pamoja na: *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulio katika Mulokozi (1999); Mieke na wenzake (2004) ambayo ni kazi iliyoyakusanya mashairi na nyimbo ambazo zinadaiwa kuwa zilitungwa na Fumo Liyongo; *Takhmisaya Liyongo*; *Emperor Shaka the Great: A Zulu*

Epic ambao ni utenzi uliotarjumiwa na Masizi Kunene na kuchapishwa mnamo mwaka wa 1979; Omer-Cooper (1966) ambayo ni kazi inayoelezea kwa kina misukosuko ya kivita iliyomzua Shaka Zulu ikiwemo historia kumhusu na pia kuhusu jamii yake, miongoni mwa kazi nyingine muhimu za kihistoria

Katika utafiti wetu, hatujaingilia katika mjadala wa, "Mswahili ni nani?" Tumemchukulia Mswahili kuwa mwenye asili ya Kibantu na kitovu chake ni kwenye sehemu za kati mwa bara la Afrika kama walivyo Wabantu wengine. Hata hivyo, tumetilia maanani athari za kigeni na hususan athari za Waarabu katika janibu za pwani ya Afrika Mashariki

Mashujaa huwa hawazuki katika ombwe tupu bali huzuka katika mazingira, kipindi na hali fulani za kijamii. Shujaa huzuka ili kutekeleza jukumu fulani katika kipindi maalum na hii ndiyo sababu wanajamii humtazama shujaa wao kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, imetuhalisi kuyachunguza angalao kwa kifipi mazingira ya kihistoria ambamo mashujaa hawa wanapatikana. Tumejaribu kufafanua usuli wa jumuiya wanamopatikana Shaka Zulu na Fumo Liyongo ili kuweza kuwaelewa mashujaa hawa kwa kina. Ni katika kuelewa muundo na hali halisi ya kijamii (mivutano au migogoro iliyopo, hali ya uchumi, siasa, mila na desturi za wanajamii, mahusiano na jamii au watu wa nje, sanaa yao; mathalan, upana wa utamaduni wa jamii) ndiposa tunaweza kuvielewa na kuvifasiri vitushi vyote vinavyomzunguka shujaa.

Ni kutokana tu na uelewa wa hali halisi ya kijamii ambapo tunaweza kupata majibu ya maswali yafiiatayo: Ni kwa nini shujaa akazuka katika kipindi fulani katika historia ya jamii fulani? Ni nini kilichosababisha shujaa kufanya namna alivyofanya? Matatizo yanayomkumba shujaa yanatoka wapi? Umuhimu wa shujaa katika jamii yake unadhihirika kwa nini? Ni sifa zipi za kishujaa ambazo shujaa anazo na ambazo ni tofauti na wanajamii wengine? Mchango wa shujaa katika jamii yake ni upi?

1.7 Udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu somo

Kuna kazi nyingi zilizoandikwa kuhusu mashujaa duniani. Baadhi ya kazi hizi ni za kinadharia na zinapambanua masuala anuwai kuhusiana na mashujaa kwa jumla. Kazi zingine ni mahsusi na zinalenga katika kuwasawiri mashujaa wa jamii fulani, kwa mfano, zile zinazohusiana na Fumo Liyongo au Shaka Zulu. Kadhalika, maandishi mengine yanaelezea historia ya jamii ambapo mashujaa hawa walipatikana. Kazi hizi zote ni muhimu katika kuzipambanua sifa za mashujaa wa somo letu na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zao.

Katika kurasa zinazofiiata, tumezionesha kazi ambazo ni muhimu katika utafiti wa somo letu.

Steere (1870) ni kazi muhimu katika utafiti wetu. Edward Steere alizikusanya katika maandishi ngano za Waswahili kama zilivyosimuliwa kwake na wakaaji asilia wa Unguja. Ngano hizi zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. *Hadithi ya Liyongo* (uk.440-453), *Mashairi ya Liyongo* (uk.456-471) na *Utumbuizo wa Gungu* (uk.474-483) zimekuwa muhimu kwani zimetusaidia katika upambanuzi wa sifa za kishujaa za Liyongo pamoja na kuelezea umuhimu wake kwa jamii ya Waswahili.

Riwaya ya kihistoria ya Mofolo (1931) *Chaka* na ambayo ilitajumiwa kwa lugha ya Kiingereza na P. Kunene (1981) pia ni muhimu katika somo letu. Riwaya hii ni miongoni mwa kazi nyingi za kifasihi za awali kabisa ambazo zimeandikwa kuhusu Shaka kama mfalme na shujaa wa Wazulu. Kazi hii ni muhimu katika utafiti wetu kwa vile imetusaidia kumwelewa Shaka kwa undani na pia kupambanua umuhimu wake kwa jamii yake.

Bryant (1949) ni kazi ambayo inatoa ufafanuzi wa kina kuhusu mfumo wa kijamii na kihistoria wa Wazulu kabla ya majilio ya mabeberu. Kazi hii inaelezea masuala kuhusu uhamaji, mila na desturi, visasili, sanaa, vyakula, kilimo na mahusiano ya kijamii ya Wazulu. Kazi hii imekuwa yenye umuhimu katika utafiti wetu kwa vile imetupa mwanga kuhusiana na mazingira ya kijamii alimozuka Shaka.

Harries (1962) anatoa maelezo ainati kuhusiana na ushairi wa Kiswahili Maelezo muhimu ambayo yametusaidia katika utafiti wetu ni yaJe yanayomhusu Liyongo. Anatoa maelezo kuhusiana na migogoro kati ya Liyongo na binamuye, Daudi Mringwari; nasaba yake; na pia ufafanuzi kuhusiana na *Utenzi wa Liyongo*. Kwa jumla, kazi hii imekuwa yenye umuhimu mkubwa kwetu kwa vile imetuangazia maelezo ya ziada (yaliyo nje ya *Utenzi wa Fumo Liyongo*) kumhusu Liyongo.

Omer-Cooper (1966) ni kazi ya kihistoria ambayo imekuwa yenye manufaa makubwa katika utafiti wetu. Kazi hii inalenga katika kuchanganua masuala mbalimbali kuhusiana na hali ilivyokuwa katika jamii ya Wabantu wa kusini mwa Afrika kabla ya *mfecane* {*mfecane* ni neno ambalo hutumiwa kurejelea kipindi kirefu cha vita kilichokuwepo katika maeneo ya kusini mwa Afrika mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Tumeelezea zaidi kuhusiana na mchakato mzima wa kipindi hiki katika faslu ya pili) na hali ilivyokuwa wakati wa *mfecane*, ikiwemo kuibuka kwa mfalme Shaka miongoni mwa masuala mengine mengi na muhimu. Kwa jumla, kazi hii inahusisha msururu mrefii wa vita, magurio, pamoja na michakato ya halafu katika mabadiliko ya kisiasa na kijamii. Mwandishi amejaribu kuonyesha umuhimu wa *mfecane* katika historia ya maeneo ya kusini na kati mwa Afrika na hususan jinsi ilivyoathiri maendeleo ya baadaye, ukiwemo pia mchango wa *mfecane* katika kuelewa hali zilivyo katika wakati wa sasa. Kazi hii imekuwa muhimu katika utafiti wetu kwa vile imetusaidia katika kuelewa historia ya Wazulu kabla ya *mfecane*, maelezo kuhusu misukosuko ya kivita iliyomzua Shaka Zulu, yakiwemo pia maelezo kuhusu historia ya Shaka Zulu. Masuala haya yote yamekuwa muhimu katika kuzipambanua sifa za kishujaa za Shaka na kuonyesha umuhimu wake kwa jamii ya Wazulu.

Werner (1968) ni kazi inayotoa mkusanyiko wa maelezo kuhusu visasili na visakale vya baadhi ya Wabantu wakiwemo Wazulu na Waswahili. Mwandishi anadai kuwa (uk.18), licha ya uhusiano katika lugha, Wabantu wote wana mila na desturi nyingi zinazofanana. Kufanana huku ndiko kunakotuwezesha kuwatazama majagina wa somo letu kiulinganishi. Aidha, ameirejelea *Hadithi ya Liyongo* (uk 145-154) na kutoa maelezo mwafaka na ya manufaa katika utafiti wetu. Maelezo yake kuhusu aila ya Liyongo na mgogoro uliokuwepo ni muhimu katika kuiunda historia ya shujaa huyu.

Isitoshe, ameelezea kuwahusu mashujaa wengine wa Kibantu na kutoa picha za baadhi ya watu, shughuli zao na fenomena mbalimbali katika jamii ya Wabantu. Masuala yote haya ni muhimu katika kuelewa utamaduni wa jamii wanamotoka mashujaa wetu pamoja na kuwaelewa kwa kina mashujaa hawa.

Were (1974) anatuangazia vitushi muhimu katika historia ya Afrika Kusini. Mojawapo wa suala muhimu ambalo analizungumzia ni kuinuka kwa ufalme wa Zulu (*The Rise of the Zulu Kingdom*). Licha ya kumsawiri Shaka kama mfalme na shujaa wa Wazulu, tunaonyeshwa hali halisi ya jamii ya Wazulu, kabla ya kuzuka kwa shujaa huyu. Juu ya hayo, tunaelezwa hali ilivyokuwa hata baada ya kifo cha Shaka. Kutokana na upana wa maelezo yake, tumekuwa na nafasi nzuri ya kuweza kuyaelewa kwa undani mazingira ya kijamii na pia hali zilizomzua Shaka.

Kuhusiana na maelezo kuhusu kipindi alichopata kuishi Liyongo, historia ya Waswahili pamoja na maelezo mengine muhimu kumhusu Liyongo na tungo zake, Knappert (1979) ni kazi ambayo imekuwa yenye manufaa katika utafiti wa somo letu. Kazi nyingine ya mwandishi yuyu huyu na ambayo imekuwa muhimu kwetu ni ile ya mkusanyiko wa visasili na visakale vya Waswahili (*Myths and legends of the Swahili* (1970)). Kazi hii imetusaidia kuelewa masuala kadhaa kuhusiana na jamii ya Waswahili kwa jumla. Kazi za kifasihi na hususan fasihi simulizi za hapo awali, huchota kwa upana maudhui yake kutokana na hali na migogoro ya kijamii iliyopo. Mtalaa wa kazi hizi hutupa taswira angavu ya jamii zinamopatikana.

M. Kunene (1979) ameutunga kwa ustadi utenzi kwa jina, *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic*. Hapo awali, Kunene alikuwa ameuandika utenzi huu kwa lugha ya Kizulu na kisha akautafsiri kwa lugha ya Kiingereza. Utenzi huu unayasawiri kwa upana maisha ya Shaka Zulu. Unaonyesha: utabiri wa kuzaliwa kwake, kuzaliwa kwake, maisha ya ujana, aila yake, migogoro ya kimaisha aliyokutana nayo, namna alivyoinuka na kuwa mfalme wa Wazulu, ushujaa wake vitani na mbinu zake za kupigana vita na hata mauko yake. Kwa jumla, utenzi huu unaonyesha takribani kila chembe katika maisha ya Shaka. Utenzi huu kama tulivyokwisha kutaja umekuwa muhimu sana katika utafiti wetu kwani ndio umekuwa msingi wa uchanganuzi wetu kumhusu Shaka.

Katika kuelezea historia ya Pate alikotembelea Fumo Liyongo, imetubidi turejeele *Utenzi wa Al-Inkishafi*. Maelezo ya Mulokozi (khj) na tafsili ya Nasiri (1980) kuhusu utenzi huu yamekuwa yenye manufaa kwetu Utenzi huu unasawiri maanguko ya mji wa Pate chini ya utawala wa Wareno. Licha ya kusawiriwa maanguko, tunasawiriwa hali ilivyokuwa katika kipindi cha ustawi wa mji huu. Hali hii ya ustawi imetusaida kuelewa mfumo wa kijamii wa mji huu wakati alipoishi Liyongo. Tulikisia kwamba utenzi huu una chembechembe za hali ilivyokuwa wakati alipoishi jagina huyu.

Nurse na Spear (1985) ni kazi nyingine muhimu katika utafiti wa somo letu. Kazi hii inapigia darubini historia ya Waswahili pamoja na lugha ya Kiswahili baina ya karne ya saba na karne ya kumi na nne (800-1500 B.K). Waandishi wa kazi hii wanajaribu kuiunda historia ya Waswahili na lugha ya Kiswahili kama ilivyokuwa katika kipindi hiki. Wanaelezea masuala kadhaa muhimu kama vile: utamaduni asilia wa Waswahili; asili ya lahaja mbalimbali za Kiswahili; kuibuka kwa miji mbalimbali kama vile Mogadishu, Kilwa, Pate, Malindi, Lamu na Mombasa kutokana na kupanuka kwa jamii ya Waswahili; miundo ya kijamii na kiutawala katika miji mbalimbali; hali ya kiuchumi katika jamii hii; na maingiliano baina ya Waswahili na watu kutoka jamii zingine za Kiafrika, zile za Mashariki ya Kati na sehemu zingine ulimwenguni. Kazi hii imekuwa yenye umuhimu mkubwa katika utafiti wetu kwa vile imetusaidia kuelewa hali ilivyokuwa katika kipindi alichoiishi Liyongo na kwa hiyo kumwelewa shujaa huyu kwa undani; maulama wengi wanadai kuwa Liyongo aliishi baina ya kipindi hiki. Baadhi ya masuala yaliyomkumba Liyongo yanaweza yakafahamika iwapo tu tutaelewa jumla ya utamaduni wa Waswahili na mfiimo wa kijamii katika kipindi alichowahi kuishi.

Mbele (1986) ni makala ambayo yanarejelea utamaduni wa Liyongo na kuchunguza namna ambavyo masuala anuwai kumhusu Fumo Liyongo yanavyosawiriwa na maulama mbalimbali kama vile, Lyndon Harries, Jan Knappert, Edward Steere, Ali Jahadhmy, Sayyid Abdallah, Muhammad Kijumwa na Shihabuddin Chiraghdin. Mwandishi wa makala haya anayatazama makosa ambayo baadhi ya maulama wanayafanya na hususan kutokana na kuyapapia maelezo ya maulama wengine pasipo kuyatathmini kwanza. Anasisitiza umuhimu wa maulama kusoma na kuyaelewa maoni

ya maulama wengine na kwa hiyo kuwezesha kuwepo kwa ile hali ambayo itaondoa tashwishi zilizoko kuhusiana na utamaduni wa Liyongo.

Licha ya maelezo haya, Mbele anagusia kuhusu jina la Liyongo Anatoa mtazamo wake kuhusu jina halisi la Liyongo (anaonelea kuwa jina lenyewe linafaa kuwa, Liongo Fumo na wala sio Fumo Liongo na kwamba kuna uwezekano kwamba Fumo Liongo alikuwa babake) na kushadidia dai lake kwa kutoa mifano kadhaa kutoka tungo mbalimbali. Inajitokeza kuwa, hana uhakika wa jambo hili na kwa hiyo tunapata kuwa hata yeye amenaswa katika ulimbo ambao umewanasa maulama wengine. Anategemea kazi za awali na hususa nyimbo na mashairi katika kulitetea dai lake. Kuna hatari kubwa katika kufanya hivyo kutokana na kile ambacho hurejelewa kama 'uhuru wa kishairi'. Mshairi huwa na uhuru wa kubadilishabadilisha baadhi ya masuala ili kukidhi haja za urari au uwiano wa vipashio kadhaa kwenye tungo zake. Si hoja wala jambo la ajabu mimi nikiitwa Mungai Julius. Ninabakia tu kijana yule yule na hivyo basi, sioni sababu za maulama huyu kujiingiza katika kuwalaumu maulama na kisha kujitanza katika utando uleule uliowatanza maulama anaowalaumu kwa kujaribu kuyafafanua masuala ambayo ni finyu.

Katika utafiti huu, sijajiingiza katika utando kwa kujaribu kutanzua muundo wa jina la Fumo Liyongo kwani katika kufanya hivyo, tutakuwa tukijaribu 'kuzamia¹ katika kisima kisicho na kina kirefu na hivyo kuishia katika kutapatapa tu. Tumemchukulia shujaa wa Waswahili kuwa Fumo Liyongo kama anavyojulikana kutoka jadi katika fasihi simulizi ya Waswahili. Hata hivyo, utando huu ambao maulama hawa wamejitanza ni muhimu katika uga mzima wa kiusomi kwa kuwa unauweka utamaduni wa Liyongo ukiwa hai. Isitoshe, umetusaidia kuibua sifa mojawapo ya mashujaa ambayo tumeirejelea katika faslu ya tatu (majagina huwa hawaeleweki kwa uwazi). Kwa jumla, kazi hii imetufaa katika utafiti wetu kwa vile imetuangazia masuala muhimu katika utamaduni wa Liyongo, masuala ambayo yametusaidia katika kufafanulia historia yake pamoja na kupambanulia sifa zake za kishujaa na kuelezea umuhimu wake kwa jamii yake.

Tasnifu zisizochapishwa, zilizo katika lugha ya Kiswahili na zinazotalii suala la mashujaa si nyingi Tasnifu tuliyoiona ya manufaa kwetu ni ya Mutiso (1985). Katika faslu ya tatu, maulama huyu anaangalia hurafa-linganishi juu ya majagina Anairejelea *Kasida ya Hamziyya* ili kuona vile inavyosema kuhusu Mtume Muhammadi, shujaa na Mtume wa Waislamu. Analinganisha sifa za shujaa huyu na majagina wengine katika hurafa za jamii tofauti tofauti ili kuweza kueleza hurafa na uya kinifu katika kasida hiyo. Kazi hii ni muhimu kwetu kwani ni mojawapo ya kazi ambazo zimeorodhesha sifa bia za mashujaa ambazo ni msingi mzuri katika kuwafafanulia Shaka Zulu na Fumo Liyongo.

Makala ya Mberia (1989) yanamtazama Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi katika ngano za Waswahili. Katika makala haya, mwandishi anazibainisha sifa nne za Liyongo na kudai kuwa sifa hizi hupatikana katika masimulizi ya mataifa mengine duniani. Sifa hizi ni pamoja na ushupavu, nguvu za kimwili, wepesi wa akili na stadi katika gungu na mwao Aidha, anatoa mfano wa ngano kumhusu Sundiata ili kuonyesha vituko sawia na ngano ya Liyongo. Tofauti na mtazamo wa makala haya, utafiti wetu haumwangalii Liyongo kama shujaa katika ngano bali kama shujaa wa kihistoria. Isitoshe, sifa za kishujaa za Liyongo ni zaidi ya nne kama tutakavyoona haapo baadaye. Shaka Zulu, shujaa wa Wazulu hajatajwa mahali popote wala sifa zake za kishujaa kuonyeshwa katika makala haya. Waaidha, umuhimu wa Liyongo kwa jamii ya Waswahili haujaelezwa katika makala haya. Madhumuni ya utafiti wa somo letu yamekuwa kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu na kuelezea umuhimu wao kwa jamii zao jambo ambalo makala haya hayajaelezea.

Makala ya Mutiso (1999) yanatazama kiulinganishi maisha na sifa za mashujaa wawili wa kidini, Buddha na Muhammadi huku yakirejelea sifa bia za mashujaa. Aidha, katika kuwasawiri mashujaa hawa, yanataja kwa kupitia tu baadhi ya majagina wengine duniani wakiwemo Liyongo na Shaka. Nia mojawapo ya somo letu ni kuzipambanua sifa za Liyongo na Shaka na kuonyesha kiwango cha kutofautiana na kushabihiana kwa sifa zao jambo ambalo makala haya hayajaonyesha. Hata hivyo, makala haya ni muhimu kwa vile yanaeleza ingawa kwa kifupi kuhusiana na zawadi ya jagina kwa umma wake kama mojawapo wa sifa za majagina. Anadai kuwa, Liyongo aliwaachia

Waswahili gungu. Hata hivyo, hajatuelezea zawadi ambayo / ambazo Shaka Zulu aliiachia jamii yake. Utafiti wetu umeangalia kwa kina michango mbalimbali ya Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamii zao.

Mulokozi (1999) amezihariri na kuzitolea maelezo tenzi tatu muhimu katika fasihi ya Kiswahili. Tenzi hizi ni: *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa A/-Inki shaft* na *IJtenzi wa Mwanakupona*. Katika maelezo yake kuhusiana na *Utendi wa Fumo Liyongo*, Mulokozi (uk. 11) anadai kuwa shujaa wa tenzi za Kiafrika huwa na sifa tatu nazo ni: nguvu (za kimwili, za kiakili, urijali na nguvu za kivita); uganga na nguvu za sihiri; na mshikamano na kundi au jumuiya fulani inayomuunga mkono. Ingawa sifa hizi ni muhimu katika kumwelezea Liyongo kama shujaa, kuna sifa nyingine nyingi za mashujaa ambazo ameziacha nje na ambazo kama tutakavyoona ni muhimu katika kumsawiri Liyongo kama shujaa.

Hata hivyo, kazi hii ni muhimu kwetu kwa vile imetusaidia kuielewa historia ya wakati na tarehe aliyoshi Liyongo. Isitoshe, maelezo kuhusiana na maneno ya kilahaja katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni muhimu kwetu katika kuelewa utenzi huu kwa kina. Vilevile, tunapata kwamba, Mulokozi hajatuelezea kwa uwazi umuhimu wa Fumo Liyongo katika jamii ya Waswahili. Lengo mojawapo la utafiti huu limekuwa ni kuelezea kwa uwazi umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu katika jamii zao.

Miehe na wenzake (2004) wamekusanya na kuyaweka pamoja mashairi na nyimbo ambazo zinadaiwa kuwa zilitungwa na Fumo Liyongo. Waliyadondoa mashairi na nyimbo hizi kutoka kwa kazi za awali zilizochapishwa ilhali nyingine walizidondoa kutoka katika maktaba na hifadhi za nyaraka katika taasisi kadhaa duniani. Kazi hii ni zao la warsha - zilizowahusisha maulama kadhaa - ambazo zilifanyika huko Bayreuth, Ujerumani katika miezi ya Juni/ Julai 2003 na MachiJ Aprili 2004. Lengo la warsha hizi lilikuwa ni kutalii na kuchambua mashairi na nyimbo zinazohusishwa na Fumo Liyongo ili kuibuka na toleo kamilifu ambalo lingekidhi mahitaji ya kiusomi kote duniani. Licha ya kuzionyesha tungo za Liyongo, wametoa maelezo mwafaka kuhusiana na utamaduni wake, fani zilizotumiwa katika tungo hizi miongoni mwa masuala mengine muhimu katika utamaduni wa Waswahili. Kazi hii imekuwa ni kazi

mojawapo muhimu na ya kimsingi katika kuyafafanulia masuala kadhaa kuhusiana na utamaduni wa Fumo Liyongo kama tutakavyoona hapo baadaye.

Kwa jumla, kama ambavyo tulitanguliza kudokeza, kuna kazi chungu nzima ambazo zimeandikwa kuhusiana na Fumo Liyongo na Shaka Zulu zikiwemo pia kazi zingine za kijumla kuhusu mashujaa duniani. Kazi ambazo tumerejelea katika sehemu hii ni baadhi tu ya kazi nyingi muhimu ambazo zinayasawiri masuala muhimu kuhusiana na majagina wa somo letu. Kwa kuwatalii Shaka Zulu na Fumo Liyongo kiulinganishi, utafiti huu umenuia kulijaza pengo la kiusomi ambalo limekuwepo. Kama tulivyokwisha kueleza, hakuna utafiti tujuao unaowatalii Shaka Zulu na Fumo Liyongo kiulinganishi na kuelezea kwa kina umuhimu au mchango wao kwa jamii zao.

1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti wetu ulikuwa hasa wa maktabani. Tulidurusu vitabu, tasnifu na makala mbalimbali yaliyohusiana na somo letu. Nia ya kufanya hivi ilikuwa kujiandaa kinadharia na pia kuyafahamu kwa kina masuala yanayohusiana na mashujaa na hususan Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Aidha, tulifanya upekuzi wa hapa na pale kuhusiana na somo nzima la mashujaa katika tovuti mbalimbali kwenye mtandao ili tupambanukiwe zaidi na viumbe hawa wenye sifa za kiajabuajabu.

Isitoshe, tulitilia maanani ushauri tulioona ungetufaa kutoka kwa wahadhiri na baadhi ya wanaflinzi. Baada ya kusoma kwa kina na kukusanya data ya kutosha, tulitafakari na kisha tukairatibu kazi yetu kwa mpangilio tuliyoona mwafaka; ambao ungetoa taswira bayana ya Shaka Zulu na Fumo Liyongo kama mashujaa wa jamii za Kiafrika.

TANBIHI

1. taz. *Saturday Nation*, Tarchc 9 Aprili, 2005, uk.2, katika makala. ⁴*Powerful and weak come together to mourn Pope *
2. 'Mashujaa' wa kike katika historia ya jamii mbalimbali duniani si wengi Baadhi ya maulama wamejaribu kuwasawiri mashujaa' wa kike kutokana na michango yao anuwai katika jamii zao. Njau na Mulaki (1984), kwa mfano. wanatoa wasifu wa 'mashujaa' kumi wa kike katika baadhi ya jamii nchini Kenya. Wanasisitiza hasa mchango wa baadhi yao na hususan katika upingaji wa unyakuzi wa ardhi katika enzi ya mabcbcru Mashujaa' hawa ni pamoja na: Ndiko wa Githura, Ciokaraine M'Bamngu, Syotuma. Sikinan, Njoki wa Thuge. Me Katilili. Syokimau. Njuguru. Syombesa na Katulu wa Kilatya. Ingawa ameyonesha mchango wao, hajawasawiri wanawake hawa kwa mujibu wa sifa bia za mashujaa. Isitoshe, katika jamii za Kiafrika, ilikuwa muhali kwa mwanamke kuwaongoza wanaume na kwa hiyo, liawakuwa na nafasi ya kukuzwa na wanajamii kikamilifu kama mashujaa.

FASLU YA PILI

HISTORIA YA FUMO LIYONGO NA SHAKA ZULU KWA KUFUNGAMANISHWA NA ILE YA JAMII ZAO

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutaielezea salua ya Fumo Liyongo na Shaka Zulu, pamoja na ile ya jamii ambamo walizuka. Tutaangazia kwa undani vipengele vya maisha ya mashujaa hawa - miondoko yao, vitushi walivyovitenda, mahusiano baina yao na wanajamii wengine na jambo la muhimu zaidi, tutairejelea misukosuko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo iliwazua. Katika kutoa ufafanuzi wetu, tutajaribu kuelezea ingawa kwa kifupi salua ya jamii ya Waswahili na ile ya Wazulu katika kipindi cha kabla ya kuzuka kwa majagina hawa, kipindi walimoishi na hata kipindi cha baada ya mauko yao. Mchango au umuhimu wa majagina hawa kwa jamii zao utajadiliwa kwa kina katika sura ya nne.

Kama tulivyokwisha kudokeza katika sura ya kwanza, majagina wa kihistoria huwa hawazuki katika ombwe tupu bali huzuka katika mfiimo na hali fulani mahsusi za kijamii. Kufasiri historia ya jamii walimopatikana Fumo Liyongo na Shaka Zulu kutatusaidia kuwaelewa mashujaa hawa kwa kina pamoja na kupata uvumbuzi wa mazingira na hali zilizowazua na vipindi vya wakati walimozuka.

Liyongo na Shaka waliishi duniani miaka mingi iliyopita. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mijadala na mitazamo ainati kuwahusu mashujaa hawa na hususan kuhusu uyaikinifii wa Liyongo ambaye maulama mbalimbali wanakisia kuwa aliishi takribani baina ya karne ya kumi na tatu na kumi na tano.

Katika kuelezea historia ya jamii zao na vilevile historia kuwahusu, itatubidi tuzirejeele kazi za kifasihi kama vile tenzi na ngano za jamii husika yakiwemo maandishi mengine ya kihistoria. Kiango na Sengo (? : 8) wakielezea kuhusu nafasi ya fasihi kwa jamii wanadai kuwa, **"Watu hujenga utamaduni: utaratibu wa maisha. Utamaduni hujenga fasihi. Fasihi huhifadhi utamaduni, huuelezea vilivyo... Fasihi ni kioo cha jamii..."** Aidha, Vansina (1985:xi-xiv) akifananua kuhusu thamani ya fasihi simulizi

anadai kuwa historia ya jamii yoyote ile duniani inaweza ikaundwa kutokana na fasihi simulizi ya jamii husika Msisitizo wake ni kwamba, mawazo yaliyo katika akili ya mwanadamu na ambayo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine huakisi kwa kiwango kikubwa na kwa kweli tajiriba za hapo awali za maisha ya binadamu Tajiriba hizi hutumika kama hazina kwasi ambayo inatufanya kuelewa sababu za kuwepo kwa hali fulani katika wakati uliopo

Ni kwa mintarafu ya maelezo haya ambapo tuna imani kuwa tungo za kifasihi tutakazozirejelea zina maelezo muhimu yanayowahusu Shaka Zulu na Fumo Liyongo pamoja na tamaduni za jamii zao. Ni vema tukumbuke kuwa jamii husika zina vipengele vya kiasili na kitamaduni ambavyo kwa kiasi fulani vinafanana (kwa mujibu wa nadharia ya vikale). Vilevile, Fumo Liyongo na Shaka Zulu, kama mashujaa, wana vipengele vya kimaisha ambavyo vinashabihiana.

2.1.0 Historia ya Waswahili

Jamii ya Waswalihi imekuwepo katika upwa wa Afrika Mashariki kwa muda mrefii ingawa upwa huu haukuwa kitovu chao. Kwa upande mmoja, historia kuwahusu imeundwa kutokana na visasili na visakale vilivyopitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. Tamaduni kuwahusu zimekusanywa na Wazungu kutoka kwa wenyeji wa pwani na kuhifadhiwa katika maandishi. Baadhi ya Wazungu hawa ni kama vile, Alice Werner, Ernst Dammann, Sutton, Derek Nurse, Jan Knappert, Lyndon Harries, Freeman-Grenville, James de Vere Allen, Spear, miongoni mwa Wazungu wengine. Kadhalika, wanaakiolojia kama vile Neville Chittick na Schofield wamechangia pakubwa katika kuelewa baadhi ya tamaduni za watu waliokuwa wakiishi katika maeneo yaliyoachwa kama mahame au magofu kutokana na misukosuko mingi iliyotokea katika eneo la pwani hapo awali. Baadhi ya maeneo haya ni kama vile Gedi, Manda na hata Pate. Uchimbaji wa kitaalamu wa maeneo haya umepelekea ukusanyaji wa vyombo kama vile vyungu, mifiipa, makaka, mbao, vyombo vya mawe, vioo, shanga, vifaa vya vyuma, sarafu. Chittick (1984) amejaribu kufanya utafiti kuhusiana na vifaa ambavyo alivipata katika eneo la Manda Utafiti huu umesaidia katika kujaribu kuunda historia ya awali ya eneo hili ambayo ingawa kwa

kiasi fulani ina mushkili, inafaa sana katika uelewa wa tamaduni za jamii za pwani na hasa za Waswahili wa awali

Mbali na ngano kutoka kwa Waswahili wenyewe, visasili kutoka kwa jamii jirani kama vile Wapokomo, Wasegeju na Wamijikenda zimesaidia katika uundaji wa historia ya Waswahili kwa ujumla. Isitoshe, kumekuwepo na maandishi ya awali ambayo yaliandikwa na watalii wa awali kabisa waliozuru maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki.

Maandishi haya yanajaribu kufafanua mandhari ya eneo hili na kuwaelezea watu walioishi humo. Kwa mujibu wa Allen (1993:21), ufafanuzi wa awali kabisa na wa kina kuhusu makazi ya watu wa maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki unapatikana katika kitabu cha kumbukumbu cha Kichina kilichochapishwa mnamo mwaka wa 1225 B.K. Anadai kuwa, ingawa kitabu hiki kilichapishwa mwaka huu, maandishi wake wanaweza wakawa walizipokea habari kuhusu pwani ya Afrika Mashariki kutoka kwa mabaharia wa Kiarabu ambao walikuwa wakizuru eneo la upwa huu tangu zama Kijitabu kingine kinachoelezea baadhi ya sehemu za upwa na Bahari ya Hindi zikiwemo sehemu za bandari zilizo katika Bahari ya Shamu na Ghuba la Aden pamoja na maelezo kuhusu safari za mashua kueleka Uhindi zikitegemea pepo za misimu ni *The Periplus of the Erythraen Sea*. Kijitabu hiki kiliandikwa na Mgiriki baina ya karne ya kwanza na ile ya tatu baada ya Kristo na anaurejelea upwa na upembe wa Afrika kama Azania. Ingawa mwandishi hakuwa na uelewa mzuri wa eneo lililoko sehemu za chini za eneo hili, kijitabu chake kilikuwa nguzo muhimu katika maelezo ya Ptolemy kuhusiana na jiografia ya upwa wa Afrika Mashariki (Sutton 1966:6).

Waswahili kama walivyo Wazulu, ni Wabantu. Asili au kitovu cha Wabantu - kabla ya kuhamia katika sehemu mbalimbali za Afrika - ni katika eneo ambalo hivi sasa linakaliwa na nchi za Cameroon na eneo la mashariki mwa nchi ya Nigeria. Kutokana na kuongezeka kwa idadi yao miongoni mwa visababishi vingine, baadhi yao walihamia katika janibu za kusini mwa Afrika ilhali wengine walielekea mashariki. Waswahili walikuwa miongoni mwa wale ambao walihamia mashariki na kukalia katika eneo la Shungwaya¹. Nurse na Spear (1985:33), wanadai kuwa Khoisan

(*Bushmen* na *Hottentots*) ndio walikuwa jamii ya awali kabisa katika maeneo ya Afrika Mashariki kabla ya Wabantu na makundi mengine ya watu kama vile Wakushi na Waniloti kuhamia huku. Jamii hii ya watu inatambulikana kutokana na kuwa na mwaliko sauti katika uzungumzaji wao. Waliishi nyikani na misituni na walijishughulisha na uchumaji wa matunda na asaji na uwindaji wa wanyama pori. Hata hivyo, kabla ya kuwasili kwa Wabantu katika maeneo ya Afrika Mashariki, Wakushi wa kusini walikuwa tayari wakimiliki maeneo haya (Nurse na Spear khj: 45-46). Kwa mujibu wa Walsh (1987:21), Wazungumzaji wa lugha za Sabaki walipokuwa wakipitia kwenye maeneo yaliyokuwa yamemilikiwa na Wakushi hawa (walipokuwa wakitoka sehemu zilizo kwenye maeneo ya kaskazini mashariki mwa Tanzania) hakukuwa na maathiriano wala maingiliano baina ya makundi haya mawili.

Kwa mujibu wa Walsh (khj:21), kundi la Wabantu la Wazungumzaji wa lugha za Sabaki lilitengana na Wabantu wengine katika eneo la kaskazini mwa nchi ya Tanzania na kuelekea katika maeneo ya kaskazini kupitia Kenya na kuingia katika nchi ya Somalia (Shungwaya). Walifika katika eneo hili takribani katika kipindi cha nusu ya karne ya kwanza baada ya Kristo au hata baadaye. Mwishoni mwishoni mwa karne ya kwanza, kundi hili la Wasabaki lilitengana kwa mujibu wa makabila tofauti tofauti kama tuyajuavyo: Waswahili, Wapokomo, Waelwana na Wamijikenda. Baadaye kidogo, Waswahili walianza kwa taratibu kuhamia katika sehemu za kusini mkabala na Bahari ya Hindi. Wamijikenda na Wapokomo hawakuondoka kutoka katika eneo hili hadi katika kipindi cha baadaye. Ni katika kipindi hiki ambapo Wakushi waliomiliki maeneo ya kusini waliingiliana na Wabantu na baadhi yao wakasimilishwa na kuwa Wabantu.

Kugura kwa Waswahili hadi katika maeneo ya kusini ya pwani hakukutokea vivi hivi tu. Tamaduni za jamii mbalimbali za Waswahili zinadai kuwa kugura kwao kulitokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Wagalla. Stiles (1981: 858) anadokeza kuwa Wabajuni katika tamaduni zao wanadai kwa yakini kuwa Wagalla ndio waliowafukuza kutoka eneo la Shungwaya. Wagalla walifanya mashambulizi ya mara kwa mara kwenye maeneo yao ya makazi. Aidha, Werner (1915:328) pia anashadidia kwa kusema kuwa mashambulizi ya Wagalla ndio yaliyoyafanya makundi ya

Wazungumzaji wa lugha za Sabaki kukimbilia katika sehemu za kusini Hata hivyo, kama ambavyo tumekwisha kutaja, hawakuguria kwenye maeneo haya kwa wakati na kwa kundi moja

Mashambulizi ya Waswahili hayakusita hata baada ya kuhamia pande za kusini Nurse (1994:48) anadai kuwa magurio ya Waswahili na wabantu wengine hadi katika sehemu za kusini zaidi yalizidishwa na vamio la ghafla la Waarabu Jambo hili liliwafanya wabantu kuhamia katika eneo lililoko baina ya mto Juba ulio baina ya eneo la kusini mwa Somalia na mto Tana

Ingawa masuala haya yote yanatokana na tamaduni za jamii mbalimbali za pwani, kuna baadhi yake ambayo yanahitilafiana, ingawa si kwa kiasi kikubwa. Nurse (khj:48) anadai kuwa maelezo kuhusu kipindi kinachohusiana na 'Shungwaya', eneo halisi linalorejelewa kama Shungwaya na sababu za magurio mbalimbali hadi kusini mwa eneo hili yanatiliwa shaka. Hata hivyo, anapendekeza kuwa kuna mambo mengi ambayo bado yanastahili kukusanywa na kuwekwa katika maandishi. Aidha, anaendelea kudai kuwa hakuna maulama ambaye amethubutu kukusanya na kuzichambua tamaduni za Wabarawa, Waelwana, Waorma na Wakorokoro kuhusiana na tamaduni zao kuhusu 'Shungwaya.'

Baada ya Waswahili kukalia katika maeneo ya pwani, walijikusanya katika makundi madogo madogo kwenye visiwa na sehemu nyingine mbali kidogo na ufuko. Walitapakaa katika pwani yote kuanzia huko Somalia na kuteremka hadi Msumbiji. Mazingira ya bahari na mito mingine iliyotiririka hadi baharini ilikuwa hifadhi kwasi ya samaki na wanyama wengine wa majini na kwa hivyo, pamoja na shughuli zao za kawaida, waliingilia shughuli ya uvuvi. Kwa hiyo, walijiingiza katika utengenezaji wa mitumbwi, makasia, jahazi, nyugwe, nyavu na vyombo vingine walivyofanikisha shughuli ya uvuvi.

Licha ya uvuvi, shughuli zao zingine za kiuchumi zilimithiliana na zile za asili za Wabantu. Shughuli hizi zilikuwa ni pamoja na: *ufngaji* wa wanyama kama vile mbuzi, ng'ombe, kondoo na kuku; *kilimo* cha mpunga, malenge, mtama, nazi, mboga na

matunda, mawele na jamii kunde (kwa mfano, njegere na maharagwe). Ndizi na yugwa zililetwa hapo baadaye kutoka katika janibu za kusini mashariki mwa bara la Asia; *uhunzi*, uliowawezesha kuunda zana za kilimo kama vile majembe, panga, shoka na visu. Zana hizi zilitumiwa katika ufyekaji wa mashamba bikira, upandaji, uvunaji na upaliliaji. Aidha, waliunda zana za kivita kama vile mishale, nyuta, mafumo, vitara, jambia, ngao, msu na panga Baadhi ya vifaa vingine walivyoviunda ni pamoja na: vinu, mchi, kamba, vyano vya kupepetea na vinoo/tupa Isito she, *useremala* uliendelezwa ili kuunda baadhi ya vifaa vya nyumbani.

Mandhari ya bahari yaliwawezesha Waswahili kusafiri kutoka sehemu moja ya pwani hadi nyingine kwa urahisi huku wakifanya biashara na wenzao pamoja na kutembelea jamaa zao. Aidha, mazingira haya yalileta mabadiliko makubwa katika utamaduni na muundo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi wa Waswahili Bahari ilirahisisha usafiri wa wageni kutoka maeneo mengine ya ulimwengu hadi katika pwani ya Afrika Mashariki. Wageni wa awali katika maeneo haya walikuwa ni wafanyibiashara pamoja na wasomi (wanajiografia), wamishenari na watalii walioabiri mashua. Wageni hawa walitoka huko Uarabuni, Ghuba ya Uajemi, Uhindi, Ugiriki, Ureno na sehemu zingine za ulimwengu na hususan kutoka katika maeneo ambayo yamepakana na fukwe za bahari. Baadaye, bahari iliwawezesha Wareno na mwishowe kabisa Waingereza kufika katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki wakiwa na nia ya kujitwalia maeneo muhimu pamoja na kusambaza dini

Kwa mujibu wa Freeman-Grenville (1954-1955:1) kati ya waandishi na wanajiografia wote wa Kiarabu wa enzi za kati (baina ya miaka 1100-1500) wanaoirejelea Afrika Mashariki, hakuna mwandishi aliyetembelea pwani ya Afrika Mashariki ambayo kwa sasa inajumuisha pwani za Somalia, Kenya na Tanzania ila tu Muhammed ibn Abdallah ibn Batuta ambaye aghalabu hujulikana kama ibn Batuta². Mwandishi huyu alikuwa na ufahamu wa kipekee wa upwa huu na maelezo yake (ambayo Freeman-Grenville khj:l-6 anayaelezea) kuhusiana na ustaarabu, mandhari, desturi na mahusiano aliyokuwa nayo na wenyeji, yana umuhimu mkubwa katika uelewa wa historia ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki.

Kwa vile teknolojia haikuwa ya haJi ya juu kama ilivyo hivi sasa, wafanyi biashara wakiwemo watu wengine walitegemea sana pepo za Kusi na zile za Kasikazi ili kufika na kuondoka katika pwani hii. Mali hii ya kuzitegemea pepo za kasikazi na zile za kusi ilikuwepo tangu zama na ilitumiwa na mabaharia waliolitembelea eneo hili. Njia hii ndiyo iliyokuwa ya kipekee na ya haraka iliyokuwepo na iliyotumiwa kuzifikia pwani mbalimbali za maeneo tofautitofauti duniani Pepo za Kasikazi zilianza kuvuma katika mwezi wa Novemba na kufikia hadi mwezi wa Februari. Waarabu, Wahindi na Waajemi walitumia msimu huu kufika katika pwani ya Afrika Mashariki. Baada ya pepo za Kasikazi kutulia, pepo za Kusi zilianza kuvuma na kwa hivyo walichukua fursa hii na kurudi makwao baada ya shughuli zao za kibiashara Pepo hizi zilikuwa zenye nguvu sana. Wakati mwingine, ziliweza kupindua baadhi ya mashua na kuwaua watu wote waliokuwemo pamoja na kuharibu bidhaa zilizokuwemo. Aidha, wakazi wa pwani na hasa katika karne ya kumi na tisa wangeweza kujua kipindi ambapo maadui kutoka maeneo ya mashariki na kwingineko wangefika huko pwani kwa nia ya uvamizi na hivyo kujiandaa kivita ipasavyo. Muyaka bin Haji al-Ghassany (1776-1840), anazirejelea pepo hizi katika baadhi ya mashairi yake. Kwa mfano, katika shairi, *'Ngoma ya Kizungup'ia'* (Abdulaziz 1979:132), anatoa changamoto kwa vikosi vya Omani vilivyokuwa katika kisiwa cha Unguja, kufika Mombasa kwa vita Anasema:

**Gongwa la Mwana Mkisi kwamba wataka lingia
Kaageni wenu mbasi wake na watumba goya
Muie kwa p'epo za kusi mupate kuangukia
Ngoma ya kizungup'ia Wagonjwa waipigile.**

Wageni waliofika katika pwani ya Afrika Mashariki kwa shughuli za kibiashara walinunua na kuuza bidhaa mbalimbali. Baadhi ya bidhaa ambazo walinunua kutoka kwa Waswahili ni pamoja na: mbao, dhahabu, pembe za ndovu, magome ya kobe, watumwa waliotekwa kutoka bara, rangi za nguo, manukato, miongoni mwa bidhaa zingine. Aidha, Waswahili walinunua bidhaa kama vile vyungu, majora ya vitambaa, shanga za vioo, vitara, vyombo vya vioo vya nyumbani, mvinyo, shaba na ngano miongoni mwa bidhaa zingine kutoka kwa wageni.

Pindi biashara iliposhamiri ndipo ambapo vijiji vilizidi kupanuka na hatimaye vikawa miji. Baadhi ya wageni kama vile Waarabu walikuja na familia zao na kustakimu katika eneo hili. Allen (1993:7), anadai kuwa Waarabu na Waajemi, ambao wamekuwa

wakitumia pepo za misimu katikia Bahari ya Hindi ili kufika katika pwani ya Afrika Mashariki kwa muda wa miaka elfu mbili au zaidi, ndio waliokuwa waasisi wa ustaarabu katika eneo hili. Miji iliyozuka katika kipindi hiki na ambayo hadi sasa ipo na imesambaa kote katika upwa wa Afrika Mashariki ni kama vile: Mogadishu, Lamu, Mombasa, Pemba, Unguja, Malindi, Barawa, Kilwa, Gedi, Pate, miongoni mwa miji mingine. Miji ya awali kabisa katika upwa wa Afrika Mashariki inasawiriwa vizuri kwenye ramani kama ilivyotolewa na Idrisi mnamo mwaka wa 1154 B.K. Tumeionyesha ramani* hii katika uk.164. Licha ya biashara, Waarabu walisambaza dini ya Kiislamu kwa Waswahili ambao hapo awali waliwachukulia kuwa makafiri kutokana na imani zao asilia (imani katika mapanga, sayari za anga za juu, nyota, jua na hata mwezi). Usambazaji wa dini hii ulikuwa wa kasi, jambo ambalo lilisababisha asilimia kubwa kabisa ya Waswahili kuwa Waislamu. Si ajabu kwamba, hata sasa, mtu akisema kuwa yeye ni Mswahili, baadhi ya watu humchukulia mara moja kuwa ni Mwislamu. Baadhi ya watu hawatofautishi kati ya Uswahili (utamaduni wa Waswahili) na Uislamu (dini). Misikiti ilijengwa, mashekhe kutawazwa na buibui kama mavazi rasmi ya wanawake wa dini ya Kiislamu yakajipenyeza katika janibu hizi, miongoni mwa matambiko na sherehe nyingine (kwa mfano, *Maulidi*) zinazohusishwa na Uislamu. Athari za kigeni katika janibu za pwani na hususan kwenye utamaduni wa Waswahili ni nyingi mno.⁴

Jamii ya Waswahili imepitia katika misukosuko ya kila nui katika vipindi mbalimbali vya historia yake. Maisha yao yalikuwa yamevurugwa kwa kiasi kikubwa na wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani. Aidha, jamii mbalimbali za Waswahili zilifarakana zenyewe na hata vita kuzuka na kusababisha uharibifu mkubwa wa vitu na pia vifo. Isitoshe, mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa majirani zao walioishi bara kama vile Wasanye (Waboni), Walangulo, Wadahalo, Wasegeju na Wagalla yalifanyiwa makazi ya Waswahili. Mitafaruku hii iliyotokea hasa baina ya karne ya kumi na mbili na kumi na tano iliwavuruga Waswahili kwa kiasi kikubwa hivi kwamba hawakuwa na mtu wa kuwaongoza wala kuwaunganisha. Ni kwa sababu ya tafrani na misukosuko hii ambapo Fumo Liyongo, shujaa wa Waswahili alizuka.

2.1.1 Misukosukoya kivita iliyomzua Fumo Liyongo

Kama ambavyo tumekwisha kutokeza, jamii ya Waswahili ilipitia katika misukosuko ya kila nui. Vita mbalimbali vimeelezwa hasa katika visasili na visakaJe vya jamii ya Waswahili wakiwemo majirani zao kama vile Wagalla, Wasegeju na Wapokomo. Aidha, maelezo kuhusu misukosuko hii katika vipindi mbalimbali yamefafanuliwa katika tarihi mbalimbali za jamii hii kama vile: *Tarihi ya Pate*, *Tarihi ya Ki/wa*, *Tarihi ya Lamu*, *Tarihi ya Mombasa* na *Tarihi ya Vumha* (Prins 1958:27-29) yakiwemo maelezo mengine ya kihistoria ambayo yameungwa mkono na wanahistoria katika harakati zao za kupigia darubini salua ya Waswahili.

Biashara ya watumwa iliyoendelezwa na Waarabu ilisababisha misukosuko katika jamii za bara na vilevile jamii za pwani Biashara hii ilishamiri sana kwa karne nyingi katika eneo hili. Waarabu kwa ushirikiano na baadhi ya Waafrika walitumia nguvu (walikuwa na bunduki na mapanga) katika kuwateka watu na kisha kuwasafirisha hadi katika eneo la Mashariki ya Kati zikiwemo sehemu nyinginezo ulimwenguni. Walipotekwa kutoka bara, watumwa hawa walifunganishwa kwa kamba na minyororo kwenye shingo zao; nyumba zao zikachomwa moto; watoto wao wakauawa; na wakasafirishiwa katika mazingira yenye hatari mno wakiwa wametwikwa baadhi ya bidhaa kutoka pwani. Wengi wa mateka hawa walifika njiani kabla ya kufika pwani kutoka bara. Isitoshe, baadhi yao walitoswa baharini wakiwa wamefungwa kamba na minyororo miguuni na mikononi. Taswira ya hali ilivyokuwa inaelezwa kwa ustadi katika kitabu, *Uhuru wa Watumwa* cha James Juma Mbotela kilichochapishwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1934. Shughuli za utekaji wa watumwa zilizua vita vya mara kwa mara baina ya Waarabu na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki (Waswahili wakiwemo) na hata bara.

Waarabu walikuwa wakipora na kuzua vita vya mara kwa mara katika jamii ya Waswahili wa Afrika Mashariki. Katika utenzi, *Qisa cha watu wa Lamu*⁵ tunaeleza kuwahuu Waarabu waliopanga njama ili kutwaa dhahabu na fedha za waAmu. Ilipojulikana, Sultan (Bwani Zaidi Mgumi) aliandikia raia wote nyaraka na kuwatahadharisha dhidi ya shambulio la Waarabu. Aliwaambia wajiandae kivita dhidi ya maadui zao kama tunavyoeleza:

**13. Mfalume aziwize,
khabari siitangaze,
ni kheri tuitangaze,
ili pote ikieneya.**

**14. Akaandika baruwa,
watu akawamkuwa,
panga wakazisugua,
yuani wakadeteya.**

Baada ya mfalme kutoa arifa, waAmu wanakaa chonjo ili kujilinda dhidi ya Waarabu. Tena, katika utenzi huu huu, Waarabu wanarejelewa kama wezi na waporaji waliowasumbua Waswahili kwa muda mrefu:

**24. Wakanena kwa kituwo,
hawa ni wao kwa wao,
mngine asiokwao,
ni upesi kumgenya.**

**25. Tukizidisha makazi,
wata tupoka jahazi,
badua hawa ni wezi,
hushinda wakituibiya.**

Waarabu walipigana vita na dola takribani zote katika pwani ya Afrika Mashariki Dammann (? :61) ameyanukuu maelezo aliyosimuliwa kuhusu Siu na Pate na katika unukuzi huu, tunapata kuona Waarabu wakienda Pate ili kufanya vita Tunaelezwa:

**Waarabu wakapata xabari: amefungwa mthu wao, nao ni wathu arba'ini.
na fitina ile ni safu mbili, Nabahani wa diwani na Nabahani wa gongwa-
na wathu wa ezi mbwa gongwa. Wa'arabu wakaizihiri wakataka mthu
wao wakenda kwa mfalme kwa zita.**

Kwa jumla, ingawa Waarabu walikuwa washiriki kwenye biashara na uasisi wa ustaarabu katika pwani ya Afrika Mashariki vikiwemo baadhi ya vitongoji vyake, hawakukosa kuwakera Waswahili. Kero na mashambulizi yao yanarejelewa hata na washairi wa baadaye kama vile Muyaka bin Haji.

Mbali na tafrani zilizosababishwa na Waarabu, jamii za Waswahili katika maeneo tofauti tofauti zilipigana vita zenyewe kwa zenyewe. Wafalme wa dola mbalimbali walichukua kila hatua ili kuona kwamba utawala wao hautishiwi. Maangamizi ya Liyongo kwa mujibu wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*, yanahusishwa na mapinduzi ambayo Daudi Mringawari (binamuye) alidhania kuwa Liyongo angeyafanya dhidi ya utawala wake:

**49. Fitina zikamngiya
mfalume miya miya
mwa hila hokusudiya
kumuwa fahamiya.**

**51. Na Sulutwani niseme
alikucha mwanamume
tampoka ufalume
dhana alimdhaniya.**

Kadhalika, dola mbalimbali zilipigana vita ili kuonyesha umahiri wao katika 'ucheza ngoma\ Wapate, kwa mfano, walipigana vita na jamaa kutoka Lamu kama ambavyo tunaelezwa na al-Murshedy (1927:1):

Na waPate walikuya Shela ili kupiga Amu. Hapo zikawa vita qabila mbili hizi. Na wa Amu wakapigana sana, wakashinda watu wa Amu. Wakafa katika Mazru'i na Wa Pate taqriban ya watu 300. Wakakimbiya wakapanda majahazi yao. Kisha ba'ada ya vita hizina dola ya Amu haikuwa na mfalme...

Katika kushadidia madai kuhusiana na mashambulizi yaliyofanywa na dola moja dhidi ya nyingine, Sutton (1966:18) anadokeza kuwa baina ya miaka 1200 na 1500 B.K. kulikuwepo na ugomvi, mitafaruku na mashambulizi baina ya dola mbalimbali au baina ya makundi yaliyokuwa yakizozana katika dola hizi. Anaendelea kusema kuwa masultani wa awali wa Kilwa walikuwa na matatizo na majirani zao. Anaendelea kusema kuwa hata *Tarihi ya pate* inatuelezea kuhusu mapigano, uporaji na mapinduzi katika visiwa vya Bajuni ukiwemo umwagikaji mwingi wa damu na uharibifu wa mali katika kisiwa cha Pate. Isitoshe, Malindi ilizozana na Mombasa na ni baada ya Wareno kuingilia kati kwa kutumia bunduki ambapo uporaji mkubwa ulitokea katika mji wa Mombasa. Waaidha, anaelezea kuwa (uk.19) imedaiwa kuwa kufifia kiuchumi na kisiasa kwa mji wa Kilwa mwishoni mwishoni mwa karne ya kumi na tatu na mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na nne kulilingana na kuinuka kiuchumi kwa mji wa Pate. *Tarihi ya Pate* inaelezea kuwa kuinuka kiuchumi kwa mji wa Pate kulisababisha utekaji katika maeneo mbalimbali ya pwani kutoka Mogadishu hadi katika visiwa vya Kirimba vilivyo pande za kusini.

Misukosuko ya kivita haikutokea tu baina ya Waswahili wenyewe au baina ya Waswahili na Waarabu. Baadhi ya majirani wa Waswahili waliokuwa katika bara pia walikuwa tisho katika utangamano wa Waswahili Hapo awali tulidokeza ya kwamba sababu mojawapo ya Waswahili kuhamia kusini kutoka Shungwaya ilikuwa ni kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Wagalla katika makazi ya Waswahili. Mashambulizi haya hayakutekelezwa dhidi ya Waswahili pekee bali pia yalifanyiwa Wapokomo na vilevile Wasegeju yakiwemo makundi mengine ya Wamijikenda. Wagalla wanaelezwa katika tamaduni za jamii mbalimbali katika janibu za pwani kama watu ambao ni wakatili.

Baada ya kuwatimua Waswahili na makundi mengine kutoka Shungwaya, Wagalla waliwafiiata hadi sehemu za kusini na kuzidisha mashambulizi yao Werner (1915:328), anadokeza kuwa Wasegeju na Wakauma, kwa mfano, walitoka kutoka katika makao yao ya awali ili kuwahepa Wagalla ambao walikuwa wakatili na wenye nguvu zaidi na kwa hiyo hawangeweza kuwashinda katika vita. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya Wapokomo walikubali kushindwa na Wagalla na kisha kutekwa na kufanywa watumwa wao. Hata hivyo, tamaduni za Wapokomo zinaeleza kuwa Wapokomo wengine walijificha kwenye mashimo karibu na fuo za mito na Wagalla walipokuja kulisha mifiigo yao, walifumwa na Wapokomo waliojijami kwa mishale iliyokuwa na vyembe vilivyokuwa na sumu. Wagalla hawakuweza kung'amua yalikotokea mashambulizi haya na kwa hiyo wakakimbilia katika sehemu za chini za mto. Usiku ulipoingia, Wapokomo waliwafiiata kwa kutumia mitumbwi yao midogo na kuwaua. Baadaye, waliificha mitumbwi yao kwenye mchanga, chini ya mto. Hatimaye, Wagalla walichoshwa na tafrani hii na wakajaribu kufanya urafiki na Wapokomo ambao waliapa kuwa hawangewashambulia tena. Tena, Wagalla nao walisitisha dhuluma dhidi ya Wapokomo.

Tamaduni za Wamijikenda na vilevile zile za Waswahili zinadai kuwa nyumba zao za awali zilikuwa zimezekwa kwa nyasi kwenye paa na hata kwenye pande zake. Hali hii iliwapa Wagalla nafasi ya kuwafuma mikuki, kutoka nje, walipokuwa wamelala. Allen (1993:218), anadai kuwa kuna hadithi mojawapo kuhusu *kaya* ya hapo awali ya Wagiriama kwa jina *Kaya Murikwa* iliyokuwa na nyumba za sampuli hiyo ambayo ilishambuliwa kikatili na Wagalla na hatimaye ikabadilishwa jina na kuitwa *Kaya Mwijo* (Kaya ya adhabu).

Ni nini kilichowafanya Wagalla kuwashambulia majirani zao? Kwanza, inadaiwa kuwa Wagalla walifanya hivyo kwa sababu ya fahari yao tu - waliridhika ghaya baada ya kuona mikuki yao ikipasua ngozi nyororo za wanadamu wasiokuwa na hatia na kutumbukia kwenye sehemu za ndani za miili yao na kisha kuwafanya kuanguka na kuwa maiti. Katika kisasili kimoja kuwahusu Wagalla kilichonakiliwa na Dammann (? :73) tunadokezewa:

Ule mfalme wa Urma kamwambia sultani. ndiyo sababu, ndiyo asili ya kwamkuliwa Wagala. wakasuhubiyana na kupidja. na Wagala

**wakaguria kwa huku tangu kiunga hata Mambrui wakazidi
kutakabari, Wagala wakiuwa wathu na sababu ya kuuwa wao
ni faxari kwao.**

Sababu nyingine ambayo iliwapanya Wagalla kuwashambulia majirani zao ilikuwa kutwaa mifugo yao. Werner (1915:335) anaelezea kwamba, wakati walipowaona Wapokomo wakiwa na n'gombe wengi, walihangaika katika nafasi zao hadi wakafikia kiwango cha kuwatwaa ng'ombe hao na kisha kuwapanya Wapokomo kuwa watumwa wao.

Katika utungo mojawapo alioutunga Liyongo, *Gungu la mnara m/>>ambe* (Miehe na wenzake 2004:54), Liyongo anawataja Wagalla na hata Wangazija kama maadui wa jamii yake. Anaelezea kuwa watu hawa walikuwa na nia ya kuzua tafrani na hatimaye vita katika mojawapo ya sherehe za harusi iliyokuwa imetayarishwa na jamii yake. Liyongo katika utungo huu anasema kuwa 'watawatilia ukuta', yaani watawazuia kwa kuwapiga vita ili wasije wakawaingilia pale mjini kulikokuwa na sherehe za harusi. Utungo wenyewe ni kama ufuatao:

Gungu la mnara mpambe

**Mama nipeka haowe kaowe urembo na shani Ungama
Haowe mnara mpambe mpambe uzainiweo heshima
Na wenye kupamba pambato pambato wavete vitindi na kama
Wavete swaifo ziamba ziamba na mikili mbee na nyuma
Wavete libasi teule teule kwa zitwana mbee na nyuma
Watukuze p'anga na ngao na ngao mtu hutosheya kuona
Kuyiye Mngazija na k'umbo na kumbo uyiye kutaka harubu
Kuyiye Mgala na mata na mata uyiye kutaka kuteta
Tutawatiliya ukuta ukuta wasiungiliye muyini.**

Misukosuko ya kivita iliyotokea katika janibu za pwani kama ambavyo tumekwisha kuonyesha iliwavuruga Waswahili zikiwemo jamii zingine za maeneo haya kwa kiasi kikubwa. Walikuwa hawana mtu wa kuwaongoza wala kujitambulisha naye na hata kuwakinga kutokana na mashambulizi ya maadui zao. Isitoshe, palihitajika mtu wa kuwaunganisha pamoja kama jamii moja. Ni katika misukosuko na kuvurugika huku katika jamii ya Waswahili na jamii zingine za pwani ambapo Fumo Liyongo, shujaa wa Waswahili alizuka. Kama ambavyo tutakavyoona hapo baadaye, Fumo Liyongo hakuwa tu shujaa wa Waswahili bali alikuwa pia shujaa wa Wapokomo, Wasegeju na jamii zingine za pwani. Jamii hizi pia zilihitaji kujitambulisha na kuwa na kiongozi wa

kuwaongoza kutokana na dhuluma za maadui zao Tamaduni za jamii hizi zinamwonyesha Fumo Liyongo kama shujaa wao.

2.1.2 Historia ya Fumo Liyongo

Fumo Liyongo alizuka kutokana na misukosuko ya kivita iliyokuwa imesheheni katika upwa wa Afrika Mashariki kwa muda mrefu. Maelezo yake yanapatikana hapa na pale na yametokana na tamaduni za jamii mbalimbali za pwani. Hata hivyo, kuna ukuruba au uwiano wa aina fulani kuhusiana na maelezo tofautitofauti ambayo yalipitishwa kwa muda mrefu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya utambaji. Kuna maandishi chungu nzima ambayo yameandikwa na maulama mbalimbali kumhusu Fumo Liyongo. Isitoshe, kumekuwepo na mijadala mirefii kuhusu iwapo shujaa huyu wa Waswahili aliwahi kuishi na ikiwa kweli aliishi kama alikuwa na sifa ambazo amepewa. Kwetu sisi, hatuna shaka kwamba Fumo Liyongo aliwahi kuishi na kwamba alikuwa na sifa za kipekee - sifa zilizokuwa tofauti na zile za wanajamii wengine. Yumkini, sifa hizi zinaweza zikatiliwa chumvi katika maandishi ya kifasihi yanayomsawiri na hii ni kaida ya mashujaa wote duniani. Shujaa hukuzwa na wanajamii ambao humwona kama kiumbe wa ajabu mno. Licha ya hayo, tumeyadokeza mazingira na hali ya kijamii ambayo ilimzua Fumo Liyongo. Hali kama hii hudhihirika katika uzukaji wa majagina wengine duniani.

Mengi ya maandishi ya awali yanayomhusu Liyongo yaJikusanywa na Wazungu kama vile: Lyndon Harries, Jan Knappert, Edward Steere, William Hichens, Ernst Dammann, William Taylor miongoni mwa Wazungu wengine Waafrika wa awali walioandika masuala kumhusu Liyongo, kwa mfano, Muhammad Kijumwa (katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*), walifanya hivyo kwa hisani ya Wazungu ambao walikuwa wakifanya utafiti kuhusiana na fasihi ya Kiswahili. Licha ya kukusanya maelezo muhimu kumhusu Liyongo, Wazungu walikusanya fani mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitia katika maandishi. Mische na wenzake (2004:8) wanaeleza kuwa, licha ya juhudi za Wazungu za kukusanya tamaduni kumhusu Liyongo na kuziweka katika maandishi, Waafrika wachache kama vile Ahmed Nabahany na Ahmad Nassir pasipo utegemezi wa Wazungu wamefanya juhudi za kukusanya na kuweka katika

maandishi baadhi ya tamaduni za watu wa Lamu na Mombasa zikiwemo tamaduni kumhusu Liyongo.

Haijulikani kwa yakini ni lini Liyongo alizaliwa lakini wasomi wanakisia kwamba aliishi takribani katika karne ya kumi na tatu na kumi na tano. Liyongo hakuwa shujaa wa Waswahili tu bali anatajwa pia katika utamaduni, kwa mfano, wa Wapokomo. Ikumbukwe kwamba, Waswahili walioana na baadhi ya majirani zao na kwa hivyo, mengi ya makabila yalidai kuwa Liyongo alikuwa shujaa wao Ni kawaida kwamba, mwanadamu yeyote duniani hupenda kujihusisha na mtu ambaye ni maarufu. Mamake alijulikana kwa jina Mwana Mbwasho ilhali babake alikuwa Mringwari I. Kijakazi wake alikuwa Saada na anadhihirika mno katika tungo ambazo inadaiwa Liyongo amezitunga. Mpenzi wake alijulikana kwa jina Kundazi. Kwa mujibu wa Mieke na wenzake (khj:5), tamaduni kumhusu Liyongo na jamaa wake wa karibu kama vile mamake, kijakazi chake, mpenziwe na mpinzani na adui wake mkubwa kwa jina Daudi Mringwari zimehifadhiwa akilini mwa watu wa pwani na zimekuwa sehemu muhimu ya urithi wa utamaduni wa kitaifa wa Kenya na hata Tanzania. Isitoshe, kiini cha utamaduni wa Liyongo huhusishwa na nyimbo za sifa na uchezaji ngoma na nyingi za nyimbo hizi bado zipo kwenye fikra za wazee waliokomaa wa Mombasa na Lamu.

Wapokomo katika tamaduni zao wanadai kuwa Liyongo alikuwa mtawala wa dola ya Ozi (katika karne ya kumi na tano) iliyokuwa katika upande wa chini wa Mto Tana (kuna madai kwamba Liyongo alikuwa akitembelea ufuko wa mto Tana ili kufua nguo zake pamoja na kuoga) lakini baadaye alipinduliwa na dola ya Pate na ufalme wake kutwaliwa (Allen 1993:95). Mji mkuu wa dola hii ulikuwa Shaka. Kwa mujibu wa *Tarihi ya Pale*, inadaiwa kuwa Liyongo alipanua ufalme wake kutoka Malindi hadi janibu za Wapokomo, eneo ambalo ni mkabala na hori la kisiwa cha Pate Liyongo mwenyewe, kama mtawala wa dola hii, hakupendwa na Wapokomo. Jambo hili lilitokana hasa na kodi aliyowatoza. Vijiji vikubwa vilitozwa kodi ya wasichana wawili na wavulana wawili ilhali vijiji vidogo vilitozwa kodi ya msichana mmoja na mvulana mmoja kutoka kila kijiji, miongoni mwa kodi zingine na hasa kutoka kwa mazao ya kilimo. Hali hii ya kumchukua inadhihirika katika maelezo ya *Hadithi ya Liyongo* (Steere 1870:339-452). Katika hadithi hii anasawiriwa kama mtu mbaya - aliyekuwa

anawaudhi watu sana. Hadithi hii ilisimuliwa kwake Steere na Hamisi wa Kayi (Khamis bin Abubekr) huko Unguja

Hata hivyo, utamaduni wa Waswahili unadai kuwa Liyongo alipendwa sana na watu. Hali hii inadhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, pale ambapo baada ya kifo chake, watu wengi walisikitika na kuhuzunika. Hata hivyo, kama ilivyo kawaida ya wanadamu kote duniani, si watu wote walihuzunika. Maadui zake waliftirahia kwa vile tisho lao kubwa lilikuwa tayari limeondolewa.

Allen (1993:121) anadai kuwa Fumo Liyongo alitokana na ukoo wa al-Bauri Mpinzani wake mkubwa (ambaye alikuwa binamuye) kwa jina Daudi Mringwari pia alitokana na ukoo huu. Ukoo huu ulichukuliwa kuwa ukoo bora (ukoo wa kifalme) ambao uliheshimiwa na kupewa mamlaka ya kuwaongoza wanajamii. *Utenzi wa Fumo Liyongo* unagusia masuala muhimu yaliyomkumba Liyongo kutokana na uhusiano wake na Daudi Mringwari kuhusu utawala wa dola ya Pate. Mzozo huu ulitokana na tofauti za uhalali wa urithi wa mamlaka baada ya Mringwari I kufa (Harries 1962:51). Daudi Mringwari ndiye aliyetwaa mamlaka ya kuitawala dola ya Pate. Baada ya Daudi kuutwaa uongozi wa dola hii, Liyongo alianzisha utawala wake karibu na Mto Ozi, makao makuu yakiwa ni Shaka. Kwa vile Liyongo alikuwa ni shujaa wa kivita, binamuye alidhanja kwamba angempokonya ufalme wa dola ya Pate na kwa hiyo akamtafutia mbinu za kumwangamiza. Mzozo huu umeangaziwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambao ulitungwa kwa ustadi mkubwa na Muhammad bin Abubakar bin Umar al-Bakari (kwa jina jingine, Muhammad Kijumwa) katika mwaka wa 1913. Tutatoa muhtasari wa hadithi iliyomo kwenye utenzi huu hapo baadaye.

2.1.3 Thibitisho la kuwahi kuwepo kwa Fumo Liyongo

Kama ambavyo tumedokeza hapo awali, baadhi ya watu hutilia shaka suala la kuwahi kuwepo kwa Fumo Liyongo. Hata hivyo, kuna ushahidi ambao tunaweza tukatumia kuthibitisha kuwa Liyongo licha ya kuwa na sifa za kiajabuajabu, sio kiumbe wa kufikirika bali ni mtu aliyeishi na kutalii sehemu mbalimbali katika janibu za pwani ya Afrika Mashariki.

Ushahidi wetu wa kwanza unatokana na fasihi simulizi ya Waswahili na Wapokomo miongoni mwa fasihi simulizi za jamii zingine ambapo maelezo kumhusu Liyongo (shujaa wa Waswahili) na sifa zake za kustaajabisha yalipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Maelezo haya yalibadilishwabadilishwa Hali hii ni ya kawaida katika fasihi simulizi ambayo huchukuliwa kuwa mali ya jamii Mtu yeyote anaweza akaibadilishabadilisha ili kukidhi mahitaji yake mwenyewe katika muktadha fulani. Tungo kumhusu Liyongo na ambazo mali ghafi yake ni fasihi simulizi zimeandikwa kwa wingi zote zikiwa zinashadidia kuwahi kuwepo kwa Liyongo.

Licha ya tofauti katika masimulizi kumhusu Liyongo, jamii ya Waswahili imeshikilia kwa muda kuwa Liyongo alikuwa na angali shujaa wao na kwamba 'yu hai' miongoni mwao. Steere (1870: vi), anadai kuwa hakuna ajuaye kwa yakini ni lini Liyongo alikufa lakini yeye hukumbukwa daima na kutajwa tu kwa jina lake huibua hisia miongoni mwa Waswahili (akirejelea jamii ya wakati huo). Isitoshe, anaendelea kusisitiza kuwa hadithi kumhusu Liyongo ilipotambwa katika sherehe, watu wote walisimka na kulia kama watoto na hususan pale ambapo mama yake alingusa na kupata kuwa alikuwa mfu.

Suala lingine linaloonyesha kuwepo kwa Liyongo ni ushahidi wa kimaeneo. Maeneo yanayorejelewa ni ya kweli - si ya kubuni - na yanapatikana katika janibu za Waswahili hata sasa. Isitoshe, hata mahali Liyongo alipofia na pale alipozikwa panafahamika. Kwa mujibu wa Knappert (1979: xii), kaburi la Liyongo linaweza kuonekana karibu na mto Ozi (huko Kipini). Swali analouliza ni: **'Ni nani anaweza kuamini kuwa kaburi lililo na futi kumi na mbili ni la binadamu?'** Hii ni ithibati moja ya baadhi ya maulama wanaotilia shaka kuwepo kwa Liyongo. Hata hivyo, tunafahamu kwamba hata sasa, wanadamu hutofautiana kwa urefii miongoni mwa sifa zingine na ndiposa kukawa na kile kitabu maarufu cha kuhifadhi majina pamoja na sifa za watu ambao huvunja rekodi za ulimwengu. Kitabu hiki si kingine ila ni, **"~~712~~ Guinness Book of Records"** Aidha, Werner (1968:145) anakiri kuwa mnamo mwaka wa 1912, alionyeshwa kaburi la Liyongo lililoko huko Kipini na hata mahali mahsusi alipofia, karibu na kisima. Vilevile, mmojawapo wa wasimamizi wangu (Dkt. Mutiso), katika

kumhoji alinidokezea kwamba hata yeye aliwahi kuonyeshwa kaburi la Liyongo (pamoja na kile kisima) alipotembelea mji wa Kipini na Pate

Isitoshe, masuala ya kijamii na hususan migogoro ya kijamii kuhusiana na urithi wa madaraka, fitina na usaliti yamekuwepo katika jamii za Kiafrika - si mambo mapya Mambo haya yangalipo hadi sasa. Vilevile, Liyongo kusawiriwa akiwa na sifa za kipekee ni jambo ambalo linapatikana katika mashujaa wa kihistoria wa jamii zingine Tena, kuzuka kwa Liyongo kama ambavyo tumekwisha kudokeza hakukutokea vivi hivi tu bali kulitokea katika muktadha na hali fulani za kijamii kama ambavyo mashujaa wengine huzuka. Alizuka ili kuikomboa jamii yake kutokana na misukosuko ya kivita pamoja na kuwaunganisha wanajamii Hali hii pia inlandana na kuzuka kwa Shaka Zulu kama ambavyo tutakavyoona hapo baadaye. Kwa hiyo, mtu yeyote hastahili kufikiri kwamba, kwa vile yeye hana uwezo au sifa fulani, basi wengine hawana. Hakosi mtu, kitu au jambo fulani katika jamii ambalo lina sifa za kipekee. Sifa hizi za kipekee ndizo huonyesha kwa yakini kuwa mtu fulani ni shujaa tofauti na watu wengine.

2.1.4 Tungo zinazohusishwa na Fumo Liyongo

Liyongo anadaiwa kuwa alikuwa stadi katika kubuni na kutongoa mashairi na nyimbo. Anarejelewa kama shaha wa gungu na mwao katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ubeti 79). Baadhi ya tungo ambazo anadaiwa kuwa amezitunga zimekusanywa na kuhifadhiwa katika maandishi. Kadhalika, kuna tungo nyingine ambazo zimetungwa na watu wengine kumhusu.

Tungo ambazo Liyongo anadaiwa kuwa alizitunga ni nyingi mno. Tungo hizi zimepitishwa kwa njia ya masimulizi kwa muda mrefii kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika jamii ya Waswahili. Tungo hizi zilianza kunakiliwa na Wazungu mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Ni bayana kuwa, baadhi ya sehemu za tungo hizi zilikuwa zimebadilishwabadilishwa kama ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi simulizi. Mfano mzuri wa utungo kama huu ni *Utenzi wa Mwana Ninga*. Utenzi huu umenukuliwa na Knappert (1979:84-91), Ridhiwani (1977:23-32), na vilevile Miehe na wenzake (2004:65). Kuna tofauti katika idadi ya beti baina ya tenzi zilizonukuliwa na

maulama hawa watatu. Utenzi aliounukuu Knappert una beti hamsini na moja; ule wa Ridhiwani, una beti arobaini na saba; ilhali ule ulionukuliwa na Miehe na wenzake una beti hamsini na mbili. Hii ni athari mojawapo ya fasihi simulizi Inadaiwa kuwa utenzi huu ulitungwa na Fumo Liyongo ili kumsifu mpenzi wake (kwa jina Yanga au Mwana Ninga au Mwana Munga). Anatusawiria na kutusifia umbile la mwanamke huyu - na hususa sehemu zake mbalimbali za upande wa mbele wa mwili wake; kuanzia utosini na kuteremka kwa hatua ya asteaste hadi nyayoni. Hasiti kuzielezea sehemu zake za siri ambazo anazilinganisha na mandhari ya bahari ambayo huhanikiza upepo mwanana unaowatuliza wote waendao kuyatalii mandhari hayo. Lugha iliyotumiwa katika utenzi huu ni chakavu mno.

Hakuna ithibati ya kutosha kuonyesha kuwa Liyongo ndiye mtunzi asilia wa tungo zinazodaiwa kuwa ndiye aliyezitunga. Hata hivyo, kama tutakavyoona hapo baadaye, kitu chochote katika jamii, kote duniani ni sharti kiwe na asili. Ni jambo la kawaida kuwa vitu vingi vizuri katika jamii huhusishwa na mashujaa. Kwa hiyo, si ajabu kwa Fumo Liyongo kuhusishwa na tungo ambazo yeye mwenyewe hakuzitunga.

Maulama kadhaa wamejaribu kuzikusanya tungo hizi. Maulama hawa ni pamoja na: Edward Steere, William Taylor, Ernst Damman, Ahmad Nabahany na Ahmad Nassir. Pia, kuna maulama wengine wengi ambao wamejaribu kuzifasiri tungo hizi nao ni kama vile: Jan Knappert, Lyndon Harries, Mugyabuso Mulokozi, Miehe na wenzake (2004), Mutiso (1990), wakiwemo maulama wengine wengi; pasi na kumsahau maulama wa kazi hii.

Miehe na wenzake (2004) wamekusanya tungo mbalimbali (mashairi na nyimbo), zinazodaiwa kuwa zilitungwa na Liyongo na kuziweka pamoja kwenye kitabu. Ama kwa hakika, hili ni jaribio mufti la kuweza kuwapa wasomi wa sasa na hata wale wa baadaye hazina wanayoweza kuirejelea wanaponuia kushughulikia tungo za Liyongo. Tungo hizi ni pamoja na: *Utumbuizo wa dhiki*, *Utumbuizo wa kikowa*, *Utumbuizo wa Liyongo hamsini*, *Utumbuizo wa kumwongoa mtoto*, *Utumbuizo wa kumwawia Liyongo*, *Utumbuizo wa Uta*, *Utumbuizo wa Ndoto*, *Utumbuizo wa mayi*, *Utumbuizo wa uchi na Embekungu*, *Natani niliye*, *Gungu la mnara mp'ambe*, *Utendi wa Mwana*

Manga, Utumbuizo wa Mwana Mnazi, Utumbuizo wa mkoma, Utumbuizo wa wasiya wa kuolewa na Utumbuizo wa kujisifu. Tungo hizi ni muhimu sana katika kuichanganua historia ya Waswahili katika kipindi ambacho Fumo Liyongo alipata kuishi. Licha ya hayo, uchambuzi wa tungo hizi unatupa taswira nzuri kuhusiana na hali ya lugha ya wakati huo.

Kusanyiko hili lilikuwa tokeo la warsha zilizofanyika huko Bayreuth, Ujerumani katika miezi ya Juni / Julai 2003 na Machi / Aprili 2004. Mashairi haya yalitolewa kutoka kwenye kazi za awali zilizoandikwa na maulama kama vile: Hichens, Steere, Harries, Knappert miongoni maulama wengine. Baadhi ya mashairi haya yalitolewa kwenye miswada iliyokuwa imehifadhiwa kwenye hifadhi ya nyaraka ya SOAS, London; Maktaba ya Taasisi ya Masomo ya Kiafrika na Kiasia katika Chuo Kikuu cha Hamburg; Maktaba ya Umma ya Berlin; na maktaba ya umma na ile ya Chuo Kikuu huko Hamburg. Mashairi haya yamepewa vichwa mbalimbali ili kuyatambulisha au kuyatenganisha moja na jingine. Hata hivyo, hivi sivyo vichwa vilivyokuwa vimepewa mashairi haya. Si ajabu kwamba ushairi mmoja unatajwa kwa vichwa tofauti na maulama tofauti. Kwa mfano, *Utumbuizo wa Dhiki* ulio katika Mieke na wenzake (2004:34) unarejelewa na maulama wengi kama *Wimbo wa kijakazi Saada*.

Utungo mwingine ambao baadhi ya mishororo ya beti zake inadaiwa kuwa ilitungwa na Fumo Liyongo na ambao Mieke na wenzake (2004) hawajauonyesha kama utungo mmojawapo alioutunga Liyongo ni *Takhmisa ya Liyongo*. Takhmisa hii inaonyesha baadhi ya sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na hasa msimamo wake juu ya maadui zake ikiwemo utetezi wa cheo. Steere (1870) anaurejelea utungo huu kama *Mashairi ya Liyongo* (uk.455-471). Idadi ya beti katika utungo huu ni ishirini na sita. Harries (1962:188-192) ametuonyesha beti kumi na mbili tu za utungo huu. Hakuna ushahidi wa kutosha unaothibitisha kuwa Liyongo ndiye aliyetunga takhmisa hii. Baada ya kuisoma kwa makini, tulipata kwamba ushairi huu umetungwa kwa nafsi mbili - nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu.

Kwa mujibu wa Harries (1962:187), takhmisa huwa na mishororo mitano ambapo mtunzi hutoa mishororo miwili ya mwisho kutoka katika ushairi wa mashairi wa awali

na kisha kuijumlisha na yake mitatu Hata hivyo, mtunzi huhakikisha kuwa kuna ukuruba au uwiano katika suala linalozungumziwa katika mishororo katika kila ubeti. Inadaiwa kuwa mishororo miwili ya mwisho katika *Takhmisa ya Liyongo* ilitungwa na Liyongo mwenyewe ilhali ile mitatu ya mwanzo ilitungwa na Saiyid Abdallah bin Nasir, mtunzi wa *Al-Inkishafi* kama inavyodhihirika katika ubeti wa 27 wa takhmisa hii:

**Na mwenyi kutunga mbaarifu yakwe isimu,
Ni Abdallah Muyuweni mumfahamu,
Ibun Ali bun Nasiri mwenyi makamu,
Farii ya Makka Shimukati leo Farimu,
Fungu la Muthari Mutalibu na Hashima.**

Inabainika kuwa, lugha iliyotumika (kwa mujibu wa uchakavu wake) katika mishororo mitatu ya kwanza ni tofauti na ile ya mishororo miwili ya mwisho. Mishororo hii ya mwisho ina msamiati chakavu zaidi kuliko ile mitatu ya kwanza. Kwa hiyo, ingawa hatuelezwi mtunzi wa mishororo miwili ya mwisho ni nani, tunakisia kuwa mishororo hii kutokana na uchakavu wa lugha yake huenda ikawa ilitungwa na Liyongo na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Tungo ambazo zimetungwa na waandishi wengine kumhusu Liyongo ni: *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Hadithi ya Liyongo*. Tungo hizi mbili zinatokana na ngano za Waswahili zilizopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kuna tofauti ndogo kati ya tungo hizi mbili. *Hadithi ya Liyongo* inamsawiri Liyongo kama mtu mbaya na sababu za kufanya hivi tayari tumezionyeshwa hapo awali. Hadithi hii ndiyo ya awali kabisa kuandikwa kumhusu Fumo Liyongo. *Utenzi wa Liyongo* kwa upande ule mwingine unamsawiri Liyongo kama shujaa na unaangazia hasa mzozo baina ya Liyongo na binamuye Daudi Mringwari. Mzozo huu ndio kiini cha kazi hizi mbili ingawa kuna vipengele vidogo vidogo vinavyotofautiana.

2.1.5 Muhtasari wa hadithi ya Liyongo kwa mujibu wa

Utenzi wa Fumo Liyongo

Liyongo anasawiriwa kama mtu mwenye kimo kirefu na mwenye nguvu sana. Wagalla wanatoka kule kwao na kufika katika dola ya Pate ili kufanya biashara pamoja na kumtazama Liyongo. Wanamwomba sultani wa Pate apate kumwita ili wapate

kumtazama Sultan anaridhia na kuwasifia Wagalla kumhusu Liyongo. Kwa wakati huu, Liyongo alikuwa anaishi na nduguze huko Shaka. Sultani anamtuma mjumbe kumpasha Liyongo habari na anapokea ujumbe huo, anakubali wito wa mfalme Anachukua siku mbili kufika Pate akiwa amebeba vyombo chungu nzima vikiwemo vyungu vya kupikia, mawe, kinu, na jiwe la kupanza kuti. Kwa kawaida, safari ya kutoka Shaka hadi Pate humchukua mtu wa kawaida siku nne. Anapofika pale mjini, anapuliza na kuzipasua panda tatu. Wagalla wanapomwona, wanamwajabia sana kwani ingawa wao walikuwa mashujaa wa mwituni, Liyongo hangemithilishwa nao kwa vile alikuwa jitu na kwa urefu walimfika magotini tu. Wanamwomba sultani ruhusa ya kumwoza mke ili aweze kuwazalia mtoto aliye kama yeye. Sultani na Liyongo wanakubali na Wagalla wanamchukua na kumpeleka mpaka kwao na kisha kumpa mke. Mkewe anachukua mimba na kisha kujifiingua mtoto mwanamume. Liyongo anachukua jukumu la kumlea na kumtunza kwa mapenzi na kwa hiyo kijana huyu anamlanda babake kimaumbile.

Sultani anajawa na fitina dhidi ya Liyongo kwa kuwa anadhania kuwa kutokana na sifa zake za kishujaa, atampokonya madaraka. Kwa hiyo, anaamua kumwangamiza. Liyongo anang'amua mpango huu na kutorokea mwituni ambako anaishi. Sultani anawaahidi Wasanye na Wadahalo (waloishi huko msituni) riale mia moja iwapo watamwangamiza Liyongo. Wanaridhia na kumwendea kwa urafiki na kisha kumwomba wale kikoa cha makoma. Kwa upande wake, Liyongo analikubali ombi lao. Kila mmoja anahitajika kupanda juu ya mkoma na kuyaangua makoma. Wakati zamu ya Liyongo inapofika, wanauzungea mkoma ambao ni mrefu zaidi ili wakati apandapo, wamfiime wote kwa pamoja. Liyongo anatambua mipango yao na anatumia weledi wake wa kutumia mishale na kuyaangusha makoma mengi mno. Wanastaajabu na kurudi kwa sultani kumfahamisha kuwa wameshindwa kumwangamiza.

Juhudi za sultani za kumporomosha Liyongo hazikomei mahali pale. Kwa vile Liyongo anapenda gungu na mwao, anawatuma Wasanye na Wadahalo kwenda kumfahamisha kuwa hakuna uadui tena na amelikwa katika hafla ya gungu na mwao ambayo ameandaa. Liyongo anakubali na hapo sultani anapata fursa ya kumkamata. Wakati wa hafla hiyo, Liyongo anakamatwa na askari wengi mno ambao wamejihami

)
na anatiwa gerezani Sultani anafanya uamuzi auawe lakini baadhi ya watu hawaoni sababu yake ya kuuawa kwa vile wanamwona kama silaha yao dhidi ya maadui zao. Hata hivyo, sultani anaona kuwa hana budi kuuawa na kwa hiyo anamtuma mjumbe wake kumuuliza kile anachokitaka kabla ya kifo chake. Liyongo anapendekeza kuwa anatamani kuandaliwa gungu na mwao na kwamba watu wote waalikwe (Jamii ya Waswahili inadai kuwa Liyongo ndiye mwasisi wa gungu na mwao na kwamba ni hidaya yake kwa jamii hii).

Kijakazi wake (Saada) anapompelekea chakula, wale askari ambao humlinda Liyongo huwa kila mara wanakula kile kizuri na kumbakishia makombo. Anapofika pale, anaambiwa na Liyongo kwa ushairi kwamba arudipo nyumbani amfahamishe mamake amtengenezee mkate wa wishwa na humo katikati atie tupa Ushairi huu ni maarufu na wasomi wameupa jina *Wimbo wa kijakazi Saada*. Miehe na wenzake (2004:34) wameupa jina *Utumbuizo wa Dhiki* nao ni kama ufuatao:

Utumbuizo wa Dhiki

**Kiyakazi Sada nakutuma huyatumika
Kamwambile mama ni muinga siyalimka
Afanye mkate pale kati tupa kaweka
Nikereze p'ingu mandakozi yakaniuka
Pano k'akunduwa mandakozi yuu karuka
Nit'at'ate k'uta na madari yakiukuka
Ningiye ondoni nitambae ja mwana nyoka
K'ateleze nde kama kozi k'atoroka
Yuu la k'onde jangwa pwani k'itiririka
Ningile muyini ningurume ja simba buka
Niwane na wawi wake na wana wawe mateka
Ayute adui waliyao wawe huteka
Suu ndio mwiya enda wima upate fika
Wala siliwaye moyo towa kuajizika
Nali mti pweke nimezee katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye kuwak'upuka
Nduu ali mame uwasiwe kwenda kiitika
Mwambiye apike tupa kati wishwa kaweka**

Mamake anafanya kama anavyoagizwa na Saada anapompelekea mkate huo, wale askari hawautamani bali wanamruhusu ampelekee. Liyongo anauvunja kwa siri na kuitoa ile tupa. Jambo hili linamfurahisha ghaya. Usiku unapofika na ngoma kurindima, Liyongo anaikereza minyororo aliyokuwa amefungwa nayo. Anafaulu na hatimaye

)
anatoka gerezani akiwa huria. Watu wanapomwona, wanakimbilia usalama kwa vile wanahofia maisha yao.

Liyongo anakimbilia hadi kule Shaka Baada ya jaribio la sultani la kumwangamiza Liyongo kuambulia panangwe, anaiona njia ambayo ni rahisi ni ile ya kumtumia mwanawe. Anamhadaa mwanawe kuwa atamwoza bintiye iwapo atafaulu kumshawishi babake amfunulie kile ambacho kinaweza kumwangamiza. Isitoshe, anapewa vyakula, mavazi na malazi mema na kisha anatoka kutekeleza jukumu lake. Anapofika nyumbani na kumuuliza babake kile ambacho kinaweza kumwangamiza, Liyongo anang'amua mara moja kuwa kijana wake ametumwa na maadui zake ambao wana azima ya kutaka kumwangamiza. Hata hivyo, anakubali kumfunulia siri kwa kumwambia kuwa yeye anaweza tu kufa baada ya kutiwa msumari wa shaba kitovuni mwake.

Baada ya kuipokea ile habari, yule kijana anaenda moja kwa moja hadi kwa sultani na kumpasha habari. Sultan anafurahi ghaya na kuamrisha msumari wa shaba kutengenezwa. Unapokuwa tayari kijana anapewa na kushauriwa aende amtie babake msumari huu kitovuni mwake. Akiwa njiani, kijana huyu anakosa utulivu kwani anafahamu bayana kuwa anayahatarisha maisha yake na yale ya babake.

Baada ya mwezi mmoja hivi, anafaulu kumtia babake msumari ule kwenye kitovu chake wakati amelala na kisha kutoka mbio hadi kwa sultani. Babake anapoamka, anachukua mshale na uta na kuelekea nje ya mji karibu na kisima. Huko, anapiga goti lake na kutia mshale wake kwenye uta tayari kufuma. Watu wanapomwona pale, wanaogopa kukaribia kwa vile wanadhani kuwa amekasirika. Isitoshe, wanakosa nafasi ya kuteka maji na hali hii inasababisha kuwepo kwa uhaba mkubwa wa maji kwani hata yale ambayo yapo msikitini yamekwisha. Wanamwita mamake ili apate kumbembeleza. Mamake anamtongolea nyimbo na mashairi lakini Liyongo habanduki kutoka katika hali ile. Baada ya siku kadhaa, jagina anaanguka na hapo watu wanang'amua kuwa ni mfu. Watu wengi wanahuzunika na kusikitika mno na baadaye wanaandaa mazishi na kumzika.

Kijana wa Liyongo anapotekeleza tendo la kumwangamiza babake, anamwendea sultani ili kupatiwa haki yake. Mambo yanamwendea mvange baada ya sultani kumkashifu kwa tendo ambalo amefanya kwani anamwona kama asiye kuwa na imani. Anamfukuzilia mbali baada ya kumvua nguo zake za thamani ambazo alikuwa amemtunukia. Kijana huyu anakimbilia kwa jamaa zake (Wagalla) lakini hata huku hapati mapokezi mema kwani tayari wanafahamu kitendo ambacho ametenda. Mama yake vilevile hampendi na hata anamnyima chakula. Kutokana na majonzi yanayompata, anashikwa na maradhi na kisha kujifia.

2.2.0 Historia ya Wazulu

Historia kuhusiana na jamii ya Wazulu na pia kumhusu Shaka Zulu imeundwa kutokana na: kazi zilizochapishwa kuhusiana na maelezo ya watalii wa awali katika maeneo ya kusini mwa Afrika na pia yale ya wamisionari wa Kizungu; fasihi simulizi ya Wazulu; na pia kutokana na kazi za kihistoria na kiantropolojia zinazoelezea hali na vipindi mbalimbali katika jamii za janibu za kusini mwa Afrika.

Kama walivyo Waswahili, Wazulu ni Wabantu. Tulikwisha kuelezea hapo awali kwamba chimbuko la Wabantu ni kwenye maeneo ya katikati mwa bara la Afrika. Wazulu ni baadhi ya Wabantu walioelekea kusini na kukalia maeneo ya kusini mwa bara la Afrika na hasa katika eneo la mashariki mwa upwa na Bahari ya Hindi. Wakati halisi wa uhamiaji hadi kwenye maeneo ya kusini mwa Afrika haujulikani kwa yakini lakini kwa jumla, inakisiwa kwamba ni takribani zaidi ya miaka elfu moja iliyopita (Were 1974:9). Kufikia karne ya kumi, Wabantu wachache walikuwa tayari wakiishi na walitapaka kwenye maeneo ya kusini mwa bara la Afrika. Hawakuhamia katika sehemu hii kwa wakati mmoja na kwa kundi moja bali waliwasili wakiwa kwenye vikundi vidogo vidogo na kwa nyakati tofauti tofauti.

Hapo awali kabisa - kabla ya Wabantu kufika - maeneo ya kusini mwa Afrika yalikuwa yakikaliwa na Wakhoisan (*Bushmen* na *Hottentots*). Haya yalikuwa makundi ya watu walioishi maisha sahili mno na shughuli zao za kimsingi za kiuchumi zilikuwa hasa uwindaji wa wanyama pori na nyika pamoja na uchumaji wa matunda na mboga na uzoaji wa asali miongoni mwa shughuli zingine ndogo ndogo tu. Walitumia vifaa sahili

kama vile, mifupa ya wanyama, mawe yaliyochongoka, vijiti vyenye ncha kali na mishale iliyokuwa na vyembe vyenye sumu katika shughuli zao. Tena, waliishi katika jamii ndogo ndogo za wawindaji ambazo zilimiliki maeneo tofauti tofauti. Kila jamii ilikuwa na eneo lake mahsusi ambalo ilifanyia shughuli zake na wanajamii walitambua bayana upeo wa maeneo yaliyokuwa yao. Jamii hizi zilikuwa zimetapakaa kote kote. Isitoshe, waliishi katika vibanda vya muda tu na kwenye mapango ambayo waliyarembesha kwa michoro ya wanyama, wanadamu na mandhari ya usasini.

Baada ya Wabantu kufika katika eneo hili, waliwapokonya Wakhoisan maeneo haya. Wabantu walikuwa wahunzi na walikuwa na zana za kivita na kilimo zilizokuwa stadi na zenye uwezo zaidi kuliko zile za wenyeji. Wakhoisan walisukumiwa mbali kutoka kwenye maeneo yaliyokuwa na rotuba na wakahamia sehemu za magharibi zilizokuwa duni kirotuba. Baadhi yao waliguria kwenye maeneo ya Jangwa la Kalahari lililo kwenye upande wa mashariki. Ama kwa hakika, majilio ya Wabantu kwenye janibu hizi yalivuruga kabisa mfumo asilia wa kijamii na kiuchumi wa Wakhoisan - walinyang'anywa maeneo yao ya usasi, baadhi yao wakauawa, jamaa wakatenganishwa na ikawalazimu kuhamia katika maeneo yasioafikiana na hali zao za kimaisha. Ingawa mahusiano baina ya Wabantu na Wakhoisan yalikuwa yenye uhasama, ndoa baina yao hazikuepukika. Kimaumbile, wanadamu wote duniani ni sawa na ashiki za kimapenzi walizokuwa nazo Wabantu ni kama zile walizokuwa nazo Wakhoisan. Kwa hiyo, baadhi ya wanawake wa Wakhoisan waliolewa na wanaume wa Wabantu ilhali wanaume wa Wakhoisan waliwaoa wanawake wa Wabantu. Hali kadhalika, Wabantu waliathiriwa kiisimu na jamii hii hivi kwamba walizichukua baadhi ya sauti zao zenye mwaliko (*click sounds*) kwenye fonolojia yao.

Tofauti na Wakhoisan, Wabantu walifuga ng'ombe waliotumika kama chakula na pia kulipia mahari. Vilevile, waliendeleza kilimo cha mtama na mahindi miongoni mwa mimea mingine kama ilivyokuwa desturi ya Wabantu. Kwa jumla, kilimo mseto kilifanikiwa kwa vile hali ya anga katika eneo hili ilikuwa shwari kwa shughuli za kilimo na ardhi ilikuwa yenye rotuba nyingi. Kunawiri kwa mazao ya kilimo kuliwafanya Wabantu kuongezeka kwa haraka sana katika idadi yao. Ongezeko hili pia lilichangiwa kwa kiasi fulani na mfumo wa ndoa wa Wabantu uliowaruhusu wanaume

kuoa zaidi ya mke mmoja. Ni kutokana na mabadiliko katika idadi ya watu ambapo taasisi za kijamii na kisiasa zilielekea kuwa changamano. Jamii kwa mfano, zilianza kugawanyika katika koo. Isitoshe, kulikuwa na haja ya kupanua maeneo yaliyotumika kwa shughuli za makazi na kilimo ili kukidhi mahitaji ya idadi hii kubwa ya watu iliyokuwa ikizagaa kila kukicha

Baada ya mapisi ya wakati, jamii ya Wabantu wa Afrika Kusini iligawanyika katika makundi matatu ya lugha (Makundi haya hayafai kuchukuliwa kama makundi ya kisiasa). Kundi la kwanza lilijumuisha Wazungumzaji wa lugha ya Kinguni. Awali, Wanguni walikalia eneo la Wazulu (Zululand) na Natal hadi kwenye mpaka wa jimbo la utawala wa kikoloni la Cape (Cape colony). Kwa sasa, Wanguni hukalia sehemu za Transvaal, Natal, Cape Province na Zululand. Baadhi ya makabila katika kundi hili ni pamoja na Wazulu, Wandebele, Waswazi na Waxhosa. Hawa wote huzungumza lahaja za lugha moja na kwa hiyo huelewana katika mazungumzo yao Kundi la pili linajumulisha: Watswana, ambao wengi wao huishi Botswana; Wasotho wa Kusini ambao huishi Lesotho; na Wasotho wa Kaskazini ambao huishi kwenye eneo la kati na kaskazini mwa jimbo la Transvaal. Kundi kuu la Wabantu wa Afrika Kusini huwakilishwa na Waherero na Waavambo. Makabila haya huishi katika maeneo ya kusini magharibi mwa Afrika kusini na kwa jumla hujulikana kama 'Wabantu wa Kusini Magharibi'. Makundi haya yote yameathiriwa na Wakhoisan waliowapata kwenye maeneo haya. Jambo hili ndilo huwafanya Wazungumzaji wa lugha za Kinguni kuwa na mwaliko sauti katika mfumo wa fonolojia yao kama zilivyo lugha za Wakhoisan (Were 1974:10-12).

Baada ya kutalii maenezi ya Wabantu wa Afrika Kusini, tutajikita katika kuangalia mfumo wa kijamii, kiutawala na kimahusiano katika jamii ya Wazulu. Wazulu waligawanyika katika makundi madogo madogo yaliyokalia maeneo tofauti tofauti na kila jamii ilitawaliwa na chifu. Chifu alikuwa na mamlaka na nguvu nyingi mno. Kadhalika, wanajamii walimchukulia kama ishara ya umoja katika kabila lao na pia kama kitovu cha uaminifii kwenye kabila hilo. Wanajamii wengine walifikia hadi katika hatua hata ya kumwabudu chifu kutokana na taadhima ambayo alikuwa ametunukiwa na jamii nzima. Aliwapa wanajamii uwezo wa kutumia sehemu fulani za

ardhi kwa shughuli za kilimo na malisho ya mifigo kwa muda fulani Hakukuwa na umiliki wa kudumu wa mtu mmoja wa eneo fulani la ardhi. Mfiimo wa mtu mmoja binafsi kumiliki au kujitwalia eneo fulani uliletwa baadaye na walowezi Ardhi yote ilikuwa mali ya umma. Isitoshe, chifii alifanya uamuzi wa kesi za rufaa zilizokuwa zikipelekwa kwake na mahakama ndogo zilizowajumlisha wazee. Tena, alikuwa na mamlaka ya kupokea kodi kutoka kwa wanajamii Utozaji wa kodi katika jamii yoyote ile ni jambo la kawaida. Kodi huiwezesha serikali (au mamlaka yoyote) ile kutekeleza majukumu yake ya kuwatumikia raia. Kwa jumla, chifu wa eneo fulani alikuwa kiongozi wa raia, mkuu wa vikosi vya kijeshi, mwamuzi wa kesi na mkuu wa kidini wa watu wake. AJiogopwa sana na kupewa hadhi aliyostahili na wanajamii

Chifii alisaidiwa kutekeleza majukumu yake na baraza la washauri kwa jina *induna*. Wanachama wa baraza hili waliteuliwa na chifu mwenyewe na walihitaji kuhifadhi siri zote za vikao vyao na chifii. Aidha, kulikuwa na *induna* mkuu. Jukumu la *induna* huyu lilikuwa ni kumfahamisha chifu kuhusiana na hali zote katika dola yake pamoja na kumripotia habari zozote za usaliti wa aina yoyote ile. Pia, alimwakilisha chifu katika vikao vya kisheria na kutoa amri kwa jina la chifu.

Baadhi ya masuala ya kijamii kama vile upashaji tohara kwa vijana ulifanywa chini ya uongozi wa chifu. Vikundi vya vijana wa umri fulani waliotahiriwa kwa wakati mmoja walijumuika kama kikosi kimoja cha kijeshi. Vikosi hivi vilihitajika kwa vile mitafaruku au mizozano ya kikabila ilikuwa imeanza kushamiri. Hata hivyo, hakukuwa na jeshi la kudumu (hakukuwa na jeshi lilikokuwa limetengwa na kupewa mafiinzo spesheli au lenye msonge wa madaraka) na iwapo maadui wangeshambulia, vijana hawa waliitwa ili kujaribu kuzima mashambulizi haya.

Visababishi vya magonjwa havikujulikana kwa yakini. Magonjwa yote katika jamii hizi za awali yalichukuliwa kama yaliyotokana na ushirikina au kero za wahenga. Ama kwa hakika, suala la ulozi ni suala ambalo liliogopewa na wanajamii kwa ujumla. Si jamii ya Wazulu tu bali katika jamii zote duniani Kulikuwepo na ibada za ufichuzi wa uchawi na wachawi. Hatima ya wote waliopatikana kuwa wamehusika katika kashfa hii yakiwemo pia makosa mengine ya jinai ilikuwa ni kifo[^]. Hali hii pia inapatikana katika

jamii nyingi duniani na hasa katika jamii za Kiafrika. Ngo'mbe wa waliohusika hatimaye walitwaliwa na chifu.

Maeneo mbalimbali yaliyokaliwa na makabila tofauti tofauti yalizidi kupanuka kutokana na ongezeko kubwa la watu. Wakati mwingine, shughuli za kabila moja zingehitilafiana na zile za kabila lingine jambo ambalo lingesababisha vita vya mara kwa mara baina ya makabila haya. Vita hivi vilikuwa kwa uchache na vilisababisha kuwepo kwa wizi wa ngo'mbe, utekaji wa maeneo ya malisho na hivyo kusababisha uhasama wa muda mfupi baina ya makabila husika. Mwanzo wa ngoma ni Iele.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na nane, idadi ya Wazulu na ile ya Wabantu wengine katika maeneo ya Afrika Kusini ilikuwa imeenda juu mno. Ukanda wa pwani ya mashariki uliokaliwa na Wazulu ulikuwa kwa kiasi kikubwa wenye mvua nyingi, ardhi yenye rotuba, nyasi iliyonawiri na mazao mazuri ya mtama, mahindi na malenge. Kama tulivyokwisha kuona, hii ni sababu mojawapo iliyosababisha kuwepo kwa nyongeza ya watu katika eneo hili - Kuwepo kwa lishe bora, hali nzuri ya anga katika eneo hili ukiwemo mfiimo wa ndoa wa Kibantu ni masuala muhimu na ya kimsingi yaliyochangia nyongeza kubwa kabisa ya watu. Omer-Cooper (1966: 25), anadai kuwa kuna ushahidi wa kuwepo kwa idadi kubwa ya watu katika maeneo ya Wazulu na hata eneo la Natal katika karne ya kumi na saba.

Ukanda uliokaliwa na Wazulu ulikuwa mdogo kwani ulikuwa baina ya genge na Bahari Hindi. Upanuzi wa eneo lililokaliwa na Wabantu ungeweza tu kutokea aidha katika upande wa kusini au kaskazini. Upanuzi katika maeneo ya kusini ulifikia hadi katika Mto Fish na upanuzi zaidi ungezua mtafaruku baina yao na makabila mengine. Hata hivyo, walifanya jaribio la upanuzi zaidi na hii ilisababisha vita vya mara kwa mara.

Kutokana na vita vya mara kwa mara, mfiimo wa kijeshi wa Wazulu na hata wa jamii zinginezo ulibadilika. Tofauti na kuwepo kwa vikosi vidogo vidogo vya vijana waliotiwa jandoni pamoja, kuliundwa majeshi makubwa ya kudumu yaliyoshirikisha vikosi mbalimbali. Vikosi hivi vilikuwa na jukumu la kutwaa kwa nguvu maeneo ya makabila jirani na hivyo kupanua himaya yao pamoja na kuwalinda wanajamii dhidi ya

kushambuliwa na maadui. Aidha, mfumo wa kiutawala ulibadilika na wakuu wa vikosi hivi wakawa ndio viongozi wa jamii pana - utawala wa kikabila wa machifu ulitupiliwa mbali. Misukosuko ilizidi kukithiri na kuathiri mataifa mengine ya karibu na yale ya mbali jambo ambalo lilisababisha kuwepo pia mabadiliko ya haraka ya kijamii na kiutawala katika mataifa hayo. Huu ukawa ndio mwanzo wa kipindi maarufu na kirefu cha vita vikali zaidi katika historia ya Afrika Kusini kwa jina *mfecane*.

2.2.1 *Mfecane*: Kipindi cha vita kilichomzua Shaka Zulu

Mfecane ni neno ambalo hutumika kurejelea kipindi kirefu cha mapigano baina ya jamii mbalimbali za Wabantu wa Afrika Kusini katika sehemu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa. Kipindi hiki ndicho kilichosababisha kuibuka kwa ufalme mpana wa Zulu. Ama kwa hakika, ni katika kipindi hiki ambapo mabadiliko makubwa mno katika mifiimo ya kiutawala, kijamii, kiuchumi pamoja na maenezi na magurio ya watu yalitokea. Isitoshe, wafalme na mashujaa wa kivita kama vile Shaka Zulu ambao waliacha kumbukumbu katika historia ya Afrika Kusini na ya ulimwengu mzima kwa jumla, walizuka katika kipindi hiki. Kwa mujibu wa Omer-Cooper (1966:2), migogoro kati ya makundi mbalimbali yaliyoibuka na yaliyokuwa yakizozana yalizidisha mabadiliko katika vipengele vyote vya maisha katika makundi haya. Baina ya mwaka 1818 na 1828, mabadiliko haya yalifikia upeo baada ya uundwaji wa ufalme mpana wa Zulu chini ya mfalme Shaka.

Mfumo wa kiutawala ulibadilika kabisa mwanzoni mwa *mfecane* Katika eneo lililokaliwa na Wanguni, makundi matatu makubwa yalizuka chini ya wafalme mbalimbali. Kundi la kwanza ni Ndwandwe ambalo liliongozwa na mfalme Zwide; la pili ni Ngwane, liliongozwa na Sobhuza; na la tatu ni Mthethwa lililoongozwa na Dingiswayo. Wazulu walikuwa jamii ndogo tu iliyokuwa chini ya kundi kubwa la Mthethwa. Makundi haya matatu yalikuwa mahasimu na kila moja lilitaka kuyaangusha yale mengine na kupanua himaya yake. Kuchipuka kwa makundi haya ya kisiasa kulifiingamana na mabadiliko ya kijeshi. Vikosi vya kivita vya kudumu viliundwa na kupewa mafunzo kabambe ya kijeshi. Mashambulizi ya mara kwa mara

yalifanywa baina ya milki hizi na yakaacha athari kubwa kwenye miundo msingi ya jamii hizi.

Dingiswayo ndiye aliyekuwa maarufii zaidi baina ya wafalme hawa watatu katika kipindi hiki. Mfalme huyu alikuwa mwana wa chifu wa kabila la Mthethwa. Tangu ujana wake, hakupendezwa na mbinu za uongozi za baba yake. Kwa hivyo, wakati mmoja, alifanya jaribio la kumuua babake akishirikiana na mmoja wa ndugu zake. Jaribio hili halikufanikiwa na ilimbidi atafute hifadhi miongoni mwa Waqwabe. Alirudi hapo baadaye na kupata kuwa babake alikuwa amefariki na nduguye alikuwa tayari ametwaa madaraka. Alifaulu kumwondoa nduguye kwa kutumia nguvu na kuchukua hatamu za uongozi. Kadhalika, ufanisi wake ulitokana na sababu kuwa alikuwa kipenzi cha watu na wafuasi wake walikuwa si haba. Baada ya muda kupita, alianzisha kimaksudi sera ya upanuzi wa milki yake kwa kuyafanya makabila yaliyokuwa jirani zake kuwa chini ya utawala wake. Kwa wakati huo, Wareno walikuwa wamefika katika Ghuba ya Delagoa na kwa vile Dingiswayo alitaka ushirika wa kibiashara na Wareno, alichukua nafasi hii kuzipata baadhi ya bidhaa kutoka Ulaya.

Azima kuu ya Dingiswayo ilikuwa ni kuyaweka maeneo yote yaliyomilikiwa na makabila mbalimbali chini ya himaya yake. Hali hii ilizua vita vikali zaidi baina yake na dola hizo zingine. Wafalme wale wengine wawili walikuwa pia na azima kama ile ya Dingiswayo na hali hii ikazua vita vya mara kwa mara na vikali zaidi kuwahi kutokea katika historia ya jamii za Afrika Kusini. Vita hivi vilikuwa na athari kubwa zaidi katika mfiimo wa kijamii, kiutawala na kiuchumi. Watu wengi na hasa wanaume waliuawa, wanawake na watoto wakatekwa, ng'ombe na mazao mengine mengi kutwaliwa, makabila madogo madogo 'kumezwa', watu wengi waliguria kwenye maeneo yaliyokuwa na usalama, sheria kali dhidi ya vikosi mbali mbali kuwekwa na mbinu na mikakati ainati ya kivita kuasisiwa. Aidha, ni kutokana na shamrashamra na misukosuko hii ambapo shujaa na mfalme wa Wazulu kwa jina Shaka Zulu alizuka

2.2.2 Historia ya Shaka Zulu

Shaka alizaliwa katika kipindi ambacho kilikuwa na misukosuko ya kivita katika jamii za Wabantu wa eneo lililokuwa mashariki mwa Afrika Kusini. Tarehe kamili ya

kuzaliwa kwake haijulikani kwa yakini lakini maulama wengi wanakisia kuwa alizaliwa mwishoni mwa karne ya kumi na nane Ritter (1979: xvi) anadai kuwa Shaka alikopolewa mnamo mwaka wa 1787 (taz. pia, Roberts 1974:34), ilhali Masizi Kunene anadai kwamba Shaka alikopolewa mnamo mwaka wa 1795. Kwa vile historia kumhusu Shaka imeundwa kutokana na masimulizi yaliyopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine yakiwemo maandishi ya awali yaliyoandikwa na makaburu, tarehe halisi ya kuzaliwa kwake haina budi kuhitilafiana ingawa kwa kiwango kidogo tu. Babake kwa jina Senzangakhona ndiye aliyekuwa mtawala (chifu) wa Wazulu katika kipindi hiki. Mamake kwa jina Nandi naye alikuwa ametoka katika kabila jirani la Abasema-Langeni.

Nandi alitunga mimba ya Shaka kabla yeye na Senzangakhona kufunga ndoa. Wakati jamaa yake Nandi walimtuma mjumbe kumfahamisha Senzangakhona kuwa Nandi alikuwa mjamzito, aliambiwa kuwa hilo lilikuwa jambo ambalo ni muhali kufanyika na kwamba Nandi alikuwa akiugua *I-tshaka* (Omer-Cooper 1966: 29). Huu ni ugonjwa ambao huathiri matumbo na unaweza ukamfanya mwanamke kuwa wazimu na pia kukatiza hedhi yake. Kinyume na porojo hizi, Nandi hatimaye alijifiingua kijitoto (Shaka) na kwa hiyo madai kwamba Senzangakhona hakuwa mshirika yalitupiliwa mbali Ni kutokana na jina la ugonjwa uliodhaniwa (*I-tshaka*) ambapo Shaka alipata jina lake. Baadaye, Senzangakhona alimchukua Nandi kuwa mkewe.

Ingawa Nandi na Senzangakhona hawakuishi kwa amani kutokana na shutuma na wivu wa Mkhaba (mke wa pili wa Senzangakhona) na Mkhabayi (shangaziye Shaka) dhidi ya Nandi na Shaka, Nandi alitunga mimba nyingine na akajifiingua mtoto wa kike kwa jina Nomchoba. Kwa hiyo, Shaka akawa na dada ambaye alimpenda sana Nafsi na hamaki kali za Nandi hazingemruhusu kuendelea kuishi katika boma la Senzangakhona - hulka yake haingemfanya kuwa mwanamke mtiifu na mnyenyekevu kwa bwanake. Kwa vile alitokana na ukoo bora, alijiona kama mwakilishi wa ukoo wake mahali popote pale na kwa hiyo alistahili kupewa heshima na mwanamume yeyote yule katika jamii.

Tofauti baina ya Nandi na mumewe zilimfanya hatimaye kugura na kutafuta hifadhi kwa jamaa zake wa abasemaLangeni. AJigura pamoja na Shaka na Nomchoba Kugura huku kulikuwa ni chanzo cha 'safari ya kishujaa' iliyomwanda Shaka kukabiliana na ugumu wa maisha na kuinuka hadi katika ngazi za juu. Huu ulikuwa tu mwanzo wa madhila yaliyompata Shaka jambo ambalo lilimfanya Shaka kuwa na kero na machungu katika nafsi yake. M. Kunene (1979: xvi) anadai kwamba, si ile hali ya kumkosa baba iliyomfanya kuwa na machungu lakini ni ule mzozo mkali uliotokea baina ya wazazi wake. Machungu haya yalizidi alipotaniwa na watoto wengine huko uhamishoni kuwa hakuwa na baba.

Kuhamia kwa Nandi hadi kwa abasemaLangeni kulifanya vikosi vya Senzangakhona kuzua vita na jamaa hii, jambo ambalo lilisababisha Nandi kuchukiwa na kuhamia kwingine. Nandi hakuchoka kuhama kutoka kwa jamaa moja hadi nyingine. Jamaa zake takribani wote walikuwa na uhasama naye na kwa vile hangeweza kuvumilia uhasama huu, yeye pamoja na wanawe walienda kuishi kwa Waqwabe waliokuwa wenye nasaba moja na Wazulu. Huku, Nandi alipata kuolewa tena na mwana wa mfalme kwa jina Ngendeyana. Ni kutokana na ndoa hii ambapo kakake Shaka kwa jina Ngwadi alizaliwa.

Katika ujana wake, Shaka alikuwa mwenye nguvu na mkakamavu na jambo hili lilimwezesha kukomesha kero kutoka kwa vijana waliomtania pamoja na utani kutoka kwa baadhi ya jamaa zake. Hapo baadaye, aliamua kwenda hadi katika kitala cha Mthethwa ili kusajiliwa kama mkufunzi wa kijeshi. Katika mafunzo yake, alijizatiti vilivyo jambo ambalo lilimfanya Dingiswayo (mfalme wa dola ya Mthethwa) kumtambua. Isitoshe, alijitokeza kama kijana mwenye hekima na mkakamavu na muda si muda, Dingiswayo akampa mamlaka ya kukiongoza kikosi kimoja cha kijeshi kwa jina izeChwe. Akiwa kama mkuu wa kikosi hiki, aliasisi na kuratibu mbinu maridhawa na kabambe za kijeshi zilizomwezesha kutambulikana na kuinuka katika wadhifa wake. Aliasisi matumizi ya mikuki mifupi (*assegai*) tofauti na mikuki mirefu iliyokuwa ikirushiwa adui kutoka mbali. Mkuki huu mfupi uliwawezesha wanajeshi wake kumkabili adui sako kwa bako. Aidha, kila mwanajeshi alitakiwa kurudi nyumbani na mkuki wake na hangeuachilia kamwe ila pale ambapo ndimi za mauti zingemnyemelea

akiwa vitani (kutokana na shambulio kali la adui). Isitoshe, hapo awali, vikosi vya kijeshi vilienda vitani vikiwa vimevaa makubadhi Shaka aliiona hali hii kama iliyopunguza kasi ya kumkimbiza na kumfikia adui na kwa hiyo, akashauri kuwa haifai kamwe wanajeshi kuingia kwenye uga wa vita wakiwa wamevalia makubadhi Matokeo ya mbinu hii ni kwamba, wanajeshi wake walikuwa wepesi mno jambo ambalo liliwawezesha kuwapata adui (waliokuwa wanayaburura makubadhi yao) kwa urahisi na kisha kuwaangamiza. Kando na mbinu zingine za kivita alizoziyasi, Shaka alipigania kuwepo kwa mamlaka imara ya kiutawala yaliyounganisha sio tu vikosi mbalimbali vya kijeshi bali pia wanajamii wote kwa jumla. Kutokana na mbinu na maarifa yake ya hali ya juu, umaarufii wa Shaka ulizidi kuenea na watu wakampa lakabu ya 'shujaa wa Dingiswayo' (Omer-Cooper khj:30).

Baada ya Senzangakhona kufa - alikufa Shaka akiwa bado chini ya utawala wa Dingiswayo - Sigujana, aliyekuwa ndugu wa kambo wa Shaka, alichukua hatamu za uongozi. Shaka hakupendezwa na jambo hili kwani alijiona kuwa ndiye aliyekuwa mrithi halali. Kwa vile Dingiswayo alitaka kuwashirikisha Wazulu katika kampeni zake dhidi ya maadui zake (kama vile Zwide wa Ndwandwe na Phungashe wa taifa la Buthelezi), alimruhusu Shaka kwenda na kikosi chake cha izeChwe ili kuyatwaa mamlaka na kuwaongoza Wazulu. Katika msukosuko huu, Sigujana aliuawa na Shaka akatamalaki. Baada ya kipindi kifupi tu, Shaka kama mfalme, alianza kufanya mabadiliko makubwa kabisa ya kiutawala. Alikuwa na nafasi nzuri ya kuwaunganisha Wazulu wote na kupanua milki yake kwa kutumia mbinu na mikakati maridhawa ya kijeshi aliyoiyasi, jambo ambalo hatimaye alifaulu.

Kwa wakati huu, mfalme Zwide wa Ndwandwe alikuwa tayari amempiga vita Sobhuza (mfalme wa Ngwane) na kutwaa himaya yake⁷. Hakusitia hapo. Alimshambulia Dingiswayo katika mapigano makali na akafanikiwa kumteka. Alikikata kichwa chake na kukitumia kuipambia nyumba ya mama yake (mamake Zwide) kama ilivyokuwa desturi yake. Baada ya mfalme wao kuuawa, jeshi la Mthethwa lilitawanyika Azima ya Zwide kwa sasa ilikuwa ni kutwaa himaya yote ya Mthethwa ikiwemo pia ile la Wazulu. Juhudi zake hazikufanikiwa kwa vile Shaka pia alikuwa na azima ya kumwangusha Zwide na kuwaunganisha Wazulu wote yakiwemo makabila mengine madogo madogo na kuyaweka chini ya himaya yake.

Baada ya ufalme wa Mthethwa kuporomoka, mfalme Shaka ajiyaunganisha kwa haraka makabila madogo madogo na kuyaweka chini ya ufalme wake Isitoshe, aliviunganisha vikosi vidogo vidogo na kuliunda jeshi moja kubwa la kudumu pamoja na kuratibu mbinu mpya za kijeshi, ili kuweza kumkabili Zwide miongoni mwa maadui wengine Kulikuwepo na vita vya mara kwa mara baina ya vikosi vya Shaka na vile vya Zwide kila kimojawapo kikiwa na lengo la kukiangamiza kingine. Katika mwaka wa 1818, kulikuwepo na vita vikali zaidi katika historia ya *mfecane* kati ya vikosi vya Shaka na vile vya Zwide. Zwide alikuwa ameliamrisha jeshi lake lote kwenda kuliteka eneo lote la Wazulu pamoja na kuutwaa ufalme wao.

Shaka alitumia ujuzi wake wa kivita wa miaka mingi kuliangamiza jeshi hili. Baada ya majeshi haya kuingia eneo la Wazulu, Shaka aliwaamuru watu wake wote yakiwemo majeshi kuondoka ili kujifanya kana kwamba walikuwa wakimhepa Zwide. Walibeba vyakula vyote ikiwemo mifiigo yao. Wanajeshi wa Zwide walipozidi kuwafuata ndivyo njaa ilivyozidi kuwakaba kwa kuwa hawakuwa wamebeba hifadhi ya vyakula. Baada ya siku kadhaa, wanajeshi wa Zwide walikuwa dhaifii sana na hapo Shaka akaamuru vikosi vyake kugeuka mara moja na kuwakabili. Vikosi vya Shaka vilivishambulia vilivyo vikosi vya Zwide na kuiacha miili mingi ya wanajeshi wake ikiwa imetapakaa katika uga wa vita. Wanajeshi wa Zwide walioponyoka ulimbo huu walikuwa wachache mno na haikuwa rahisi kwa Zwide kuweza kuwaunganisha tena.

Jeshi la Zwide liliposhindwa na lile la Shaka, Zwide mwenyewe hakuwa na lingine ila kukimbilia uhamishoni. Katika vita vya mara kwa mara baina ya majeshi ya Zwide na yale ya Shaka, wana wengi wa Zwide waliuawa vitani. Nomahlanjana ambaye angerithi madaraka baada ya babake pia aliuawa. Wana wengine wa Zwide waliouawa ni pamoja na: Nobengula, Mphepha, Ngobe, Ngabeni, Sixholoba na Dalingubo. Kwa sasa, mfalme Shaka hakuwa na upinzani mkali na kwa hiyo aliweza kuyaunganisha makabila mengi mno na kuunda ufalme mmoja na mkubwa kabisa wa Wazulu. Waaidha, kama mfalme na shujaa wa Wazulu, aliweka mikakati na taratibu mpya katika mfumo wa utamaduni, utawala, jamii na itkisadi ambao uliendelea kudhihirika na kuendelezwa na watawala wengine hata baada ya mauko yake.

Katika maisha yake, Shaka hakuwahi kuoa Aidha, wanajeshi wake pia hawakupata kuoa ila pale tu alipowapatia ruhusa kufanya vile. Suala hili ndilo lililomfanya kuzozana mara kwa mara na mamake. Mamake alimshauri kila mara aoe, ili apate mjukuu lakini Shaka aliyapuuza mawaidha haya, kwani alijiona kama aliye mzalendo kamili na alikuwa na jukumu kuu la kuwahudumia Wazulu - kuwaunganisha na kujitoa mhanga kuwatumikia. Hata hivyo, alikuwa na vimada walioituliza ashiki yake ya kiume. Wale waliofanya mapenzi naye walichukua tahadhari ya juu sana ili wasije wakatunga mimba kwani kama wangalifanya hivyo, basi mimba hiyo ingalitumbuliwa kadamnasi ya watu kwa kutumia mkuki - mama na kijusi chake wanguawa

Hata baada ya ufalme wa Zwide kushindwa na Shaka kuendelea na mikakati yake ya kuwaunganisha na kuleta amani katika maeneo yote ya Wazulu, makabila madogo madogo kama vile Wachunu na Wathembu waliendelea kutishia umoja huu. Ingawa vikosi vya shaka viliweza kuyakomesha makabila haya ambayo mara kwa mara yalipotelea msituni, mashambulio yao wakati mwingine yalimwacha Shaka katika lindi la huzuni. Mgobhozi, rafiki wa karibu sana wa Shaka, kwa mfano, aliuawa katika vita baina ya vikosi vya Sikhunyana na vile vya Shaka. Jambo hili lilimwacha Shaka akiwa na huzuni nyingi mno kwa vile alikuwa amempoteza mwandani na mshiriki wa karibu sana katika vita.

Wakati Shaka alikuwa akitawala eneo pana la Wazulu, makaburu tayari walikuwa wamewasili katika pwani ya Afrika Kusini. Shaka mwenyewe alitumia mbinu za kidiplomasia ili kuweza kuwadhibiti. Ikumbukwe kwamba makaburu hawa walimiliki bastola ambazo zilikuwa zenye uwezo zaidi kuliko mikuki mifupi waliyoitumia Wazulu. Shaka alifanya urafiki nao ingawa kwa tahadhari sana. Kila mara alituma wajumbe (hata hadi huko Uingereza, kwa mfalme George) ili kupata kuelewa mienendo ya walowezi hawa. Wakati mwingine, aliwashirikisha walowezi hawa katika vita dhidi ya maadui zao na hatimaye akawapa kibali cha kumiliki ardhi iliyokuwa mkabala na upwa wa Bahari ya Hindi. Walowezi hawa walikuwa wenye manufaa kwa Wazulu kwa vile walikuwa na dawa zenye nguvu na za kisasa za kutibu magonjwa vikiwemo vidonda. Wakati mmoja, Shaka alipopata jeraha kwenye mkono kutokana na shambulio mojawapo la mpango wa usaliti, alitibiwa kwa dawa hizi na kwa hiyo

akaajabia kiwango cha ujuzi wa Wazungu hawa. Shaka mwenyewe aliamini katika nguvu za mababu waliokufa katika heri na shari. Ili kuweza kufuatilia mienendo ya walowezi hawa na vilevile kutokana na tahadhari dhidi ya maadui zake - wasaliti waliokuwa wakimpangia njama kila kukicha - Shaka aliyahamisha makao yake makuu kutoka Bulawayo hadi Dukuza.

Nandi alipougua, Shaka alifanya kila jitihada kuona kuwa mamake amepata afua Aliwashirikisha hata makaburu katika kuipata dawa ya kumtibu lakini pia nao hawakufanikiwa. Hatimaye, Nandi alijifia. Kifo cha Nandi kilikuwa pigo kubwa sana katika maisha ya Shaka na hata katika maisha ya Wazulu wote. Ili kuomboleza pamoja na shaka na pia kuipa heshima jamaa ya kifalme ya shujaa wao, Wazulu walijadili na kukubaliana mbinu ambazo wangetumia katika kuomboleza (M. Kunene 1979:340). Walikubaliana kwamba wangetenga mwaka mzima kufanya maombolezi na katika mwaka huu, hakukuwa na ulimaji wala upandaji wa mashamba; ng'ombe wote walitakiwa wasikamuliwe maziwa kote katika nchi ya Wazulu; mwanamume yeyote hakuruhusiwa na liwe liwalo kujamiiana na mkewe; wapenzi hawakuruhusiwa kutembeleana; na mwisho, mwanamke yeyote yule hakutakikana kuvaa mapambo (ya kujirembesha) katika mwaka huo. Amri hizi zote zilisambazwa kote katika nchi ya Wazulu na watu wengi walizikubali. Kipindi cha maombelezi kilipozidi kuendelea, matatizo yalizidi kuenea katika maeneo ya Wazulu kwa vile chakula kilichokuwa mashambani na hata maghalani kiliendelea kuwa haba. Ilikuwa kana kwamba kulikuwa na ukame. Ng'ombe na mbuzi ikiwemo mifugo mingine ilikonda na kudhoofika kiafya: baadhi ya watu waliwadhulumu wengine kwa kuwachomea miji na makazi; wasikwao wakawa wanazurura ovyoovyo kama wanyama wa pori; wizi ukaongozeka Aidha, udhaifu na kutengana kwa watu vikiwemo vikosi - katika harakati za kutafiita vyakula - kulihatarisha usalama wa Wazulu. Isitoshe, maadui wa Shaka na hasa nduguze (Mhlangana na Dingane) kwa ushirikiano wa shangazi yao (Mkhabayi) waliuonea wivu utawala wa Shaka na walichukua nafasi hii kuendeleza kampeni za shutuma dhidi yake. Waliandaa mikutano mingi ya siri na kujadili maanguko ya utawala wa Shaka. Tena, walieneza uvumi kwa watu kwamba Shaka ndiye aliyekuwa amemua mamaye. Baada ya maombolezi kufikia hatima, Shaka aliandaa karamu ya kuirudia hali ya kawaida. Kwa mujibu wa Ritter (1955:363), karamu hii iliandaliwa

mnamo tarehe 7 Septemba 1828 ambapo Shaka alitangaza hatima ya mwaka uliokuwa umetengwa ili kuomboleza kifo cha mamake.

Mkhabayi aliwachochea Dingane na Mhlangana wamwangamize Shaka na kutwaa uongozi. Kwa wakati huo, Mbopha aliyekuwa mjumbe 'mwaminifu' na wa karibu mno alikuwa ameungana nao na wote walikula yamini pamoja kumwangamiza mfalme wao. Walifanya majaribio mengi ya kumwangamiza lakini hawakufaulu. Walisusia kwenda kwenye uga wa vita kwa madai kwamba walikuwa wakiugua. Walifanya mambo yote haya kimaksudi wakiwa na lengo la kuidhoofisha mikakati ya kivita iliyoratibiwa na Shaka. Katika harakati zake, Mkhabayi alimwendea mmoja wa wapenzi wanawake wa mfalme waliokuwa wakiishi kwenye boma la kifalme ili kumwangamiza mpwa wake (kwa kumchoma mkuki) lakini kutokana na uelewa wa Shaka, alianza kumdhania kwa vile alielewa fika wivu na mizozo mingi iliyokuwepo baina ya wanawake (wanawake kwa kawaida huoneana wivu na hili ni jambo lililopo hata katika jamii za kisasa). Jaribio hili halikufanikiwa. Jambo hili lilimfanya Shaka awahamishe watumishi wote wa kike waliokuwa wanafanya kazi kwenye nyumba ya kifalme hadi kwenye maeneo yaliyokuwa mbali na mji wa Dukuza.

Ufanisi wa mfalme Shaka ulizidi kuonewa kijicho. Kila mara, Mkhabayi aliwachochea Dingane na Mhlangana wamwangamize Shaka kwa mikono yao wenyewe badala ya kuwatumia watu wengine kufanya vile. Mahasimu hawa wanne walikuwa wamekula yamini kuwa ni lazima wangemwua Shaka. Siku moja, Shaka alituma ujumbe katika upande wa kaskazini kwenda kutafuta vyuma miongoni mwa bidhaa nyingine. Ujumbe huu ulikuwa umeongozwa na Nxazonke, mjombake Shaka. Wakati wa kurudi kwa ujumbe huu, Mbopha, mtumishi 'mwaminifu' wa Shaka ndiye alitakiwa kuandaa mapokezi ya ujumbe huu. Kama desturi, ujumbe huu ungekutana na Shaka ili upate kumpa ripoti. Mahasimu wa Shaka walikiona kikao hiki kama kilicho mwafaka katika kutimiza ashiki ya mioyo yao. Walipanga mipango maridhawa kwa siri na ambayo hatimaye ilikuja kufanikiwa.

Wakati ujumbe huu ulikuwa ukitoa ripoti, Mbopha alijitokeza na kujifanya kana kwamba amekasirika na kuropokwaropokwa maneno kwa sauti ya juu huku

akiwakashifu wale wajumbe. Hakukomea mahali pale. Aliinua mkuki wake na kuwatishia wale wajumbe. Jambo hili lilimshangaza sana Shaka kwa kuwa hakuwa amemwona Mbopha akiwa katika hali hiyo hapo kabla. Mbopha alifanya hivi kama njia ya kuyateka mawazo ya Shaka na hivyo kuwapa Dingane na Mhlangana nafasi ya kuliporomosha windo lao. Katika mtafaruku huu, Dingane na Mhlangana walijitokeza wakiwa na wafiiasi wao. Walikuwa wamejihami kwa mikuki mipya kabisa iliyokuwa imetiwa makali vilivyo. Ghafla, Shaka aling'amua njama alizokuwa amepangiwa. Alitaka kuuwahi mkuki wake lakini wakamwahi hapo kabla na wakamdunga kutoka pande zote. Damu ilimtoka kwa wingi na nyingine ikapitia hata kwenye mdomo. Shaka alipong'amua kuwa hatima ya mwili wake kuachana na roho ilikuwa imefika, alisema (taz. *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* uk. 425 na pia Ritter 1955:369):

Kwa hiyo ndugu zangu mnaniangamiza?

Ni nini nilichowatendea?

Hata pia wewe Mbopha, mwana wa Sithayi!

Mnafikiria mtatawala ufalme wa Zulu baada ya kifo changu?

La hashu, hamtatawala. Mbayuwayu (Wazungu) ndio watakaotawala.

(Tafsiri yangu)

Haya ndiyo maneno ya mwisho kabisa ambayo Shaka aliyanena kabla ya kuanguka na kuwa mfii. Waliendelea kumdunga mikuki hata baada ya yeye kufa kwani walidhani kuwa jagina huyu angeamka kwa ghadhabu na kuwashambulia vilivyo. Kilio kikubwa kilihanikiza kote katika jamii ya Wazulu kutokana na kifo cha mfalme na shujaa wao. Watu wengi waliamua kufika Dukuza ili wapate kujionea wenyewe kwani hawakuamini waliyoyasikia. Wanajeshi pia walishiriki katika kuomboleza kifo cha jemadari wao. Ritter (khj:368) anaeleza kuwa, kwa mujibu wa shajara ya Isaacs, Shaka aliuawa tarehe 22 Septemba 1828. Baadaye, mazishi yaliandaliwa na watu wengi kuhudhuria kumpa shujaa na mfalme wao mkono wa buriani.

Baada ya Shaka kuuawa, Dingane ndiye alichukua hatamu za uongozi wa jamii ya Wazulu. Kutokana na uchu wake wa kuwa mtawala wa pekee (asiye na upinzani), alipanga njama za kumwangamiza nduguye Mhlangana aliyemwona kuwa tisho kwake. Alifanikiwa katika kufanya hivyo. Hakukomea mahali hapo Pia, alipanga njama na kumwangamiza Mbopha aliyemwona kama msaliti ambaye angemsaliti kama alivyomsaliti nduguye Shaka.

2.3.0 Hitimisho

Maelezo tuliyoyatoa hapo juu kuhusiana na historia ya Fumo Liyongo na Shaka Zulu na ile ya jamii zao ni ya manufaa katika kuwaelewa kwa undani mashujaa hawa; kuelewa hali, mazingira na vipindi katika jamii zao vilivyowazua. Kama inavyodhihirika, kuna masuala chungu nzima ambayo tunaweza kuyaelezea kuhusu historia ya mashujaa hawa na ile ya jamii zao yakiwemo mazingira ya kijamii yaliyowazua. Tumeyaelezea yale muhimu na ya kijumla ambayo tuna imani kuwa ni msingi mzuri ambao unatusaidia kuwaelewa mashujaa hawa kwa kina. Vilevile, maelezo haya yatakuwa kielelezo kizuri katika kufafanulia masuala tutakayoyarejelea katika faslu ya tatu na ile ya nne.

TANBIHI

1. Shungwaya ni enco ambalo wanahistoria wanadai kuwa Wabantu wa mashariki waliishi baada ya kugura kutoka kitovu chao. Eneo hili linasawiriwa vizuri katika ramani 1 (taz. uk 163) ambayo tumcidondoa kutoka Allen (1993:78). Kwa mujibu wa Allen (khj:39), tamaduni nyingi za jamii za pwani zilizorekodiwa zaidi ya karne moja iliyopita zinaonyesha Shungwaya kama enco ambalo lilifahamika na watu wengi. Baadhi ya watu wanaojihusisha na Shungwaya ni pamoja na Waswahili. Wascgeju. Wapokomo na Mijikenda. Anacndelea kudai kuwa tamaduni za kale za watu hawa huyarejelea makabila mengine ambayo pia valihusishwa na Shungwaya. Makabila haya ni kama vile: Wasomali. Wakikuvu. Wameru. Watharaka. Wakamba. Wataita, Wapare. Wachagga. Washambaa, Wabondei. Wazaramo na Wagala. Eneo ambalo lilikaliwa na watu wa makabila haya hujumuisha kwa sasa nchi ya Somalia, enco lililoko mashariki mwa tawi la mashariki la Bonde la Ufa la Kenya na pia baadhi ya maeneo ya kaskazini mashariki mwa nchi ya Tanzania. Anaendelea kudokeza kuwa (uk.39), Shungwaya ilikuwepo kabla ya karne ya 9 B.K. na baadhi ya watu walikuwa wangali wanaikumbuka akilini mwao hata katika mwaka wa 1725 B.K.

2. Ibn Batuta alizaliwa huko Tangier katika mwaka wa 1304 B. K. na akafa katika mwaka wa 1377 B.K. Alitembelea nchi mbalimbali za Kiislamu na hususan zilizokuwa zimepakana na fuko za bahari. Alienda mara nne kuhiji huko Mecca na ni baada ya mojawapo wa safari hizi ambapo alitembelea pwani za Afrika Mashariki katika miaka ya thelathini kabla ya kuzuru upwa na kusini mwa eneo la Arabia na hatimaye India. Masimulizi ya Ibn Batuta kuhusu sehemu alizotembelea katika pwani za Afrika Mashariki yakiwemo mahusiano na watu wa pwani hizi yametolewa kwa lugha ya Kiingereza na Freeman-Grenville (1954:1-6) baada ya kuyafasiri kutoka lugha ya Kifaransa. Hata hivyo, masimulizi ya safari za Ibn Batuta katika sehemu kama vile Zeila, Mogadishu, Mombasa na Kilwa yalikuwa hapo awali kabisa yamechapishwa (mnamo mwaka wa 1863) katika hati za kiarabu kabla ya kutafsiriwa katika lugha ya kifaransa.

3. Tuliidondoa ramani hii kutoka katika makala ya J. Spencer Trimingham. 'Reflections on the Arab Geographers and the East African Coast,' ambayo hayakuwa na tarehe ya kuchapishwa wala hayakuonyesha mahala ilimochapishiwa.

4. Licha ya dini, Waarabu walileta mifiimo ya kiuchumi kama ile ya kwao (ya kitabaka). Biashara iliwafanya baadhi ya watu kujilimbikizia mali ilhali wengine ambao 'hawakubahatika' wakawa vibaraka (watumwa) wa mabwanyenye hawa. Mfumo huu wa kiuchumi wa kikabaila unadhihirika katika tenzi na ngano za Waswahili na asili yake ni Uarabuni. Katika *Al-Inkishafi*, tunapewa taswira ya mji wa Pate (kabla ya maanguko) ambapo mfumo huu unabainika (beti 34-43). Hebu tuonyeshe baadhi ya beti hizi:

34. Uwene wangapi watu wakwasi
w alo wakiwaa kama shamshi
wa muluku zana za adharusi
dhahabu na fedha wakhiziniye.

37. Nyumba zao mbake zikinawiri
kwa taa za kowa na za sufuri
masiku yakale kama nahari
haiba na jaha iwazingive.

42 Pindi walalapo kwa masindi/i
Wali na wakandi na wapepci
Na wake wapambe watumbuizi
Wakitumbuiza wasinyamae.

Isitoshe, mfumo huu unabainika katika *Utenzi wa Mwana Kuponu* (beti 15-20) pamoja na baadhi ya ngano za Waswahili (Steere 1870) miongoni mwa tungo zingine anuwai za kale.

Athari za Kiarabu hazikukomea mahali pale. Walileta pamoja nao mfumo wa kiutawala uliowapendelea wenye mali. Familia za mabwanvenye zilichukuliwa kuwa ndizo zilizokuwa koo bora zilizofaa kuwaongoza raia. Kwa hiyo, wadhifa wa sultani (mkuu wa mji) uliundwa. Ili sultani afanikishe utawala wake, mawaziri waliteuliwa, kukawekwa askari. magereza yakajengwa na vyombo vingine vya dola vikaundwa. Mfumo huu ulipatikana katika kila mji na unadhihirika katika tungo kama vile *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na ngano mbalimbali za Waswahili.

Mabadaliko ya kijamii hayana budi kuleta mabadiliko katika lugha. Hapo awali kabisa. Waswahili walizungumza Kingozi (Kiswahili cha zamani kabisa). Kutokana na maingiliano na lugha zingine za kigeni, kutengana kijiografia miongoni mwa visababishi vingine, lahaja mbalimbali zilizuka. Si ajabu kwamba lahaja hizi zimepewa majina kulingana na visiwa au mahali ambamo zinazungumzwa. Kuna lahaja za kaskazini na zile za kusini. Tofauti iliyopo katika lahaja hizi ipo kwenye kiwango cha fonolojia. Tofauti hii haiwafanyi Wazungumzaji wa lahaja mbalimbali kutoelewana katika mazungumzo yao. Lahaja za kaskazini ni pamoja na: Chimiini, Kibajuni, Kisiu, Kipate, Kiainu, Kimvita na Chichifimdi. Zile za kusini ni kama vile: Kivumba, Kimtang ata, Kipemba, Kihadimu, Kitumbatu, Kimakunduchi, Kiunguja, Kimafia na Kimgao.

Isitoshe, maingiliano na wageni na hasa Waarabu na Wareno yaliwafanya Waswahili kukopa inaneno mengi kutoka lugha za Kiarabu na Kireno miongoni mwa lugha zingine. Hali hii ndiyo huwafanya baadhi ya Wasomi kuchukulia Kiswahili kama lugha chotara (mkusanviko wa maneno ya Kiarabu na Kibantu) au kama iliyotokana na Kiarabu. Hata hivyo, msimamo wetu ni kwamba, Kiswahili cha awali kabisa (Kingozi) hakikutokana na Kiarabu. Kaida ya lugha ni kwamba, lugha huathiriana na hakuna lugha ambayo haikopi misamiati na miundo mingine kutoka lugha zingine.

Tangu jadi, Waswahili wamekuwa na fasihi yao iliyofungainana na mazingira yao ya kijamii. Kabla ya kuwepo kwa fasihi andishi, Waswahili walikuwa na fasihi simulizi ambayo ilijumuisha fani kama vile: methali, vitendawili, nyimbo, ushairi, ngano na vichekesho. Baadhi ya fani hizi zimekusanywa katika maandishi. Uchanganuzi wa kazi hizi hutuchorea taswira ya utamaduni wa Waswahili. Vipengele vya kitamaduni kama vile, uganga na ushiri, uvuvi, uwindaji, tohara, kilimo, utawala, ndoa na mapenzi,

biashara. vita, maadili. dini. sheria. ngoma na sherche zingine vinadhihirika. Wanyama wa mwituni kama vile simba, kima. sungura. paa. panya. fisi na nvoka; ndege mbalimbali wa angani: na wanyama wa majini waliopatikana katika janibu za Waswahili pia wamerejelewa. Aidha. tunasawiriwa mandhari ya maeneo mbalimbali yaliyokaliwa na jamii hii huku tukitajiwa aina ya mimca iliyokuwemo.

Athari za kigeni pia zinadhihirika katika fasihi ya Waswahili. Masuala vanayoihusu dmi ya Kiislamu yanajitokeza kwa wingi hasa katika tenzi ikiwemo mifumo ya kiutawala na kiuchumi kama tulivyokwisha kuona hapo awali. Isitoshe. Waswahili walitohoa baadhi ya ngano za Wahindi. Waarabu na Waajemi kama inavyodhihirika katika Steere (1870). Mifano ya ngano hizi ni kama vile: *Hekavya Kiohammadi Mtepetevu* (uk. 150-189), *Sultan Majinuni* (uk. 197-283) na *Kisa cha Kihindi* (uk.139-147).

Miji ya pwani ilivyoziidi kunawiri ndivyo ilivyoziidi kuvutia wageni wengi zaidi. Kutokana na ustawi wa miji hii na pia mandhari mazuri ya pwani, wageni wengine kama vile Wareno. katika karne ya kumi na tisa. waliteka baadhi ya miji kama vile Kilwa. Mombasa. Pate na Lamu. Jambo hili lilizua vita vilivyosababisha kuporomoka kwa uchumi na hatimaye maanguko makubwa ya miji hii Miji mingine kama Pate iligeuka na kuwa magofu kama inavvosawiriwa katika *Utenzi wa AI-In ki shaft*.

Wamishenari walipofika katika pwani ya Afrika Mashariki mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. walipiga marufuku biashara ya watumwa iliyokuwa inaendelezwa na Waarabu. Ufanisi wao ulitokana na sababu kuwa. walikuwa na manowari za kivita zilizokuwa na uwezo zaidi zikimithilishwa na zile za Waarabu. Hadithi kuhusiana na kukomeshwa kwa biashara ya utumwa imeelezwa kwa wcedi na James Juma Mbotela katika kitabu chake maarufu, *Uhuru wa Watumwa* kilichochapishwa mnamo mwaka wa 1934. Msimamizi wangu, Dkt. Ayman Al-Asar hakutosheka na maelezo niliyoyatoa; kwamba Waarabu walikuwa wakatili na kwamba Wazungu walifanya wema kwa kukomesha biashara ya watumwa. Swali ambalo alitaka tujiulize ni, ' Watumwa hawa walikwenda wapi?' Alikuwa na maoni kwamba. baada ya kutekwa, watumwa hawa walipelekwa Ulaya na Marekani. Ikumbukwe kuwa, mataifa haya yalihitaji wafanyikazi wengi kwa ajili ya ustawi wa viwanda vyao na kwa hiyo, walitumia biashara hii haramu iliyoendelezwa na Waarabu kuwapata Waafrika waliofanya kazi viwandani mwao. Baada ya Wazungu kufikia matawi ya juu ya ustawi wa kiviwanda kwa kutumia jasho la Waafrika, Wazungu wawa hawa walirudi hapo baadaye na kuizuia biashara hii haramu. Si ajabu kwamba kuna Waafrika wengi weusi wazaliwa na walio wenyeji wa huko Ulaya na Marekani. Hii ni ithibati ya kutosha kuwa, watumwa hawa waliishia kupelekwa katika maeneo haya. Kwa mujibu wa Dkt. Asar. msimamo wa dini ya Kiislamu kuhusiana na biashara ya watumwa uko wazi. Alidai kuwa. dini ya Kiislamu imeharamisha biashara hii tangu awali ya kushuka kwake kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Alishadidia kuwa. haifai kuchukuliwa kuwa Waarabu wote ni wabaya na kwamba ni baadhi tu ya Waarabu waovu wa enzi hizo walioshiriki katika biashara hii haramu. Licha ya mtazamo huu, ambao ni mzuri. msimamo wetu ni kuwa, Waafrika walitendewa unyama na ukatili kwa kutekwa. kupigwa na kufanviwa madhila ya kila nui.

5. Tumeona ni vema tuonyeshe utenzi huu kama kiambatanisho katika tasnifu hii. Sababu ni kuwa. tuliupata utenzi huu ukiwa katika hali ya mswada (mss 308), katika inaktaba ya Taasisi Ya Uingereza ya Afrika Mashariki na hatujawahi kuuona ukiwa umechapishwa mahali pengine popote.

6. Kwa mujibu wa Roberts (1974:28), janiii ya Wazulu ilikuwa na njia anuwai zilizotumiwa katika kuwaangamiza watuhumiwa wa makosa tofauti tofauti. Anadai kuwa. njia iliyotumiwa kuwaangamiza watuhumiwa hawa ilitegemea kiwango cha uhalifii waliokuwa wametenda. Waliokuwa na bahati walikufa kifo cha haraka; aidha. walisongonyolewa shingo zao na machakari mahiri waliokuwa wametengwa kwa shughuli hiyo, au kupigwa vichwani kwa kutumia rungu hadi kufa. Wale waliotuhumiwa kuwa *abaThakathi* (walozi), walikiona cha mtema kuni kabla ya roho zao kuachana na miili yao. Machakari waliwavuta hadi kwenye kiduta kilichokuwa kimetengwa kwa shughuli ya kuwaulia walozi hawa. Kisha, tendo la kuwaadhibu lilianza. Vikingi vyenye ncha kali ajabu vilipigiliwa kwa nguvu kwenye mikundu yao. Hatimaye, waliwaacha wakiwa wanatapatapa na kuchacharikachacharika kutokana na uchungu uliokithiri. Mwishoni. wahasiriwa hawa waliaga dunia na kisha kuliwa na fisi. Hafla ya kutekelezwa kwa adhabu hii ndiyo iliyokuwa ya kutisha zaidi katika jumla ya vipengele vyote katika maisha ya Wazulu. Roberts (ambaye ni Mzungu) anaendelea kudokeza kuwa. Shaka mwenyewe alitumia njia hii ili kuwaadhibu watuhumiwa na kwamba alifanva hivi ili kuwavutia wageni na kudhihirisha uwezo wake. Kama wahakiki. tunafaa kulichukulia suala hili kwa tahadhari kubwa. Tukumbuke kuwa, hawa ni mabeberu ambao kamwe hawakuthamini taasisi za jamii za Kiafrika au hata kuwathamini Waafrika wenyewe na kwamba walielezea masuala kuwahusu Waafrika kwa njia ambayo ilionyesha kuwa Waafrika walikuwa washenzi. Kwetu sisi, ingawa tunaewa fika kuwa walozi waliuawa kwa kikatili katika jamii nyingi za kale za Kiafrika. namna ya mauaji yaliyosawiriwa na Roberts yalikuwa kinyume kabisa na matarajio ya binadamu yeyote yule na kwa hiyo, kuna uwezekano kuwa maelezo haya yalikuwa yametiliwa chumvi ili kuzidi kudunisha ustaarabu wa Mwafrika.

6. Zwide alichochewa na mamake kwa jina Ntombazi kuyapiga vita mataifa mengine ili abaki kuwa aliye na mamlaka zaidi katika maeneo yote ya Wanguni. Ntombazi alikuwa mchawi gwiji na aliogopewa sana hata na wanawe. Aliyahifadhi mafuvu ya viongozi mashuhuri waliouawa katika vita kwenye jumba alilokuwa amelitenga kwa shughuli hiyo. Baadhi ya watu waliokuwa wameuawa na mafuvu yao kuhifadhiwa kwenye jumba hili ni kama vile: Mlotha wa Matshalini. Zayi na Ngudhubela ambaye alikuwa shujaa mmojawapo katika inaeneo ya Wanguni. Kutokana na uchochezi wa mamake. Zwide alizishambulia koo tulivu na zenye amani kama vile Matshalini. Aidha. alifanva uvamizi kote katika maeneo ya Wanguni jambo ambalo lilifanya aogopwe na makabila mengi. Zwide aliapa kumwangamiza Dingiswayo ili awe mfaline aliyekuwa mkuu na mashuhuri kabisa katika maeneo ya Wanguni. Hali hii ilifanva Dingiswayo kuyaweka majeshi yake katika hali ya tahadhari kila wakati.

FASLU YA TATU

SIFA ZA KISHUJAA ZA FUMO LIYONGO NA SHAKA ZULU

3.0 Utangulizi

Katika faslu hii, tutapambanua kwa sawia sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Tutaonyesha kiwango cha kufanana na pia kutofautiana kwa sifa zao za kishujaa. Kama ambavyo tumekwisha kudokeza, maelezo kumhusu Liyongo yako katika vipandevipande na yamekusanywa kutoka tamaduni za jamii mbalimbali za pwani Kwa hiyo licha ya kuurejelea *Utenzi wa Fumo Liyongo* na baadhi ya tungo zingine zilizotungwa na waandishi wengine kumhusu Liyongo, itatubidi turejeelee maelezo ya tamaduni mbalimbali na pia tungo ambazo anadaiwa kuwa alizitunga mwenyewe ili tupate sifa jumlishi za kishujaa kumhusu.

Maandishi kumhusu Shaka Zulu ni mengi mno na hayatofautiani sana baina ya waandishi. Shaka aliishi miaka ya baadaye kabisa akilinganishwa na Liyongo. Wazungu kama vile H. F. Fynn na F. G. Farewell, miongoni mwa Wazungu wengine, walikuwa tayari wamefika katika maeneo mbalimbali ya kusini mwa Afrika. Maelezo kumhusu yalikusanywa kwa urahisi na kuhifadhiwa katika maandishi. Kadhalika, kama vilivyo vitushi vya Liyongo, vitushi vya Shaka Zulu vimekitwa hadi sasa katika akili za jamii mbalimbali katika taifa la Afrika Kusini na hata ulimwenguni kwa jumla. Katika kuzisawiri sifa za kishujaa za Shaka, utenzi wa *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* utatufaa sana. Hata hivyo, tutarejeelea baadhi ya kazi zingine ambazo zimeandikwa kumhusu.

Tenzi ambazo huandikwa kuhusiana na mashujaa au tukio lingine lolote hufumbata na kusawiri kwa kina masuala muhimu ya kihistoria. Chiraghdin, Nabhany na Baruwa (1975:63) wanaeleza kuwa maudhui ya tenzi katika fasihi mbalimbali za ulimwengu ni kutukuza utaifa katika historia za jamii na pia kuwatukuza watu waliotenda vitendo vikubwa (mashujaa) katika historia hizo. Vansina (1985:53), anadokeza kuwa kufinywa na kupanuliwa katika ufafanuzi wa matukio pamoja na udondoshaji na nyongeza ya mambo katika tenzi ni jambo la kawaida. Anaendelea kusesitiza kwamba, tofauti kati ya matukio ya kihistoria na yale ya kifasihi tukirejeelea usawiri wa ploti, mandhari,

wahusika na mtiririko wa vitushi ni finyu mno. Ni kwa mintarafij ya maelezo haya tunaamini ya kuwa tenzi (*Utenzi wa Fumo Liyongo na Emperor Shaka Ihe Great: A Zulu Epic*) miongoni mwa tungo zingine zitatufaa katika kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu.

3.1 Ulinganishi: Sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu

3.1.0 Kuzuka kwa Mashujaa

Mashujaa kote duniani na hususan mashujaa wa kihistoria wa kijamii huwa hawazuki vivi hivi tu bali huzuka katika hali, kipindi na mazingira fulani maalum ya kijamii. Majagina huzuliwa na misukosuko au migogoro ambayo husheheni katika kipindi fulani cha jamii hiyo. Kwa hiyo, jagina huzuka ili kuikomboa jamii yake kutokana na ugumu fulani katika maisha ya jamii hiyo. Kama ambavyo tumekwisha kutaja, jamii ni mfumo ambao huwa na mahitaji mengi. Mahitaji haya huibua taasisi mbalimbali mojawapo ikiwa ni 'taasisi ya ushujaa' Taasisi hii ni muhimu sana katika kusawazisha hali zilizoenda mvange katika mfumo wa jamii. Jagina huzuka katika wakati mahsusi katika jamii yake na huishi hadi pale ambapo anatekeleza dhamira yake. Si ajabu kwamba jagina huwa hafi hadi pale atakapotekeleza dhima yake katika jamii Ni kutokana na sababu hii ambapo wanajamii katika jamii mbalimbali kote duniani humtazama shujaa wao kama hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mfano mzuri wa jagina wa hivi karibuni anayeweza kuchukuliwa kama hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ambaye ameingia katika kumbukumbu ya mashujaa wa kihistoria wa kijamii wa Kiafrika ni Dkt. John de Mabior Garang (1945-2005). Jagina huyu anaweza akawekwa katika kiwango sawa na Shaka Zulu na hata Fumo Liyongo. Alizuka ili kuikomboa sehemu ya kusini mwa Sudan iliyokuwa imetengwa na serikali ya Sudan kwa muda mrefu. Serikali hii ilitilia tu maanani maendeleo katika sehemu za kaskazini mwa Sudan. Kwa hiyo, kama walivyo mashujaa wengine, Garang alizuka ili kutimiza mahitaji fulani ya watu wake wa kusini mwa Sudan. Kwa hakika, alifaulu pakubwa katika kutimiza mahitaji haya na alifariki muda mfupi tu baada ya kutimiza dhamira yake¹.

Wengi wa mashujaa wa kijamii wa kihistoria na vilevile wale wa kidini walizuka aghalabu katika mazingira ambamo mna vita. Kwa mfano, Lwanda Magere, shujaa wa Wajaluo alizuka kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Walang'o. Ngano kumhusu imeelezwa kwa ustadi na Onyango-Ogutu na Roscoe (1974:143-148). Mashujaa wengine wa kijamii kama vile Shaka Zulu, Fumo Liyongo na Dedan Kimathi pia walizuka katika mazingira mlimokuwa na vita.

Tumeyasawiri kwa uwazi mazingira ya kijamii yaliyowazua Fumo Liyongo na Shaka Zulu katika faslu ya pili. Fumo Liyongo alizuka kutokana na misukosuko ya kivita iliyosababishwa na baadhi ya maadui wa Waswahili miongoni mwa jamii zingine za pwani. Vivyo hivyo, Shaka Zulu naye alizuka kutokana na kipindi kirefu cha vita (*mfecane*) kilichokuwepo katika nchi ya Afrika Kusini. (Rejelea sura ya pili ili kuipata taswira bayana ya mazingira, kipindi na hali zilizowazua mashujaa hawa).

3.1.1 Ubashiri wa kuzaliwa kwa jagina

Kuzaliwa kwa majagina wengi duniani mara nyingi huwa kumbashiriwa Mtabiri huelezea kuwa jagina ataibuka siku moja na kuiondolea jamii yake madhila ambayo yameisibu kwa muda mrefii. Mbashiri pia huhimiza wanajamii waendeleo kustahimili kwa kuwa mkombozi atakuja kuwaokoa siku moja. Tena, yeye huwafahamisha kuwa mkombozi huyu ataasisi ufalme ambao utakuwa mkubwa ajabu ukilinganishwa na falme zingine. Hali hii inadhihirika sana katika kuzaliwa kwa mashujaa wa kidini. Kuja kwa Mtume Isa (Yesu Kristo) kulitabiriwa na nabii kama vile Isaya (taz. *Isaiah* 1:14 kwenye *Biblia*) na hata malaika Jibrili (taz. *Luka Mtakatifu* 1:26-37 kwenye *Bihlia*). Vilevile, kuzaliwa kwa Samsoni (taz. *Kitabu cha Waamuzi* 13:3 kwenye *Biblia*) kulitabiriwa na malaika wa Mwenyezi Mungu.

Baada ya upekuzi wa kina wa maandishi ya kazi zinazohusishwa na Fumo Liyongo, tulipata kuwa hatuonyeshwi mahali popote ambapo kuzaliwa kwa Fumo Liyongo kulibashiriwa. Kwa upande mwingine, kuzaliwa kwa Shaka Zulu kama tunavyoelezwa katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* kulibashiriwa. Babu yake Shaka kwa jina Jama ndiye aliyepata kuwa na maono akiwa katika ndoto kumhusu shujaa mkuu

(Shaka) ambaye angezaliwa na kuunda ufalme mkubwa ajabu. Shaka analinganishwa na mto unaotiririka kwa kasi kuelekea ziwani Tunaeleza (uk. 2):

Tazama! Mashindano makali ya mito inayotiririka
Mto mmoja unameza ile mingine karibu na bahari
Na ktigeuka na **kuwa jito moja kubwa**
Linaloingia baharini kwa shangwe.
Na kuzua mawimbi makali... (Tafsiri Yangu)

Katika maelezo haya, mto mmoja unaomeza mito ile mingine ni taashira inayorejelea kuibuka kwa ufalme mkubwa wa Shaka ambao utazithibiti falme zingine na kuziunganisha na kuwa ufalme mmoja mkubwa (bahari). Jama alipomweleza Senzangakhona kuhusiana na maono hayo, Senzangakhona alikasirika sana na hata hapo baadaye (baada ya Shaka kuzaliwa), alipanga njama za kumwangamiza kwa vile alidhani kwamba Shaka angempoka ufalme wake. Hata hivyo, hakufaulu kumwangamiza.

Akifafanua kuhusu maisha ya utotoni ya Shaka Zulu, Roberts (1974:33) anadai kuwa, maisha ya Shaka yalisimuliwa kama ngano nyingine yoyote ile. Jambo hili linatokana na sababu kuwa, hadithi kuhusiana na kuzaliwa kwake, utotoni mwake na amali yake ya awali kabisa hutegemea fasihi simulizi ya jamii yake - hadithi hizi zimepitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi. Anaendelea kufafanua kuwa, hadithi hizi zimechukuliwa kama masimulizi ya visasili na visakale na huelezewa kwa lugha ya kishairi na kwamba maelezo yake huwa yamepambwa kwa hisia za kishujaa na kuvutia kama ilivyo katika masimulizi ya sanaa za jadi.

3.1.2 Jagina kwa kawaida huwa ni mwanamume

Majagina kote duniani aghalabu huwa wa kiume Ingawa wakati mwingine mwanamke fulani anaweza akarejelewa kama shujaa, huwa kwa jumla hana zile sifa bia za kishujaa kama walizo nazo wanaume ambao hurejelewa kama mashujaa (sifa za toka utabiri wa kuzaliwa kwao hadi mauko yao). Mwanamke kama huyu anaweza kuwa ametenda tendo moja la ujasiri lakini tendo hili halimpi kibali cha kuwa jagina. Ujasiri ni sifa mojawapo tu ya mashujaa. Sifa hii pia hupatikana hata kwa wanadamu wengine wa kawaida ambao huwa hawachukuliwi kuwa majagina Mashujaa wa kidini pia huwa ni wanaume. Kwa mfano, Yesu Kristo, Samsoni, Buddha, Mtume Muhammadi, na

wengine wengi ni wanaume. Kadhalika, waumini wa dini mbalimbali duniani humchukulia Mwenyezi Mungu (jagina wa majagina) kuwa mwanamume.

Tunapowarejelea mashujaa wa somo letu, tunapata kuwa hata nao pia ni wanaume. Katika kushadidia kuwa Fumo Liyongo ni mwanamume, *Utenzi wa Fumo Liyongo* unaeleza:

**6. Liyongo kitamakali
akabalighi riiali
akawa mtu wa kweli
haiba kaongeya.**

**13. Ni mwanamume swahihi
kama simba una zihi
usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya.**

**26. Liyongo akikabili
ndiya kenenda riiaii
alikuwenda siku mbili
na ya pili ni kungiya.**

Katika *Takhmisaya Liyongo*, Liyongo analinganishwa na simba ndume. Tunaelezwa:

**20.... Simba bora ndume watetea jaha na cheo;
Watetea jaha hatta mato yakafunama.**

Katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic*, mamake Shaka anamrejelea kama mwanawe wa kiume. Anasema (uk 22), "**Nilijua kuwa siku moja mwana wangu wa kiume [Shaka] atakua na kuzagaa kote duniani. Atainuka na kuwa juu ya viumbe wote waishio**" (Tafsiri Yangu). Isitoshe, katika kumsifii Shaka, Gendeyana (mojawapo wa jamaa ya Waqwabe) anamrejelea Shaka kama mwanamume mwenye nguvu na mkali. Anadokeza (uk 43), "**Shaka si mtu hivi hivi tu. Yeye ni mwanamume mkali na mwenye nguvu. Yeye hula akiwa ameishikilia silaha yake mkononi...**" (Tafsiri Yangu).

Kwa jumla, kama ambavyo tumeeleza, majagina takribani wote kote duniani huwa wa kiume. Lakini kwa nini iwe vile? Hali hii inatokana na dhana iliyo katika akili razini za wanadamu wote kwamba, mwanamume wakati wote yuko juu ya mwanamke na kwa hiyo, ukombozi (uongozi) ni sharti utokane na uongozwe na mwanamume. Isitoshe, wanawake duniani husawiriwa kama watu waoga na wadhaifu, tofauti na wanaume ambao hukabiliana na kustahimili masuala mazito katika jamii na hususan yale

yanayohusishwa na vita. Si ajabu watu wote wakiwemo wanawake husema, **Jikaze kiurne'**

3.1.3 Utoto na ujana wa jagina

Kwa kawaida, utoto na ujana wa jagina huwa hauelezwi kwa kina. Unaelezwa kijuujuu tu na huenda wakati mwingine usielezwe. Hata pale ambapo unaelezwa, wasanii au wanahistoria hujaribu kuunga kipengeee kimoja na kingine cha utoto na ujana wake wakiwa na lengo la kutoa taswira ya maisha yake toka utabiri wa kuzaliwa kwake hadi mauko yake. Wakati mwingi, maelezo haya huwa ya kumbabanya tu. Huenda wasimaizi maisha ya jagina ya utotoni au hata ya ujanani na wakati mwingi huishia kukisia tu. Lakini, ni kwa nini iwe hivyo? Kwa kawaida, jagina huzaliwa tu kama mtoto wa kawaida na kwa hiyo, huenda wanajamii wasing'amue kuwa mtoto fiilani ni jagina. Hata hivyo, baadhi ya wanajamii huing'amua vitushi visivyo vya kawaida (vya kiajabuajabu) vya jagina na hasa anapolinganishwa na vijana wengine.

Kazi zinazohusishwa na Fumo Liyongo zinatuelezea masuala machache mno kuhusu ujana wake. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, hatuelezwi kuhusu maisha ya utoto wala ya ujana wa Fumo Liyongo. Hatuelezwi kwa mfano, mazingira ya nyumbani kwao, uhusiano wake na vijana wengine, uhusiano wake na wazazi wake au wanajamii wengine akiwa mtoto, maeneo aliyotembelea akiwa kijana, hulka yake na matamanio yake. Tunatajiwa tu kuwa Liyongo alibaleghe na kuwa mwanamume mwenye haiba, kimo kirefu, mpana na maarufii hivi kwamba watu walienda kumwanguka:

**6. Liyongo kitamakali
akabalighi rijali
akawa mtu wa kweli
na haiba kaongeya.**

**7. Kimo kawa mtukufu
mpana sana mrefu
majimboni yu maarufu
watu huya kwangaliya.**

Tofauti na Liyongo, tunaelezwa baadhi ya dhiki zilizomsibu Shaka Zulu utotoni na ujanani mwake kama tulivyoonyesha katika sura ya pili. Shaka anagura na mamake pamoja na dadake kutoka nyumbani mwa babake na kwenda kuishi kwa jamaa zake (Waqwabe) ambapo anapata dhiki nyingi mno ikiwemo kutaniwa na watoto wengine kuwa ni mtoto asiye na baba. Dhiki hizi ni muhimu sana kwake (na kwa jagina yeyote yule) kwani humwandaa vya kutosha katika kulikabili jukumu (dhamira) lake la kishujaa katika jamii yake. Tena, safari ya kugura kutoka nyumbani kwao ni muhimu

sana katika kumkakamaisha Shaka. Jambo hili pia hudhihirika katika safari za majagina wengine duniani.

Licha ya dhiki na safari hizi, Shaka anasawiriwa kama kijana aliye tofauti na vijana wengine - alikuwa na sifa za kipekee Alikuwa mkali mno na aliogopewa na vijana wengine, jambo ambalo lilimfanya mamake kumpa jina, "*Mlilwanalinalomaanisha*, kijana mkali na mwenye hamaki'. Kutokana na hamaki zake, wanawake walimwogopa sana kwani walimwona kama aliye na ari ya fahali apiganaye ugani. Licha ya maelezo haya, kuna vipengele anuwai vya utotoni na ujanani mwake ambavyo hatuelezwi. Isitoshe, kama ambavyo tulionyesha katika sura ya pili, hata tarehe yake ya kuzaliwa inatatanisha na inarejelewa kwa njia tofauti na waandishi mbalimbali.

Hata hivyo, maelezo ya utotoni na ujanani tuliyo nayo kumhusu Shaka Zulu ni mengi zaidi kuliko yale yanayomhusu Fumo Liyongo. Kama ambavyo tulieleza hapo awali, Liyongo aliishi miaka mingi mno iliyopita akilinganishwa na Shaka Zulu. Kwa hiyo, maelezo yake mengi yaliyohusu ujana wake yalisahaulika. Yale yaliyokumbukwa na Waswahili na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine mpaka vikatiwa kwenye maandishi ni pamoja na hali zilizomsibu, vitushi alivyotenda na umbo lake la kustaajabisha.

3.1.4 Shujaa hutokana na ukoo bora / ukoo wa kifalme

Kwa kawaida, jagina hutokana na ukoo bora au ukoo wa kifalme. Babake jagina aghalabu huwa mfalme au kiongozi wa jamii yake. Ukoo huu huchukuliwa na wanajamii kuwa ukoo ambao umetengwa au kuteuliwa (na Mwenyezi Mungu au hata na wanajamii) kama ambao unafaa kuiongoza jamii. Baada ya anayeongoza kutoka kwenye hatamu za uongozi na hasa kutokana na mauti, jamaa mmoja kutoka ukoo wake ndiye huirithi utawala. Utawala huu huwa hauji vivi hivi tu. Inabidi kuwe na utetezi wa cheo cha uongozi kama tutakavyoonyesha katika sehemu 3.1.5.

Kama tulivyoelezea katika faslu ya pili, Fumo Liyongo alitokana na ukoo wa al-Bauri (Allen 1993:121). Ukoo huu ulichukuliwa kuwa ukoo bora ulioheshimiwa na kupewa jukumu la kuiongoza jamii na hususan jamii ya Waswahili wa Pate. Babake Fumo

Liyongo kwa jina Mringwari I alikuwa sultani wa dola ya Pate kabla ya kifo chake Daudi Mringwari aliyechukua hatamu za kuitawala dola ya Pate pia alitokana na ukoo wa al-Bauri.

Kwa upande ule mwingine, Shaka Zulu pia alitokana na ukoo bora Babake Shaka, Senzangakhona, alikuwa chifu wa Wazulu katika kipindi cha uhai wake. Kadhalika, mamake Shaka, Nandi, pia alitokana na ukoo bora (kutoka kabila la abasemaLangeni). Kama tulivyodokeza katika sura ya pili, Nandi alijiona kama mwakilishi wa ukoo wake mahali popote pale na kwa hiyo kwake yeye alistahili kuheshimiwa hata na wanaume kutoka jamii zingine. Jambo hili ndilo lililosababisha mtafaruku baina yake na Senzangakhona.

Kama walivyo mashujaa wa somo letu, mashujaa wa kidini kama vile Nabii Isa, Mtume Muhammadi na Gautama Buddha pia walitokana na ukoo bora. Nabii Isa alitokana na ukoo bora wa mfalme Daudi; Mtume Muhammadi alitokana na ukoo bora wa kabila la Kikureshi; ilhali Gautama Buddha alitokana na ukoo bora kwa jina Sakya.

3.1.5 Utetezi wa cheo

Ingawa jagina hutokana na ukoo bora, mara nyingi hakipati cheo (cha kifalme) vivi hivi tu. Ni sharti akitetee au akipiganie cheo kile. Shujaa akiwa katika cheo cha kifalme huwa na nafasi nzuri ya kutekeleza mabadiliko au kuratibu mbinu na mikakati kabambe ya kuikomboa na kuiongoza jamii yake hadi kwenye ufanisi. Shujaa anaweza kufanya jambo lolote lile - hata kuuu - ili kuona kuwa anabakia kama kiongozi wa watu wake. Shujaa kwa kawaida hutetea cheo chake dhidi ya maadui zake ambao yumkini huwa na nia ya kumwangamiza.

Uteteaji wa cheo cha ufalme wa Fumo Liyongo unadhihirika vizuri katika *Takhmisa ya Liyongo* ambapo suala hili linatiliwa maanani katika beti kadhaa. Analionea fahari jambo hili na anajitokeza kama mtu anayeweza kutenda jambo lolote lile, ili kuhifadhi cheo chake. Hebu tushadidie madai haya kwa kurejelea baadhi ya mishororo katika beti kadhaa za takhimisa hii:

4. ...Mtetea cheo mwenyi cheo ateteapo; hambiwi ni nawi hatta roho nengakoma.

9. ...Teteapo cheo kiwa muyi nawa meupe.

**15. ...Simba bora ndume watetea jaha na cheo;
Watetea jaha hatta mato yakafunama.**

Kama alivyo Fumo Liyongo, Shaka Zulu naye pia alipigana ili kuona kuwa amerithi cheo cha uongozi wa Wazulu, baada ya kifo cha babake. Babake alipofariki dunia, Sigujana (ndugu wa kambo wa Shaka) ndiye alichukua hatamu za uongozi. Hata hivyo, Shaka alijiona kama mrithi halali na kwa kibali cha Dingiswayo, alikichukua kikosi cha iziChwe na kuelekea hadi nyumbani kwao na kumng'oa Sigujana kutoka uongozini. Baada ya kushika hatamu za uongozi, alihakikisha kuwa wasaliti wake wote waliadhibiwa kwa mujibu wa sheria kali alizokuwa ameweka. Hukumu ya wasaliti ilikuwa ni kifo. Ili kutetea cheo chake kutokana na mashambulizi ya nje kama yale ya Zwide, Shaka aliratibu mbinu na mikakati mwafaka ya kivita ili kuyakabili mashambulizi hayo. Alitumia cheo au wadhifa wake kuupanua ufalme wake kwa kuunganisha falme zingine ndogondogo.

3.1.6 Maadui / wapinzani wa shujaa

Jagina kwa kawaida huwa hakosi maadui au wapinzani. Hali hii pia hujitokeza katika maisha ya kawaida ambapo ingawa mtu fulani ni mashuhuri (kipenzi cha watu) au ana ufanisi mkubwa, hapakosi maadui kadhaa ambao humwonea kijicho na kumtakia maovu na hata kujaribu kumwangamiza. Si ajabu kwamba hata Mwenyezi Mungu (shujaa wa mashujaa) pia ana maadui. Adui mkubwa wa Mwenyezi Mungu ni shetani. Mashujaa wengine, kwa mfano, shujaa Kimathi hawakupendwa na Wakoloni na walitafutwa kwa udi na uvumba ili wauawe. Hakuna jagina yeyote ulimwenguni mzima ambaye hana maadui.

Maadui wa shujaa ni muhimu sana katika kuwaelezea au kuwafafanua mashujaa. Yumkini, kama adui wa jagina hayupo, basi huenda shujaa naye pia asiwepo. Lengo kuu la kuzuka kwa jagina katika jamii yoyote ile kama ambavyo tumekwisha kuona huwa ni kuikomboa jamii yake kutokana na mashambulizi au maonevu ya maadui. Tunapomlinganisha shujaa na wapinzani wake, tunapata kuwa jagina huwa na sifa za kipekee tofauti na wapinzani wake. Mara nyingi, maadui wa jagina humwogopa sana

na hufanya kila juhudi kumwangamiza baada ya kushindwa kukabiliana naye sako kwa bako.

Kama walivyo majagina wengine duniani, majagina wa somo letu pia walikuwa na maadui wao. Maadui wa Fumo Liyongo ni kama vile Wagalla waliowashambulia Waswahili miongoni mwa jamii zingine za pwani; binamuye (Daudi Mringwari) na hata mwanawe ambaye katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ub.214) anarejelewa pia kama adui wa Mwenyezi Mungu. Kwa kawaida, maadui wa jamii anayoiwakilisha au kuitawala shujaa huwa maadui wa shujaa huyo; Wagalla wanarejelewa kama maadui katika utungo unaodaiwa kuwa ulitungwa na Liyongo kwa jina *Gungu la Mnara Mpambe* (Miehe na wenzake 2004: 54):

Gungu la Mnara Mpambe

**...Watukuze p'anga na ngao na ngao mtu hutosheya kuona
Kuyiye Mngazija na k'umbo na k'umbo uyiye kutaka harubu
Kuyiye Mgala na mata na mata uyiye kutaka kuteta
Tutawatiliya ukuta ukuta wasitungiliye muyini.**

Tukumbuke pia kuwa, Wagalla walikuwa mashujaa (mashujaa wa mwituni) lakini licha ya ushujaa wao, waliingiwa na hofu na hata kuogopa ghaya baada tu ya kumtazama Liyongo. Kwa hiyo, tunaweza kudai kuwa ushujaa pia huwa na ngazi mbalimbali. Ngazi hizi huanzia kwenye matawi ya chini (shujaa wa kiwango cha chini) na kupanda hadi katika kiwango cha juu kabisa cha ushujaa (kinachomilikiwa na Mwenyezi Mungu). Shujaa wa kiwango cha chini kwa kawaida humcha shujaa wa kiwango cha juu. Katika *IJtenzi wa Fumo Liyongo*, tunaeleza:

**9. Wagala hao yuwani
ni wakuu wa mwituni
kabila ya sulutwani
mashujaa wote piya.**

**34. Napite akamwambiya
kipita akatokeya
Wagala wakashuhudiya
khaufu zaliwangiya.**

**35. Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukoma ondo
huyo ni bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya.**

Binamuye Fumo Liyongo kwa jina Daudi mringwari alipanga njama za kumwangamiza Liyongo kwani alimwona kama tisho dhidi ya utawala wake. Alimtumia mwanawe Liyongo kumsaliti babake, kama ambavyo tumeelezea katika faslu ya pili.

Kama alivyo Fumo Liyongo, Shaka Zulu pia alikuwa na maadui. Maadui wa Shaka walikuwa si haba. Tangu utotoni mwake, Shaka aliandamwa na maadui zake ambao walimwonea wivu na wakataka hata kumwangamiza. Ufanisi na umaarufu wake haukuwapendeza watu wote. M. Kunene (1979:167) anatudokezea kuwa, ufalme wa Shaka ulivyozidi kupanuka ndivyo maadui wake ndani na nje ya eneo la Wazulu walivyozidi kuongezeka. Wapinzani / maadui wa Shaka walikuwa ni pamoja na babake, malkia Mkhaba (mojawapo wa wake wa Senzangakhona), nduguze wa kambo (Dingane na Mhlangana), na Mbopha. Mbopha alikuwa msaidizi wa karibu mno wa Shaka katika utawala wake lakini hatimaye alibadilika na akamsaliti bwana wake. Isitoshe, maadui wa Shaka wa viwango vya kifalme na ambao alipigana nao vita ni kama vile Zwide, wafalme wa Chunu na Thembu miongoni mwa falme zingine. Maadui hawa walikuwa na azima ya kumwangamiza Shaka ili watwae uongozi wa eneo la Wazulu.

Baada ya Senzangakhona kuelezwa kuhusu utabiri wa kuzaliwa kwa Shaka, alisumbuka sana katika nafsi yake kwa kuwa alimwona Shaka kama ambaye angemnyang'anya ufalme wake hapo baadaye. Hata baada ya Shaka kuzaliwa na kugura pamoja na mamake kwa kabila la abasemaLangeni, ili kutafiita hifadhi, Senzangakhona alizua vita dhidi ya kabila hilo. Mkhabayi alimchukia Shaka mno na ndiye aliyemchochea Senzangakhona kuwashambulia wale waliompa hifadhi. Lengo lake lilikuwa ni kuona kuwa Shaka ameporomoka. Aliuona umaarufij wa Shaka kama tisho kwake na kwa utawala wa nduguye. Hata baada ya Shaka kuchukua hatamu za uongozi na vita kuzuka mara kwa mara, baadhi ya watu walimchukia na kumwona kama aliyekuwa akisababisha vita hivi. Isitoshe, baadhi ya watu kupitia fitina za Mkhabayi walidai kuwa Shaka ndiye aliyemuua mamake. Walisambaza fitina dhidi ya Shaka kutoka nyumba moja hadi nyingine. Mkhabayi, Dingane na Mhlangana kwa ushirikiano wa Mbopha walifanya mikutano ya siri ya mara kwa mara ili kutafiita mbinu za kumwangamiza mfalme wao, jambo ambalo hatimaye lilifanikiwa.

3.1.7 Shujaa huwa kipenzi cha wanajamii

Ingawa tumedokeza hapo juu kuwa jagina huwa na maadui, kwa kawaida jagina huwa kipenzi kikumbwa cha wengi wa wanajamii wa jamii yake. Ufanisi na mapenzi ya

umma kwa jagina wao ndicho chanzo cha wivu wa watu wachache ambao hukirihika baada ya kuuona umma unavyoajabia ufanisi wa jagina wao Kama tulivyotaja hapo awali, wanajamii humchukulia jagina wao kama mkombozi anayewatoa kutoka hali ngumu ya kijamii hadi katika ufanisi. Kutokana na jukumu hili la ukombozi, kuna haja kubwa ya wanajamii walio wengi kumsifia jagina wao wanayemtarajia kuwaletea mabadiliko. Si ajabu kuwa wanajamii huyahusisha mambo yote mazuri katika jamii na jagina wao. Umaarufu wa jagina huenea kote kote na watu wa jamii yake hutarajia kila wakati mambo makubwa kutoka kwake.

Fumo Liyongo anarejelewa kama mtu maarufu aliyependwa na kuajabiwa sana na jamii ya Waswahili, wakiwemo watu wengine kutoka jamii zingine. Kwa mfano, katika ubeti wa saba wa *Utenzi wa Fumo Liyongo*, tunaelezwa:

**7. Kimo kawa mtukufu
mpana sana mrefu
majimboni yu maarufu
watu huya kumwangaliya.**

Baada ya Liyongo kukamatwa na kutiwa gerezani, sultani aliomba mashauri kutoka kwa wanajamii kuhusu kuuawa kwake. Waliposikia mpango uliopangwa na sultani kumhusu Liyongo, walijaribu kumtetea kwa kila njia kwa vile walimwona kama mtetezi wao dhidi ya maadui zao. Tunaelezwa haya kwenye *Utenzi wa Fumo Liyongo*:

**88. Kukifanywa mashauri
auawe madhukuri
tulepuwe lake shari
Liyongo namcheleya.**

**89. Wenginewe wakanena
kumuwa siyo sana
huyu nda mui zana
Ni mwenye kukuteteya.**

Aidha, kifo cha Liyongo kiliwasikitisha watu wengi mno. Katika kuonyesha kiwango cha kusikitika, mshairi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* ametumia fumbo, '**imeanguka paziya**' (ub. 226), kumaanisha kuwa jamii ile imeachwa 'uchi\ bila mtu wa kuwaongoza au wa kuwaunganisha na kwa hiyo adui anaweza kuwashambulia wakati wowote atakapo. Mshairi anaeleza kusikitika na kuhuzunika kwa jamii baada ya kifo cha Liyongo katika beti zifuatazo:

**224. Make Liyongo hakika
matanga aliyaweka
watu wakasikitika
kwa Liyongo kuifiya.**

**225. Liyongo silaha yetu
kwa wut'e khasimu zetu
alikuwa ngao yetu
wut'e wakinena haya.**

**226. Mui walisikitika
hakuna wa kutosheka
kwa Liyongo kutoweka
imeanguka paziya.**

**227. Sana wakahuzunika
na matanga wakaweka
kisa mamake katoka
kana ada katembeya.**

Umaarufu wa Liyongo pia unajitokeza pale ambapo sherehe za gungu na mwao zinafanywa kabla ya Liyongo kuuawa. Wakati watu walitangaziwa kuwa kungekuwa na gungu na mwao kama alivyotamani Liyongo, watu walijitokeza kwa wingi katika sherehe hizi hivi kwamba hakukubakia mtu hata mmoja huko majumbani. Liyongo alisifika sana kama shaha wa gungu na mwao na watu wengi walimpenda na kujihusisha naye. Tunaelezwa haya katika Utenzi wa Fumo Liyongo:

**79. Liyongo nikwambiao
Shaha wa gungu na mwao
tena ni mkuu wao
huwashinda wut'e piya.**

**111. Hata usiku kifika
matezo wakayandika
kana ada wakaweka
t'asa, pembe, siwa piya.**

**112. Na ngoma na nyingi kusi
kusalie unasi
ikawa kama harusi
watu wakiangalia.**

**113. Wut'e wakakutanika
mahala pakatandikwa
na uzuri wakaweka
deuli na subahiya.**

Shaka Zulu ingawa alikuwa na maadui kadhaa, alikuwa kipenzi kikubwa cha watu. Hali hii ilitokana hasa na ari na juhudi zake za kuona kuwa maadui wa jamii wameporomoshwa na umoja na utengamano wa Wazulu umedumishwa. Wazulu wakiwemo watu wengine wengi kutoka mbali walimsifia kwa ukakamavu wake jambo ambalo liliwafanya watongoaji wa mashairi kumsifu shujaa wao kwa kumtongolea mashairi chungu nzima ya kumsifu. Kwa mfano, mfalme Mbengi alimsifia Shaka alipokuwa bado kijana kwa kumtungia ushairi wa kishujaa (M. Kunene 1979:31), "Shaka si kijana tena, bali ni simba mdogo anayevunja shingo za nyati wa mwituni." (Tafsiri Yangu)

Shaka alipojiunga katika jeshi la Dingiswayo, alijikakamua vilivyo na kuwavutia wanajeshi wengi hadi wakampa lakabu, 'shujaa wa Dingiswayo'. Dingiswayo naye alivutiwa na umaarufu na ukakamavu wa Shaka hata akamruhusu kukiongoza kikosi cha kijeshi cha iziChwe. Wanajeshi wa kikosi chake walimpenda mno kwani aliwashajiisha na kuwapa mbinu mpya za kuwakabili maadui. Katika kikosi hicho cha

iziChwe, kulikuwepo pia mashujaa wa kivita watajika kwa jina Mgobhozi na Nqoboka ambao walikuwa marafiki wa dhati wa Shaka.

Kwa sababu ya umaarufu wa Shaka, jamii ya Wazulu wakiwemo watu wengine kutoka nje walijadili na kukubaliana mbinu za kuomboleza kifo cha mamake, kama tulivyoona katika faslu ya pili. Umashuhuri na mapenzi ya Wazulu kwa Shaka wakiwemo watu kutoka makabila ya mbali ulionekana wazi baada ya kifo cha shujaa wao. M Kunene (khj: 425-427) anatumbea picha ya hali ilivyokuwa. Kwa mfano, katika uk. 425 tunafahamishwa, "**Kote katika nchi ya Wazulu, watu wengi sana walilia; wengi walienda hadi Dukuza kwa vile hawakuamini.**" (Tafsiri Yangu) Majeshi yote ya maeneo ya Wazulu pia hayakuachwa nyuma (uk. 427):

Majeshi yote ya maeneo ya Wazulu yalianikiza eneo lote kwa nyimbo za maombolezo. Waliimba na kuigiza vita... Inadaiwa pia hata mbingu zililia... nyimbo za kumwaga shujaa wao ziliimbwa toka vijiji vidogo, vile vikubwa na hata maeneo mengine ya mbali... (Tafsiri Yangu)

Mapenzi ya wanajamii kwa jagina hayaishi baada ya kifo chake. Wanajamii wa hata vizazi vya baadaye kabisa huonyesha mapenzi ya dhati kwa jagina wao na si ajabu wengi huamini kuwa atarudi kuwakomboa. Kadhalika, shujaa huwa hai miongoni mwa wanajamii na si ajabu kama tunavyoelezwa katika Steere (1870:vi) kuwaona Waswahili wakimlilia na kumsikitia Liyongo aliyekuwa amewaaga zaidi ya karne tatu zilizokuwa zimepita. Hali hii pia inaafiki kwa Shaka Zulu ambaye hadi hivi leo kutajwa tu kwa jina lake huacha athari fulani mioyoni mwa Wazulu na ulimwengu mzima kwa jumla.

3.1.8 Jina la shujaa.

Shujaa hapewi jina vivi hivi tu. Jina lake huashiria sifa fulani aliyo nayo. Kutokana na jina la shujaa, tunaweza tukaelezea hulka yake kwani wanajamii wenyewe ndio humpa jina hilo kwa mujibu wa tabia yake katika jamii. Aghalabu, shujaa hupewa lakabu nyingi mno na wanajamii kutokana na tabia, mienendo na matendo yake ya hapo baadaye.

Shaka ni jina ambalo lilitokana na jina la Kizulu, *i-tshaka*. Neno hili huwa na maana ya ugonjwa ambao huathiri matumbo na unaoweza kumfanya mwanamke kuwa wazimu na pia kukatiza hedhi yake (Omer-Cooper 1966:29). Baada ya Senzangakhona

kumtungua Nandi mimba, alitakiwa na jamaa wa kabila la abasemaLangeni amchukue kama mkewe. Senzangakhona alikataa kuwa alitenda kitendo hicho na kwamba Nandi alikuwa akiugua *i-tShaka*. Mtoto alipoendelea kukua tumboni na hatimaye kuzaliwa, jamaa kadhaa wa abasemaLangeni walitumwa na wazee wakiandamana na Nandi na kumwambia Senzangakhona achukue *i-tShaka* kama alivyodai. Baadaye, watu walizoea na wakawa wanamrejelea kama Shaka.

Zulu ni jina ambalo Shaka alipewa kutokana na uongozi wake stadi wa jamii ya Wazulu. Jina hili linapotajwa, watu mara moja hulihusisha na jamii pana ya Wazulu na si ajabu Shaka mwenyewe akarejelewa kama mwakilishi wa jamii nzima ya Wazulu. Kwa hakika, Shaka ni mhimili au kiwakilishi cha jamii ya Wazulu na ni muhali kuirejelea jamii hii pasi na kumtaja. Kadhalika, ni muhali pia kumrejelea Shaka pasi na kumhusisha na jamii yake. Tunakisia kuwa alipewa jina hili kwa vile alisaidia katika kuwaunganisha Wazulu wote na jamii ya Wazulu haingepanuka iwapo Shaka mwenyewe hakuwepo. Pia, kwa kumtali Shaka, tunapata historia tosha ya jamii nzima ya Wazulu.

Shaka pia alipewa lakabu mbalimbali za kumsifu. Alipewa jina, "*Nodumehlezi*" kwa maana ya mtu ambaye sifa zake huvuma akiwa ametulia tu mahali alipo. Lakabu nyingine aliyopewa ni, "*Mlilwana*." Alipewa jina hili na mamake katika miaka ya awali ya ujana wake na liliashiria hulka yake ya kukasirika haraka na kuwachokoza watu wengine. Pia, aliitwa "*Ndaba*" jina ambalo lilitumiwa kuashiria jina la mmojawapo wa wahenga wa kadimu katika jamii ya Wazulu (M. Kunene 1979: xxviii). Kama tulivyotaja hapo awali, wanajeshi wa Dingiswayo walimpa Shaka lakabu ya, Shujaa wa Dingiswayo', kuashiria umahiri na ujasiri wake katika vita. Hizi ni baadhi tu ya lakabu ambazo mfalme Shaka alipewa na Wazulu na zote zinaashiria sifa fulani ambayo Shaka alihusishwa nayo.

Fumo Liyongo pia amepewa jina kulingana na sifa yake. Jina, *Fumo'* ni jina ambalo hutumiwa na Waswahili kurejelea chombo kimojawapo cha kivita - hurejelea mkuki wenye chembe kipana mno na ambao hutumika katika vita kuangamiza maadui. Fumo Liyongo mwenyewe ni shujaa wa kivita kama tunavyoelezwa na ana uwezo wa

kuwaangamiza watu wengi kama ilivyo fumo. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**12. Mfalume kawambiya
Wagala kiwasifiya
huwegema watu miya
wasiweze kukimbiya.**

**35. Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukoma ondo
huyo ni Bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya.**

Isitoshe, tunaelezwa kuwa Liyongo alikuwa na mapenzi makubwa kwenye vyombo vya kivita. Katika utungo, *Utumbuizo wa uta* (Miehe na wenzake 2004:46), Liyongo anayaonyesha mapenzi yake kwa vyombo vyake vya kivita na pia anaelezea ustadi wake katika kuvitumia vyombo hivyo:

Utumbuizo wa uta

**Sifu uta wangu wa chitanzu cha mpingo
Upakwe mafuta unawiri kama chiyoo
Mwanzo ch'ondokeya nifumile nyoka umiyo
Hafuma na ndovu shikiyole kama uteyo
Hafuma na k'ungu na kipaa chendacho mbiyo
Wanambia hepe Mwana Mwasho nacha matayo.**

Allen (1993:228) akielezea kuhusu nembo au mapambo ya Waswahili, anadai kuwa nembo ya mkuki wenye chembe kipana (fumo) hupamba mojawapo wa msikiti wa Gedi (*Gedi's Friday Mosque*) na pia hujitokeza kwenye maeneo ya juu ya mashubaka ya misikiti mingi ya kaskazini. Anaendelea kuelezea kuwa neno 'fiimo'¹ lilifasiriwa kama 'mwana mfalme' na lilitumiwa na familia ya kifalme ya Pate kwa jina Nabahani, kama neno la heshima na huenda walilitoa jina hilo kutokana na jina la Fumo Liyongo baada ya ushindi wao dhidi yake katika karne ya kumi na tano. Liyongo mwenyewe alikuwa mwana wa mfalme na kisha akawa mfalme wa dola ya Ozi. Isitoshe, *Utenzi wa Fumo Liyongo* unatueleza kuwa Liyongo alikuwa mwenye heshima na adabu, hasa pale ambapo anaombwa na sultani wa Pate afike mjini Pate ili Wagalla wapate kumtazama. Kwa hivyo si ajabu kuwa Nabahani walitumia neno, 'Fumo' kuashiria heshima. Katika utenzi wa Fumo Liyongo tunaelezwa:

**20. Tumi kenda kwa haraka
kwa Liyongo akafika
kampa kaumunika
akasoma yot'e.**

**21. Na Liyongo akajibu
kwa hishima na adabu
nitakuja kwa karibu
nitwiiye Maulaya.**

Mbele (1986:138-140), anadai kuwa, jina la Liyongo linafaa kuwa Liongo Fumo na wala sio Fumo Liongo kama anavyofahamika na watu wengi. Suala hili tulilipambanua

katika sura ya kwanza na tukaonyesha namna ambavyo Mbele alivyonaswa kwenye ulimbo uliowanasa maulama wengine wanaojaribu kuelezea masuala mbalimbali kumhusu Liyongo. Hata hivyo, kama wanajamii na maulama wengine, maulama huyu ana uhuru wa kumsawiri Liyongo kama atakavyo lakini pia kuna haja ya kuchukua tahadhari ili isije kuibuliwa kwa Liyongo mwingine aliye tofauti kabisa na yule tunayemfahamu na hivyo kupotosha umma.

3.1.9 Kugura kwa shujaa kutoka nyumbani kwao / safari ya shujaa

Kwa kawaida, shujaa hutoroka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika nchi au sehemu za mbali na nyumbani. Sababu mojawapo na iliyo kuu ya jagina kugura kutoka nyumbani kwao hutokana na tisho la maangamizo la maadui zake. Maadui zake ambao sanasana ni wafalme au viongozi huhofia kuwa huenda jagina ambaye huwa na uwezo mkubwa kuwaliko akawavamia wakati wowote na kufanya mapinduzi katika dola zao na kisha kutamalaki. Safari ya shujaa kutoka nyumbani kwao ni muhimu sana kwani humtayarisha jagina kutekeleza jukumu au dhima yake katika jamii.

Huenda shujaa asirejee nyumbani kwao baada ya kugura kutoka mahali pale. Mbega, shujaa wa Washambaa (Hemedi'lAjjemy 1962) aligura kutoka Nguu hadi Kilindini baada ya jamaa zake wa karibu kukusudia kumuua. Kwa mujibu wa Werner (1968:131), Mbega akiwa mtoto aliota meno ya juu kwanza na kulingana na mila na desturi za Wabantu, mtoto kama huyu alichukuliwa kuwa asiyekuwa na bahati hata kidogo maishani mwake. Alisemekana kuwa katika utu uzima wake, angekuwa mhalifii mkubwa ambaye angeuawa hapo baadaye. Kwa hiyo, kutokana na tisho la kuuawa na nduguze, Mbega aliugura mji wake asirudi tena. Vivyo hivyo, shujaa Kimathi naye aligura nyumbani kwao na kuingia msituni ili kumkabili mbeberu katika harakati za kupigania uhuru wa nchi ya Kenya. Hakurudi nyumbani kwao tena kwani alishikwa na walowezi na hatimaye kutiwa kitanzi.

Mutiso (1999:31) anadai kuwa, safari ya shujaa inaweza kuwa ya kiwakati, kimahali, kifikira au kisaikolojia. Katika safari ya kisaikolojia, jagina huzindukana kutokana na elimu (au mawazo) mpya anayoipata Baadaye, yeye huwafiinza wafuasi wake mambo wanayostahili kutenda na hivyo kuubadilisha mftimo wa jamii. Msisitizo wa maulama

huyu ni kuwa, safari ya shujaa ya aina yoyote ile, huhusu kule kutoka kwenye mazingira au hali ya ukawaida na kuingia kwenye mazingira au hali nyingine tofauti. Jambo hili humfanya shujaa kuyatazama masuala yaliyomo kwenye jamii yake kwa mtazamo tofauti kabisa.

Fumo Liyongo, shujaa wa Waswahili, aligura kutoka nyumbani kwao na pia kutoka kwenye maeneo ya miji na kuishi porini. Sababu ya kutenda tendo hili ni kutokana na tisho la sultani wa Pate la kutaka kumwangamiza. Kwa hiyo, safari ya Liyongo ilikuwa ya kimahali - aligura kutoka eneo moja hadi eneo lingine. Huko porini, aliyazoea mazingira ya huko. Waliishi pamoja na Wasanye na Wadahalo. Hata hivyo, baadaye tunamwona akihadaiwa na jamaa hawa waliokuwa wamepanga njama na sultani kwa kumwambia kuwa sultani wa Pate hakuwa tena na ubaya naye. Katika mazingira yale ya mwituni, Liyongo anaonyesha ustadi wake katika kutumia mishale pale ambapo anaangua makoma mengi ajabu baada ya kuyafuma akiwa pale chini ya mkoche.

Kugura kwa Shaka kutoka nyumbani mwa babake kunadhihirika wazi kama ambavyo tumekwisha kuelezea katika faslu ya pili. Safari ya Shaka ilikuwa ya kiwakati, kisaikolojia na pia kimahali. Alitoka nyumbani mwa babake akiwa mchanga mno na kuhamia kwenye maeneo ya mbali na akarudi baada ya wakati mrefu, tayari kuutwaa uongozi wa Wazulu. Kugura huku pia kulihusisha suala la kisaikolojia; alizindukana kutokana na dhuluma alizotendewa na aila yake na kila mara aliapa kulipiza kisasi ikiwemo kuleta mabadiliko katika mfumo mzima wa jamii yake. Kwa jumla, safari hii ilikuwa muhimu mno katika kumshajiisha na kumtayarisha kukabili kwa ukakamavu na ujasiri majukumu mazito yaliyokuwa mbele yake. Aliporudi nyumbani kwao, aliingia kwa ushindi mkubwa na kutokea hapo akaleta mabadiliko makubwa kabisa katika jamii ya Wazulu.

3.2.0 Mashujaa huwa na akili pevu / uwezo wa kung'amua au kutabiri

Tofauti na wanajamii wengine wengi, mashujaa kote ulimwenguni huwa wenye akili pevu au wenye uwezo wa kung'amua mambo yaliyofichika. Akili pevu huwasaidia mashujaa kukwepa mitego ya maadui wao na hivyo kuishi hadi pale ambapo

wametekeleza jukumu lao kwa jamii kwa kikamilifu. Licha ya haya, shujaa huweza kuyatabiri mambo ambayo hatimaye yatakuja kutokea hapo baadaye. Kwa mujibu wa *Bibilia Takatifu*, Masihi (shujaa wa Wakristo) aliyatabiri mambo mengi mno alipokuwa duniani ambayo yalikuja kutokea hata baada ya kupaa mbinguni. AJibashiri kufa, kufufuka na hata kupaa kwake mbinguni miongoni mwa mambo mengine mengi ambayo yalitimia au yanayoaminika kuwa yatatimia hapo baadaye.

Fumo Liyongo anasawiriwa kama mtu aliye na akili pevu na pia mwenye uwezo wa kutabiri mambo. Uwezo wake wa ung'amuzi ndio uliomwezesha kuihepa mitego mingi aliyokuwa amewekewa na sultani. Baada ya sultani wa Pate kuingiwa na fitina dhidi ya Liyongo, alitaka kumwangamiza kwa madai kuwa angempokonya ufalme wake. Tunaelezwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuwa Liyongo aling'amua njama hizo na kuguria mwituni:

**49. Fitina zikamngiya
mfalume miya miya
kwa hila kakusudiya
kumuua fahamiya.**

**50. Liyongo akatambuwa
huzengea kuuawa
pale Pate kuyepuwa
barani akitembeya.**

Isitoshe, Wadahalo na Wasanye walipoahidiwa na Sultani reale mia moja na kuambiwa wakamuue Liyongo, waliutafiita mkoma uliokuwa mrefii sana ili akiupanda, wamfume wote kwa pamoja. Liyongo aling'amua na akatumia ujuzi wake kuyaangusha makoma mengi mno akiwa tu pale chini ya mkoma:

**62. Wakitembea kwa safu
kuuzengea mrefu
na hata wakaushufu
ni huno wakamwambiya.**

**63. Liyongo akiuona
ni mrefu mno sana
yakamwelea maana
yale alowadhaniya.**

**64. Na yeye una hadhari
kilala huwa tayari
awayuwa wana shari
wut'e piya kwa umoya.**

**65. Akawawambia ngojani
akatowa mkobani
chembe katia ngweni
makoma kiwanguliya.**

Liyongo aliposhikwa na kutiwa kizuizini, alitumia akili zake pevu kujinasua kutoka kifungoni kwa kutumia ushairi ambao ni mama yake tu angeweza kung'amua ujumbe uliokuwemo kwenye shairi hilo. Hatimaye, alipata kutoka kizuizini jambo ambalo liliwashangaza wengi akiwemo sultani.

Mwanaye Liyongo alipofika pale nyumbani akiwa na nia ya kumwangamiza, Liyongo aling amua na hata kumtaja kuwa alikuwa ametumwa na maadui zake ili kumwangamiza Waaidha, alimfahamisha kuwa alikuwa amehadaiwa na wale waliokuwa wamemtuma jambo ambalo lilikuja kutimia hapo baadaye. Tunaeleza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**136. Babake akamwambiya
wewe kuuliza haya
dhana nimekudhania
kuniuwa huzengeya.**

**140. Akamwambia nayuwa
kijana umefundiwa
na wewe utahadawa
hayo wamezokwambiya.**

Shaka pia anajitokeza kama mtu mwenye akili pevu mno na pia mwenye uwezo wa kutabiri. Katika vita vyake vikuu zaidi dhidi ya mfalme Zwide, kama tulivyoona katika sura ya pili, Shaka alidhihirisha upevu wake wa kutumia akili katika kumkabili Zwide na vikosi vyake. Ingawa wanajeshi wa Zwide walikuja wakiwa wengi mno, aliweza kuwaangamiza kwa urahisi mno.

Uwezo wa Shaka Zulu wa kung'amua mambo ulijulikana hata na watu wengine. Njama za kumwangamiza alizofanyiwa na Mkhabayi na washirika wake zilifanywa kwa uangalifu mkubwa kwani walihofia uwezo wake wa kung'amua njama alizokuwa anafanyiwa. Kwa mfano, Mkhabayi anamtahadharisha Dingane dhidi ya kumpangia Shaka njama za kumwangamiza (M. Kunene 1979:245). Anasema:

**Hata hivyo, si rahisi kupanga njama dhidi ya Shaka.
Kutokana na akili zake razini, atagundua ukweli wote
kuhusu njama zetu ovu. Ametunukiwa masikio elfu moja na
nguvu za kiajabu. (Tafsiri Yangu)**

Kabla ya kifo cha Mgobhozi, mwandani wa Shaka, Shaka alikuwa ameota ndoto kuhusiana na kuangamia kwake katika vita. Jambo hili lilimsikitisha sana Shaka na kumkosesha utulivu. Shaka hangemzuia kwenda vitani kwani Mgobhozi mwenyewe alikuwa shujaa na aliamini kuwa si hasara kwa shujaa kuifia jamii yake katika medani. Katika mazungumzo yake na Mgobhozi (uk. 284, katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic*) anasema:

**Ninasumbuliwa na woga kama ambao hukumba roho za
wapenzi wawili wanaoachana.
Lakini hakuna kitu ambacho ninaweza kukifanya.
Siwezi kumzuia shujaa ambaye anajiandaa katika vita.
(Tafsiri Yangu)**

Utabiri wa Shaka ulikuja kuwa wa kweli kwani Mgobhozi aliuawa katika vita na vikosi vya Sikhunyana

Katika uk.371 wa utenzi huo huo, Mkhabayi akizungumza na dadake kwa jina Mawa kumhusu Shaka anasema, **"Ni dhahiri kwamba Shaka anazijua njama anazopangiwa... Ninamwogopa mtoto huyu; anazo nguvu za kishetani"**.

Mbopha, msaidizi wa karibu wa Shaka, alikuwa ameshauriwa na Mkhabayi kumuua Shaka lakini alikataa katakata, kwani alijua uwezo wa bwanake wa kung'amua mambo. Anasema katika uk. 412 wa utenzi huo:

**Naapa kwa jina la baba yangu aliyekufa, ninamwogopa kama
nimwogopavyo nyoka.
Licha ya hayo, sikubaliani na mpango huu.
Atafahamu nia yangu kutokana na mienendo yangu.
Yeye ni kama mwaguzi stadi.
Ninapomtazama nikiwa na mawazo mabaya akilini,
Yeye hunigeukia na kunikashifu. (Tafsiri Yangu)**

Shaka anapouawa, anayanena maneno muhimu sana ambayo yalikuwa na athari kubwa sana kwa taifa nzima la Afrika Kusini katika siku za halafu. Aliwaambia wasidhani kuwa wangeitawala nchi ya Wazulu baada ya kumuua. Alieleza akiwa na uchungu mwingi kuwa ni 'mbayuwayu', yaani walowezi wa Kizungu ambao wangetawala. Hali hii ilikuja kutimia baada ya walowezi hawa kukalia eneo la Afrika Kusini na kueneza ubaguzi wa rangi kwa muda mrefu sana hadi kufikia miaka ya tisini ya karne ya ishirini ambapo Afrika Kusini ilijipatia uhuru wake.

3.2.1 Mashujaa kwa kawaida huwa ni washairi

Kwa kawaida, mashujaa wote duniani ni washairi. Mshairi kwa jumla huwa na falsafa nzito kuhusiana na maisha katika jamii yake na hasa kwenye nafsi yake, na ambayo hupitisha kwa wanajamii wake. Wanajamii huyakariri mashairi haya na kuyapitisha kwa vizazi vya halafu. Kwa vile mashairi haya huwa yametoka kwa mkombozi wao, basi wao huwa na imani kuwa hayana budi kuwa na nguvu au uwezo fiilani wa kudumu hata baada ya shujaa wao 'kuondoka'. Mashairi yaliyotungwa na shujaa au hata maneno fulani ya kifalsafa aliyopenda kuyatumia maishani mwake huwa kama zawadi ya shujaa kwa jamii yake baada ya mauko yake. Isitoshe, mashujaa wengi hutungiwa

na watu wengine mashairi chungu nzima ya kuwasifti Mashairi haya hujaribu kuelezea historia ya mashujaa hawa pamoja na kusawiri umuhimu wao kwa jamii zao.

Kama ambavyo tumekwisha kutaja, Fumo Liyongo alikuwa mshairi stadi. Mashairi au nyimbo alizozitunga zimewekwa pamoja katika Miehe na wenzake (2004). Uchanganuzi wa kina wa nyimbo na mashairi haya unatupa taswira ya hulka ya Liyongo mwenyewe, uhusiano wake na jamii yake, dhiki zilizomkumba na hata baadhi ya mila na desturi za Waswahili kama ambavyo tumekwisha kuona Licha ya haya, ni bayana kuwa mashairi haya ni muhimu sana katika kuzifafanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo. Ikumbukwe pia kwamba, Liyongo alikuwa shaha wa gungu na mwao na jamii ya Waswahili inadai kuwa yeye ndiye mwasisi wa gungu na mwao. Wanajamii huamini kwamba kila kitu kizuri katika jamii yao hutokana na shujaa wao hata kama kwa hakika yeye siye aliyekiasisi. Kwa hiyo kuna uwezekano kuwa Liyongo siye mtunzi wa baadhi ya nyimbo anazodaiwa kuwa ndiye aliyezitunga.

Shaka pia alikuwa mshairi, mwimbaji na mchezaji ngoma mashuhuri sana. Hakuachwa nyuma katika kuzitongoa nyimbo na mashairi ya kuelekea vitani na pia yale ya kuondoka kutoka kwenye medani baada ya ushindi wa jeshi lake dhidi ya maadui wao. Ngoma hizi ama kwa hakika ziliwaunganisha wanajeshi kwa kuwapa mshawasha wa kumvamia adui wakiwa kama jeshi moja.

Ugwiji wake katika kucheza ngoma unadhirika pale ambapo babake alikuwa ameenda kumtembela Dingiswayo wakati Shaka akiwa anahudumu katika kikosi cha kijeshi cha Dingiswayo. Watu wa aina mbalimbali vikiwemo vikosi mbalimbali vya kijeshi viliitwa kwenye uga wa kuchezea ngoma ili kumtumbuiza Senzangakhoma Shaka pia alijitokeza na uchezaji wake uliwavutia watu wengi sana akiwemo babake. Katika uk. 66 wa *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* tunaeleza:

Mwanamume mchanga (Shaka) aliyekuwa mrefu, mwenye kujionea fahari aliruka juu. Ni kana kwamba upepo uliacha kuvuma, ili ushuhudiye. Wachezaji waliinua shingo zao kama ndege wa mwituni; kama kundi la kwezi kabla ya kuruka kwao. Aliuyumbisha mwili wake na alionekana kana kwamba angeanguka chini. Alionekana kana kwamba miguu yake mirefu ingemporomoshwa hadi chini. Hatimaye aliinuka akiwa amekiinua kichwa chake huku akitazama pande zote... Senzangakhona akamwambia

jamaa aliyekuwa karibu naye, ⁴*Naapa kwa jina la habangu, huyu mwanamume ni stadi katika uchezaji ngoma'...* (Tafsiri Yangu)

Aidha, kama shujaa na mfalme wa Wazulu, Shaka alitungiwa mashairi na tungo chungu nzima za kumsifu. Alitungiwa mashairi na magwiji wa utongoaji wa mashairi ya jamii ya Wazulu wa zama zake kama vile Nomnxamama na Magolwane wakiwemo wanajamii wengine. Washairi hawa walimpenda Shaka mno na baada ya Shaka kuuawa, Nomnxamama alighani shairi la kumsifu akiwa na uchungu mwingi mno moyoni mwake na kisha akajitia kitanzi.

Licha ya utongoaji wa mashairi na uchezaji wa ngoma, Shaka alikuwa na maneno aliyokuwa akiyaradidi kila mara ili kuwapa motisha wanajeshi wake. Kwa mfano, kila mara, alifananisha vita na uchezaji ngoma na angesema, "**Gunge katika upiganaji vita huiga uvumaji wa upepo. Vita ni kama uchezaji ngoma.**" Usemi mwingine aliopenda kuusema ni, "**Kasi katika upiganaji wa vita, ndio huamua matokeo katika vita vyovyote vile.**" Hapa, alikuwa akihimiza umuhimu wa kumvamia adui kwa ghafla na kwa ari. Mazungumzo ya Shaka aghalabu yalihusu vita na uundaji wa taifa pana la Wazulu.

3.2.2 Maisha ya mashujaa huwa ya dhiki tupu

Majagina kutoka katika jamii zote ulimwenguni huishi maisha ya dhiki. Baadhi ya dhiki ambazo shujaa hupitia tumezionyeshwa katika sehemu kadhaa zilizotangulia; kugura kwa mashujaa kutoka kwao na kuishi uhamishoni; tisho la kutaka kuuawa na maadui zao; maisha ya upweke na hususan wakiwa uhamishoni; madhila wanayotendewa na maadui wakiwemo wasaliti wao; kwa jumla, maisha ya jagina toka kuzaliwa hadi mauti yake huwa ni yenye dhiki kuu.

Lengo kuu la jagina huwa ni kuikomboa jamii yake na kwa hiyo hawezi akatulua mpaka pale ambapo ataitekeleza dhamira yake. Katika kuitekeleza dhamira yake, jagina ni lazima ateswe, aonewe, ashutumiwe, asingiziwe, audhiwe, asalitiwe na hata auawe. Si ajabu kwamba hata Mwenyezi Mungu (shujaa wa mashujaa), pia hushutumiwa na hata kulaumiwa na baadhi ya watu ulimwenguni kwa hali zinazowakumba.

Dhiki huzidi kwenye nafsi ya shujaa pale ambapo anaiona jamii yake ikiteseka Kutokana na hali hii, anaweza kutenda jambo lolote lile ili kuikomboa jamii hiyo na hususan kutoka kwenye mikono ya adui au dhiki nyingine zinazowakumba Kadhalika, matarajio ya jamii kwa jagina wao pia humweka katika hali ya hatari kwani jamii humkuza shujaa ili alete mabadiliko katika jamii hiyo. Shujaa Kimathi, kwa mfano, alitarajiwa na wanajamii na hasa jamii ya Wakikuyu kuikomboa jamii hii kutokana na hulka ya wakoloni ya unyonyaji na utekaji wa mashamba na rasilimali zingine za nchi ya Kenya. Baada ya kung'amua mahitaji ya watu wake, Kimathi kwa ushirikiano wa wazalendo wengine aliingia mwituni na kuanzisha harakati za kupigana kishujaa Jambo hili lilimweka katika hali gumu sana ambapo kila mara alisakwa na mabeberu ili aangamizwe. Hatimaye, aliuawa lakini ndoto yake ilikuja kutimia - nchi ya Kenya kuwa 'huria'.

Maisha ya Fumo Liyongo na yale ya Shaka Zulu kama ambavyo tumeonyesha katika sehemu za awali, na hata itakavyozidi kudhihirika baadaye, yalijaa rundo la dhiki Ama kwa hakika, dhiki hizi ziliwashajiisha mashujaa hawa na pia zikawafanya wapanie kutekeleza na kukamilisha dhamira yao katika jamii zao. Dhiki ambazo jagina hupitia huakisi kwa kiasi kikubwa dhiki au hali zingine gumu zinazokumba wanajamii.

3.2.3 Kimo na nguvu za shujaa

Majagina na hususan majagina wa kihistoria wa kijamii kwa kawaida huwa ni majitu - majagina hawa huwa na vimo virefu na nguvu nyingi mno tofauti kabisa na wanajamii wengine. Sifa hii huwa ni mojawapo wa sifa muhimu ambazo huwafanya wanajamii wastaajabie jagina wao. Si ajabu kuwa watu wenye vimo vikubwa katika jamii huchukuliwa kuwa wababe wa kivita.

Fumo Liyongo na Shaka Zulu walikuwa ni majitu. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, Liyongo anasawiriwa kama mtu mkubwa mno mwenye nguvu nyingi na ambaye anatisha. Sultani katika kuwaelezea wagalla kumhusu Liyongo anasema:

**13. Ni mwanamume swahihi
kama simba una zihi
usiku na asubuhi
kutembea ni mamoja.**

**14. Ghafula kikutokeya
mkoyo hukupoteya
tapo likakuwiliya
ukapata na kuliya.**

**15. Mato kikukodoleya
ghafula utazimiya
kufa kutakurubiya
kwa khaufu kukungiya.**

Waaidha, nguvu zake za kimwili pia zinadhihirika pale ambapo anapuliza na kuzipasua panda tatu. Jambo hili liliwafanya wanajamii wengi kukusanyika ili kumtazama Liyongo anapolinganishwa na Wagalla (ambao pia ni mashujaa wa mwituni), vimo vyao vilimfika magotini. Ulinganishi huu unaonyesha namna liyongo alivyokuwa mrefu - kimo chake kilikuwa kama mara tatu hivi au hata nne ya kile cha Wagalla. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tunaelezwa:

**34. Napite akamwambiya
kipita akatokeya
Wagalla wakashuhudiya
khaufu zaliwangiya.**

**35. Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukoma ondo
huyo ni Bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya.**

Katika kuelezea zaidi kuhusu kimo cha Liyongo tunapata kuwa hata kaburi lake kama tulivyoona katika faslu ya pili lilikuwa refii sana jambo ambalo lilishangaza maulama wa hapo awali na pia wa halafu.

Shaka naye, kama alivyokuwa Liyongo, alikuwa mwanamume mrefii na pia mwenye nguvu nyingi mno. Masizi Kunene, katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* anamsawiri Shaka kama aliye na miguu mirefii mno na pia mwenye nguvu ajabu. Tulipokuwa tunamwelezea Shaka kama mchezaji ngoma mashuhuri, tuliyadondoa maelezo yanayoonyesha kwamba Shaka alikuwa mtu mrefii. Katika uk. 79 wa utenzi huo, tunaelezwa kuwa Shaka alikuwa mwanamume mrefu, mkali, aliyepewa heshima na kuogopewa na wanajamii wote. Tunadokezewa:

Shaka alisimama ili kutoa hotuba kwa waliokusanyika. Alikuwa mrefu na mkali ajabu.

Alisema, 'Nimerudi katika ufalme wa baba yangu. Safari zangu zimenifunza yale yote ambayo ninastahili kuyajua kuhusiana na jukumu lililo mbele yangu...' (Tafsiri Yangu)

Shaka anadhihirisha nguvu zake na uwezo wake wa kivita baada ya kuliangusha jitu la mwituni lililokuwa likiotea watu na kuwaua kwa kutumia shoka. Takribani watu wote waliliogopa sana jitu hili lakini Shaka aliapa kukabiliana nalo na liwe liwalo akiwa pweke. Makabiliano na jitu hili yalikuwa ni mojawapo wa jukumu la Shaka katika

jamii yake - kuwaondolea vikwazo vinavyotishia amani na utangamano katika jamii yake. Katika uk. 63 wa *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* tunaelezwa:

... Alilidunga mara kadhaa kwa kutumia mkuki wake. Jitu lilianguka ardhini mithili ya mti mkubwa uangukapo; kama jabari literemkalo kwenye mteremko mkali hadi kwenye bonde lenye kina kirefu... (Tafsiri Yangu)

Roberts (1974:148) ameionyesha picha ya mfalme Shaka Zulu ambayo inamsawiri Shaka akiwa mrefii, mwenye nguvu ajabu na akiwa ameushika mkuki na ngao yake. Anadai kuwa picha hii ndiyo tu iliyo halisi na ilichorwa na James Saunders King. Tumeonyesha nakala ya picha hiyo katika uk.166.

3.2.4 Maisha na matendo ya mashujaa huwa ya kimiujiza

Kama ambavyo tumekwisha kuelezea hapo awali, mashujaa ni watu wa kawaida. Wao hujipambanua na wanajamii wengine kutokana na uwezo wao wa kutenda miujiza - mambo yasiyo ya kawaida. Mashujaa wa kidini kama vile Mtume Muhammadi, Buddha na Yesu Kristo walitenda miujiza chungu nzima jambo ambalo liliwafanya watu kote ulimwenguni kuwafuata kwa wingi na hata kuwaajabia. Maisha ya majagina kote duniani huwa yamejaa matendo ya kimiujiza. Kila tendo ambalo jagina hulifanya - hata likiwa la kawaida au la kiupuuzi - huwastaajabisha sana wanajamii, ambao kila mara humchukulia jagina wao kama kiumbe aliyetofauti sana na watu wengine. Isitoshe, matendo ya kawaida kama vile: kukohoa, kutembea, kula, kucheka, kuimba, kufuma, kupigana vita, kuoga, kuzungumza, kutema mate, kuota moto, kuteleza na kisha kuanguka chini na mambo mengine kama hayo huonekana ya ajabu mno. Kukohoa tu kwa jagina au mfalme katika jamii za awali kabisa kwa mfano, kungechukuliwa kama ishara ya kuwamwagia wanajamii 'baraka' na hivyo haikuwa ajabu kuwaona baadhi ya wanajamii wakimsujudia ili kuzipokea 'baraka' hizo.

Kuna ithibati kadhaa zinazoonyesha kuwa Fumo Liyongo na Shaka Zulu walifanya mambo yasiyokuwa ya kawaida. Tukianza na Fumo Liyongo, vitendo visivyo vya kawaida alivyovifanya ni kama vile kusafiri kutoka Shaka hadi Pate kwa siku mbili tu (safari ya mtu wa kawaida humchukua siku nne) huku akiwa amebeba mkoba ambao ndani yake mlikuwa na kinu, mchi, jiwe la kupondea majani, vyungu na hata mafiga. Ajabu ni kwamba, alipofika huko mjini Pate, tunaelezwa katika *Utenzi wa Fumo*

Liyongo (ub. 36), kuwa alipumua kidogo tu; uwezo wake wa kuzipasua panda tatu kwa kuzipuliza; tendo la kutoroka kutoka gerezani; tendo la kuyaangusha makoma mengi mno kwa kutumia mishale; na pia, kifo chake kilikuwa si kifo cha kawaida

Shaka pia alitenda na kukumbwa na vitushi vingi tu visivyokuwa vya kawaida kama vile, kuyaunganisha makabila madogo madogo na kuliunda taifa moja kubwa kabisa la Wazulu kwa muda mfupi wa miaka kumi tu; kuliangamiza jitu ambalo lilikuwa likiwahangaisha wanajamii kwa muda mrefii. Watu wengi walikuwa wameshindwa kuliangamiza na hata wengine walimvunja Shaka moyo kwa kumtahadharisha kuwa yeye pia angekuwa mhasiriwa; kushiriki katika vita vingi na hatimaye asiawe kwenye medani; mbinu na mikakati ya kivita aliyoasisi kupigana na adui haikuwa ya kawaida; kugura kwake kutoka nyumbani mwa babake na kisha kurudi na kushika hatamu za uongozi; na hata pia uombolezaji wa kifo cha mamake Nandi, halikuwa jambo la kawaida.

Kwa jumla, vitushi vinavyowakumba majagina kutoka kabla ya kuzaliwa kwao, maisha na vitendo vyao duniani hadi kufikia kufa ni mambo yasiyokuwa ya kawaida

3.2.5 Mapenzi ya mama kwa jagina

Mamake jagina na jagina mwenyewe huwa kwa kawaida wanapendana kwa dhati. Hawa wawili, yaani jagina na mamake huelewana pakubwa na hushiriki mambo au siri fiilani ambazo wanajami wengine hawazifahamu. Kadhalika, mamake jagina huwa kama kitulizo wakati mwanaye yuko katika dhiki na humpa motisha ili kuona kuwa ameitekeleza dhamira yake. Kwa hivyo, kutokana na ukaribu wa jagina kwa mamake, tunaweza tukamchukulia mamake jagina kuwa pia ni jagina ingawa huenda asiwe na zile sifa bia za mashujaa.

Hali hii ya mama na jagina kupendana sana inaoana na ile dhana ya kisaikolojia ambayo huelezea kwamba mwana wa kiume huvutiwa kimapenzi na mamake (*Oedipus Complex*). Mwana hana budi kusikitika aonapo dhiki za mamake ilihali mama naye hana budi kusikitika aonapo dhiki za mwanaye. Babake shujaa humwona shujaa kama mpinzani wake na hana budi, apatapo nafasi, kumwangamiza mara moja.

Mamake Liyongo na liyongo mwenyewe wanajitokeza kama mahabubu wakubwa ajabu. Tunaweza kusema kuwa hakuna mtu amwelewaye Liyongo kuliko mamaye Mamake anazielewa hata hisia za ndani kabisa za mwanawe.

Liyongo akiwa gerezani, tunaelezwa kuwa mamake alikuwa akimtayarishia chakula kizuri mno na kisha kumpa Saada kumpelekea huko. Kutokana na uzuri wa chakula hicho, askari walikuwa wanakila na kumbakishia makombo. Hali hii iliendelea kwa siku kadhaa. Liyongo alipoona kuwa maisha yake yalikuwa hatarini baada ya kupewa tisho la kuuawa na sultani, alimtuma Saada kwa mamake kwa kumtongolea shairi / wimbo ambao ulikuwa umefiimbwa. Tuliurejelea ushairi / wimbo huu kwa jina, *Wimbo wa Kijakazi Saada (Utumbuizo wa Dhiki)* katika faslu ya pili. Ni mamake pekee ambaye angefasiri yaliyokuwemo kwenye utungo huo. Hata askari waliokuwa wanamlinda Liyongo na ambao wanarejelewa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* (ub. 105) kama 'makozi', hawangeweza kutanzua fumbo lililogubikwa kwenye utungo huo. Ni dhahiri shahiri kuwa mamake Liyongo alikuwa mshairi kama mwanawe. Baada ya kufasiri yaliyokuwemo kwenye ushairi huo, alifanya kama alivyoagizwa na hivyo kusaidia kukomesha jaribio la sultani la kumuua mwanawe.

Baada ya Liyongo kutiwa msumari wa shaba na kukimbilia kule kisimani hivi kwamba watu hawangeweza kuteka maji, mamake ndiye aliyeitwa ili kumbembeleza aondoke mahali pale ili watu wapate kuyateka maji. Tunaelezwa kuwa mamake aliyatongoa mashairi ya kumbebeleza akiwa mbali na aliogopa na kutetemeka kwani hakuwahi kumwona mwanawe akiwa katika hali hiyo. Haikuwa hulka ya Liyongo ya kukaidi amri ya mamake na hivyo hii ikawa sababu moja ya mamake kumwogopa wakati huo. Hakujuwa kuwa alikuwa tayari amekufa. Mamake aliwaona wanajamii kama waliokuwa wamemkosea mwanawe. Katika kueleza hulka ya Liyongo, mamake anadai kwamba yeye hukasirika kwa nadra sana na akasirikapo, hasira zake huwa ni za moyoni. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**197. Mwanangu megadhabika
si ada kutopulika
ameiza kuinuka
siisi yetu khatiya.**

**198. Siyo yakwe mazoweya
kwa nasaha kimwendeya
husikiya mara moya
Sasa udhia metiya.**

**199. Mamake kumkurubiya
hatari aicheleya
ghadhabu zikimngiya
yoyote huiyuliya.**

Kadhalika, tunaelezwa kuwa, baada ya Liyongo kufa, mamake kutokana na mapenzi yake kwa mwanawe aliandaa matanga ili waombolezaji watoe rambirambi zao.

Mapenzi ya Nandi kwa mwanawe na yale ya Shaka kwa mamake ni dhahiri kabisa. Roberts (1974:35) anadai kuwa, uhasama wa Senzangakhona kwa Nandi, ulichangia katika kuuzidisha umoja baina ya Shaka na mamake na kwamba Shaka kwa kiasi fulani alimhusudu mamake. Katika kugura kwake kutoka kwa Sengezakhona, Nandi hakumwacha Shaka nyuma bali aligura pamoja naye. Maneno ya Nandi kwa mwanawe Shaka yalikuwa ya kutia moyo sana. Licha ya kudhihakiwa na watoto wengine na kudharauliwa na baadhi ya jamaa zake, Nandi alizidi kumhimiza mwanaye kwamba siku za halafu zingebadilika na wakapata kuishi maisha mema - alikuwa na matumaini makubwa na mwanawe. Kwa mfano, katika uk. 22 wa *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic*, anasema:

...Nilijua tu siku moja mwanangu wa kiume (Shaka] atakua na kusifika kote duniani.

Atainuka juu ya viumbe wote waishio.

Wadudu (maadui wao] waliotutania watatetema mbele zake.

Watasema, '*Shaka ni hatari ajabu. Shaka hushamhuUa lakini hakuna anayethubutu kulijibu shambulizi lake*'. (Tafsiri Yangu)

Nandi aliwalea wanawe kwa taabu hadi wakawa wakubwa. Mapenzi ya mama kwa mwanawe yalizidi kudhihirika baada ya Nandi kumsihi Shaka mara nyingi aoe ili apate kuwa na mjukuu lakini Shaka alikataa katakata. Jambo hili lilizua hali ya sintofahamu baina yao. Kila wakati, Shaka alidai kuwa alikuwa na kazi kubwa mno iliyokuwa mbele yake na kwamba maisha ya kifamilia yangemzuia kuitimiza dhamira yake.

Nandi alipougua, Shaka alifanya jitihada kuona kuwa dawa za kumtibu zimepatikana. Aliwaendea hata walowezi (kwa mfano, Henry Francis Fynn) na kuwanasihi wamtafutie dawa za kumtibu mamake lakini pia nao hawakufaulu. Nandi mwishowe alijifia. Baada ya kifo chake, Shaka aliandaa maombelezio ya ajabu kama tulivyokwisha kuona. Madai ya baadhi ya watu kwamba Shaka ndiye aliyemuua mamake hayana

mashiko hata kidogo. Hizo zilikuwa chongea za maadui zake (Mkhabayi na wenzake) ambao kutokana na umashuhuri wake, walitaka kumpromosha - jambo hili tulilidokeza hapo kabla.

3.2.6 Mashujaa huwa hawaeleweki kwa uwazi

Kama tulivyokwisha kuona hapo awali, mashujaa kwa kiasi kikubwa huwa hawaeleweki kwa uwazi. Si ajabu kuona kila mwanajamii akiwa na mtazamo wake binafsi kumhusu shujaa wa jamii yake. Aidha, maulama mbalimbali huwa na mitazamo tofautitofauti kuwahusu mashujaa wanaowarejelea. Jambo hili ni la kawaida na huwa linakubalika. Mitazamo mbalimbali ya wanajamii na maulama hulenga katika kuwakuza mashujaa na kuuweka utamaduni wao ukiwa hai. Katika fasihi simulizi, wanajamii huwa na uhuru wa kuelezea masuala kwa namna ambayo wanaona inafaa zaidi. Tumetaja kuwa, kila jagina huwa na maadui na wafiiasi wake na kwa hiyo kila mojawapo wa makundi haya huwa na mitazamo tofauti kumhusu jagina.

Ili wanajamii na maulama kutimiza malengo yao, wanaweza wakachukua mielekeo tofauti kuhusiana na usawiri wa majagina. Kila mwanajamii au maulama ana uhuru wa kumpigia debe au kumtazama shujaa wa jamii yake na kumpa sifa zinazomfaa kwa mintarafu ya maoni yake mwenyewe. Kuna uwezekano pia wa kuwapa majagina sifa ambazo zimetiliwa chumvi. Maadamu kuna mitazamo mingi kuhusiana na mashujaa, hatuna budi kuelewa kuwa mashujaa watabaki katika hali ambayo haeleweki kwa uwazi na hili ni jambo linalokubalika katika usomi.

Kama walivyo mashujaa wengine, Fumo Liyongo na Shaka Zulu pia nao hawaeleweki kwa uwazi. Katika sehemu za hapo awali, tumepata kuwa kuna masuala kadhaa kuwahusu mashujaa hawa ambayo yanatatanisha. Si ajabu kwamba baadhi ya watu wanamwona Fumo Liyongo kama ambaye hakuwahi kuishi duniani. Suala la kipindi alichishi, mwaka aliozaliwa, sifa alizo nazo miongoni mwa masuala mengine ni baadhi pia ya mambo ambayo yanakanganya maulama hadi sasa. Vivyo hivyo, Shaka Zulu naye hajulikani kwa yakini alizaliwa lini pamoja na kwamba kuna mitazamo anuwai kumhusu na hususan kuhusu namna anavyosawiriwa na maulama mbalimbali. Wazungu, kwa mfano, wanamwona kama mtu mwovu aliyeendeleza utawala wa

kimambavu ilhali Waafrika wanamwona kama jagina aliyepigania haki zao na kuwaunganisha kwa njia ya ajabu. Suala hili la kuwa na mitazamo tofautitofauti baina ya wanajamii kuwahusu mashujaa wakiwemo pia maulama lipo hata katika kuwatazama mashujaa wengine duniani.

3.2.7 Majagina aghalabu huwa magwiji katika vita

Majagina wengi na hususan majagina wa kijamii huzuka ili kukomboa jamii zao kutokana na mashambulio dhidi ya maadui zao. Kwa hiyo, shujaa ni sharti awe na uwezo wa kupigana vita kwa ustadi na kuikomboa jamii yake kutokana na mashambulizi ya adui. Mashujaa huwa hawaogopi chochote. Mara nyingi, wao hufurahia vita kwani ni katika vita ambapo ushujaa wa mashujaa na hususan mashujaa wa kijamii hudhihirika. Samson katika *Biblia*, kwa mfano, anasawiriwa kama shujaa wa kivita aliyeutumia utaya wa punda na kuwaua Wafilisti elfii moja (*Kitabu cha Waamuzi* 15:14-17). Uwezo wake wa kivita uliwawezesha Waisraeli kujikomboa kutoka kwa Wafilisti baada ya miaka arobaini ya dhuluma na unyanyasaji. Vivyo hivyo, Lwanda Magere, shujaa wa Wajaluo, Dedan Kimathi, shujaa wa Wakikuyu, miongoni mwa mashujaa wengine walikuwa magwiji katika medani

Fumo Liyongo kama alivyo Shaka Zulu, alizuka katika kipindi kilichojaa misukosuko ya kivita katika janibu za Afrika Mashariki. Liyongo anasawiriwa kama gwiji wa kivita aliyeweza kuwakabili watu wengi kwa wakati mmoja. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**12. Mfalme kawambiya
Wagala kiwasifia
huwegema watu miya
wasiweze kukimbiya.**

**35. Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukoma ondo
huyo ni bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya.**

Isitoshe, Liyongo anajitokeza kama gunge katika utumiaji wa mishale. Jambo hili linadhihirika pale ambapo anayaangusha makoma kwa wingi kwa kuyafuma akiwa chini. Pia, tunamwona Liyongo akifa akiwa na mshale mkononi huku amepiga goti moja chini tayari kufuma. Hebu tuonyeshe beti katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* zinazoshadidia madai haya:

**65. Akawambia ngojani
akatowa mkobani**

**66. Achangusha ngaa ndima
ni mangi mno makoma**

**chembe katia ngweni
makoma kiwanguliya.**

**kwa wu'te wakaatama
ajabu zikawangiya.**

**180. Babake akishutuka
chembe uta akashika
kwa haraka akatoka
nde mui kuyendea.**

**181. Akapija ondo lake
katambika chembe chake
kama hai ada yake
chembe utani katiya.**

Takhmisa ya Liyongo inamsawiri Liyongo kama asiyeogopa mikuki wala mishale na anakiona kifo kama kitokanacho tu na Mwenyezi Mungu; lakini si kutokana na kufumwa mikuki na wanadamu:

**16. ...Siche mata yao na mafumo yanganawiri;
mangi mafumati na magao maoya nyuma.**

**22. ...Sichi kikwi chao nami ume ndio nilio;
moyo wangu kikwi kwa ajili ya kushangama.**

**23. ... Kifa tenda ngao paziwapo kipazua;
nisikhofu miwa wala tome za kunitoma.**

**24.... Kufa kwa Muungu na shabuka limkuta;
Si kwa walimwengu mivi kikwi ingakufuma.**

Tena, kuhusiana na kuvipenda vita, Liyongo anasawiriwa kama mtu anayependa vita sana na anajilinganisha na 'mwana kozi' na 'mwana tai' na kwamba yeye hupenda kuanzisha vita sana. Katika takhmisa hiyo hiyo, tunaelezwa;

**8.... Ninga mana kozi sioneki niwakuapo;
ni mui wa nyuni naakua katika jama.**

**9.... Ninga mana taya shirikeneni na mata tope;
na mlisha yani lenyi tani na zingulima.**

**14. ... Pindi uonapo moto zita ukinguruma;
la Allah, ni mimi niwashao maa kazima.**

Shaka pia anajitokeza kama gwiji katika vita. Takriban maisha yake yote yalikusiana na upiganaji vita. Kama alivyo Liyongo, Shaka alizuka katika kipindi cha vita vikali zaidi katika historia ya Afrika Kusini. Katika ujana wake, alijiunga na majeshi ya Dingiswayo na kutokana na uhodari wake katika kupigana vita, ukakamavu, ujuzi na uratibu wake wa mbinu za kivita, alipewa uongozi wa kikundi cha kijeshi cha iziChwe. Kama tulivyotaja hapo awali, Shaka alilinganisha vita na uchezaji ngoma (alivionea fahari) na daima hakuamini kushindwa. Hata hivyo, licha ya kwamba alivifurahia vita,

lengo lake hasa lilikuwa kuvitumia vita katika kuyaunganisha makabila mbalimbali na kuliunda taifa moja kubwa la Zulu

Shaka anasifika sana kwa kuasisi mbinu na mikakati ya kivita zikiwemo sheria kali kuhusiana na mienendo ya wanajeshi wake. Kama kiongozi wa kijeshi na mfalme wa Wazulu, Shaka aliyaleta mabadiliko makubwa katika kumkabili adui. Baadhi ya mbinu alizoasisi na taratibu alizoziweka kuhusiana na mienendo ya wanajeshi wake ni pamoja na:

- Matumizi ya mikuki mifupi badala ya mikuki mirefu iliyorushiwa adui.
- Matumizi ya ngao zilizowambwa ili kukidhi mahitaji ya vikosi vyake.
- Kila mwanajeshi alihitajika kurudi nyumbani akiwa na mkuki wake mfupi pamoja na ngao yake atokapo vitani.
- Vikosi vya kijeshi vilihitajika kufanya mazoezi ya mara kwa mara katika mazingira tofautitofauti ili kuvizoesha na kuviweka tayari kupigana na adui katika mazingira na hali zozote zile. Aidha, kulikuwa na vita bandia (*mock battles*) ili kuwapa mafunzo ya kukabiliana na adui vyema.
- Shaka alisisitiza umuhimu wa kasi katika medani na kila mara alidai kuwa kasi ndiyo iliyoamua matokeo ya vita - kwa hiyo, alipiga marufuku matumizi ya makubadhi ambayo aliyaona kama yaliyochangia katika kushindwa kwa majeshi ya hapo awali.
- AJivifanya visigino vya wanajeshi wake viwe vigumu ajabu kwa kuwafanya watembe juu ya miiba iliyokuwa imemwagwa uwanjani Hawakuhitajika kutoa sauti yoyote wala kuchacharika kwa vyovyote vile kutokana na maumivu - walihitajika kusimama tisti licha ya hisi zilizowakumba.
- Aliwagawanya wanajeshi wake katika vikosi maalumu na kila kikosi kilikuwa na ngome yake chini ya kamanda wao. Kulikuwepo na vikosi vya wanaume na vilevile vikosi vya wanawake. Vikosi vya wanaume vilikuwa ni pamoja na uFasimba, uGibabanye, uFojisa, uMfolozi, uNdabankulu, uNomdayana, amaPhela, amaKhwenkwe,

iziKwembu, iziZamazana, uMgumanqa, isiPhezi, uNteke, uMonambi, uDlangezwa, iziNyosi, amaWombe, uDlambedu na uJubinqwanga. Vile vya wanawake vilikuwa ni pamoja na: uMvuthwamini, uNhlabathi na uCeyana (M. Kunene 1979: xxxv). Ugawanyaji wa wanajeshi katika vikosi mbalimbali na kuviweka katika ngome au kambi fulani chini ya kamanda ni jambo lililopo hata katika jamii za ulimwengu wa sasa. Hali hii inadhihirisha athari za baadhi ya mikakati ya kadimu kwa jamii ya sasa.

Matumizi ya wapelelezi wa siri.

Wasaliti wote wa kijeshi kuuawa kadamnasi ya watu.

Kudumisha heshima na nidhamu ya kiwango cha juu kabisa baina ya vikosi vya kijeshi.

Wanajeshi hawakuhitajika kuoia ila pale tu Shaka alitoa ruhusa.

Katika kumkabili adui, Shaka aliasisi mbinu maridhawa ambapo vikosi viwili vilijitenga na kumzingira adui kwa pande zote mbili huku kikosi kikuu kikiwa mkabala na adui. Hivyo, adui angeshambuliwa kutoka pande zote na hangepata nafasi ya kutorokea.

Mwanajeshi yeyote yule hakuruhusiwa kutoka kwenye medani na liwe liwalo kutokana na mashambulio ya adui - walihitajika kufa kama mashujaa. Mwanajeshi yeyote aliyemkimbia adui katika vita, alichukuliwa kama msaliti wa nchi yake na hatima yake ilikuwa ni kifo.

Wanajeshi wote walihitajika kumpa Shaka Zulu hadhi yake kama mkuu wao.

Shaka alitoa amri kwamba watu wote tokea yule mdogo hadi yule mkubwa wawe na ujuzi wa kivita.

Nafasi za uongozi katika jeshi zilipewa tu wanajeshi waliokuwa na tajiriba katika vita na nidhamu ya hali ya juu na sio kwa mujibu wa mahusiano ya kifamilia au eneo ambalo mtu alitoka.

Kama' mojawapo ya hatua ya kuhakikisha kuwa wanajeshi wake hawatoki kwenye uga wa vita hadi ushindi upatikane, Shaka aliwaruhusu vijana wachanga (wakufunzi wa kijeshi) kuandamana na

vikosi vya kijeshi wakiwa wamebeba hifadhi ya silaha za ziada na pia vyakula.

Mbinu hizi zilimwezesha Shaka kuliunda jeshi kubwa ajabu kwa kuyaunganisha mataifa madogo madogo na hatimaye kuliunda taifa moja kubwa ajabu la Wazulu. Umahiri, utanashati na ulimbwende wake katika mfiimo mzima wa kivita na utawala unasifika hadi leo. Tena, uratibu wake katika vita ulimwezesha kuyaangusha makundi makubwa ya kijeshi kama lile la mfalme Zwide.

Kama alivyokuwa Fumo Liyongo na kama walivyo majagina wengine, Shaka hakuogopa chochote. Kwa muda fulani, Shaka alikuwa akilindwa au kuandamwa na kikosi cha wapambe (waliotoka katika kikosi cha ulinzi wa nyumba ya kifalme cha Mbelebele) lakini alifikia katika hatua fulani katika uongozi wake na kukivunjilia mbali kikosi hiki. Katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* uk.138, Shaka anasema:

**Kutoka leo sitaki kuwa na wapambe
Sitaki kulindwa kama mtu mwoga
Katika maisha yangu siogopi kifo; siogopi yeyote!
Yeyote anayetamani kuniua na adhubutu.** (Tafsiri Yangu)

Kutokuogopa kitu, mtu au jambo lolote lile pamoja na kuwa gwiji katika vita ni sifa mojawapo muhimu sana inayodhihirika katika majagina wengi duniani. Ili kuikomboa jamii (kutimiza dhamira ya jagina), ni sharti jagina ajitolee kufa kupona. Ukombozi huu hauji tu vivi hivi. Ni sharti damu ya wanadamu (wapinzani) aghalabu ichirizike na miili yao itatarike kama bisi na kisha kuanguka kwenye medani wakiwa maiti. Mutiso (1999:3), anashadidia dai la mashujaa kuwa magwiji wa kivita anapoeleza kuhusu kuzuka kwa majagina wa Wajaluo (kabila mojawapo nchini Kenya). Anasema, **"Majagina wa Kijaluo hupatikana kwenye mpaka wa Wajaluo na Wakalenjini - pale ambapo pamewahi kutokea vita kati ya makabila haya "** Kwa hiyo, ni bayana kuwa wengi wa mashujaa wa kijamii wa kihistoria walikuwa magwiji wa kivita; walipenda vita na waliwaongoza wanajamii wengine katika kuwakabili maadui wao.

3.2.8 Shujaa na suala la ndoa

Mashujaa wengi duniani ama kwa hakika hawatilii maanani sana suala la ndoa. Ili jagina aweze kutekeleza dhamira yake, ni sharti awe huria Ndoa kwa kawaida humfunga' mtu na kwa vile jagina yuko kwa ajili ya jamii nzima, ni vigumu kwake kukosa kuitumikia kwa madai kuwa analiwaza mtu mmoja pekee Matamaniao ya wanajamii kuhusu ukombozi wao yako kwenye jagina wao na jagina mwenyewe huchukulia kama 'aliyeioa jamii'. Ikumbukwe kwamba wanawake wengi (wapenzi) wamechangia pakubwa katika kuporomoka kwa majagina wa hapo awali katika jamii mbalimbali duniani. Hivyo ndivyo ilivyo hata katika maanguko ya nguli wengi wa kiume katika kazi bunilizi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya majagina ambao huoa. Ndoa hizi huwa wakati mwingi zinayumbayumba kwa kuwa jagina huwa hatulii katika sehemu moja. Hebu tuchukulie kwa kwa mfano Kimathi, shujaa wa Wakikuyu. Ingawa alioa, aliiacha familia yake na kuingia msituni kuitetea jamii yake. Ajabu ni kwamba, alishikwa na mabeberu na kuuawa na hata wa leo, hakuna ajuaye kaburi lake liliko - hata bibiye na wanawe.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, tunafahamishwa katika sehemu ndogo tu kwamba alioa (ub. 45 na 46). Hata hivyo, hatumwoni mkewe akitajwa katika sehemu nyingine yoyote. Tunaelezwa tu kuwa Wagalla ndio waliompa mke aliyechukua mimba na hatimaye kujifungua mwana wa kiume. Basil Mkewe harejelewi tena katika utenzi huo hata pale ambapo Liyongo alipatwa na dhiki.

Licha ya hayo, katika mashairi yanayodaiwa kuwa yalitungwa na Liyongo, tunaelezwa kuwa Liyongo alikuwa na mpenzi kwa jina Kundazi na ambaye alimpenda sana. Waaidha, baadhi ya mashairi haya yanaashiria kuwa Liyongo alitilia maanani sana umuhimu wa mwanamke na hususan katika maisha ya mwanamume. *Utumbuizo wa wasiya wa kuolewa* (Miehe na wenzake 2004. 74), mojawapo wa utungo unaodaiwa kuwa ulitungwa na Fumo Liyongo, tunaelezwa kuhusu mwanamke mchanga anayepewa mashauri kuhusiana na tabia njema katika maisha ya ndoa:

Utumbuizo wa Wasiva wa Kuolewa

**Pani kiti nikaye kitako niwauze neno wandaniwa,
Niwauze sababu na kisa nini wake kuiza kuowa?
Mke hawi ela kwa mumewe wanginewe nini kutukiwa?**

**Mwanamke ni mwenye mumewe haibudi na kusitahiwa
Wako mume mshikato sana wake nduzo watatenda ngowa..**

Katika *Utumbuizo wa Mwana Mnazi*, Liyongo anaonyesha umuhimu wa mke na hasa kwa mumewe Anatoa mfano kwa kumtumia mwanamke aliyekuwa mpenzi wake - yeye ndiye aliyezituliza/ poesha zile ashiki zake za kiume na kumwondolea huzuni (**...mpangua hamu na simanzi**). Aidha, Liyongo alipochelewa kufika nyumbani, mpenziwe aliwaambia vijakazi wake kwa jina Saada na Rehema, waandae chakula kizuri na kisha waende kwakamtafute aliko. Kuchelewa kwa Liyongo kuliufanya moyo wa kipenzi chake kuuma na hata machozi kutiririka. Akisaidiana na kijakazi wake mwingine, wanaenda hadi katika hatua ya kumlisha. Wimbo wenyewe ni kama ufiatao:

Utumbuizo wa Mwana Mnazi

**Pani kiti, nikaye kitako, t'umbuize wangu Mwana 'Nazi,
T'umbuize wangu mwanamke, mpanguwa hamu na simanzi.
Husimama tini mwa mlango, k'iyawa nde k'enda matembezi,
K'iyawa nde k'angia shughuli, kiwambiya wakwe waandazi,
Kawambiya Sada na Rehema waandani, pasiwe ajizi,
Waandani, tendani haraka, muwandaye wali na mtuzi.
Akimbona nalilimatiya kamwondowa chakwe kiyakazi,
Mwangaliye usita wa yumbe, au kwao kwa Fumo wa Ozi,
Mwangaliye t'engoni pa nduze, au kwao kwa mama shangazi,
Kampate, hima uye naye, watendani hata njeo sizi?
Kamwambiya, bwana, wamkuwa, twende hima, sifanye ajizi.
Yunga lako limile tutule na matoni hutuuza tozi.
Kamba twende tanguliya, naya, kamtuze aate simanzi.
Kamwandama nyuma kiyongoya, zinuk'a misiki na mbazi.
Akangiya kampa salamu, kamjibu mwana wa Hijazi.
Saa hiyo kondoka akima kamwandika mkono wa fuzi,
Kamwombeya Muungu jabari, ewe mama, Mola ngwakuajazi.
Akinuwa mkonowe mwana kaupeka yuu la muwanzi.
Akanguwa kisutu cha kaye, cha kinisi chema mtwarazi,
Kamweka kituzo cha mato, buni ami, mwana wa shangazi.
Kimwambia, bwana na tukaye, sime mno, ukataajazi.
Nitiyani hoyo Time aye, na anguse ate masindizi.
Apakuwe pilau ya Hindi, mzababu isiyo mtuzi.
Ete kiti chema cha Ulaya, na siniya njema ya Shirazi.
Mnakashi inakishiweyo na sahani hung'ara ja mwezi.
Kaamuru khudama na waja, ai, nyinyi, hamtumbuizi?
Basi, hapo akamwandikiya, naye Time yushishiye kuzi,
Yapijeto mayi ya inabu kimnoshwa kama mnwa shizi.
Kimlisha akimpa hiba kimuonya yakeye maozi,
Kimlisha tambuu ya Siyu yi laini ya Ozi.
Kiukuta k'ono kimwakiza, kwa iliki pamwe na jauzi,**

Nikomele kusifu mbeja mteule wangu Mwana Nazi.

Katika *Utenzi wa Mwana Ninga*, utenzi ambao unadaiwa ulitungwa na Liyongo, anatusawiria na kutusifia sehemu mbalimbali katika mwili wa mwanamke kuanzia utosini na kuteremka hatua kwa hatua hadi nyayoni. Inadaiwa kuwa mwanamke huyu alikuwa mpenziwe Liyongo.

Tofauti na Liyongo, Shaka hakuwahi kuoa. Maisha yake yote yalibusu vita tupu na hakuwa na wasaa wa kuliliwa na vijitoto vidogo wala kupoteza muda wake akimbembeleza na kumwongoa mwanamke. Alisisitiza mara kadhaa kuwa alikuwa na jukumu la kuwaunganisha Wazulu na tendo la kuoa halingemruhusu kutimiza dhamira yake kwa ukamilifu. Kitendo chake cha kutoa kilikuwa chanzo cha mtafaruku mrefii kati yake na mamake. Mamake alishikilia kani kuwa alitaka mjukuu lakini Shaka mwenyewe hakuwa tayari hata kidogo kutenda kama alivyotaka mamake.

Hata hivyo, Shaka, kama walivyo wanaume wengine kote ulimwenguni, alikuwa na ashiki ya kiume. Ili kuitosheleza ashiki hii, alikuwa na wapenzi wahudumu katika nyumba ya mfalme aliofanya mapenzi nao. Wanawake hawa walichukua tahadhari ya hali ya juu ili wasitunge mimba kwani kama ingetokea kuwa walikuwa wajawazito, mimba zao zingetumbuliwa kwa mkuki kadamnasi ya watu. Mbopha ndiye aliyekuwa amepewa jukumu la kupeleleza na kutoa siri kwa Shaka kuhusu masuala nyeti yaliyomhusu kama haya.

Katika *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic* (uk.321), tunaeleza kisa ambapo mpenzi mmoja mhudumu katika nyumba ya kifalme kwa jina Nomazibuko alikuwa amejifungua kwa siri mtoto wa kiume baada ya kufanya mapenzi na Shaka Mtoto huyu alitunzwa na kulelewa kwa siri kubwa na Nomagwebu baada ya maagizo ya Nandi. Mtoto huyu alifichwa kwa kuwa, kama desturi, Shaka angewaua pamoja wote wawili (mama na mwanawe) iwapo angetambua kuwa alikuwa mwana wake. Shaka alipopata kusikia fiinunu kuhusiana na siri hii iliyokuwa imefichwa kwa muda mrefii na mamake, alisikitika na kughadhabika mno. Hata hivyo, Shaka hakutekeleza kitendo cha kumuua kutokana na maombi ya mamake. Badala yake, alitoa amri kwamba mtoto huyo ahamishiwe mbali na aishi na jamaa mojawapo wa koo za Wazulu. Aliwaambia

waliokuwa wakimtunza akiwemo mamake kuwa wamtie ishara fulani kwenye panja lake iii wakati angemtaka baadaye basi ingekuwa ni rahisi kwake kumpata Shaka alifanya hivi iii asije akashtumiwa na wanajamii na hususan wanajeshi aliowaonya dhidi ya kuoa kabla hajapata idhini ya kufanya hivyo. Hatuelezwi zaidi ya hayo kumhusu mtoto huyu.

Kwa jumla, mtazamo wa Fumo Liyongo na ule wa Shaka Zulu kuhusiana na ndoa unatofautiana pakubwa. Fumo liyongo alitilia maanani suala la ndoa na umuhimu wa wanawake. Shaka naye hata hakutaka kusikia akitajiwa suala lolote kuhusiana na ndoa wala watoto. Kinyume na Shaka aliyetaka kumwangamiza mwanawe, Fumo Liyongo alimtunza kwa mahaba ya hali ya juu. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**47. Kamuyeya kimtunda
kwa mahaba kimpanda
kama wa matoni wanda
na kwa t'unu na hidaya.**

**48. Hata kijana kakuwa
na babake wachenda sawa
kabaleghe kwa sitawa
na haiba zot'e piya.**

**131. Babake kafurahika
akanena akiteka
wali mwema kaupika
maana wale pamoya.**

3.2.9 Kifuasi cha shujaa

Kwa kawaida, mashujaa huwa na vifiasi ambavyo huandamana nao na ambavyo huwa muhimu sana katika maisha yao. Vifuasi hivi vinaweza vikawa ala, mnyama au dhana fulani ambayo humsaidia shujaa kutekeleza dhamira yake. Vifuasi hivi huwa vina uwezo wa kipekee na huchukua sehemu muhimu katika maisha ya shujaa; husaidia katika kumkamilisha shujaa.

Mbega, shujaa wa Washambaa, aliandamana na mbwa wengi kila mahali alipoenda. Alikuwa amewafiindisha mbinu za usasi wa nguruwe wakiwemo wanyama wengine wa porini. Kuna mbwa fulani ambaye alimpenda sana. Kwa mujibu wa Werner (1968:133), mbwa huyu alijulikana kama 'Chamfiiu'. Anaendelea kudai kuwa, jina hili limehifadhiwa na wanajamii wa jamii hii hadi leo. Mbwa huyu alimsaidia Mbega sana katika usasi wa nguruwe na aliandamana naye kila mahali alipoenda. Baada ya usasi, aliwapa wanajamii nyama ya nguruwe kwa wingi. Wanajamii hawa walifirahi na

kumwajabia. Licha ya mbwa hawa, Mbega alikuwa na mkoba uliokuwa na hirizi ambazo alitumia kutenda mambo yasiyo ya kawaida

Mtume Musa, shujaa wa Waisraeli, naye alikuwa na kijiti alichokitumia kutenda miujiza chungu nzima katika harakati za kuwakomboa wana wa Israeli kutoka huko Misri. Kijiti hiki kilikuwa hata na uwezo wa kugeuka na kuwa nyoka (taz. *Kutoka* 4:1-5 kwenye *Biblia Takatifu*). Yesu Kristo, kwa upande wake, aliandamwa na Roho Mtakatifu (taz. *Luka Mtakatifu* 3:22 kwenye *Biblia*) aliyemwezesha kutenda miujiza chungu nzima.

Fumo Liyongo na Shaka Zulu pia walikuwa na vifuasi vilivyowasaidia katika utekelezaji wa dhamira zao. Fumo Liyongo alikuwa na mkoba alioubeba kila mahali alipoenda. Mkoba huu ulikuwa na vifaa kadhaa lakini cha muhimu zaidi ilikuwa ni ile mishale aliyoitumia kuwakabili maadui. Katika ushirika wa kiko, tunaelezwa kuwa Liyongo alikuwa ameubeba mkoba ambao ulikuwa na uta na mishale. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*:

**65. Akamwambia ngojani
akatowa mkobani
chembe katia ngweni
makoma kiwanguliya.**

Aidha, katika kufa kwake, Liyongo alikufa akiwa ametia mishale kwenye uta huku akiwa tayari kufuma. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**180. Babake akishituka
chembe uta akashika
kwa haraka akatoka
nde mui kayendeya.**

**181. Akapija ondo lake
katambika chembe chake
kama hai ada yake
chembe utani katiya.**

Shaka, kwa upande wake, aliubeba mkuki na ngao kila mahali alipoenda. Wakati wa kuuawa kwake na nduguze, tunaelezwa kuwa alikuwa akitaka kuuwahi mkuki wake aliokuwa ameuweka karibu naye ili kuyajibu mashambulizi lakini kwa bahati mbaya, wakawa wamemdunga mikuki na hatimaye kumuua. Ni bayana kwamba, wengi wa majagina wa kihistoria wa Kiafrika walikuwa wakibeba zana za kivita kwani wengi wao walizuka katika mazingira ambayo yalikuwa na misukosuko ya kivita. Zana hizi ni

muhimu sana katika maisha ya mashujaa na zinastahili kutiliwa maanani kila mara mashujaa kutoka jamii yoyote ile wanaporejelewa.

3.3.0 Shujaa huhusishwa na zaidi ya jamii moja

Kwa kawaida, ingawa jagina hutokana na jamii au ukoo fulani (kitovu chake), yeye hachukuliwi kuwa tu wa jamii au ukoo huo bali pia, watu kutoka jamii zingine hujihusisha naye. Hata hivyo, jagina na hususan jagina wa kijamii mwenyewe hujihusisha kwa ukaribu na jamii yake - huitetea kwa vyovyote vile ingawa pia hushirikiana na wafalme wa jamii zingine katika kuimarisha hali ya amani na utangamano na kuendeleza maisha ya raia wake hadi kwenye ufanisi. Si ajabu kuwaona baadhi ya watu katika jamii mbalimbai wakidai kuwa jagina fulani na hasa jagina mtajika wa kadimu, alitoka kwenye jamii au ukoo wao. Hapo awali, tulitaja kuwa, ni kaida ya watu kupenda kujihusisha na watu maarufu au vitu visivyo na sifa za kawaida (vya kiajabu). Kwa vile jagina ni kiumbe kisicho cha kawaida - kwa mujibu wa wanajamii - kila jamii hupenda kujihusisha naye.

Tunapowatazama majagina wakuu wa kidini, kama vile Yesu Kristo, Mtume Muhammadi na Buddha, tunapata kuona kuwa wao si wa jamii moja mahsusi bali ni wa ulimwengu mzima. Ingawa, kwa mfano, inaelezwa kwamba Yesu Kristo alitokana na ukoo wa Daudi, yeye anachukuliwa na Wakristo wote kote duniani kama mkombozi wao. Mtume Muhammadi ni shujaa na Mtume wa Waislamu wote duniani ilhali Buddha ni shujaa wa Wahindi wote kote duniani.

Ingawa huenda ikaonekana kana kwamba tunamrejelea Fumo Liyongo kama shujaa wa Waswahili tu, ama kwa hakika, yeye si wa Waswahili tu bali jamii zingine pia hujihusisha naye na hudai kuwa ni wao. Hata hivyo, tunachukulia kuwa kitovu chake ni katika jamii ya Waswahili. Wasegeju, Wabajuni na Wapokomo pia hudai kuwa Liyongo alikuwa ni shujaa wao. Katika kuelezea kuhusu asili ya Wabajuni, Nurse (1994:69) katika mahojiano yake na mmojawapo wa Wabajuni, alielezwa kuwa Fumo Liyongo alikuwa Mbajuni. Mjadala ulikuwa kama ifiatavyo:

Swali: Fumo Liongwe alizaliwa wapi?

Jibu: Fumo Liongwe alikuwa huko Shungwaya. Fumo Liongwe ni Mbajuni. Alizaliwa na kulelewa huko shungwaya...(Tafsiri Yangu)

Werner (1915:333) naye anaeleza kuwa alifahamishwa na mmojawapo wa kijumbe mtoa habari kuwa Fumo Liyongo alikuwa Msegeju. Anasema:

Kijumbe mmoja mtoa habari alinieleza nikiwa huko Witu kuwa Liongo alikuwa Msegeju; taarifa hii inaweza kuwa yenye umuhimu kuhusiana na asili ya Wasegeju ambao kwa kiasi fulani inatatanisha...(Tafsiri Yangu)

Shaka Zulu kwa upande wake pia hakuwa jagina wa Wazulu pekee Alikuwa pia jagina wa jamii nyingi (makabila) alizoziunganisha katika kuiunda jamii moja pana ya Wazulu. Vilevile, alikuwa jagina wa jamii nyingine nyingi na hususan zilizoguria katika sehemu mbalimbali wakati na baada ya vita vya *mfecane*. Baadhi ya watu katika jamii hizi ni kama vile, Watswana, Wandebele na Wasotho. Wazulu wengi walioana na makabila mengine ya Wabantu na kwa hiyo jamii nyingi zilimchukulia Shaka kuwa shujaa wao. Si ajabu kwamba hata sasa, Shaka anachukuliwa na taifa lote la Afrika Kusini na pia jamii nyingine katika mataifa yaliyo kusini mwa Afrika na ulimwengu mzima kwa jumla kuwa shujaa wao. Hata mie, ninamchukulia kuwa shujaa wangu (kama pia ninavyowachukulia Liyongo na vilevile Yesu Kristo) kwa vile baada ya kusoma maelezo anuwai kumhusu, aliniathiri pakubwa na hasa katika namna ya kuyatazama mambo - mtu anaweza akaonekana duni tu na kudharauliwa (kama alivyokuwa Shaka) lakini kutokana na uvumilivu na ari yake, huenda baadaye akainuka na kuvuma miaka na dahari na hivyo kuwatahayurisha daima mahasimu wake. Isitoshe, jina la Shaka na vitushi vyake vimesifika kote ulimwenguni na watu kwa njia moja ama nyingine hupenda kujihusisha naye - kwa mfano, katika kuzisoma kazi za kitawasifii zilizoandikwa kumhusu.

Kwa mujibu wa Omer-Cooper (1966:48), jina 'Zulu' lilivuma ajabu kutokana na mchango wa Shaka, hivi kwamba linatumika kuwarejelea hata wazungumzaji wengine wa lugha za Kinguni. Anadai kuwa umaarufu wa jina hili pamoja na kwamba Wazungu aghalabu hilitumia bila mpango wowote katika kurejelea wazungumzaji wote wa lugha za Kinguni za Kibantu katika eneo la Natal, ni jambo ambalo limepelekea watu wengi ambao hawakuwa chini ya himaya ya Shaka kuamini na kujihisi kama walio pia Wazulu. Isitoshe, jukumu lilioasisiwa na Shaka la kuhakikisha kuwepo kwa umoja wa jamii ya Wazulu ni suala ambalo linaendelea hadi sasa. Kwa jumla, jamii nyingi za kusini mwa Afrika wakiwemo pia watu wengine duniani wanapenda kujihusisha pakubwa na jamii ya Wazulu pamoja na shujaa wao, Shaka Zulu.

3.3.1 Jamho au kitu chochote kizuri katika jamii huhusishwa na shujaa

Jagina hupewa nafasi kubwa zaidi na wanajamii wa kipindi chake na hata wale wa vipindi vya baada ya mauko yake. Hadhi ambayo jagina hutunukiwa na wanajamii huwa ya juu zaidi na hali hii huwafanya wanajamii kulihusisha jambo, dhana au kitu chochote kizuri na shujaa wao. Si ajabu shujaa wa jamii fulani kutajwa kuwa ndiye mwasisi wa kitu, jambo au dhana fulani nzuri katika jamii hata kama siye aliyeasisi. Hali ya shujaa kuchukuliwa kuwa ndiye mwasisi hutokana na imani ambayo wanajamii huwa nayo kwa shujaa huyo. Iwapo mtu yeyote yule katika jamii atajitokeza na kuasisi jambo, kitu au dhana nzuri, kuna uwezekano wa wanajamii kueleza kuwa alikuwa amepewajukumu hilo na shujaa wao na kwamba analifanya kwa niaba ya shujaa

Shaka Zulu anadaiwa ndiye mwasisi wa mkuki mfupi (*assegai*) ambao ulifanikisha ushindi dhidi ya maadui waliokuwa wakiitumia mikuki mirefu iliyorushwa kutoka mbali. Hivyo ndivyo Wazulu wakiwemo watu wengine kote duniani wanavyoamini hadi sasa. Isitoshe, wanahusisha vipengele vingi vya utamaduni wao kama vilivyoasisiwa na Shaka na huwa tayari wakati wowote kuhakikisha kuwa tamaduni hizi zinafiindishwa na kurithishwa vizazi vya baadaye.

Kuna uwezekano kuwa Shaka siye aliyeasisi matumizi ya *assegai* na kwamba ala hii ya kivita iliasisiwa na Dingiswayo. Shaka aliyapata mafunzo yake ya kivita wakati alipokuwa akihudumu katika jeshi la Dingiswayo. Ingawa alikuwa mbunifii, aliyatoa baadhi ya mafunzo kuhusu mbinu na mikakati ya kivita kutoka kwa mafunzo yake ya awali. Ari na juhudi zake za kulikuza jeshi lake na kuiendeleza mikakati na mbinu za kivita kwa msukumo mkubwa zaidi, ndizo zilizowafanya wanajamii kumhusisha Shaka na uasisi wa mbinu na mikakati hii miongoni mwa masuala mengine ya kitamaduni katika jamii ya Wazulu.

Fumo Liyongo naye anachukuliwa kuwa ndiye mwasisi wa ngoma za gungu na mwao na kwamba alikuwa mshairi mahiri aliyeyatongoa mashairi na nyimbo na hivyo kuwavutia watu wengi - watu hawa walijitokeza ili kumsikiliza na kushiriki katika

utongoaji. Maulama wengi wanamtazama Fumo Liyongo kama mshairi. Jambo hili ni dhahiri na hususan tunapoyachanganua mashairi na nyimbo anazodaiwa kuwa alizitunga. Hata hivyo, kuna uwezekano kwamba kuna baadhi ya mashairi na nyimbo ambazo zinahusishwa naye ingawa si yeye aliyemitunga. Ikumbukwe kuwa, fasihi simulizi ilichukuliwa kuwa mali ya jamii nzima na hakuna mtu aliyedai umiliki wa utungo fulani. Tungo hizi hazikupewa anwani wala kubeba jina la mtunzi na kwa hiyo, ilikuwa vigumu kuuhusisha utungo fulani na mtu mahsus. Hata hivyo, wanajamii wa kipindi cha halafu huzihusisha baadhi ya tungo na jagina wao na kuchukulia kuwa, hiyo ni hidaya ya jagina kwa wanajamii. Kuna uwezekano kuwa Liyongo siye mtunzi wa baadhi ya tungo anazohusishwa nazo. Hata hivyo, vizazi vya baadaye vimechukulia kuwa yeye ndiye mtunzi asilia.

Hali hii ya majagina kuhusishwa na uasisi wa jambo, kitu au dhana yoyote muhimu katika jamii ni hali ya kawaida inayokubaliwa na wanajamii wenyewe wakiwemo maulama kadhaa. Dhana kwamba, kitu chochote duniani ni lazima kiwe na asili huwafanya wanajamii kuyachukulia masuala muhimu kama hidaya kutoka kwa jagina au hata kwa Mwenyezi Mungu.

3.3.2 Usaliti na kifo cha jagina

Mashujaa hawafi vivi hivi tu - vifo vyao huwa ni vya ajabu kama ambavyo wao walivyo wa ajabu. Baadhi yao hufa baada ya kushambuliwa tu katika sehemu fulani kwenye miili yao au mahali pengine panapohusiana na miili yao (kama vile, shambulio kwenye kivuli). Uwezo na nguvu za Samsoni, kwa mfano, zilikuwa zimehifadhiwa kwenye nywele zake na Wafilisti hawangeweza kumwangamiza iwapo hawangetafuta njia ya kuzikata kwanza. Lwanda Magere, shujaa wa Wajaluo naye angedhuriwa tu iwapo maadui wangekifima kivuli chake. Vivyo hivyo, Liyongo pia hangeathirika ila tu pale ambapo angetiwa msumari wa shaba kwenye kitovu chake. Tunaeleza haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**143. Nisikiya wangu baba
liniuwalo ni haba
ni msumari wa shaba
kitovuni nikitiya.**

**144. Jamii silaha piya
haziniuwi swabiya
ila nimezokwambiya
Ni ya kweli yo'te piya.**

Liyongo mwenyewe katika nyimbo zake, anakiri ya kwamba mikuki na hata mishale haiwezi ikamwangamiza na kwamba maadui zake walimwona kama moto au jini - kwa vile ilikuwa muhali kumwangamiza baada ya kufanya majaribio kwa mara kadhaa. Katika *Utumbuizo wa Kumwongoa Mtoto*, tunaieleza kuhusu Wagalla walivyoshindwa kumwangamiza Liyongo na hivyo kumwona kama aliyekuwa jini na vilevile moto (hawezi kushikika):

Utumbuizo wa Kumwongoa Mtoto

**... Wakarudi asi za Muungu, kamwambiya Fumo Mringwari
Hawezeki Liyongo ni moto si kiumbe huyule ni nari
Hawezeki Liyongo ni jini awezao nyani kumughuri.**

Hali hii pia inadhihirika katika *Utumbuizo wa Kikowa* ambapo tunaieleza.

Utumbuizo wa Kikowa

**...Kafuma ngaa huyu si mtu yu nga jini
Liyongo Fumo hakufikilika, hodari Liyongo kuuka.**

Kwa vile mashujaa huwa hawafi vivi hivi tu, maadui zao hutumia njama za kuwaangamiza kwa kuwatumia wasaliti. Wanawake katika historia za jamii nyingi duniani na hata katika kazi bunilizi wametumiwa na maadui katika kuwaporomosha majagina au nguli. Wanawake hawa huwa wake au wapenzi wa majagina hawa. Wanawake hawa hutumiwa ili kudadisi kile ambacho humuua jagina au sehemu ambayo jagina hudhuriwa ili apate kufa. Kwa kawaida wao huvuruga saikolojia ya wanaume kwa kujidekeza na kujifanya wanyonge kwa muda mrefu. Unyonge' huu aghalabu hutokana na ile picha ambayo mwanamke humsawiria jagina; kwamba anaogua moyoni kutokana na kutojua kile ambacho huweza kumwua 'bwanake' au 'mpenziwe'. Kufichuka kwa siri hii huwa ndicho chanzo cha kuporomoka kwa jagina. Shujaa huwa hakai hai kwa siku nyingi baada ya siri ya asili ya kifo chake kufichuka. Baada ya wanawake hawa kuipata siri waitafitayo, wao hupotelea mbali mara moja na kwenda kuwapa adui siri. Si ajabu kwamba mashujaa wengi hawapendi kuoa wanawake kwa vile wengi (kama vile, Shaka Zulu) huwaona kama wasaliti.

Licha ya wanawake, wasaliti wengine wa mashujaa huwa ni jamaa wa karibu sana kinasaba au marafiki wa mashujaa ambao huzijua siri za mashujaa nje ndani. Fumo Liyongo alisalitiwa na mwanawe ilhali Shaka Zulu alisalitiwa na msaidizi wake ^a

utongoaji. Maulama wengi wanamtazama Fumo Liyongo kama mshairi Jambo hili ni dhahiri na hususan tunapoyachanganua mashairi na nyimbo anazodaiwa kuwa alizitunga. Hata hivyo, kuna uwezekano kwamba kuna baadhi ya mashairi na nyimbo ambazo zinahusishwa naye ingawa si yeye aliyezitunga. Ikumbukwe kuwa, fasihi simulizi ilichukuliwa kuwa mali ya jamii nzima na hakuna mtu aliyedai umiliki wa utungo fulani. Tungo hizi hazikupewa anwani wala kubeba jina la mtunzi na kwa hiyo, ilikuwa vigumu kuuhusisha utungo fulani na mtu mahsusi. Hata hivyo, wanajamii wa kipindi cha halafu huzihusisha baadhi ya tungo na jagina wao na kuchukulia kuwa, hiyo ni hidaya ya jagina kwa wanajamii. Kuna uwezekano kuwa Liyongo siye mtunzi wa baadhi ya tungo anazohusishwa nazo. Hata hivyo, vizazi vya baadaye vimechukulia kuwa yeye ndiye mtunzi asilia.

Hali hii ya majagina kuhusishwa na uasisi wa jambo, kitu au dhana yoyote muhimu katika jamii ni hali ya kawaida inayokubaliwa na wanajamii wenyewe wakiwemo maulama kadhaa. Dhana kwamba, kitu chochote duniani ni lazima kiwe na asili huwafanya wanajamii kuyachukulia masuala muhimu kama hidaya kutoka kwa jagina au hata kwa Mwenyezi Mungu.

3.3.2 Usaliti na kifo cha jagina

Mashujaa hawafi vivi hivi tu - vifo vyao huwa ni vya ajabu kama ambavyo wao walivyo wa ajabu. Baadhi yao hufa baada ya kushambuliwa tu katika sehemu fulani kwenye miili yao au mahali pengine panapohusiana na miili yao (kama vile, shambulio kwenye kivuli). Uwezo na nguvu za Samsoni, kwa mfano, zilikuwa zimehifadhiwa kwenye nywele zake na Wafilisti hawangeweza kumwangamiza iwapo hawangetafuta njia ya kuzikata kwanza. Lwanda Magere, shujaa wa Wajaluo naye angedhuriwa tu iwapo maadui wangekifiima kivuli chake. Vivyo hivyo, Liyongo pia hangeathirika ila tu pale ambapo angetiwa msumari wa shaba kwenye kitovu chake. Tunaelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

**143. Nisikiya wangu baba
liniuwalo ni haba
ni msumari wa shaba
kitovuni nikitiya.**

**144. Jamii silaha piya
haziniuwi swabiya
ila nimezokwambiya
Ni ya kweli yo'te piya.**

Liyongo mwenyewe katika nyimbo zake, anakiri ya kwamba mikuki na hata mishale haiwezi ikamwangamiza na kwamba maadui zake walimwona kama moto au jini - kwa vile ilikuwa muhali kumwangamiza baada ya kufanya majaribio kwa mara kadhaa Katika *Utumbuizo wa Kumwongoa Mtoto*, tunaeleza kuhusu Wagalla walivyoshindwa kumwangamiza Liyongo na hivyo kumwona kama aliyekuwa jini na vilevile moto (hawezi kushikika):

Utumbuizo wa Kumwongoa Mtoto

**... Wakarudi asi za Muungu, kamwambiya Fumo Mringwari
Hawezeke Liyongo ni moto si kiumbe huyule ni nari
Hawezeke Liyongo ni jini awezao nyani kumughuri.**

Hali hii pia inadhihirika katika *Utumbizo wa Kikowa* ambapo tunaeleza:

Utumbuizo wa Kikowa

**...Kafuma ngaa huyu si mtu yu nga jini
Liyongo Fumo hakufikilika, hodari Liyongo kuuka.**

Kwa vile mashujaa huwa hawafi vivi hivi tu, maadui zao hutumia njama za kuwaangamiza kwa kuwatumia wasaliti. Wanawake katika historia za jamii nyingi duniani na hata katika kazi bunilizi wametumiwa na maadui katika kuwaporomosha majagina au nguli. Wanawake hawa huwa wake au wapenzi wa majagina hawa. Wanawake hawa hutumiwa ili kudadisi kile ambacho humuua jagina au sehemu ambayo jagina hudhuriwa ili apate kufa. Kwa kawaida wao huvuruga saikolojia ya wanaume kwa kujidekeza na kujifanya wanyonge kwa muda mrefii. 'Unyonge huu aghalabu hutokana na ile picha ambayo mwanamke humsawiria jagina; kwamba anaugua moyoni kutokana na kutojua kile ambacho huweza kumwua 'bwanake¹ au 'mpenziwe'. Kufichuka kwa siri hii huwa ndicho chanzo cha kuporomoka kwa jagina. Shujaa huwa hakai hai kwa siku nyingi baada ya siri ya asili ya kifo chake kufichuka. Baada ya wanawake hawa kuipata siri waitafiitayo, wao hupotelea mbali mara moja na kwenda kuwapa adui siri. Si ajabu kwamba mashujaa wengi hawapendi kuoja wanawake kwa vile wengi (kama vile, Shaka Zulu) huwaona kama wasaliti.

Licha ya wanawake, wasaliti wengine wa mashujaa huwa ni jamaa wa karibu sana kinasaba au marafiki wa mashujaa ambao huzijua siri za mashujaa nje ndani. Fumo Liyongo alisalitiwa na mwanawe ilhali Shaka Zulu alisalitiwa na msaidizi wake wa

karibu sana - kwa jina Mbopha - na kisha kuuawa na nduguze wa kambo, Dingane na Mhlangana. Shaka alifanyiwa haya yote baada ya shinikizo la muda mrefu baada ya shinikizo la shangazi yake Mkhabayi.

Kwa kawaida, wasaliti wa mashujaa mara nyingi huwa hawaishi duniani kwa muda mrefu baada ya shujaa kuporomoka. Yuda Iskarioti (taz. *Biblia Takatifu, Mathayo Mtakatifu* 27: 3-5) alijitia kitanzi baada ya kumsaliti Yesu Kristo; mwana wake Liyongo, kwa mujibu wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* alifariki kutokana na madhila aliyoyapata kutoka kwa jamaa zake. Hata hivyo, *Haciithiya Liyongo* inatuelezea kuwa mwanawe aliuawa na wanajamii. Tunaeleza, 'Wakamkamata Waka'mua, wasimpe ufaume' (Steere 1870: 452); Mbopha naye aliuawa na Dingane ambaye alimdhania kuwa pia naye angemsaliti kama alivyomsaliti Shaka.

3.3.3 Mashujaa aghalabu huwa hawarithiwi na wanao

Kwa kawaida, iwapo jagina ana watoto, watoto hawa huwa hawarithi ile hadhi au nafasi yake baada ya mauti yake. Ibainike kuwa jagina huzuka katika kipindi, muktadha na hali mahsusi katika jamii ili kutatua mgogoro au matatizo yaliyopo katika jamii yake. Si ajabu kuwa jagina kama tulivyodokeza katika sehemu iliyotangulia, hafi vivi hivi tu. Yeye hufa baada tu ya kuikamilisha dhamira yake. Na kwa hiyo, iwapo dhamira yake imekamilika, basi! Hahitajiki mtu mwingine kusimama kwenye pengo aliloacha shujaa. Ama kwa hakika, nafasi ya shujaa katika jamii yake huwa hairithiwi. Aidha, jagina huwa hamwandai mtu yeyote kuchukua mahali pake. Kifo chake huwa cha ghafla mno. Hali hii ndiyo huwafanya mashujaa wasirithiwe na wanao au hata na jamaa wengine katika jamii yake. Shujaa wa jamii fulani akiondoka, basi huchukuliwa kuwa hakuna pengo lililoachwa na kwamba jagina huyu amekamilisha dhamira yake.

Mwanawe Fumo Liyongo alimuua babake na hata baada ya babake kufa hakumrithi. Badala yake, hata naye pia alifariki baada ya siku chache kutokana na hujuma za wanajamii kwa tendo alilolitenda. Liyongo alikufa kwa wakati uliofaa na hata ingawa jamii ya Waswahili ilikuwa ikiomboleza, alikuwa tayari amekamilisha dhamira yake ya kuwaunganisha Waswahili na kuwaokoa kutokana na kero za maadui zao.

Shaka naye katika kuuawa kwake alikuwa tayari ametimiza dhamira yake - kuyaunganisha makabila madogo madogo na kuliunda taifa moja kubwa kabisa la Wazulu. Ingawa Dingane alichukua hatamu za uongozi, si kwamba alikuwa anachukua nafasi au mahali pa Shaka. Alikuwa tu akipapia matokeo ya juhudi za muda mrefii za mfalme na shujaa Shaka Zulu. Shaka alikuwa tayari ametimiza dhamira yake. Utawala wa Dingane ulikumbwa na misukosuko na hata hakuitawala jamii ya Wazulu kwa muda mrefu kama Shaka alivyotabiri wakati wa kifo chake. Dingane alikabiliana na walowezi wa Kizungu ambao hatimaye walimporomoshwa.

3.3.4 Shujaa huwa ⁴hafP na hukumbukwa daima

Suala hili ni dhahiri shahiri hadi kufikia hapa. Watu wa kawaida (tofauti na mashujaa) hufa na husahaulika baada tu ya miaka michache. Wanajamii huwa hawaamini kuwa shujaa wao kafa na wengi huchukulia kuwa ameenda safari na atarudi siku moja. Kwangu mimi kuweza kutafiti mashujaa walioishi takriban zaidi ya karne mbili zilizopita ni thibitisho ya madai kuwa shujaa huwa hai miongoni mwa vizazi na vizazi. Kwa miaka na dahari, Fumo Liyongo na Shaka Zulu watazidi kukumbukwa na kufanyiwa utafiti sio tu na watu kutoka jamii zao bali pia na maulama anuwai kutoka katika pande mbalimbali za ulimwengu kwa jumla - kuna kazi nyingi zaidi, hii ikiwemo, ambazo zimeandikwa na zitakazoendelea kuandikwa ili kujaribu kuwasawiri kwa kina majagina hawa wawili. Kazi hizi zitawapa vizazi vijavyo taswira halisi ya mashujaa hawa.

Wengi wa majagina wa kihistoria wa kijamii wakiwemo pia wale wa kidini (Mtume Muhammadi, Yesu Kristo na Buddha miongoni mwa wengine) hukumbukwa daima. Kila jamii huwa na wajibu wa kuwafunza watoto wake kuwahusu mashujaa wao ambao wametokea katika mazingira, vipindi na hali mbalimbali katika jamii hiyo. Jamii moja inaweza ikawa na zaidi ya shujaa mmoja lakini ni muhali kwa mashujaa wawili kutokea katika hali na kipindi kimoja katika jamii. Aidha, katika kukumbukwa, mashujaa hawa hutungiwa nyimbo, tenzi, mashairi; pia, maandishi chungu nzima huandikwa kwa maumbo mbalimbali na kuhifadhiwa kama kumbukumbu kwa minajili ya vizazi vijavyo.

3.3.5 Umuhimu wa shujaa kwa jamii yake

Kila shujaa huwa na umuhimu mkubwa kwa jamii yake. Hii ni sifa mojawapo muhimu sana ya majagina. Suala hili tutalishughulikia katika faslu ya nne kwani linajitokeza kama madhumuni mojawapo katika utafiti wetu na linastahili kuchunguzwa kwa jicho kali. Aidha, ni vema tukumbushe hapa kuwa kuna ukuruba wa aina fulani katika sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao kama tutakavyoona hapo baadaye.

3.4 Hitimisho

Hadi kufikia hapa, tunapata kuwa sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na zile za Shaka Zulu zinafanana kwa kiasi kikubwa. Tofauti tulizoziona ni katika utabiri wa kuzaliwa kwao na suala la ndoa. Katika kubainisha utabiri wa kuzaliwa kwa Fumo Liyongo, tulipata kuwa hatuna data - kwenye maandishi - inayothibitisha kuzaliwa kwake na jambo hili hasa linatokana na kuwa Liyongo aliishi katika kipindi cha zamani mno akilinganishwa na Shaka Zulu. Huenda mambo mengi ya kuzaliwa kwake kama ilivyo kuhusu ujana wake yakawa yamesahaulika. Kuhusu suala la ndoa, mtazamo wa Liyongo kama tulivyothibitisha ni tofauti kwa kiasi kikubwa na ule wa Shaka Zulu. Sifa zingine zote zinashabihiana pakubwa. Hali hii inashadidiwa na matumizi ya nadharia ya vikale kama tulivyoeleza katika faslu ya kwanza.

TANBIHI

1. Ingawa Dkt. Garang alikuwa na shahada ya uzamifu (Ph D), alitumia miida wake mrefu huko msituni katika harakati za kupigania haki za watu wa kusini mwa Sudan Aliliongoza jeshi la ukombozi wa watu wa Sudan (SPLA) katika mapambano makubwa ajabu dhidi ya senkali ya Kiislamu - iliyokuwa na makao yake makuu katika mji wa Khartoum - kwa zaidi ya miongo miwili. Serikali ya Sudan, kwa muda mrefu, ilikuwa ikitumia rasilmali zake katika kuendeleza maeneo ya kaskazini yaliyomilikiwa na Waislamu na kuyatenga maeneo ya kusini yaliyokuwa yakimilikiwa na Wakristo. Baada ya jeshi la SPLA kuzua vurugu na kukazana kiume ili kuhakikisha kuwepo kwa usawa katika ugawanyaji wa rasilmali za nchi ya Sudan, serikali ya Sudan ililazimika hatimaye kutia sahihi inkataba wa amani nchini Kenya (tarehe. 2 Januari,2005) ili kusitisha mapigano ya muda mrefu ya wenyewe kwa wenyewe. Makubaliano haya ya amani, yalinuia kuhakikisha kuwa utajiri (rasilmali) na uongozi wa nchi ya Sudan unagawanywa kwa njia iliyo sawa baina ya maeneo ya kaskazini na vale ya kusini mwa Sudan, kuwepo kwa uchaguzi wa kidemokrasia baada ya miaka mitatu na kuwepo kwa kupigwa kwa kura ya maoni kuhusiana na kujitenga kwa eneo la kusini kutoka kwa lile la kaskazini.

Wiki tatu tu baada ya kuapishwa kwake (aliapishwa tarehe 9 Julai, 2005) kama makamu wa rais wa kwanza wa serikali ya Sudan, chini ya makubaliano ya amani yalivotiwa sahihi mnamo mwezi wa Januari 2005 nchini Kenya, alikufa (tarehe 30 Julai 2005) katika ajali ya helikopta huko kusini mwa Sudan katika bonde la Kidepo. Alikuwa akielekea nyumbani baada ya ziara yake ya kukutana na rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni huko Mbarara nchini Uganda. Wasaidizi sita wa Dkt. Garang wakiwemo pia wahudumu saba wa ile helikopta waliangamia pamoja naye. Kifo cha Dkt. Garang kiliwasikitisha watu wengi waliokuwa wanampenda kwa dhati. Hata hivyo, dhamira yake ya kuregesha amani na usawa baina ya watu wote wa Sudan alikuwa tayari aineitimiza. Jambo hili ni kaida ya majagina wote duniani - wengi wao hufa muda mfiipi tu baada ya kutimiza dhamira zao.

FASLU YA NNE

UMUHIMU WA FUMO LIYONGO NA SHAKA ZULU KWA JAMII ZAO

4.0 Utangulizi

Hadi kufikia hapa, tumepata kuona kuwa majagina huwa wamepewa nafasi kubwa mno katika mfumo mpana wa jamii wanamopatikana. Wao si watu vivi hivi tu. Jamii nzima huwategemea pakubwa ajabu. Baada ya kuzirejelea zile sifa bia za mashujaa - Fumo Liyongo na Shaka Zulu na kuelezea historia zao zikiwemo zile za jamii zao, tuna nafasi nzuri ya kuelezea umuhimu wa mashujaa hawa kwa jamii zao. Ni vyema tukumbuke hapa kuwa umuhimu au mchango wa mashujaa huwa bia; hujitokeza katika mashujaa wa jamii mbalimbali kote duniani.

Kama tulivyokwisha kuona, jamii ni mfumo ambao huwa na mijiftimo mingi (taasisi) ndani yake. Kila mojawapo wa mijiftimo hii huwa na uamilifu wa kuendeleza, kudumisha au kusawazisha hali mbalimbali katika jamii ili kuunda jamii imara au 'kamilifu'. Mojawapo wa taasisi muhimu katika jamii ni utamaduni. Utamaduni huwa na taasisi nyingine ndani yake. Mojawapo ya taasisi hizi ni 'taasisi ya ushujaa'. Mashujaa katika jamii huchukua nafasi kubwa mno na huwa hasa na lengo la kusawazisha au kuleta mabadiliko fulani katika hali ambazo aghalabu huwa zimeenda mvange. Kwa hiyo, jukumu kuu la taasisi ya shujaa ni kuubadilisha mfumo wa jamii nzima kwa manufaa ya wanajamii. Jagina huzuka kwa ajili ya wanajamii na hivyo oasi, chochote akitendacho huwa cha manufaa kwa jamii nzima. Taasisi ya shujaa hushirikiana na taasisi nyingine katika jamii (wakiwemo wanajamii) kwa manufaa ya jamii nzima.

Katika faslu hii, tutaonyesha wazi umuhimu au mchango wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamii zao.

4.1.0 Umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu

4.1.1 Fahari ya watu weusi

Hakuna jambo nzuri na linaloridhisha maishani kama lile la mtu kujivunia alichonacho. Matokeo ya juhudi za mtu na hususan yakiwa mazuri humsisimua na kumpa fahari kuwa hata yeye pia anaweza akajihesabu miongoni mwa watu mahiri waliofanikiwa katika nyanja mbalimbali. Vivyo hivyo, mbali na kujivunia masuala mengine ya kitamaduni, kila jamii hujivunia shujaa wao ambaye huwa wamempa sifa za kiajabuajabu. Waaidha, kama tulivyodokeza, wao humtazama kama mkombozi wao. Isitoshe, iwapo jagina huyu ametekeleza dhamira yake kwa umma wake kwa ukamilifu, jamii humwajabia maishani mwake mwote na hata baada ya mauko yake.

Juhudi za jagina katika jamii yake hufurahiwa na kukumbukwa dahari. Wanajamii hujivumua jagina wao hivi kwamba wao huchukua jukumu la kufunza vizazi na vizazi vya halafu kumhusu shujaa huyo. Katika kufiindisha kuhusu majagina ulimwenguni, walimu wa Kiafrika katika shule hulinganisha majagina wa Kiafrika na kujaribu kuonyesha ukuruba uliopo baina ya vitushi na maumbile ya majagina hawa wote.

Ama kwa hakika, Fumo Liyongo na Shaka Zulu miongoni mwa mashujaa wengine wa Kiafrika ni majagina ambao ni fahari kubwa ya watu weusi. Fumo Liyongo na Shaka Zulu sio tu fahari ya Waswahili au Wazulu pekee. Wao ni fahari ya watu weusi kote ulimwenguni. Vitushi vyao, uwezo wao na maumbile yao huwastaajabisha watu wengi hadi leo. Mashujaa hawa, kwa kiasi kikubwa, hawakutegemea wageni kutoka ng'ambo kuimarisha na kupanua milki zao - kutimiza dhamira zao. Walitekeleza dhamira zao kwa kutumia rasilimali na mbinu za kienyeji zenye taathira kubwa katika kutekeleza masuala makubwa ajabu. Kwa hiyo, sisi kama Waafrika tunajionea fahari na kujivunia juhudi za mababu hawa watajika hadi wa leo.

Si ajabu kwamba, ingawa Waafrika walichukuliwa na Wazungu kuwa washenzi, ndani ya ushenzi huu mlikuwemo na ufahari na ustadi mkubwa na husasan kwenye mifumo ya miundo misingi ya Waafrika wenyewe. Utawala bora wa majagina, upanuzi wa milki zao, ulinzi wa watu wake, utangamano wa umma wake, matumizi ya mbinu na mikakati maridhawa za kivita na ukuzaji wa utamaduni wa jamii zao ni masuala yanayoonewa fahari na wanajamii na pia watu wengine kutoka katika uga wa

kimataifa. Kwa jicho la mbeberu, Mwafrika ni mshenzi ilhali tamaduni zake ni za kishenzi; lakini kwa jicho la Mwafrika, yeye mwenyewe ni mstaarabu na tamuduni zake ni zenye ustaarabu wa hali ya juu, ambao kwa kiasi kikubwa umetetewa na kuendelezwa na majagina wao. Jambo hili ama kwa hakika ni fahari kubwa kwa watu weusi. Waafrika walikuwa na taasisi na njia za maisha (tamaduni) ambazo zilifuata taratibu maalum zilizokubaliwa na wanajamii walio wengi. Kulikuwa na mflimo maridhawa wa utozaji kodi, uamuzi wa kesi, njia za kuabudu, njia za uzalishaji mail (kilimo, biashara, uvuvi, uwindaji, useremala miongoni mwa shughuli nyingine), ndoa, tohara, maziko, uhifadhi wa mazingira, njia za kuwakumbuka mashujaa wao miongoni mwa mbeko na tamaduni zingine.

Kwa jumla, sifa na matendo ya mashujaa wa Kiafrika hudhihirisha uwezo wa ngozi nyeusi katika kujikomboa kutoka katika hali duni na kupaa hadi katika ngazi za ufanisi mkubwa ajabu.

4 1 2 Kitambulisho cha kitaifa / kijamii

Suala jingine linaloana na lile la shujaa kuwa fahari ya watu weusi ni ile hali ya jagina kuwa kitambulisho cha taifa au cha jamii yake. Shujaa wa jamii fulani huwa kama kipengele kikuu (kiunzi) - katika mflimo mzima wa jamii yake- kinachofungamanisha vipengele vingine vyote katika jamii ile. Jambo hili lina maana kuwa, kwa kumtaja tu shujaa fulani, basi itakuwa kana kwamba unarejelea kwa jumla jamii anayoiwakilisha. Kwa kumtaja tu jina Shaka Zulu katika uga wa kimataifa, utakuwa kwa kiasi kikubwa, hata bila wewe mwenyewe kujua, ukirejea jamii pana ya Wazulu. Jamii ya Wazulu inatambulikana kote duniani kutokana na Shaka mwenyewe. Jamii hii, kwa kiasi kikubwa, haitambulikani pakubwa kwa sababu ya taasisi au tamaduni zake ainati bali hutambulikana kutokana na Shaka mwenyewe; yaani, Shaka ni kipengele kimoja muhimu kabisa amabacho aghalabu kikitolewa, jamii ile itaachwa 'ukiwa' au 'uchi' Yumkini, Shaka Zulu mwenyewe anaweza akachukuliwa kuwa jamii yenyewe. Si ajabu kwamba mtu huenda asijue jambo lolote lingine kuhusu tamaduni za jamii ya Wazulu lakini akawa anamfahamu Shaka Zulu. Isitoshe, ni muhali kutaja taifa la Zulu au kufanya utafiti kuhusiana na jamii ya Wazulu pasipo kumtaja Shaka. Kwa hiyo, Shaka (kama walivyo mashujaa wengine) ana umuhimu mkubwa katika kuitambulisha jamii yake na hususan katika ngazi za kimataifa.

Vivyo hivyo, Liyongo naye ni kitambulisho cha jamii ya Waswahili. Ingawa aliishi miaka mingi mno iliyopita, maumbile na matendo yake ya kiajabu yamewavutia maulama wengi wakiwemo pia watu wengine wa kawaida Maulama wa awali kama vile Edward Steere hawakusita kukusanya hadithi na masuala mengine muhimu kumhusu Liyongo wakiwa katika muktadha wa mazingira ya jamii ya Waswahili

Waswahili wanajitambulisha pakubwa na Liyongo na jambo hili linadhihirika katika mtazamo wao kumhusu hata baada ya miaka mingi ya mauti yake. Steere (1870:vi) anaonyesha umuhimu wa Liyongo katika kuziathiri nafsi za watu wa jamii yake. Anaeleza:

Hakuna mtu ajuaye kwa yakini ni lini Liyongo alipata kufa lakini kumbukumbu kumhusu zimehifadhiwa katika hali ya kuvutia na uchangamfu mkubwa katika mioyo ya Waswahili. Jambo la kushangaza ni kwamba, kutajwa tu kwa jina lake huibua hisia za takriban kila Mswahili halisi. (Tafsiri Yangu)

Ingawa Wapokomo, kama tulivyokwisha kuona katika faslu ya pili, wanadai kuwa Liyongo alikuwa mbaya, Waswahili kwa upande wao wanamwonea fahari kwa vile aliwasaidia kijikomboa kutokana na dhuluma na unyanyasaji wa maadui zao. Kwa hiyo, Liyongo na jamii yake ni mamoja. Tunapomsawiri Liyongo, tunamsawiri katika manzili ya jamii ya Waswahili na kwa hiyo, ana umuhimu mkubwa katika kuitambulisha jamii hii. Hata ingawa Wapokomo, Wabajuni na Wasegeju wanadai kuwa Liyongo alikuwa shujaa wao, yeye sana sana anaonekana kujihusisha au kujitambulisha na jamii ya Waswahili ambayo inampenda na kumwajabia ajabu.

4.1.3 Kioo cha jamii / historia ya jamii

Kama vile fasihi ilivyo kioo cha jamii, vivyo hivyo, tunaweza tukamchukulia shujaa wa jamii fulani aliyeishi katika kipindi fulani kuwa kioo cha jamii hiyo. Ni bayana kuwa, kama tulivyodekeza hapo awali, madhila, mateso, dhuluma, ufanisi na masuala mengine yote yanayomkumba jagina huakisi pakubwa hali ilivyo katika mfumo mzima wa jamii yake. Kwa hiyo, shujaa huwa kama kiwakilishi cha jamii na hasa katika kipindi cha kihistoria anachozuka au kuishi. Kwa kumtalii shujaa, tunaweza tukapata taswira kamili ya mfumo wa jamii ile; tunaweza tukaelewa kwa kina mfumo wa

kijamii, kiuchumi, kisiasa, mila, desturi na masuala mengine anuwai ya kitamaduni kuihusu jamii yake. Tumetaja mara kadhaa kuwa jagina huzuliwa na hali fulani katika kipindi fulani cha jamii yake. Hali hii aghalabu huwa si ya kuridhisha na huhitaji ukombozi wa aina fulani ambao kwa kiasi kikubwa hutokana na jagina. Kwa kumtalii jagina tangu kabla ya kuzuka kwake na hata pia maishani mwake, tunaweza tukapata taswira kamili kuihusu historia ya jamii anayoiwakilisha

Kwa hiyo, katika kuwatalii Shaka Zulu na Fumo Liyongo - toka kuzuka kwao, maisha waliyoishi na hata kufa kwao - tumekuwa na nafasi nzuri ya kuihakiki jamii ya Waswahili na pia ile ya Wazulu. Tumeonyesha dhahiri kuwa, jamii hizi zote zilikumbwa na mizozo ya kivita iliyozuliwa na makundi (makabila) anuwai; dola mbalimbali zilitawaliwa na wafalme; kulikuwa na ung'ang'aniaji madaraka ambao ulipelekea kutumika kwa njama ovu za usaliti, uviziaji na uvinjari; kuwepo kwa masuala mengine kama vile wizi, uvamizi, ndoa, dini, biashara, tohara, mapenzi, mauaji, kilimo, ufugaji, sheria, ngoma; hususan masuala yote ya tamaduni za jamii ambamo mashujaa hawa walipatikana.

Kwa kuwatalii majagina hawa (kwa mintarafu ya tungo walizozitunga na hata tungo zilizotungwa na maulama wengine kuwahusu) tumeweza pia kupata taswira ya mandhari /mazingira yaliyomo katika jamii zao. Shujaa huwa anagura kutoka jamii moja hadi nyingine na kwa hiyo tumeonyeshwa baadhi ya miji ambamo Shaka na Liyongo waligurua au kutembelea. Tumetajiwa miji kama vile Dukuza, Pate, Bulawayo, Shaka, Ozi miongoni mwa miji mingine. Tumeelezwa pia kuwa kulikuwepo na milima; mito (kwa mfano, Mto Tana ambapo Liyongo alienda mara kwa mara kuoga; Mto Thukela na Mto Mhlathuzi, taz. M. Kunene 1979:137-139, ambapo majeshi ya Zwide yalipigwa vita na majeshi ya Shaka hadi kufikia hatua ya kuzamishwa katika mito hiyo; miti (minazi, mikoma); ndege (kwa mfano, mbayuwayu, kozi, tai - waliofuata vikosi vya kijeshi hadi medani kwa vile walijua kuwa minofu ya miili ya wanadamu ingepatikana kwa wingi kabla ya jua kutua; wanyama wa mwituni (kama vile simba, ndovu, nyoka); mabonde; genge; miongoni mwa masuala mengine. Aidha, tuna zana za kivita kama vile mishale, mikuki, ngao, mikuki mifupi (*assegai*), fumo, mata na panga

zilikuwa miongoni mwa jamii zao na zinahusishwa kwa kiasi kikubwa na mashujaa hawa.

Maingiliano na jamii zingine na hususan kutokana na biashara yanadhihirika katika tungo zinazowahusu mashujaa kote duniani. Tunapotazama baadhi ya tungo zinazodaiwa kuwa zilitungwa na Fumo Liyongo, tunaona baadhi ya vifaa kutoka Ulaya, maeneo ya Mashariki kama vile Uchina, Uhindi, Uajemi na Uarabuni; ilhali zingine zilitoka katika jamii zingine kutoka janibu za pwani. Hebu tushadidie madai haya kwa kurejelea utungo mojawapo:

Utumbuizo wa Mwana Mnazi

**...Nitiyani hoyo Time aye, na anguse ate masindizi
Apakuwe pilau va Hindi, mzababu isiyo mtuzi
Ete kiti chema cha Ulava na siniya niema va Shirazi
Kimlisha akimpa hiba kimuonya yakeye maozi...
Kimlisha tambuu va Sivu yi laini laini ya Ozi...**

Licha ya kuingiliana na jamii zingine za Afrika Kusini, Shaka aliingiliana na Wazungu walowezi na hata akafikia hadi hatua ya kuwapa ardhi katika sehemu za pwani (za bandarini) za eneo la utawala wake. Isitoshe, alimchagua Farewell kama mkuu wa eneo lililomilikiwa na walowezi hawa. Shaka alijitia katika ushirika wa Wazungu hawa ili kwa kiasi fulani yeye na jamii yake wafaidi na zana zao za kivita miongoni mwa bidhaa zingine kutoka kule Ulaya. Kwa hiyo, tofauti na Liyongo ambaye hatumwoni akiingiliana na Wazungu, Shaka mwenyewe anafikia katika hatua ya kuwekeana mikataba nao akiwemo mfalme mkuu - mfalme George kutoka huko Ulaya. Alituma ujumbe wa mara kwa mara kwa mfalme huyu akitaka kujua nia au matamaniao yao hasa katika eneo lake la utawala.

Shujaa aghalabu kwa kiasi kikubwa ndiye huwa ameibeba historia ya jamii yake. Jamii yoyote ile hutilia maanani sana kipindi alichowahi kuishi shujaa kwani ni katika kipindi hiki ambapo mabadiliko makubwa ajabu huweza kutokea (hutolewa na jagina) katika mfumo wa jamii anamopatikana shujaa. Kwa hiyo, shujaa wa jamii yoyote ile huwa kipengele muhimu sana katika mfumo mzima wa jamii. Si ajabu kwamba, jamii (kwa mfano, ile ya Wazulu) inaweza ikakosa historia iwapo haina jagina. Kwa muda mrefii, historia ya jamii ya Wazulu imefumbatwa pakubwa kwenye Shaka mwenyewe na ni

muhali kutenganisha Shaka na historia ya jamii yake. Ama kwa hakika, Shaka ni historia tosha ya jamii ya Wazulu. Vivyo hivyo, Fumo Liyongo amechangia pakubwa katika usawiri wa historia ya Waswahili na hususan katika kuikomboa jamii yake kutokana na dhuluma za maadui wao. Jamii zenye majagina tajika wa kihistoria huwa na historia kwasi ambayo hutaamisi na kuhanikiza katika mitaala ya taasisi za kiusomi na pia hifadhi ya nyaraka na makavazi takriban katika kila nchi kote duniani.

Ikumbukwe kuwa Shaka alikuwa na nafasi kubwa katika mchakato mzima wa vita vya *mfecane* ambavyo viliacha athari si haba katika maeneo mengi ya kusini mwa Afrika. Jamii nyingi za kibantu ziligura kutoka maeneo yao wakati wa vita hivi vikuu na zikamiliki maeneo ambayo kwa hivi sasa ni mataifa huru. Baadhi ya mataifa haya ni kama vile Swaziland (Waswazi), Botswana (Watswana), Malawi (Wakololo), Msumbiji, Zambia na Tanzania. Baada ya kuguria katika maeneo haya, waliendelea dhana na mifiimo ya kitamaduni ya Wabantu wa kusini mwa Afrika na hivyo kuathiri baadhi ya makabila mengine waliyoyapata kwenye maeneo haya (hususan katika uratibu wao wa kiutawala na kijeshi yakiwemo mahusiano ya kijamii). Wangoni walioko huko Tanzania walikuwa miongoni mwa jamii zilizogura wakati wa vita hivi. Waliongozwa na mfalme Zwangendaba kutoka katika maeneo ya kaskazini mwa eneo lililomilikiwa na Wazulu (Omer-Cooper 1966:3-6). Kwa hiyo, tunapata kwamba, Shaka pamoja na vita alivyovienzi mno (vita vya *mfecane*), wamechangia pakubwa katika maenezi ya watu katika sehemu za kusini mwa Afrika. Cobbing (1988:505) ameionyesha ramani ambayo inatoa taswira ya namna watu walivyoguria sehemu mbalimbali kutokana na misukosuko ya kivita katika kipindi cha *mfecane*. Ramani hii pia inaonyesha njia zilizotumiwa kuwasafirishia watumwa ikiwemo miondoko ambayo Wazungu walifiiata katika kufikia sehemu mbalimbali za janibu za mashariki za eneo la kusini mwa Afrika. Tumeionyesha nakala ya ramani hii katika uk.165. Historia kuhusu asili ya jamii nyingi za maeneo haya, huchota pakubwa katika mchakato mzima wa vita vya *mfecane* kwa jumla.

Kwa jumla, majagina hawa huwa kama msingi ambapo maelezo ya kihistoria ya jamii zao huandikwa kama tulivyokwisha kuona. Maelezo haya husawiri mandhari ya kihistoria, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, hali zinazowakumba majagina huakisi

hali halisi ya jamii zao. Kwa hiyo, Fumo Liyongo na Shaka Zulu wana umuhimu mkubwa katika kuelezea historia ya jamii zao na ni muhali kuelezea historia ya jamii hizi pasipo kuwarejelea.

4.1.4 Ukuzaji wa utamaduni wa jamii zao

Utamaduni huhusu jumla ya vipengele vyote katika maisha ya jamii fulani Senkoro (1976:74) anaeleza kuwa utamaduni huhusu jumla ya njia zote za kuishi zinazoundwa na wanajamii katika harakati zao za maisha katika mazingira fulani ya kijamii. Anaendelea kufafanua kuwa utamaduni si ngoma wala mila tu. Utamaduni hujumulisha mambo mengi kama vile imani ya wanajamii, sayansi, njia za uzalishaji mali, sanaa, dini, mahusiano ya kijamii; hususan masuala yote ya maisha katika jamii yoyote ile. Kila jamii huwa na utamaduni wake unaofuata muundo wa jamii hiyo.

Hakuna utamaduni ulio bora kuliko mwingine. Kila utamaduni huafiki jamii mahsusi katika kipindi mahsusi. Hata hivyo, utamaduni wa jamii fulani unaweza ukabadilika kutokana na mapisi ya wakati na maingiliano kutoka jamii za nje. Maulama huweza kuchanganua tamaduni za jamii za kadimu kwa kuchanganua ngano, nyimbo, mashairi, methali, vitendawili na tanzu zingine za fasihi simulizi na hata fasihi andishi za jamii hizo. Utamaduni wa jamii fulani, kwa kiasi kikubwa, hufumbatwa katika fasihi ya jamii hiyo.

Ni kwa vipi shujaa huchangia katika ukuzaji wa utamaduni wa jamii yake⁹ Kutokana na nafasi ya jagina katika jamii katika kipindi anachoishi, yeye huwa na uwezo mkubwa na wakati mrefu wa kukuza utamaduni wa jamii hiyo. Aghalabu, yeye huwa kama egemeo katika takriban kila kipengele cha utamaduni wa watu wake na ana uwezo wa kuubadilisha mkondo wa maisha yao atakavyo. Licha ya kuzikomboa jamii zao kutokana na tisho la maadui na kupanua himaya zao, Shaka Zulu na Fumo Liyongo walileta mabadiliko makubwa katika vipengele mbalimbali (utamaduni) vya jamii zao. Hali hii, hadi kufikia hapa ni dhahiri shahiri - kutokana na maelezo anuwai ambayo tumetoa hapo kabla.

Waaidha, Fumo Liyongo na Shaka Zulu wanajitokeza kama watetezi na watendaji wa mila na desturi za jamii zao. Nyimbo na ughani wa mashairi ni miongoni mwa vipengele vya kitamaduni ambavyo walisaidia kukuza kwa kushirikiana pamoja na wanajamii wengine. Liyongo, kama tulivyoelezea hapo awali, alikuwa mshairi stadi na inadaiwa kuwa yeye ndiye mwasisi wa gungu na mwao. Ngoma hizi zimekuwa hai katika jamii ya Waswahili na zimekuwa zikichezwa katika hafla mbalimbali na hasa katika harusi. Aidha, kwa mujibu na Frankl (1993:130), ngoma ya gungu (ikijumlisha wimbo mmojawapo wa Liyongo) huwa inachezwa saa za asubuhi wakati wa kuamkia *Siku ya Mwaka*. Anasema:

Ngoma ya Gungu hujulikana kote katika maeneo ya Waswahili; Hata hivyo, huko Mombasa, ngoma hii huchezwa tu asubuhi ya kuamkia Siku ya Mwaka. Baadhi ya sehemu za nyimbo za gungu (yakiwemo pia mahadhi yake) hutofautiana na gungu kama ilivyo katika maeneo mengine ya Waswahili. Kwa jumla, kuna nyimbo tatu¹¹ za ngoma hii ambazo huchezwa, kila mojawapo ikiwa na mahadhi yake. Wanaume hucheza wakiwa wawili wawili ilhali wanawake huimba na kupiga makofi sawia na mdundo wa mahadhi ya nyimbo hizo... (Tafsiri Yangu)

Kama tulivyotaja katika sehemu iliyopita, nyimbo hizi, (nyimbo zinazodaiwa kuwa zilitungwa na Fumo Liyongo) kwa jumla, zimefiimbata vipengele muhimu katika utamaduni wa jamii ya Waswahili katika kipindi ambacho jagina huyu alipata kuishi.

Shaka Zulu naye alitetea na kukuza utamaduni wa jamii ya Wazulu pakubwa Kulikuwepo na uchezaji wa ngoma kwenye uga wa maonyesho (*arena*) na ambao ulihudhuriwa na Shaka mwenyewe. Isitoshe, Shaka alikuwa gunge katika uchezaji ngoma. Tena, vikosi vya kijeshi vilighani nyimbo vilipokuwa vinaenda vitani; kulikuwa na nyimbo wakati vipigana vita na adui kwenye medani; na pia, nyimbo za kutoka medani kuelekea nyumbani baada ya ushindi. Vilevile, kulikuwa na mashindano ya kukabiliana na fahali (wanajeshi kadhaa kutoka vikosi mbalimbali vya kijeshi walihitajika kumuua fahali mkubwa kwa kuipopotoa shingo yake bila kutumia kifaa chochote kile ila tu kwa mikono yao mitupu. Baada ya kufanikiwa, fahali yule aliandaliwa kama karamu kwa wale waliohudhuria); usimuliaji wa ngano; uandalizi wa maonyesho mbalimbali; kushiriki katika usasi wa wanyama pori; ulaji wa kikoa; mashindano ya mbio; miongoni mwa masuala mengine yaliyowaleta watu katika ushirika mmoja.

Shughuli hizi zote za kitamaduni ziliyafanya maisha ya jamii kuwa hai, pamoja na kuwaleta wanajamii pamoja na hivyo kudumisha umoja, amani na mshikamano baina yao. Licha ya shughuli hizi, maadili yaliyokuwepo kutokana na sheria kali zilizokuwa zimewekwa na majagina (ambao pia ni wafalme) hawa zilihakikisha kuwepo kwa maingiliano mazuri baina ya wanajamii kwa jumla.

Fumo Liyongo na Shaka Zulu walitumia tamaduni hizi kuweka jamii zao katika mfumo mmoja imara. Hadi kufikia leo, jamii hizi zinasifika kote ulimwenguni kutokana na umoja wao ikiwemo pia uimarishwaji na uhifadhi wa baadhi ya tamaduni zilizoasisiwa na kuendelezwa na majagina wao. Hili pia ni suala linaloonewa fahari na jamii hizi zikiwemo zile zilizoko katika ngazi za kimataifa.

4.1.5 Ukombozi na muungano wa jamii

Kabla ya jagina kuzuka, jamii yake huwa imekumbwa na matatizo au migogoro fulani. Tumelichungua suala hili na kulisawiri kwa uwazi na upana katika faslu ya pili na ile ya tatu. Kwa hiyo, jagina yeyote yule huwa hazuki vivi hivi tu. Yeye huzuka ili kuikomboa jamii yake kutokanana na ugumu au matatizo fulani. Iwapo jagina hatazuka katika kipindi anapohitajika na wanajamii, basi kuna uwezekano kwamba jamii ile itabaki katika ugumu au shida zile hadi pale ambapo jagina atazuka. Hata hivyo, kadiri wakati unavyoenda, jamii kama mfumo mwingine wowote ule huweza kubadilika na kuzua mbinu mpya za kujitanzua huku ikingojea ukombozi kamili kutoka kwa jagina wao.

Ugumu au misukosuko katika jamii inaweza ikachukua sura ya: uvamizi wa mara kwa mara wa maadui; unyakuzi wa ardhi na rasilimali zingine za wanajamii kama walivyofanya mabeberu barani Afrika; mizozo katika utawala wa jamii; matatizo ya kiuchumi; dhuluma zinazojitokeza kutokana na ukabila katika jamii - kwa hiyo, shujaa huzuka ili kuwaunganisha wanajamii au kusawazisha mfumo ambao tayari ulikuwa umeenda mvange; ukosefu wa vifaa au vita fulani muhimu katika jamii (vitu au vifaa hivi aghalabu huletwa na shujaa); na ukosefu wa mwelekeo kuhusiana na masuala ya kidini miongoni mwa masuala mengine.

Katika faslu ya pili na ile ya tatu, tumeonyesha kwa kina umuhimu wa Shaka Zulu na Fumo Liyongo katika kuzikomboa jamii zao kutokana na dhiki mbalimbali (na hususan kukomesha dhuluma za kivita dhidi ya maadui zao) na kisha kuwaongoza hadi kwenye ufanisi na muungano mmoja imara. Umoja huu uliendelea kudhihirika hata baada ya mashujaa hawa kuuka.

Kwa kipindi cha miaka kumi (baina ya 1818 na 1828) alichopata kutawala jamii ya Wazulu, Shaka aliunganisha jamii hii kwa njia ambayo inaonewa fahari na watu wengi duniani hadi hivi leo. Muungano huu ulidhihirika katika makabiliano ya baadaye (baada ya Shaka kuuka) na makaburu ambao walitaka kutwaa na kumiliki maeneo ya Wazulu pamoja na maeneo mengine ya Afrika Kusini kwa jumla. Mnamo Julai 1879, mabeberu wa Kizungu walipigana vita vikali zaidi na Wazulu; vita ambavyo baadaye vilikuja kujulikana kama *Vita vya Ulundi*. Kwa wakati huu, mfalme wa Wazulu alikuwa Cetewayo na makao yake makuu yalikuwa katika mji wa Ulundi. Wazulu walishindwa vibaya sana, Ulundi ikatekwa; na Cetewayo akachukuliwa mateka hadi Cape Town. Vita vya Ulundi ndivyo viliyokuwa hatima ya kipindi kirefii cha ufalme wa Zulu. Hata hivyo, ingawa ufalme wa Zulu ulikuwa umefika mwisho, jambo hili halimaanishi kuwa jamii ya Wazulu ilikuwa imesambaratika. Umoja wa jamii hii uliendelea kuwepo na hata sasa upo na unaonewa fahari na watu wengi (Omer- Cooper 1966:47).

Kwa upande wake, Fumo Liyongo aliwaunganisha Waswahili na jambo hili linadhihirishwa, kwa kiasi fulani na namna ambavyo wanajamii hawa walizienzi nyimbo zake - walijitokeza kwa wingi kila mara waliposikia kuwa Liyongo alikuwa akizitongoa. Mfano mzuri ni wakati alipokuwa amefungwa gereza akiingojea kuuawa na sultani. Mshairi anadokeza kwamba watu walijitokeza kwa wingi mno na anailinganisha hafla hii na ile ya harusi. Anasema:

**111. Hata usiku kufika
matezo wakayandika
kana ada wakaweka
tasa, pembe, siwa piya.**

**113. Wute wakakutanika
mahala pakatandikwa
na uzuri wakaweka**

**112. Na ngoma na nyingi kusi
kusalie unasi
ikawa kama harusi
watu wakiangaliya.**

**114. Wakatandika za zari
na libasi za Hariri
wakaimba mashairi**

deuli na subahiya.

ngoma na kusi pamoya.

Ngoma za gungu ziliendelea kuitambulisha jamii ya Waswahili na kuwaunganisha katika hafla mbalimbali hata baada ya mauko ya shujaa wao.

Kifo cha Liyongo kiliwasikitisha wanajamii wengi ambao walimwona kama ngao yao dhidi ya maadui zao. Tumeelezwa haya katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

225. Liyongo silaha yetu

Kwa wut'e khasimu zetu

Alikuwa ngao yetu

Wut'e wakinena haya.

226. Mui walisikitika

hakuna wa kutosheka

kwa Liyongo kutoweka

imeanguka paziya.

Kwa hiyo, jukumu la kuikomboa jamii ni muhimu sana. Ni kutokana na jukumu hili ndiposa wanajamii humwajabia shujaa wao na kumwona kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

4.1.6 Mabadiliko katika mfumo mzima wa jamii

Baada ya kuikomboa jamii yake kutoka katika lindi la misukosuko, shujaa huratibu mbinu na sheria mpya ambazo humwezesha kuubadilisha mfumo au mkondo wa maisha ya jamii yake. Iwapo kuna sheria ambazo zinawadhulumu wanajamii, yeye huziondoa na kuleta zingine mpya. Hata hivyo, kuna wakati ambapo shujaa anaweza kuleta sheria au mabadiliko yasiyowapendeza wanajamii. Utozaji wa kodi za juu na zisizofaa kama alivyofanya Liyongo (aliwatoza Wapokomo kodi za juu na kwa hiyo hawakumpenda) ni jambo ambalo linaweza kuwachukiza wanajamii.

Suala hili linaoana na lile la ukuzaji wa utamaduni wa jamii yake. Mabadiliko katika mbinu za kivita, uzalishaji mali, sheria, mahusiano na jamii zingine na hususan katika kuleta amani na kufanya biashara miongoni mwa masuala mengine ni mambo ambayo shujaa yeyote yule hupania kuleta katika jamii yake. Isitoshe, umoja wa wanajamii ambao aghalabu huwa wamesambaratika kabla ya kuzuka kwa shujaa ni mojawapo wa mabadiliko muhimu ambayo huhusishwa na shujaa. Kutokana na maelezo ambayo tuliyatoa katika faslu zilizotangulia, ni bayana kuwa Shaka Zulu na Fumo Liyongo walileta mabadiliko makubwa katika jamii zao. Kama ambavyo nimekwisha kutokeza, maelezo kumhusu Liyongo yako katika vipande vipande na umuhimu wake sawia na

ilivyo sifa zake unapatikana katika tungo anazodaiwa alizitunga, tungo zilizotungwa na maulama wengine kumhusu na maelezo mengine ya kihistoria

4.1.7 Ruwaza bora ya kufuatwa na wanajamii

Jagina hufanywa mambo mengi kwa manufaa ya jamii yake. Mapenzi yake kwa jamii huwa si haba na kama tulivyokwisha kuona, anaweza akafanya jambo lolote ilimradi anapata kuwa jamii yake imefanikiwa. Suala hili ni mojawapo ya masuala ambayo huwavutia wanajamii na kuwafanya wengi wao kupenda kujihusisha na jagina hata baada ya mauko yake. Isitoshe, matendo na hulka za majagina husisimua na kuajabisha mno vizazi vya halafu. Majagina hawa huwa ruwaza bora kwa watoto ambao kwa kiasi kikubwa huvutiwa na ngano (katika maandishi na masimulizi) na hata filamu zinazosawiri uigizaji wa hadithi kuhusu majagina (wanaweza wakawa majagina wa kazi bunilizi au kazi zinazohusu usawiri wa mashujaa wa kihistoria). Watoto huvutiwa na vitushi vya majagina na si ajabu kuwasikia baadhi yao kwa mfano, wakisema, **"Mimi nikiwa mtu mkubwa nitakuwa kama Liyongo [au Shaka au...]. Nitawaua adui wetu wote nikiwa peke yangu. Hamtakuwa mkinichezea..."**

Licha ya kuwa ruwaza njema kwa watoto, mashujaa huwa na athari kubwa na huibua hisia za aina fulani hata kwa watu wazima. Kwangu mimi, usomaji wa kazi na maelezo kuwahusu Liyongo na Shaka Zulu ni hali ambayo imeniathiri pakubwa na hususan katika kuyatazama mambo. Mashujaa kwa kawaida hufanya mambo sio tu kwa ajili yao binafsi bali kwa sababu ya watu wote katika jamii. Ufanisi wa wanajamii wake ni fahari kwake na hali hii huhusishwa na dhamira yake katika jamii. Kwa hiyo, tuonapo Fumo Liyongo na Shaka Zulu (au shujaa mwingine yeyote) wakijitoa kwa hali na mali kwa ajili ya jamii zao, tunapata mshawasha wa kutenda vivyo hivyo kwa manufaa ya jamii ya sasa. Tena, ari ya jagina, vitushi vyake, uratibu wa mbinu zake, umbo lake, miongoni mwa hulka zingine huwavutia wana jamii na baadhi yao huiga mienendo ya mashujaa wao.

4.2 Hitimisho

Mchango wa 'taasisi ya ushujaa' ambayo huibuliwa na haja ya kuleta mabadiliko kutokana na misukosuko inayoikumba jamii si haba. Taasisi ya shujaa hushirikiana na

taasisi nyingine kama vile dini, sheria, ndoa, utawala, elimu, kilimo, uchumi, miongoni mwa taasisi nyingine ili kusawazisha hali zilizoko katika mfumo mzima wa jamii. Kama ilivyo katika miflumo mingine yoyote, ukosefi wa mfumo mmoja muhimu (kama vile mfumo wa shujaa) humaanisha kuwa jamii ina upungufu fulani (upungufu huu hudhirishwa na matatizo yanayojitokeza katika jamii) na kuna haja ya pengo hili kujazwa. Kwa hiyo, kama ambavyo tumekwisha kuona, taasisi ya shujaa ni muhimu na haiibuki tu vivi hivi. Kuibuka kwa Shaka Zulu na Fumo Liyongo katika jamii zao sio kwa kubahatisha. Mashujaa hawa waliibuka katika hali na kipindi walipohitajika sana katika historia ya jamii zao. Tumeonyesha bayana umuhimu au mchango wao katika mfumo mzima wa jamii zao.

TANBIHI

Nvimbo hizi tatu ambazo huchezwa katika ngoma ya gungu na ambazo Frankl anadai huchezwa wakati wa *Siku ya Mwaka* zimeonyeshwa katika uk. 134. Wimbo wa kwanza ni:

Tujile shikamoo jumbe
Ndisw i wana wa Mwalipembe
Pumbavu likipumbaa pumbe
Limcscha mpunga kwa ng'ombe.

Wimbo wa pili ni:

Shee Mvita mzuwic ng'ombe
Asinwe maji kwa pembe Shee
Mvita mzuwie ng'ombe
Asinwe maji kwa pembe.

Wimbo wa tatu - tumeurejelea katika sura za awali - ni ule uliotungwa na Fumo Liyongo alipokuwa ametiwa gerezani na alikuwa akipanga njama za kutoroka kutoka mle:

Kijaka/J Saada nakutuma huyatumika
Kamw ambiyc mama ni muinga hayalimka
Nafanye mkate pale kati tupa kaweka
Nikereze p'ingu na minyoo ikinemka.

Vita vya *mfecane* viliacha athari kubwa ajabu katika maeneo ya kusini mwa Afrika yakiwcmo baadhi ya maeneo ya kati mwa bara hili. Vimeacha athari isiyofutika kwenye akili razini za vizazi vya halafiti. Tamaduni na kumbukumbu za kipindi hiki zinaamili kudumisha hali ya kujitainbulisha ya watu walioathiriwa katika kipindi hiki pamoja na kuathiri mitazamo yao kuhusiana na masuala mbalimbali ya maisha - jamii nyingi zimeweza kudumisha fahari zao ikiwemo ile hali ya kuwa na nafsi huria; yaani. isiyotegemea mabeberu kutoka Ulaya au jamaa wengine kutoka sehemu zingine za ulimwengu. Hali hizi, miongoni mwa hali nyinginezo, zimechangia pakubwa katika kuwepo kwa inabadiliko mengi ya kisiasa ya baadaye na ambayo pia yanaendelea hata leo katika nchi nyingi za bara la Afrika.

Kwa mujibu wa Omer-Cooper (1966:168), *mfecane* ilihusisha mchakato wa inabadiliko ya ndani ya kijamii, kiuchumi na kijeshi katika jamii za Kiafrika. Mchakato huu wa inabadiliko ulikuwa wa ghafla mno na maenezi yake pia yalikuwa ya haraka. Vita hivyo havikusababisha tu uharibifu wa mali na mauaji makubwa ya watu wa wakati huo lakini pia viliacha athari kubwa katika ruwaza ya maenezi ya watu katika maeneo ya kati na kusini mwa Afrika. Vita hivi pia vilisababisha kuwepo kwa watu ambao hadi sasa wanajihusisha na viongozi wao waliowaongoza (kwenye vita na utawala) katika kipindi hiki cha *mfecane*. Katika uk.180. anaendlea kudai kuwa vita hivi vilichangia pakubwa katika kuibua viongozi mahiri wa Wabantu (kama vile, Shaka Zulu wa Wazulu; Mosesh - mwasisi wa taifa la Basuto na inmojawapo wa watawala weledi katika Afrika Kusini; Zwangendaba - aliwaongoza Wangoni

katika maguro yao makubwa ajabu ya kutoka kaskazini mwa maeneo ya Wazulu hadi katika maeneo ambayo kwa sasa yanamilikiwa na nchi ya Tanzania; Faku, chifu wa Pondo, ambaye alizuia wimbi la vita kutolikumba eneo la Transkei) na kwamba kamusi nzima ya kitawasifu inaweza ikaandikwa kuhusiana na vitushi vya vigongo watawala walioibuka katika jumla ya misukosuko hii, ilivopelekea kuwepo kwa mabadiliko makubwa. Wengi wa viongozi hawa walidhihirisha ushupavu wa hali ya juu; uwezo wa kuongoza: ufundi wa matumizi ya mbinu na mikakati ya kijeshi; uwezo wa kuunda taasisi mpya ili kusuluhisha matatizo yaliyokuwa yakichipuka: na ustadi katika utawala uliopelkca jamii kuinuka juu ya mtazamo finyu wa kujinata katika misingi ya ukabila. Viongozi hawa walidhihirisha uwezo wa Wabantu wa kukabili matatizo au changamoto zote zilizoibuka.

Anaendelea kuse ma kuwa kumbukumbu na tamaduni za *mfecane* kwa muda mrefu zimeendelea kuwa na athari katika maisha ya Wabantu wengi hata leo. Kwa watu wengine, *mfecane* inaakisi kipindi muhimu cha kuudhihirisha ushujaa; ni kutokana na juhudi za viongozi na matukio ya wakati huo ambayo hufasiri umoja na utambulisho wao. Kwa jamii zingine, kipindi hiki ni kumbukumbu ya shida, mateso na kushindwa vibaya kabisa katika vita. Licha ya haya, kipindi hiki husaidia jamii hizi kufafanua au kuelezea muundo wa taasisi zake za ndani na mahusiano na jamii jirani.

FASLU YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Hitimisho

Katika utafiti huu, tulikuwa na madhumuni kadhaa ambayo tulilenga kutekeleza. Kwa hiyo, katika sehemu hii, tutaangazia kwa jumla matokeo ya utafiti wetu, huku tukiyafiingamanisha na madhumuni ya utafiti miongoni mwa masuala mengine yaliyojitokeza katika mchakato mzima wa utafiti.

Kama ambavyo imedhihirika, somo la mashujaa ni pana sana na huhitaji uelewa mpana wa mazingira yaliyowazua majagina pamoja na historia na falsafa zao za maisha. Hata hivyo, somo hili linavutia linapotazamwa kwa mkabala wa kiulinganishi. Mvuto huu pia unajitokeza hasa tunapomtazama shujaa kama taasisi au asasi ambayo ina mchango mkubwa katika jamii. Licha ya kuwepo kwa mtazamo huu, ni bayana kuwa mashujaa na hususan mashujaa wa kijamii wa kihistoria huwa hawapewi uzito wanaostahili. Inafaa ikumbukwe kuwa, mashujaa wa kihistoria wa kijamii wamechangia pakubwa katika kuwepo kwa hali mbalimbali katika jamii za sasa na kwa hiyo, mchango wao unafaa kutazamwa kwa jicho pevu ili kuuweka wazi kwa vizazi vya halafii vitakavyopata sio tu historia kwasi ya jamii za mababu zao bali pia watapata kuwa na ruwaza bora ya kufiatwa kwa manufa ya jamii nzima.

Katika kulishughulikia somo letu, tuliuchukua mwelekeo ambao ungefumbata masuala kadhaa ambayo ni muhimu katika kutoa taswira bayana ya majagina kwa jumla. Katika faslu ya kwanza, tulishughulikia masuala muhimu na ya kijumla ambayo yalitanguliza somo la utafiti wetu pamoja na kutuongoza katika mchakato mzima wa kufikia malengo yetu.

Katika faslu ya pili, tulilenga katika kuielezea historia ya Shaka Zulu na Fumo Liyongo, kwa kuifiingamanisha na historia ya mfumo mzima wa jamii zao huku tukionyesha mazingira, kipindi na hali za jamii zilizowazua. Tulipata kuwa mashujaa hawa walizuka kutokana na mahitaji fulani (kwa mujibu wa nadharia ya

uamilifu na hususan uamilifu wa kisaikolojia) katika vipindi maalumu katika historia za jamii zao Mazingira na hali zilizowazua mashujaa hawa kwa kiasi fulani zinashabihiana. Wote walizuka katika kipindi cha misukosuko ya kivita Waaidha, tulipata kuwa, uelewa wa kina wa historia za jamii zao ni muhimu katika kuwaelewa mashujaa hawa kwa kina na hususa katika kufafanua sifa zao za kishujaa na pia kuelewa mchango au umuhimu wao katika muktadha mzima wa jamii zao.

Katika faslu ya tatu, tulilenga katika kuzipambanua sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Katika kuzipambanua sifa hizi, tulipata kuwa mashujaa hawa wawili wanadhihirisha kuwepo na sifa za kishujaa ambazo zinadhihirika katika mashujaa wengine duniani. Katika kuzipambanua sifa hizi, tuliongozwa na nadharia ya uhakiki wa vikale. Kwa vile kama tulivyoeleza katika faslu ya kwanza, kuwa wanadamu wote duniani ni sawa, vivyo hivyo mashujaa nao aghalabu huwa na vipengele vya kimaisha ambavyo hufanana.

Katika kuzilinganisha sifa za kishujaa za Shaka Zulu na Fumo Liyongo, tulipata kuwa mashujaa hawa wana sifa zinazolingana kwa kiasi kikubwa. Tofauti zilizopo baina ya sifa zao ni kwenye utabiri wa kuzaliwa kwao na pia suala la ndoa. Jambo hili, tumelifafanua kwa uwazi katika faslu ya tatu. Kwa hiyo, utafiti huu umechangia katika kutilia nguvu madai kuwa majagina wote duniani huwa na sifa zilizo karibu sawa. Katika kulishadidia dai hili, tuliwalinganisha Fumo Liyongo na Shaka Zulu na mashujaa wengine duniani. Ilibainika kuwa nyingi za sifa za mashujaa zinaoana baina ya mashujaa wote duniani. Katika faslu ya kwanza - katika kuelezea yaliyoandikwa katika somo - tulipata kuwa, Mberia (1989) na Mulokozi (1999) wametusawiria tu sifa chache za kishujaa za Fumo Liyongo tofauti na ilivyo katika utafiti huu ambapo tumepata kuwa sifa za kishujaa za Fumo Liyongo ni zaidi ya zile wanazozielezea. Kuna uwezekano pia wa kupata sifa zaidi za kishujaa za mashujaa hawa.

Baadhi ya maulama wakiwemo watu wengine kama tulivyokwisha kuona katika faslu ya kwanza, wanatilia shaka kuwahi kuwepo kwa Fumo Liyongo. Jambo hili

linatokana hasa na namna alivyosawiriwa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, miongoni mwa tungo zingine. Tumeona kuwa, majagina hukuzwa na wanajamii - kutokana na kuwa na sifa za kiajabuajabu - pamoja na kwamba wao pia hujikuza Jambo hili ndilo huwatofautisha na wanajamii wengine. Kwa kumlinganisha Fumo Liyongo na Shaka Zulu, tumepata kuwa wote wana sifa za kishujaa zilizo karibu sawa. Inaaminika kwa yakini kuwa, Shaka Zulu aliishi na kutenda mambo makubwa ambayo huajabiwa na watu wengi hata leo. Kwa nini basi kuwepo kwa Fumo Liyongo ambaye pia ana sifa zilizo karibu na zile za Shaka kutiliwe shaka⁹ Kwa kumtali Fumo Liyongo na kisha kumlinganisha na Shaka Zulu, ni bayana kuwa Liyongo alipata kuishi (kama inavyoaminiwa kuwa Shaka aliishi) na sifa zake za kiajabuajabu hazipaswi kuwa kigezo cha kuchukulia kwamba yeye hakuwahi kuishi duniani. Kama tulivyokwisha kutaja hapo awali, ni kawaida kwamba, kazi za kifasihi zinazoelezea kipengele fulani cha historia ya jamii fulani huwa zimetiliwa chumvi kwa kiwango fulani. Kutiliwa chumvi katika usawiri wa shujaa yeyote yule huwa ni mchango mojawapo wa wasanii katika kuwakua mashujaa wa jamii zao.

Kuhusiana na umuhimu wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu kwa jamii zao, tumepata kuwa, mashujaa hawa hawakuzuka tu vivi hivi. Walizuka kutokana na mahitaji ya jamii zao (kwa mujibu wa nadharia ya uamilifu na hususan uamilifu wa kisaikolojia). Umuhimu wa majagina hawa ulikuwa si haba na ulidhihirika kwa mapana na marefu maishani mwao walipokuwa wanatekeleza dhamira (matamania ya jamii) zao kwa jamii zao. Waaidha, imedhihirika kuwa umuhimu wao haujitokezi tu wakati wa maisha yao duniani bali huendelea kudhihirika hata baada ya mauko yao.

Imejitokeza kuwa, kama zilivyo taasisi zingine ambazo huibuka kutekeleza jukumu fulani mahsusi, vivyo hivyo tuna 'taasisi ya ushujaa' ambayo pia huzuka ili kutosheleza mahitaji ya jamii. Ni katika harakati za kutekeleza mahitaji haya ndiposa umuhimu wa jagina hudhihirika (kama walivyo Fumo Liyongo na Shaka Zulu). Aidha, taasisi ya shujaa hushirikiana na taasisi nyingine ili kuukamilisha mchakato mzima wa kusawazisha au kutimiza mahitaji ya jamii kwa jumla na hivyo kuifanyaiwe kamilifu.

Matokeo ya utafiti wetu yamelingana na nadharia tete ambazo zilituongoza katika jumla ya utafiti wetu. Tuliwachukulia Shaka na Liyongo kuwa mifano mizuri ya majagina wa kihistoria wa Kiafrika. Jambo hili limedhihirika bayana. Mashujaa hawa wanaweza wakawekwa katika kiwango sawia na mashujaa wengine duniani na kwa hiyo, wana nafasi muhimu katika historia ya ulimwengu kwa jumla Pia, tulichukulia kuwa, sifa za mashujaa hawa kwa kiasi kikubwa zinafanana jambo ambalo limedhihirika katika matokeo ya utafiti wetu. Aidha, tulikuwa na mtazamo kuwa umuhimu wa majagina hawa katika jamii si haba. Suala hili limejitokeza vizuri katika faslu ya nne.

Katika kuwalinganisha Fumo Liyongo na Shaka Zulu na mashujaa wengine (na hususan majagina wa kidini), haikuwa nia yetu kuibomoa wala kuikuza dini yoyote ile. Ulinganishi huu ulikuwa hasa na lengo la kutusaidia kuweka wazi zile sifa za kijumla ambazo hudhihirika katika mashujaa wengine kote duniani Tulichukulia na kubainisha kuwa mashujaa wa kidini wana sifa za kishujaa ambazo hujitokeza katika mashujaa wengine (wa kihistoria wa kijamii) na kwa hiyo ni msingi mzuri katika kupambanua kiulinganishi sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na Shaka Zulu.

Tungo za kifasihi za kimsingi ambazo tulitumia katika kupambanulia sifa za kishujaa za Fumo Liyongo na kuelezea umuhimu wake kwa jamii ya Waswahili ni pamoja na: *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Takhmisaya Liyongo* na nyimbo au mashairi yanayodaiwa kuwa yalitungwa na Liyongo (kama yalivyowasilishwa na Mieke na wenzake 2004) miongoni mwa kazi nyingine. Kwa upande wa Shaka Zulu, utungo wa kifasihi ambao ulikuwa msingi bora katika kumtali jagina huyu ni, *Emperor Shaka the Great: A Zulu Epic*. Hata hivyo, tulirejelea baadhi ya kazi nyingine za kihistoria (kama vile, Omer-Cooper (1966) ambacho pia ni kitabu kilichotufaa pakubwa) ikiwemo kazi mojawapo ya kiwasifu kumhusu.

Kama tulivyotaja katika faslu ya kwanza, hakuna utafiti wa awali tuujuao unaowalinganisha Shaka Zulu na Fumo Liyongo na kuelezea umuhimu wao kwa kina kama inavyobainika katika tasnifu hii. Kwa hiyo, tuna imani kuwa matokeo ya utafiti huu ni muhimu katika kuliziba pengo la kiusomi lililokuwepo.

5.1 Mapendekezo

Kuna masuala anuwai ambayo yanaweza yakatafitiwa kuhusiana na suala nzima la majagina. Tasnifu hii ni jaribio la kutalii kiulinganishi majagina wawili wa kihistoria wa kijamii katika muktadha wa jamii za Kiafrika Kwa sababu ya wakati na nafasi, hatukuweza kuyapigia darubini masuala yote yanayowalenga Shaka Zulu na Fumo Liyongo. Kuna uwezekano wa kuwepo kwa sifa zaidi za kishujaa za Shaka Zulu na Fumo Liyongo pamoja na kuwepo kwa umuhimu zaidi kwa jamii zao na ambao hatukurejelea. Hili ni suala mojawapo ambalo linaweza likatiliwa maanani na watafiti wa baadaye katika utafiti wao.

Maandishi yaliyoandikwa kumhusu Fumo Liyongo - ikiwemo historia ya Waswahili - yako katika vipande vipande. Tulijaribu kuyaunganisha pamoja lakini bado tuna imani kwamba watafiti wa halafu wanaweza wakaendeleza ufafanuzi huu kwa kina zaidi (ni dhahiri shahiri kwamba, historia ya Waswahili ni kwasi na ndefu mno). Jambo hili litachangia katika kuzidisha uelewa wetu wa hali na mazingira ya kihistoria ya kijamii yaliyomzua Fumo Liyongo.

Watafiti wa halafu wanaweza pia wakafanya ulinganishi baina ya Shaka Zulu au Fumo Liyongo na shujaa mwingine yeyote wa kihistoria wa kijamii kutoka katika bara lingine tofauti na bara la Afrika. Aidha, ni muhimu pia watafiti wao hao wafanye ulinganishi wa kina baina ya mashujaa wa kidini na wale wa kihistoria wa kijamii ili kuona uwiano uliopo katika sifa zao za kishujaa. Itakuwa bora pia kuusawiri umuhimu wa majagina hawa kwa jamii au umma wao.

Mashujaa wengi wa kihistoria wa kijamii wa Kiafrika hawajafanyiwa utafiti wa kutosha. Kuna pengo kubwa la kiusomi ambalo linastahili kujazwa. Ni bayana kwamba mashujaa hawa walichangia pakubwa katika harakati za ukombozi na ufanisi wa jamii zao. Mchango huu unafaa kuwekwa wazi ili vizazi vya sasa na vile vya halafu viweze kuzifahamu juhudi za mababu zao katika kupigana kufa kuzikana ili kuzikomboa jamii zao na hivyo kufiata nyayo zizo hizo. Ama kwa hakika, juhudi hizi zimechangia kwa mapana na marefu katika kuziunda hali za kijamii kama zilivyo hivi leo. Majagina kama vile: Dedan Kimathi, Lwanda

Magere, Mirambo, Kinjekitile, Kibwebanduka miongoni mwa wengine wengi wanashikilia nafasi muhimu sana katika historia ya Afrika na uimwengu mzima kwa jumla. Ni vema ulinganishi wa kina uweze kufanywa baina ya majagina hawa ili kuzipambanua sifa zao za kishujaa na pia kuweka wazi michango yao kwa jamii zao. Iwapo utafiti wa aina hii utafanywa na Waafrika wenyewe, basi utakuwa na mchango mkubwa katika kuichanganua historia kwasi ya Waafrika pamoja na kuuonea fahari uwezo wa ngozi nyeusi.

Tunapendeza pia uhakiki wa kifani ufanywe na watafiti wa halafu kuhusiana na tungo za kifasihi zinazowasawiri Fumo Liyongo na Shaka Zulu.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M. H. (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*
Nairobi: Kenya Literature Bureau
- Abrams, M. H. (1981) *A Glossary of Literary Terms* (toleo la mne).
New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Allen, J. de V. (1977) *Al Inkishafi* Nairobi: East African Educational Publishers.
- _____ (1993) *Swahili Origins: Swahili Culture and the
Shungwaya Phenomenon*.
London: James Currey.
- al-Murshedy, M. H. A. (1927) 'Katika Walotawala Amu Baada ya
Zita za wa Mazrui'. Huu ni mswada (mss 706) tulioupata
katika maktaba ya Taasisi ya Uingereza ya Afrika
Mashariki (B.I.E.A).
- Bryant, A. T. (1949) *The Zulu People: As they were Before the
White Man Came*.
Pietermaritzburg: Shutter and Shooter.
- Butler, B. (1979) *The Myth of a Hero*. London: Rider and Company.^
- Carlyle, T. (1924) *On Heroes, Hero-Worship and The Heroic in History*.
London: Macmillan & Co., Ltd.
- Chiraghdin, S., Nabhany, A. S. na Baruwa, A. (1975) 'Tarehe ya Ushairi
wa Kiswahili.' *MulikaNa*. 7, uk. 59-67.
- Chittick, N. (1984) *Manda Excavations at an Island on the Kenya Coast*.
Nairobi: B.I.E.A
- Cobbing, J. (1988) 'The Mfecane as Alibi: Thoughts of Dithakong and Mbolompo.'
Journal of African History 29, uk.487-519.
- Dammann, E. (?) 'Prosatexte in Der Lamu - Mundart des Suaheli/
Afrika und Ubersee Band XXXIX, uk.65-32. •
- Eliade, M. (1957) *Myths, Dreams and Mysteries*.
New York: Harper & Row, Publishers.
- Frankl, P. J. L. (1993) 'Siku ya Mwaka: New Year's Day in Swahili-land
(With Special Reference to Mombasa)'
Journal of Religion in Africa XXI11, 2, uk. 125-135.

- Freeman-Grenville (1954-1955) 'Ibn Batuta's visit to East Africa A D 1332: A Translation.' *Uganda Journal* 18-19, uk. 1-6.
- Gaster, T. H. (1987) 'Heroes'. Katika Eliade, M. (mh.) (1987) *The Encyclopaedia of Religion, juzuu na. 6*. New York: Macmillan Publishers, uk 302-305.
- Gunnep, A. V. (1960) *The Rites of Passage*. London: Routledge & Kegan Paul.
- Harries, L. (1962) *Swahili Poetry*. Oxford: Clarendon Press.
- Hemedi'lAjjemy, A. (1962) *Habari za Wakilindi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau
- Kiango, S. D. na Sengo, T. S. Y. (?) 'Fasihi'. *Mulika Na. 4*, uk. 11-22.
- Kitsao, J. (1982) 'An Investigation of Themes in Swahili Literature and An Application of Stylostatistics To Chosen Texts' Tasnifu ya Uzamifu (*PhD*). Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Knappert, J. (1970) *Myths and Legends of The Swahili*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann Educational.
- Kunene, DP. (1971) *Heroic Poetry of the Basotho*. Oxford: Clarendon Press.
- Kunene, M. (1979) *Emperor Shaka The Great: A Zulu Epic*, y London: Heinemann.
- Maneniang, M. (1999) *Ihe Lianja Epic*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbele, J.L. (1986) 'The Liongo Fumo Epic and the Scholars.' *Kiswahili* 53/1 na 53/2, uk. 128-145.
- Mberia, K. (1989) 'Fumo Liyongo'. *Mulika Na.21*, uk. 25- 43.
- Mbotela, J. J. (1959) *Uhuru wa Watumwa*. Nairobi: Nelson.
- McGee, J R. na Warms, R.L. (2000) *Anthropological Theory: An Introductory History*. Boston: McGraw Hill.

- Meyer, M. (1993) *The Bedford Introduction to Literature*.
Boston: Bedford Books of St. Martin's press
- Miehe, G., Abdalla, A., Bhalo, A.N.J., Nabahany, A., Baschiera, A., Dittmer, C., Topan, F., Abdulaziz, M. H, Khamis, S A M , Omar, Y A na Al-Bakary, Z. M. F. (2004) *Liongo Songs: Poems Attributed to Fumo Liyongo*.
Koln: Grudiger Koppe Verlag.
- Mofolo, T. (1931) *Chaka* (mtar., Kunene, D P). London: Heinemann
- Mohamed, S. A. (1988) *Kiza Katika Num*.
Nairobi. Oxford University Press.
- Mulokozi, M M. (1999) *Tenzi Tatu Za Kale*. Dar es Salaam: TUKI
- Mutiso, K. (1985) 'Hurafa na Uyakinfii katika *Hamziyyah*
Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.
Haijachapishwa.
- (1990) 'Fumo Liyongo na Kazi Zake'. Makala haya hayajachapishwa.
- (1999) 'Sira ya Majagina: Buddha na Muhammadi'.
Makala haya hayajachapishwa. Makala haya yaliwasilishwa
kwenye kongamano, *Swahili Kolloquim Universitat*, Bayreuth.
Mei 14-15, 1999.
- Nasiri, S.A.A. (1980) *Inkishafi*. Nairobi: Longman.
- Njau, R. na Mulaki, G. (1984) *Kenya Women Heroes and their Mystical Power*.
Nairobi: Risk Publications.
- Nurse, D. (1994) 'Historical Texts from the Swahili coast.' *Swahili Forum IAAP*
Na. 37, uk. 47-85.
- Nurse, D. na Spear, T. (1985) *The Swahili: Reconstructing The History
and Language of an African Society, 800-1500*.
Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Omer-Cooper, J. D. (1966) *The Zulu Aftermath: A Nineteenth-
Century Revolution in Bantu Africa*.
London: Longmans, Green and Co. Ltd.
- Onyango-Ogutu, B. na Roscoe, A. A. (1974) *Keep my Words*.
Nairobi: East African Publishing House.
- Prins, A. H. J. (1958) 'On Swahili Historiography.' *Journal of East
African Swahili Committee* 28/2, uk.26-40.

- Raglan, L. (1965) 'The Hero of Tradition'. Katika, Dundes, A (mh) (1965) *The study of Folklore*. Berkeley: Prentice-Hall.
- Ridhiwani, P. (1996) 'Shairi la Fumo Liyongo'. *Kiswahili* 59, uk. 22-32.
- Ritter, E. A. (1955) *Shaka Zulu: The Biography of the Founder of the Zulu Nation*. London: Penguin Books
- Roberts, B. (1974) *The Zulu Kings*. London: Hamish Hamilton.
- Saturday Nation* Tarehe 9 Aprili, 2005. Katika makala, '*Powerful and Weak Come Together to Mourn Pope*
- Senkoro, F. E. M. K. (1976) 'Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili.' *Kiswahili* 46/2, uk. 74-82.
- Steere E. (1870) *Swahili Tales As Told By The Natives of Zanzibar*. London: Bell and Davy.
- Stiles, D. (1981) 'Hunters of the Northern East African Coast: Origins and Historical Processes.' *Africa* 51, uk. 848-862.
- Sutton, J. E. G. (1966) *The East African Coast: A Historical and Archaeological Review*. Nairobi: East African Publishing House.
- Trimingham, J. S. (?) 'Reflections on the Arab Geographers and the East African Coast.' Tuliyoa makala haya katika maktaba ya Taasisi ya Uingereza ya Afrika Mashariki (B.I.E.A). Hayakuwa na tarehe ya kuchapishwa na hayakuonyesha mahali ilimochapishiwa.
- TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili). Nairobi: Oxford University Press.
- United Bible Societies (1952) *Biblia*
- Vansina, J. (1985) *Oral Tradition as History* Wisconsin: University of Wisconsin Press.
- Walsh, M. (1987) 'Mijikenda Origins: A Review of the Evidence.' Makala haya hayajachapishwa. Niliyapata katika maktaba ya Taasisi ya Uingereza ya Afrika Mashariki (B.I.E.A).
- Wamitila, K. W. (2002) *Ihakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Were, G. S. (1974) *A History of South Africa*. London: Evans Brothers.

Werner, A. (1915) 'The Bantu Coast Tribes of the East Africa Protectorate '
Journal of Royal Anthropological Institute XLV, uk 326-345.

(1968) *Myths and Legends of The Bantu*
London: Frank Cass and Company Limited

KIAMBATISHO 1

UTENZI WA FUMO LIYONGO

1. Bismillahi nabutadi
kwa ina la Muhammadi
nandikie auladi
nyuma watakaokuya.
2. Unipe wino mweusi
na ya Shamu karatasi
na kalamu ya unyasi
nipate kuyandikiya.
3. Na kibao cha fadhari
nipijie misitari
khati zende kwa uzuri
zifuate moya ndiya.
4. Hadithi niwandikiye
ya ajabu musikiye
yalojiri amriye
mupate kufahamiya.
5. Niweleze kwa utnngo
hadithi yake Liyongo
niweleze na mazingo
niambo yalomzingiya.
6. Liyongo kitamakali
akabalighi rijali
akawa mtu wa kweli
na haiba kaongeya.
7. Kimo kawa mtukufu
mpana sana mrefu
majiniboni yu maarufu
watu huya kwangaliya.
8. Walienda Wagala
kwa jumbe wa Pate dola
kwa ktiniinua chakula
pamoya kumwangaliya.
9. Wagala hao yuwani
ni wakuu wa mwituni
kabila ya Sulutwani
mashujaa wote piya.
10. Sulutwani Pate Bwana
papo nave akanena
Wagala wamemuona
Liyongo kiwatokeya.
11. Wagala wakabaini
huyu Liyongo ni nyani
kwetu hayusilikani
wala hatuyasikiva.
12. Mfalunie kawambiya
Wagala kiwasifiya
hiiwegenia watu niya
wasiweze kukimbiya.
13. Ni niwanamunie swahihi
kama siniba una zihi
usiku na astibuhi
kutenibea ni mamoya.
14. Ghafula kikutokeva
nikoyo hukupoteya
tapo likakuw iliya
ukapata na kuliya.
15. Mato kikukodoleya
ghafula utazimiya
kufa kutakurubiya
kwa khaufu kukungiya.
16. Wagala wakipulika
kwa dhihaka wakateka
wakanena twamtaka
na sisi kumwangaliya.

17. Na yeye alikiketi
kwa nduze wasi katiti
i huko yake baiti
kwa waungwana mashaa.
18. Mfalume kaandika
waraka wake haraka
mtu wake kampeka
Liyongo kampekeya.
19. Piya akaniwandikiya
Wagala walomwambiya
ndoo nimekuusiya
wataka kukwangaliya.
20. Tumi kenda kwa haraka
kwa Liyongo akafika
kampa kaumunika
akasonia yot'e.
21. Na Liyongo akajibu
kwa hishima na adabu
nitakuja kwa karibu
nitwiiye Maulaya.
22. Kisa tumi akarudi
hata kwa yake Sayyidi
salamu kairadidi
Liyongo mezomwambiya.
23. Liyongo siku ya pili
ndiya akaikabili
kainenda tasihili
ndiya akaiemeya.
24. Kaifunga kwa sitawa
silaha za kutcuwa
panda tatu katukuwa
kaziwangaa panioya.
25. Na mtu kitoka Shaka
hata Pate ukafika
siku nne kwa haraka
alo hodari sikiya.
26. Liyongo akikabili
ndiya kenenda rijali
alikuwenda siku mbili
na ya pili kuingiya.
27. Liyongo kenda muini
akipata nilangoni
panda katia kanwani
kivuzia kapasuwa.
28. Kiivuzia hakika
muini wakashituka
panda ikapasuka
Wagala wakasikiya.
29. Wakauliza n'nini
vuwi melipija nani
akajibu Sulutwani
ni Liyongo amekuya.
30. Liyongo asimuhili
akaipija ya pili
pandaye isillimili
na ya pili kapasuwa.
31. Kaishika na ya tatu
wakajiimuika watu
wakazengeya mapitu
Wagala kukimbiliya.
32. Mfalume kawanibiya
ni huvo amezokuya
sasa hiyau tangiya
niutaona ni hidaya.
33. Katika havo kunena
kaya tumi mbee Bwana
ya Liyongo sayyidana
ataka ruhusa kungiya.
34. Napite akaniwambiya
kipita akatokeya
Wagala wakashuhudiya
khaufu zaliwangiya.

35.Ruhu zikenda kishindo
zimo zao hukonia ondo
huyo ni Bwana wa kondo
ashindaye jeshi miya.

36.Hapo Liyongo kaketi
akapumuwa katiti
akauweka t'iyati
mkoba alotukuwa.

37.Kisa katiti kutuwa
mkobani akatowa
zitu alizotukuwa
nyumba ndima nisikiya.

38.Katowa kinu na mt'I
na jiwe la kupanza kuti
na zunguze si katiti
na mawe ya kupikiya.

39.Na kipeto cha mtama
na ya nazi matoroma
Wagala wakaatama
ajabu ikawangiya.

41.Twaitaka mbeu yake
nasi kwetu tuipeke
kwa furaha tumuweke
apate kutuzaliya.

42.Sulutwani kamwambiya
ngoja t'amuarifu
akiriri kiridhiya
tumi wangu t'aweteya.

43.Sulutwani kitamka
Liyongo akaridhika
Masharuti kayaweka
Wakikiri t'aridhiya.

44.Sulutwani kwa ajila
akawambia Wagala
papo pasina muhula
sharuti wakaridhiya.

45.Sharuti wakatiniiza
Liyongo wakamuoza
kwa furaha na kuteza
nyumbani akaingiya.

46.Mke katukuwa niimba
akazaa mwane siniba
mwanamume wa kutamba
mwane Liyongo sikiya.

47.Kamuyeya kimtunda
kwa niahaba kimpenda
kama wa matoni wanda
na kwa t'unu na hidaya.

48.Hata kijana kakuwa
na babake wachenda sawa
kabaleghe kwa sitawa
na haiba zot'e piya.

49.Fitina zikamngiya
Mfalume miya miya
kwa hila kakusudiya
kunuuiwa fahamiya.

50.Liyongo akatambuwa
huzengea kuuwawa
pale Pate kayepuwa
Barani akitembeya.

52.Mfalunie changaliya
mwituni mekimbiliya
Wasanye kawazengeya
na Wadahalo pamova.

53.Mfalume kawambiya
Liyongo kunipatiya
kitwa mukanieteya
t'awapa riale miya.

54.Wakarudi mabarani
wakamuona niwihini
wakamwambia mwendani
natwenende ndia moya.

55.Wewe ni kama bwanetu
tena kisa ni babetu
uwe ni rafiki yetu
kula na kunwa pamoya.

56.Siku moya wakanena
natuleni waungwana
kikowa ni tamu sana
karamu 'sotindikiya.

57.Kikowa tule makoma
kukuta hatutokoma
kula tukiterema
kulla mtu siku moya.

58.Likisa shauri lao
wakenenda kwa kikao
mkoma waupatao
hupanda mm mmoya.

59.Na wao maana yao
siku Liyongo apandao
warn fume wut'e hao
zembe kwa wao umoya.

60.Wakalipa wut'e piya
Liyongo akasaliya
Ni wewe wakamwanibiya
Tumetaka fahamiya.

61.Liyongo kanena hima
uzengceni mkoma
niuyapendao makoma
nipate kuwanguliya.

62.Wakitembea kwa safu
kuuzengea mrefu
na hata wakaushufu
ni huno wakamwambiya.

63.Liyongo akiuona
ni mrefu nino sana
yakamwelea maana
yale alowadhaniya.

64.Na yeye una hadhari
kilala huwa tayari
anayuwa wana shari
wut'e piya kwa umoya.

65.Akawanibia ngojani
akatowa mkobani
chembe katia ngweni
makoma kiwanguliya.

66.Achangusha ngaa ndima
ni niangi mno makoma
kwa wut'e wakaatama
ajabu zikawangiya.

67.Wakanena kwa moyoni
amuwezao ni nyani
huyuno hawezekani
ni kutaka kwangamiya.

68.Kwa siri wakaonana
wut'e wakaulizana
wa kumahika hapana
t'atuwa sote piya.

69.Sulutwani tumjibu
kumuuwa ni dharubu
kumshika ni taabu
hatuwezi kwa umoya.

70.Sulutwani kabaini
hela kamzoezeni
mumrejeze muini
nimeomba nami haya.

71.Mwambieni tusafiri
hata Pate tukajiri
hapana tena khatari
habari tumesikiya.

72.Natuketi mabarani
natungie na muini
kiteweo utukuni
tupate kukizengeya.

73. Waboni Wadahalao
wakarudi hata kwao
Liyongo mahala pao
huyo amewatokeya.
74. Akawataka khabari
kawambiya ni nzuri
hapana tena khatari
hakuna wa kukuzengeya.
75. Mui tumeumaliza
hapana wa kukuza
sote yakatushangaza
ndipo haya kukwambiya.
76. Liyongo akasikiya
naye akaazimiya
wakenenda kwa umoya
hata Pate wakangiya.
77. Liyongo akaonana
na nianiake na kijana
mwituni asende tena
papo akaitikiya.
78. Kasikia Sulutwani
kafurahi kwa moyoni
akanena mara hini
hatoki nitamuuwa.
79. Liyongo nikwambiao
shaha wa gungu na mwao
tena ni mkuu wao
huwashinda wut'e piya.
80. Sulutwani kabaini
Ma-Shaha walo muini
kawambia kwa sirini
pijani gunguhwambiya.
81. Kwa wanaume na wake
na Liyongo mumwalike
naazimu nimshike
ni siri nimemwambiya.
82. Na hahari kisikiva
Liyongo akakimbiya
nanyi niniezomwambiya
t'awaua kwa umoya.
83. Naye huyo Sulutwani
kuuwa hawezekani
akinena ni yakini
hutimiza mara moyo.
84. Ma-Shaha wakaalika
Liyongo wakamtaka
mwao tutauandika
sote tuwe kwa umoya.
85. Na mwao wakaandika
kulla ada wakaweka
Sulutwani akapeka
majuma wapata miya.
86. Wakanenda kwa utungo
mafumo, zembe, zigongo
wakamshika Liyongo
gerezani akatiwa.
87. Akatiwa gerezani
kafungiwa kijumbani
asikari mlangoni
kwa zaniu wachangaliva.
88. Kukifanvwa mashauri
auawc madhukuri
tulepuwe lake shari
Liyongo namcheleya.
89. Wenginewe wakanena
kumuuwa siyo sana
huyu nda mui zana
ni mwenye kukuteteya.
90. Nanimfanye amiri
zikiya zita ni kheri
atakufa kwa uzuri
niaana hatokimbiya.

91. Kiuawa ndio sana
kitouwawa ni zana
hayo yot'e wakanena
Sulutwani kaambiwa.
92. Sulutwani kaflkiri
kumuuwa ndio kheri
kumuwata ni khatari
kwa hila t'anizengeya.
93. Anipoke ufalume
kisa chanda nikiume
kheri yangu mwanamume
kumuuwa mara moya.
94. Jamaa kawamkuwa
kwa shauri la kuuwa
wakamjibu ndiyo dawa
shashauri letu ni moya.
95. Wakamtuma kitwana
kwa Liyongo akanena
la kufa shaka hapana
menituma kukwambiya.
96. Watamani yambo gani
menituma Sulutwani
utapowa kwa yakini
ili uwage duniya.
97. Mekwambia Bwana wetu
menituma mimi mtu
muhula wa siku tatu
fahamu utauwawa.
98. Akajibu usikhini
kamwambie sulutwani
mwao ninieutamani
na gungu liwe pamoya.
99. Musizipije sagali
yeo na siku ya pili
umwambie tajamali
nimeomba nitendeya.
- 100. Na tumi wa Sulutwani
akitoka kijunibani
kaya tumi wa nyumbani
chakula akimweteya.**
- 101. Na 11lamake kwa hakika
chakula chema kipika
asikari humpoka
chakula wakailiya.**
- 102. Chakula wakimweteya
asikari huiliya
siku hiyo kamwambiya
mamangu nisalimiya.**
- 103. kanena kwa ushauri
enenda kamukhubiri
mama afanye tavari
haya nimezokwambiya.**
- 104. Kamba Sada nakutuma
enda kaniwambie mama
afanye mkate mwema
kati tupa ativa.**
- 105. Muinga havalimka
mle tupa na kupika
makozi yakaniuka
nyoka hawatajaliya.**
- 106. Sad a akabalighisha
mamake yakamuwasha
akaufanya wa wishwa
mkate kampikiya.**
- 107. Mkate huu sikiya
pishi mbili hutimiya
kati tupa akativa
Liyongo kampekeya.**
- 108. Asikari kitiona
ni wishwa wakatukana
wa wishwa hula watwana
mpekee haya ngiya.**

109. Ule Liyongo chumbani
kauvunda kwa sirini
tupa akaona ndani
furaha zikamngiya.
110. Mama tupa akitiya
kitambaa metatiya
kwa furaha mno ghaya
sana kawafurahiya.
111. Hata usiku kufika
matezo wakayandika
kana ada wakaweka
t'asa, pembe, siwa piya.
112. Nangoma na nyingi kusi
kusalie unasi
ikawa kama harusi
watu wakiangaliya.
113. Wut'e wakakutanika
mahala pakatandikwa
na uzuri wakaweka
deuli na subahiya.
114. Wakatandika za zari
na libasi za hariri
wakaimba mashairi
ngoma na kusi pamoya.
115. Kulla nyimbo zizidipo
na ngoma zitakatapo
alikitinda hapo
pingu na minyoo piya.
116. ZHipo kikaza kusi
alikitata upesi
hata zikikoma basi
inukani kawambiya.
117. Wakiinuka kuteza
Liyongo akatokeza
khaufu zaliwakaza
mbiyo zikawapoteya.
118. Kwa wut'e wakakimbiya
hapana alosaliya
Liyongo kaitokeya
Mabarani karejeya.
119. Sulutwani kawatiya
asikari kumzengeya
mwane Liyongo sikiya
ili kumwandaliya.
120. YVakamuona ndiyani
wakampeka asikhini
hata kwenyi Sulutwani
mwane Liyongo akaya.
121. Bawabu kenda darini
aketipo Sulutwani
akaitaka idhini
mwane ataka kungiya.
122. Sulutwani klsikiya
mno akafurahiya
kwa mwane Liyongo kuya
akamwambiya neteya.
123. kapanda naye bawabu
kijana kitaajabu
nini nimezoharibu
ni ipi yangu khatiya.
124. Kapanda wakaonana
pamoya na ule Bwana
Sulutwani akanena
nakuomba yambo moya.
125. Kamwambiya wapendani
mimi ni mwako twaani
kukhalifu simkhini
mimi ni wako raiya.
126. Kwa baba enda sikhini
umuulize yakini
kimuuwacho ni n'ni
nakuomba hili moya.

127. Au wewe wakiyuwa
nambiya sifanye tuwa
uwaziri utapowa
t'akuoza bintiya.

128. Akamjibu sisi
ya kweli hata kukisi
ila ngoja sasa basi
khabari t'akueteya.

129. Sulutwani muadhamu
kijana kamkirimu
kwa zakula zilo tamu
kampa na nguo mpiya.

130. Ule kijana katoka
akanenda hata Shaka
kwa babakeakifika
babake kamshashiya.

131. Babake kafurahika
akanena akiteka
wali mwema kaupika
maana wale pamoya.

132. Kijana kapumzika
na hamu zimemshika
ili apate haraka
haja alioyendeya.

133. Akiizengeya ndiya
ya kumuuliza haya
khaufu zimemngiya
hasubutu kumwambiya.

134. Katawakali yakini
Baba wangu wa imani
ni hamu nyingi moyoni
khatari nakucheleya.

135. Kikuuwacho ni n'ni
nami niyuwe yakini
nina hamu ya moyoni
atakuweka Jaliya.

136. Babake akamwambiya
wewe kuuliza haya
dhana nimekudhaniya
kuniuwa huzengeya.

137. Kijana akamjibu
hukunena ya thawabu
nimeapa kwa Wahabu
si wa kutendeya haya.

138. Baba ukifa yakini
mimi t'akwenda kwa nyani
nitakuwa masikini
wa chakula kuzengeya.

139. Tanipa kula ni nyani
na nguo za muilini
nipate na masikani
mahala kupumuliva.

140. Akamwambia nayuwa
kijana umefundiwa
na wewe utahadawa
hayo wamezokwambiya.

141. Baba umehadaika
wao kisa watateka
na kuzifanya dhihaka
kisa utaiyutiya.

142. Kuyuta kinyumeni
hela baba hufaani?
ni kweli nimezodhani
na yangawa t'akwambiya.

143. Nisikiya wangu baba
liniuwalo ni haba
ni msumari wa shaba
kitovuni nikitiya.

144. Jamii silaha piya
haziniwi swabiya
ila nimezokwambiya
ni ya kweli yot'e piya.

145. Kijana akisikiya
shughuli lalimngiya
kataka kusikiliya
Pate akanena haya.
- 146» Akaketi siku mbili
nafusi ina shughuli
kwa hamu tena halali
sasa huzengeya ndiya.
147. Kwa siku ya tatu yake
akamuaga babake
kamsingiza mamake
hawezi t'asikiliya.
148. Babake akamwambiya
mama kipata afiya
kheri huku sikiliya
kuketi tuwe pamoya.
149. Kijana akaitika
kamuaga akatoka
a ken end a kwa haraka
hata Pate akangiya.
150. Kenenda kwa Sulutwani
akaitaka idhini
akanena mtieni
kwa upesi nawambiya.
151. Kisa kupata idhini
kamuona Sulutwani
wakangiya faraghani
kamweleza yot'e piya.
152. Kitu kiuwacho baba
ni msumari wa shaba
menambiya ni akiba
ya hatari kucheleya.
153. Sulutwani kafurahika
akatowa kwa haraka
mhunzi akamtaka
akenda kumfuliwa.
154. Kamkirimu kijana
kwa zitu kulla namna
malalo mazuri sana
na winyi kumtumikiya.
155. Siku kumi akaketi
kipowa nzuri kuti
kusingie tafauti
ila mambo kuongeya.
156. Kijana kafurahika
tamaa zikamshika
na kuowa ni hakika
hawa watanitendeya.
157. Akaweka cha uposi
kama ni Bwana harusi
kulla siku kianisi
kipumbaza mno ghaya.
158. Kisa kumi kutimiya
Sulutwani kamwambiya
hini sindano pokeya
haya kwake sikiliya.
159. Na harusi t'atengeza
kwani nyumba nda kuwaza
na matezo tutateza
harusi kufurahiya.
160. Tushone na nguo zako
na pambo la mke wako
mwanangu harusi yako
kwa kweli t'afurahiya.
161. Kamfanyiza zakula
za ndiani ili kula
ule mwana wa Kigala
katoka kashika ndiya.
162. Naye chenenda ndiani
una khaufu moyoni
nifanye shauri gani
kwa baba kisikiliya.

163. Yakamuiya matata
iye mimi kumpata
'kitokufa ni matata
t'aniuwa mara moya.
164. Ikiwa alonambiya
ni mzaha siyo niya
kasidi kunangaliya
ni khatari nacheleya.
165. Henda kiwaza ndiani
na khaufu za moyoni
siku ya pili iyon
hata Shaka akangiya.
166. Kwa babake akangiya
baba kamfurahiya
kwa mno kamshashiya
akimnyowa na ziya.
167. Kimkanda maguuni
pamoya na muilini
kwa utofuwe ndiani
maanaye kumtowa.
168. Kijana kapumzika
kisa ndiani katoka
kwa kunena na kuteka
na wende akitembeya.
169. Na sindano kibindoni
ameisita nguoni
kamwe mtu haiyoni
akiizengeya ndiya.
170. Akimuona babake
hulipija yote lake
ili baba ashituke
na shutuki kumuwa.
171. Kimwamkuwa ghafula
huinuka kwa ajila
hujibu nipa chakula
nina ndaa humwambiya.
172. Kulla siku humwendeya
Liyongo meilaliya
kamwe haipati ndiya
kijana kishawiriya.
173. Kijana kishawiriya
kwa khaufu kuingiya
ila yeye una niya
siku zikateketeya.
174. Hata mwezi ukitimu
siku hiyo kaazimu
na yeye hana fahamu
babake meilaliya.
175. Siku zilipokithiri
Bwana akamukhubiri
huku sisi ni tayari
kutengeza mambo piya.
176. Siku kupata waraka
na babake amechoka
kwa usindizi menyoka
fahamu amepoteya.
177. Nyono zake huzivuwa
kama ngurumo za vuwa
kijana akaelewa
kwa kweli meilaliya.
178. Kayuwa hana fahamu
kijana aliazimu
kwa ile yakwe hamumu
mke kwenda kuzengeya.
179. Kamtiya kitovuni
naye ulele kwa t'ani
achamka hamuoni
kiyana amekimbiya.
180. Babake akishutuka
chembe uta akashika
kwa haraka akatoka
nde mui kuyendeya.

181. Akapija ondo lake
katambika chembe chake
kama hai ada yake
chembe utani katiya.
182. Na hapo nami t'asema
ni karibu ya kisima
watu hawakusimama
kwa wut'e walikimbiya.
183. Watu mai wasiteke
waume na wanawake
kwa pot'e khabari yake
majimbo ikaeneya.
184. Kuwa Liyongo mekwima
uko nde ya kisima
sasa watu wamekoma
mai hawapati ndiya.
185. Hapana ayapatao
nitu mai atekao
kulla mtu uko kwao
hapana wa kutokeya.
186. Wale watu wa muini
mai ya msikitini
huyateka birikani
ndiyo hayo kitumiya.
187. Yamekwisa yot'e mai
birikani mwa simai
na Liyongo hanyamai
chembe kingine metiya.
188. Kwa ndaa wakakazika
wu'e wakisikitika
ukumbi wakauweka
kufanya shauri moya.
189. Shauri likawa moya
kheri mama kumwendeya
mamakwe kusikiliya
atamsikitikia.
190. Mamakwe wakamwendeya
kwa Liyongo wut'e piya
mama kheri sililiya
ruhu zimo hupoteya.
191. Mamakwe wakamwendeya
naye mama karidhiya
wakatoka kwa umoya
nde wakasikiliya.
192. Mamakwe akaombowa
mashairi akitowa
kwa kasidi kuongowa
Liyongo haya sikiya.
193. Na mamakwe kumwegema
alikicha tema tema
kwa mbali kintizama
na nasaha miya miya.
194. Nao hayakuweleza
Liyongo ameifia
kwa khaufu kuwangiwa
hawakumkurubiya.
195. Kulla siku kumwendeya
mama wakwe akiliya
haunuki saa moya
ni hasira hudhaniya.
196. Warudipo nasahani
mama wakwe hubaini
siisi ametendani
ghadhabuzimemngiya.
197. Mwanangu meghadhibika
si ada kutopulika
ameiza kuinuka
siisi yetu khatiya.
198. Siyo yakwe mazoeya
kwa nasaha kimwendeya
husikiya mara moya
sasa udhiya metiya.

199. Mamakwe kumkurubiya
hatari aicheleya
ghadhabu zikimngiya
yoyot'e huiyuliya.
200. Kuuwa hawezekani
kighadhibika haneni
huwa zitono za ndani
na kuingurumiya.
201. Mamakwe kitaajabu
akinena ni ajabu
mara hini meharibu
ameiza kusikiya.
202. Kipata siku katiti
kaanguka ni maiti
wakatambua umati
Liyongo ameifia.
203. Wut'e wakakurubiya
mamakwe na watu piya
sana wakamwangaliya
ni sindano ametiwa.
204. Ametiwa kitovuni
shaba sindano yuwani
wakamtia muini
akazikwa kwa umoya.
205. Habari ikaeneya
Pate ikasikiliya
Mfalume kitaiwa
furaha zikamweneya.
206. Mwane Liyongo yakini
mewekwa magodoroni
na zakula anuani
huila akiinwiya.
207. Mfalume kipulika
Liyongo ameitoweka
nde mui meanguka
haya aliazimia.
208. Akanena mueteni
mwane Liyongo yakini
aye hapa hadharani
nina neno t'amwambiya.
209. Akenda akatwaliwa
kaya kwa Bwana welewa
Mfalume katongowa
Khabari akamwambiya.
210. Amekufa baba wako
akaangua kiteko
kwake kamwe sikitiko
kabisa halikungiya.
211. Mfalume kamwambiya
mbona mwana hukuliya
babako alikuyeya
kwa anasa zot'e piya.
212. Ule mwana wa swahihi
kajibu nimefurahi
menitendea Ilahi
haya menijaaliya.
213. Mfalume kabaini
kabisa huna imani
epuka mwangu matoni
na nyumbani nitokeya.
214. Usiketi mui wangu
wewe adui wa Mngu
tena vua nguo zangu
vaa yako mazoweya.
215. Kuwa mwana wa Kigala
ni adui wa dhalala
ya babakwe amekula
damu kwa kuiuliya.
216. Mfalume kamtowa
nguo zakwe kamvuwa
na watu akatukiwa
khabari ikaeneya.

217. Ikaeneya khabari
kwa jamii ya jifiri
wakanena si uzuri
kwa yot'e majimbo piya.

218. Yule mwana nikwambiye
hakwenenda kwa bibiye
kwa mama Liyongo yeye
Galani alikimbiliya.

219. Watu akitayahari
kwa ile yakwe amri
watu wakimtiriri
mayuto yakamngiya.

220. Kaingiya mayutoni
katindikia nyumbani
hata wenzi hawaoni
hamu imezongiya.

221. Ule mamakwe kijana
hakumpenda tena
kimwamba na kunon'gona
mno akamtukiya.

222. Kawa tena hampendi
kwa chakula hamtundi
yakamzidi mayondi
huzuni zikamngiya.

223. Siku chache kitimiya
maradhi yakamngiya
yasiyomuondokeya
naye kisa kaifiya.

224. Make Liyongo hakika
matanga aliyaweka
watu wakasikitika
kwa Liyongo kuifiya.

225. Liyongo silaha yetu
kwa wut'e khasimu zetu
alikuwa ngao yetu
wut'e wakinena haya.

226. Mui walisikitika
hakuna wa kutosheka
kwa liyongo kutoweka
imeanguka paziya.

227. Sana wakahuzunika
na matanga wakaweka
kisa mamake katoka
kana ada katembeya.

228. Tumcz.iye kukhitimu
hapo ndio wasalamu
Ilahi tatukirimu
kwa baraka na afiya.

229. Rabi tatusahiliya
na uzito wa duniya
tena tatujaaliya
kuwa njema yetu niya.

230. Ya Liyongo hukwambiya
Siu alikozaliwa
Pate akitembeleya
kwa mwana akafililiya.

231. Na kwa mwana ni Rasini
ya Shaka iyuweni
ni mui hapo zamani
ni mkuu hukwambiya.

232. Mui waloamirika
nyumba za mawe hakika
mayiwe waliyaweka
na misikiti pamoya.

KIAMBATISHO 3

IAKHMISA YA LIYONGO

- 1. Nabudi kawafi takhamisa kidiriji,
Niwathihishe izagale kama si raji,
Ili kufuasa ya Liongo simba wa miji.
Ai wanji wanji nazawanji kisi/a wanji;
Ma kadiliza kasiliza, mwanangwa mema.**

- 2. Pindi uonapo ali shari mume mwendo,
Pindua mtima utie kani na vindo,
Uwe ja na mire, tui mke, katika shindo.
Mwanangwa mbonaye mbuzi wako katika mwendo;
Ukimetwa pembe na mkami akimkamaa.**

- 3. Akhi ewe mbuya twambe mambo ya kujelele,
Huyu muungwana shati ^kari haiondole,
Nakuchea kufa mwenyi cheo kavilikele.
Mwanangwa mbonaje muhakara wakwe wiimile;
Asirathi kufa na mavuto yakava nyuma.**

- 4. Naapa kwa Anjili na Zaburi ili kiapo,
Simke ngeufu pindi shari liwagazapo,
Naye keeza moyo katokoza shari lilipo.
Mtetea cheo mwenyi cheo ateteapo;
Hamhiwi ni nawi hatta roho nengakoma.**

- 5. Naitenda mja kwa wenzangu kapata sono,
Wala sina yambo siwatayi kwa mavongono,
Bali sikubali lenyi thila na matukano.
Ni mwofu wa ta nishikapo na oa mno;
Ni mui wa kondo sikiapo mbi kalima.**

- 6. Siwagazi kondo msi lango kapiga kifa,
Ili kusifua kwambazo ni tule swifa,
Nitanga mizapo kondo nzito tenda hakhafa.
Ni mwana shajighi mpendeza nyemi za kufa;
Kwa kucha mpeo na adui wa kunisema.**

7. Bonapo harubu kiugua nana na afya,
Kawana furaha ja arusi ya mzofafa,
Naikeza moyo kwa Muungu nisikhilafa.
Ni mwana asadi mpendeza nyemi za kufa;
Kwa kucha nipeo na adui kumhuya nyuma.
8. Napa kwa Muungu na Muungu ili kiapo,
Nampenda mtu pindi nave anipendapo,
Bali ndugu yangu ⁴ari punde ambagazapo.
Ninga mana kozi sioneki niwakuapo;
Ni mui wa nvuni naakua katika jama.
9. Wallahi nithiika saya yangu si maongope,
Teteapo cheo kiwa muyi nawa meupe,
Nimpapo uso aduiye shatti akope.
Ninga mana taya shirikeni na mana tope;
Na mlisha yani lenyi tani na zingulima.
10. Laiti kiumbe pindi mambo yakimpinga,
Papale angani aduize akaweanga,
Awavunda paa na mifupa ya mitulinga.
Ningali kipungu niushile katika anga;
Kila nyama toto hatta simba mkuu nyama.
11. Ningatindangile kwa sayufu na kwa sakini,
Na musu mkali kiupeka juu na tini,
Kivuma ja mwamba usokaa nili na kani.
Bali muu yangu yu mawili kuwa pinguni;
Na shingoni mwangu nawishiwa peto la chu
12. Ningashahadize Korani yangu kalina,
Ilia uketeze kuwa nyimbo Mola karima,
"Wama huwa bi shairi kalilama."
Tufutufu mayi kizimbwini yawanguruma;
Ha'mwezi kwima luishapo wimbi Ungama.

13. Ata maagano na makato ujikatayo,
Sangase mkono kumtenda akutendayo,
Kumlipa deni mtu kata akupasayo.
Sipepese moyo kupepesa kwa uuwayo,
IMtawapona aduizo wakula nvania.
14. Sange kumtenda mnitenda mawi yetania,
Kama chambileo chuonimwe mwenyi athama,
"Wa in'akabitum fahakibu bi mithilima."
Pindi uonapo moto zita ukinguruma,
La Allah , ni mimi niwashao maa kazima.
15. Nyani muurudi moyo wangu hukisakawi?
Tetcapo cheo hatta mtu simtambui.
Naikutakuta kayatia katika wawi,
Katinda kitinda arithisha wangu mtima.
16. Ewe mbasi yangu twambe kwamba huitabiri,
Kiumbe mwenzio huwezaye kukuhasiri?
Tetea hakio ujitie katika shari.
Siche mata yao na mafumo yanganawiri,
Mangi mafumati na magao maoya nyuma.
17. Ni upi mchayi kicho chakwe kimokoao?
Na mjahasiri umurie ipunguwao?
\Iwazi ata kicho na wachao sandaye nao.
Wangapi wachao utamboni wangamiao,
Na wazimbiao utamboni wakisiamu.
18. Bolewe mchayi mcha kufa asiofikira,
Na kufa si suna ni farathi ya mkadara,
Bolewe mchayi mcha kufa hapati ^kura.
Akuta mpeo na hizaya na muhakara;
Kwa kucheza roho na mwisoeaya ja kutama.
19. Nionapo ⁴ari ulimwengu wanitukiza,
Moyo ukinayi hatta ndani ukawa kiza,
Na nde mwa kope tozi tule likituuza.
Simba uwalia kwa kilio akivumiza;
Kilio kikuu kifishacho mtu huruma.

20. kiliacho simba ni matule kulla matufu,
Simba uwalia elewani nawaarifu,
Sithanie simba muu mane wenda 'arufu.
Simba bora ndume watetea jaha na cheo;
Watetea jaha hatta mato yakafunama.
21. Ana mi shujaa simba ndole niwondoa 'ari,
Mvunda kilaa na husuni ki/idabiri,
Naipiga kifa haitia katika shari.
Sichi mata zao na mafumo yanganawiri;
Mangi mafumati na magao mawi ya nyuma.
22. Ana ndimi simba mfiliye jaha na cheo,
Naipiga kati kwanesa wajibagao,
Siche aduizo kukutana kwa ungi wao.
Sichi kikwi chao nami ume ndio nilio;
moyo wangu kikwi kwa ajili ya kushangama.
23. Ndimi akabiri uteteo wangu niurua,
Thili siikiri ya kiumbe mukulukua,
Naakua anjari penyi kikwi kaishambua.
Kifa tenda ngao paziwapo kipazua;
Nisikhofu miwa wala tome za kunitoma.
24. Mwanzi ata kicho na wachao sendanye nao,
Nao fawithi umuri kwa IMuungu anusurao,
Siche ya ziumbe na zituko wakutishao.
Kufa kwa IMuungu na shabuka limkutao;
Si kwa walimwengu mivi kikwi ingakufuma.
25. Watetea jaha woka nyoyo wasio changa
Watwa miwili wakalisha misu na panga
Woandoao thuli penyi ⁴ari wakaitenga.
Si simba mikia wameao vuzi na singa;
Simba mashujaa wasabili ngozi na nyama.

**26. Tamati nishi/e takhamisi kinaathimu
V a Lionga fumo nima/.iye kuikhitinui,
Mwona lahani akitoa liana laumu.
Wapata ajira kumlipa Mola karimu;
Siku ya niajaza walipwapo wawi na wema.**

**27. Na mwenyi kutunga mbaarifu yakwe isimu,
Ni Abdallah muyuweni mumfahamu,
Ibun Ali bun Nasiri mwenyi makamu,
Farii ya Makka shimukati lao Farimu;
IMungi wa karama buruhani na mashuhuri;
Kwa zamani zakwe hakwalina kaniaye kama.**

KIAMBATISHO 3


OISA C HA WA IIJ W A LAMU

1. Nanda kwa yangu nudhumu
qisa cha watu wa Amu
alotaka kti-dhultimu
IMarabu kuwa woneya.
2. Musiniu walipo kwima
hapo wakatenza chama
Warabu wakasimama
qusudi kuchangaliya.
3. Mno wakata 'ajabu
kuona nyingi dhahabu
haikubaki hiibubu
shingoni kutozitiya.
4. Roho zikawazunguka
nianeno wakanika
qaribu yakuondoka
kheri tukawangilia.
5. Lingiye tusilifanye
dhahabu tuwanyang'anye
twende tukaawanye
asikose nitu mmoya.
6. Walipofanya shauri
wakachelelya khatari
walipo mustaqiri
Amu ameiyoleya.
7. Wakamanibiamwendani
huwendi ungiye kondeni
shemeji zako muwini
sinende ukawambiya.
8. Kwa utungu akanena
kwani kunitukana
nyingi ni nduzangu sana
siwezi kuwachongeya.
9. Akishuka jaha/ini
akaongoza barazani
akamwita faraghani
mfalume kamwambia.
10. Akainuka nisemi
Bana Zaidi Mgumi
niyani anitao niinii
tayari kumsikiya.
11. Akainuka swahibu
kanena kuna ajabu
jamaa zangu Warabu
wataka kuwangiliya.
12. Jahazi watazibari
washlike alifajiri
dhahabu na mahariri
kuya kuwatukuliya.
13. Mfalume aziwize
khabari siitangaze
ni kheri tuitangaze
ili pote ikeneya.
14. Akaandika baruwa
watu akawamkuwa
panga wakazisugua
yuwani wakadeteya.
15. Mtoko wa al-asiri
niuwe katika bandari
na hata alifajiri
musiwate kuwangiye.
16. Nyivani fujo mufave
na mali niuwayangaye
yoyote asiwakanye
nanyi mukanisikiya.


17. Mumalizapo niuini
shukiyani forodhani
nmpande majahazini
niali kuwatukulia.
18. Barua akimali/a
katukua manahoza
maneno kawaagiza
ktivusha qaurmi pia.
19. Alipongiya muini
wakashukiya na pwani
wakapanda jaha/ini
niali kuitukuliya.
20. Warabu na wenye mui
khabari hawaiyui
na nyoyo zisitumai
waken (Ia kushitakiva).
21. Iiana Zaidi kajibu
niusione ni ajabu
Waswahili na Warabu
Maneno yangu sikiya.
22. Ilawa ni badui wetu
kula mwaka wana kitu
na sasa makosa yetu
ada siku wapekeya.
23. Wakavuta zao hori
kenda kufanya shauri
wakafunga na safari
upeski kuwa kimbiva.
24. Wakanena kwa kituwo
hawa ni wao kwa wao
mngine asiokwao
ni upesi kumngeya.
25. Tukizidisha niakazi
wata tupoka jahazi
badua hawa ni wezi
hushinda wakituibiya.
26. W akisha kuvondokeya
hapo kukapijwa mbia
si rukhusa kusalia
ukumbini mwangu kuya.
27. Walipokuwa tayari
tena kawapa khabari
kiswa kile chalojiri
hila alizotumia.
28. Shauri ni wachondoka
nyoyo zikafurahika
kwa hila zalotumika
kwa hakimu na raia.
29. Kondoka duniani
tarikhi yake ni hini
alifu na miatani
ishirini mbili tiya.
30. Alotunga mashairi
Rabbi anijaze kheri
ayatakao yajiri
milele kiyatimiya.

KIAMBATISHO 4

RAMANI 1: ENEO LA SHUNGWAYA



**RAMANI 2: PWA™ VA AFRIKA N^HARIKI KWA MUJIBU WA
RAMANI YA IDRISI YA MWAKA 1154 B.K**



KIAMBATISHO 6

Ramani V MAR.iiRO yaliyosababishwa na MFECANE




Fig. 3. The chain of violence in the east, 1821-1837.

KIAMBATISHO 7

SI4AKA ZULU



The **mighty** Shaka, founder of the Zulu nation. This drawing by James Saunders King is the only authentic portrait of the first Zulu King

South African Library